# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA TAMISEMI, SEKRETARIETI ZA MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA
## KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24















MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

MACHI 2025

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Mahakama, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu: +255(026)2161200-9; Barua pepe: ocag@nao.go.tz Tovuti: www.nao.go.tz.

**Kumb.Na.CGA.319/421/01** **27 Machi 2025**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya ukaguzi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua za kuchukua ambazo zinalenga kukuza uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Nawasilisha,

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mamlaka**

Wajibu wa kikatiba na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu zinazoimarisha Imani kwa Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Kauli Mbiu**

Kuwa Taasisi yenye kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

## Misingi ya Maadili

**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo:** Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo

**Kufanya kazi kwa uadilifu:** Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadilina sheria katika utoajiwa huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo:** Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi staiki

**Kufanya kazi kwa utaalam:** Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi** Tunahimiza, kuvumbua na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwaajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa ushirikiano:** Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje

# YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI ........ v

ORODHA YA VIAMBATISHO ........ ix

ORODHA YA VIELELEZO ........ xii

VIFUPISHO ........ xiii

SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI. xv

MUHTASARI ........ xvii

SURA YA KWANZA ........ 1

MAELEZO YA AWALI ........ 1

SURA YA PILI ........ 6

HATI ZA UKAGUZI ........ 6

SURA YA TATU ........ 11

UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MIAKA YA ILIYOPITA...... 11

SURA YA NNE ........ 15

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ........ 15

SURA YA TANO ........ 28

USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI ........ 28

SURA YA SITA ........ 57

USIMAMIZI WA UNUNUZI ........ 57

SURA YA SABA ........ 79

TATHMINI YA UTAWALA BORA NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI ........ 79

SURA YA NANE ........ 86

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU ........ 86

SURA YA TISA ........ 94

UWEKEZAJI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ........ 94

SURA YA KUMI ........ 109

UTENDAJI WA KISEKTA ........ 109

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na.1: Mwenendo wa hati za ukaguzi ........................................ 8

Jedwali Na.2: Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake ........................................................................................ 9

Jedwali Na.3: Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti .... 10

Jedwali Na.4: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita ............................................................................................ 12

Jedwali Na.5: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya kamati za bunde za LAAC na PAC ........................................................................................ 13

Jedwali Na.6: Tathimini ya mwenendo wa bajeti kwa miaka mitano.......... 17

Jedwali Na 7: Fedha za ruzuku za matumizi ya kawaida ......................... 17

Jedwali Na.8: Mapitio ya Fedha za Ruzuku za Maendeleo ........................ 18

Jedwali Na.9: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa miaka mitano ............................................................................................ 18

Jedwali Na.10: Halmashauri zenye makusanyo zaidi ikilinganishwa na bajeti 19

Jedwali Na.11: Halmashauri ambazo hazikufikia malengo ya makusanyo...... 19

Jedwali Na.12: Fedha ambazo hazikupelekwa...................................... 22

Jedwali Na.13: Shughuli ambazo hazikupelekewa fedha ......................... 23

Jedwali Na.14: Matumizi ya Fedha za Bakaa bila Idhini kutoka kwa ........... 24

Jedwali Na.15: Fedha za bakaa ambazo hazikutumika............................ 25

Jedwali Na.16: Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma ............................................................ 30

Jedwali Na.17: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma ........................................................................................ 31

Jedwali Na.18: Mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimekusanya ushuru wa huduma bila msingi wa ukokotoaji ................................................ 32

Jedwali Na.19: Kutokusanywa kwa Mapato kutoka kwa vyanzo mbalimbali ... 34

Jedwali Na.20: Muhtasari wa mapato yaliyokusanywa pasipo kupelekwa benki ............................................................................................ 35

Jedwali Na.21: Mamlaka ya serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa mazao ........................................................................................ 36

Jedwali Na.22: Orodha ya mamlaka ya serikali za mitaa zenye madai ......... 38

Jedwali Na.23: Mapato ya Ndani Yaliyokusanywa LGRCIS badala ya TAUSI .... 40

Jedwali Na.24: Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato bila kuzingatia matakwa ya mkataba ........ 41
Jedwali Na.25: Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato nje ya mfumo ........ 42
Jedwali Na.26: Bili zilizotolewa kupitia TAUSI na GoTHoMIS hazijalipwa ........ 43
Jedwali Na.27: Mapato yasiyokusanywa kutoka kwa kodi ya ardhi na ada za mabango ........ 45
Jedwali Na.28: Malipo Yasiyo na Stakabadhi za Kielekitroni ........ 49
Jedwali Na.29: Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslimu ........ 51
Jedwali Na.30: Fedha zilizokopwa akaunti ya amana bila kurejeshwa ........ 53
Jedwali Na.31: Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa akaunti ya Amana ........ 54
Jedwali Na.32: Malipo bila uthibitisho wa fedha kupokelewa akaunti ya Amana ........ 54
Jedwali Na.33: Uhamisho wa Mapato ya Ndani kwenda akaunti ya Amana ........ 55
Jedwali Na.34: Ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka ........ 60
Jedwali Na.35: Ununuzi yaliyofanywa bila nukuu za ushindani ........ 60
Jedwali Na.36:Taasisi za TAMISEMI zilizotekeleza mpango wa ununuzi chini ya kiwango ........ 62
Jedwali Na.37: Ununuzi bila idhini ya bodi ya zabuni ........ 63
Jedwali Na.38: Ununuzi mdogo usioripotiwa kwa Bodi za Zabuni ........ 63
Jedwali Na.39: Bidhaa zilizopokelewa bila kukaguliwa ........ 65
Jedwali Na.40: Halmashauri zilizo na vitu vilivyonunuliwa bila maelezo maalumu ........ 66
Jedwali Na.41: Taasisi zenye Ununuzi ya Vifaa vya Ujenzi Zaidi ya mahitaji ........ 67
Jedwali Na.42: Ununuzi Yanayofanywa bila LPOs ........ 68
Jedwali Na.43: Taasisi zilizofanya Malipo Kabla ya Kupokea Bidhaa ........ 69
Jedwali Na.44: Orodha ya mikataba ambayo haijahakikiwa ........ 70
Jedwali Na.45: Malipo bila Kipimo na Uidhinishaji wa Mhandisi ........ 72
Jedwali Na.46: Kutojumuishwa kwa ununuzi wa ngazi za chini katika ripoti za robo mwaka ........ 73
Jedwali Na.47: Mikataba iliyotolewa kwa kikwazo na TARURA Mkoa wa Singida pasipo uhalali ........ 74
Jedwali Na.48: Mikataba ambayo chanzo kimoja na utoaji wa zabuni uliozuiliwa ulitumika ........ 75

Jedwali Na.49: Kandarasi nyingi kwa Mzabuni mmoja kabla ya kukabidhi kandarasi nyingine kupitia njia ya chanzo kimoja .................................. 75

Jedwali Na.50:Taasisi zilicheleweshsa malipo kwa kazi zilizotekelezwa na wakandarasi ............................................................................ 77

Jedwali Na.51: Muhtasari wa Michango katika taasisi mbalimbali ............... 88

Jedwali Na.52: Taasisi Zenye Wafanyakazi Wenye Utofauti wa Tarehe za Kuzaliwa ............................................................................ 90

Jedwali Na.53: Taasisi Zenye Watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika .............................................................. 92

Jedwali Na.54: Uwekezaji uliofanywa na Kila Halmashauri ....................... 96

Jedwali Na.55: Mapato Tarajiwa dhidi ya Makusanyo Halisi kwa Miradi ya Uwekezaji.................................................................... 106

Jedwali Na.56: Halmashauri zenye miradi iliyokamilika lakini haijatumika ... 113

Jedwali Na.57: Orodha ya MSM zenye Fedha za Miradi ambazo Hazikutumika 116

Jedwali Na.58: Orodha ya Halmashauri zenye Miradi Iliyotelekezwa .......... 117

Jedwali Na.59: Utekelezaji wa Miradi ya Barabara kwa Teknolojia Mbadala . 120

Jedwali Na.60: Ulinganisho wa Gharama kati ya ECOROADS na Njia za Kawaida .................................................................................. 121

Jedwali Na.61: Mikataba Iliyovunjwa Lakini Taarifa Zake Hazikupelekwa PPRA na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ........................................... 124

Jedwali Na.62: Fidia ya Hasara Haikutolewa ..................................... 124

Jedwali Na.63: Mikataba iliyocheleweshwa zaidi ya muda unaokubalika na haikusitishwa................................................................... 125

Jedwali Na.64: Madai yasiyorejeshwa na Mfuko wa Bima ya Afya ............. 131

Jedwali Na.65: Halmashauri zenye dawa zilizoisha muda wa matumizi ..... 132

Jedwali Na.66: Fedha za uchangiaji wa gharama za dawa na vifaatiba zilizobadilishiwa matumizi ........................................................ 133

Jedwali Na.67: Halmashauri zenye salio la fedha MSD ........................... 134

Jedwali Na.68: Halmashauri zenye vifaa tiba visivyotumika .................... 135

Jedwali Na.69: Hali ya uandikishaji wa kaya mpya kwenye mpango wa iCHF 136

Jedwali Na.70: Ruzuku zinazolingana ambazo hazijatolewa .................... 138

Jedwali Na.71: Madai yaliyocheleweshwa ........................................ 138

Jedwali Na.72: Mali Zisizokuwa na Namba za Utambulisho .................... 141

Jedwali Na.73: Mapungufu kuhusiana na Ulipaji wa Fidia ...................... 146

Jedwali Na.74: Mikopo isiyorejeshwa na vikundi vilivyositisha biashara ..... 149

Jedwali Na.75: Mwenendo wa michango ambayo haikuwasilishwa kwenye mfuko ........ 151

## ORODHA YA VIAMBATISHO


Kiambatisho Na.1:Hati za ukaguzi na hitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na bajeti kwa mwaka 2023/24 ........................................... 153

Kiambatisho Na.2:Utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita ............................................................................................ 161

Kiambatisho Na.3:Utekelezaji wa maagizo ya kamati za Bunge za LAAC na PAC ............................................................................................ 165

Kiambatisho Na.4:Mwenendo wa utoaji Ruzuku na bajeti ...................... 170

Kiambatisho Na.5:Mwenendo wa Ruzuku za kawaida............................ 172

Kiambatisho Na.6:Mwenendo wa Ruzuku za Maendeleo ........................ 172

Kiambatisho Na.7:Makusanyo ya mapato ya ndani kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ........................................................................... 173

Kiambatisho Na.8:Halmashauri zilizokusanya zaidi ya bajeti .................. 173

Kiambatisho Na.9:Halmashauri zilizoshindwa kufika lengo la ukusanyaji wa mapato ya ndani.................................................................. 175

Kiambatisho Na.10:Fedha ambazo hazikulipwa .................................. 177

Kiambatisho Na.11:Ruzuku zilizotoka kwa kuchelewa .......................... 179

Kiambatisho Na.12:Kuchelewa kutumia fedha zilizopokelewa................. 181

Kiambatisho Na.13:Kutopelekwa kwa fedha kwenye miradi ya maendeleo ya maendeleo ......................................................................... 182

Kiambatisho Na.14:Mpango wa bajeti usiotosheleza malipo ya deni.......... 183

Kiambatisho Na.15:Fedha zilizochepushwa kwa shughuli zisizokusudiwa .... 184

Kiambatisho Na.16:Mapato halisi yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/24 ............................................................................................ 184

Kiambatisho Na.17:Mapato yaliyokusanywa na kutopelekwa benki ........... 188

Kiambatisho Na.18:Mapato ambayo hayajakusanywa kwa kutozingatia masharti ya mikataba ........................................................................ 190

Kiambatisho Na.19:Kodi ya zuio iliyokatwa kutowasilishwa TRA .............. 194

Kiambatisho Na.20:Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi ........................................................................... 194

Kiambatisho Na.21:Orodha ya zabuni zilizowekewa vikwazo bila uhalali katika TARURA Mkoa wa Morogoro........................................................ 196

Kiambatisho Na.22:Mikataba ya chanzo kimoja bila uhalali - TARURA-Mkoa wa Tanga.......................................................................... 197

Kiambatisho Na.23:Orodha ya mikataba isiyojumuisha maoni kutoka kwa Afisa wa Sheria ........................................................................ 199

Kiambatisho Na.24:Kuchelewa kwa malipo ya kazi zilizoidhinishwa TARURA 201

Kiambatisho Na.25:Kazi zilizoidhinishwa hazijalipwa ........................... 211

Kiambatisho Na.26:Mapungufu kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ................ 219

Kiambatisho Na.27:Mapungufu katika uthibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi ........................................................................ 220

Kiambatisho Na.28:Michango ya Wafanyakazi Isiyowasilishwa na Adhabu Zinazoweza Kuepukika ........................................................... 221

Kiambatisho Na.29:Malimbikizo ya Madai ya Watumishi ........................ 223

Kiambatisho Na.30:Watumishi waliohama/kuhamia bila kuhuisha taarifa zao kwenye Mfumo wa Utumishi ..................................................... 224

Kiambatisho Na.31:Mapungufu katika Mipango na Ushirikishwaji wa Wadau katika Uwekezaji wa Masoko .................................................... 225

Kiambatisho Na.32:Mapungufu ya Kimiundombinu na Kiusimamizi katika Masoko ........................................................................ 226

Kiambatisho Na.33:Mapungufu ya Utumiaji na Ufanisi katika Vituo vya Mabasi ........................................................................ 229

Kiambatisho Na.34:Halmashauri zilizowekeza Fedha katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Pasipokuwa na Tija............................................. 229

Kiambatisho Na.35:Kasi Ndogo ya Ujenzi na Miradi Isiyokamilika ............. 231

Kiambatisho Na.36:Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Kutembelea Miradi ya maendeleo ........................................................................ 234

Kiambatisho Na.37:Mapungufu ya Usimamizi wa Mikataba na Udhibiti wa Ubora katika Miradi ya Barabara za TARURA............................................. 235

Kiambatisho Na.38:Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Miongozo na Usanifu katika Miradi ya Barabara za TARURA ................................................... 243

Kiambatisho Na.39:Hasara kutokana na madai yasiyolipwa na Bima ya Afya NHIF ........................................................................ 257

Kiambatisho Na.40:Upungufu wa vifaa tiba vilivyo agizwa kutoka bohari ya dawa ........................................................................ 258

Kiambatisho Na.41:Orodha ya Taasisi Zenye Magari, Pikipiki na Mali Nyingine Zilizoharibika ........................................................................ 259

Kiambatisho Na.42:Orodha ya Taasisi Zenye Mali Bila Bima.................... 261

Kiambatisho Na.43:Orodha ya Taasisi zenye Mali ambazo Hazijasajiliwa katika mfumo wa GAMIS ........................................................................ 261

Kiambatisho Na.44:Miradi mipya iliyojengwa kabla ya kupata hatimiliki .... 262

Kiambatisho Na.45:Viwanja ambavyo havijaendelezwa......................... 263
Kiambatisho Na.46:Mashauri ya Ardhi dhidi ya Halmashauri ................... 264

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 1:Mwenendo wa makusanyo ya mapato ..................................29
Kielelezo Na. 2:Kushuka kwa thamani ya uwekezaji wa hisa ..........................97
Kielelezo Na. 3:Mtiririko wa Ukusanyaji Mapato kwa Miradi ya Kimkakati......... 105

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ALAT | Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania |
| AMCOS | Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko |
| AO | Afisa Masuuli |
| APA | Makubaliano ya Utendaji ya Mwaka |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BOQ | Makadirio ya ujenzi |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali |
| DART | Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam |
| DAS | Katibu Tawala Wilaya |
| DDC | Shirika la Maendeleo Dar es Salaam |
| FFARS | Mfumo wa Uhasibu na Utoaji Taarifa Katika Vituo vya Kutolea Huduma |
| G.N | Nambari ya Gazeti |
| GAMIS | Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GoTHoMIS | Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania |
| GPSA | Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini |
| H/Jiji | Halmshauri ya Jiji |
| H/M | Halmashauri ya Manispaa |
| H/Mji | Halmashauri ya Mji |
| H/W | Halmsahuri ya Wilaya |
| HCMIS | Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu |
| HESLB | Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu |
| HRM | Usimamizi wa Rasilimali Watu |
| iCHF | Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| ISSAI | Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| KKK | Kupanga, Kupima na Kumilikisha |
| LAAC | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa |
| LAAM | Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| LAN | Mtandao wa Eneo Mzunguko |
| LGFM | Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa |
| LGLB | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa |
| LGRCIS | Mfumo wa taarifa za ukusanyaji mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| LGTI | Chuo cha Mafunzo cha Serikali za Mitaa (HOMBOLO) |
| LPO | Agizo la ununuzi wa ndani |
| MLHHSD | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi |
| MoH | Wizara ya Afya |
| MoU | Hati ya Makubaliano |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MTEF | Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati |
| MUSE | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |

| | |
|---|---|
| Na. | Namba |
| NeST | Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi wa Kielektroniki |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NIDA | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| OR TAMISEMI | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PAC | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Umma |
| PFR | Kanuni za Fedha za Umma |
| PlanRep | Mfumo wa bajeti |
| PMG | Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| PMU | Kitengo cha usimamizi wa manunuzi |
| POS | Mashine za kukusanyia mapato |
| PPRA | Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma |
| PSE | Taasisi za Umma |
| PSSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma |
| R.E | Toleo Lililorekebishwa |
| RAS | Katibu Tawala Mkoa |
| S/M | Sekretarieti ya Mkoa |
| SBD | Nyaraka za Zabuni za Kawaida |
| Sh. | Shilingi |
| TALGWU | Chama cha Wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TARURA | Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TSA | Akaunti ya Pamoja ya Hazina |
| TSC | Tume ya Utumishi wa Walimu |
| UTT | Umoja wa Dhamana ya Tanzania |
| WMA | Maeneo ya Jumuiya ya Usimamizi wa Wanyamapori |

## SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ambayo inajumusiha Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na taasisi zilizopo chini yake, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Naipongeza Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kujitolea kwake katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa menejimenti za taasisi husika kwa ushirikiano wao katika kutoa taarifa na maelezo muhimu yaliyosaidia katika kuandaa taarifa hii.

Matokeo ya ukaguzi yanabainisha changamoto kadhaa katika usimamizi wa fedha, hasa udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani, mapungufu katika masuala ya utawala bora, dosari katika ununuzi, upungufu katika ukusanyaji wa mapato, kasoro katika usimamizi wa mali na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi. Ingawa taasisi zote zilizokaguliwa zimepata hati za ukaguzi zinazoridhisha, mapungufu yaliyoainishwa yanahitaji hatua za haraka za marekebisho ili kuimarisha uwajibikaji wa kifedha, uwazi wa kiutendaji na uzingatiaji wa kanuni.

Nimebaini matukio ya mara kwa mara ya matumizi yasiyofaa ya rasilimali, utekelezaji duni wa bajeti na upungufu wa ufanisi wa kiutendaji, ambayo kwa pamoja yanakwamisha utoaji bora wa huduma kwa umma. Masuala haya ya kimfumo yanaashiria umuhimu wa hatua za kina kuchukuliwa na maafisa wenye dhamana, mamlaka za usimamizi na wadau husika ili kuimarisha uwajibikaji katika sekta ya umma.

Nawahimiza maafisa wote wenye dhamana, vyombo vya usimamizi na mamlaka za kiutawala kushughulikia kwa haraka mapendekezo ya ukaguzi yaliyoainishwa katika ripoti hii. Hatua madhubuti zinahitajika ili kuimarisha udhibiti wa bajeti, kuboresha matumizi ya rasilimali, kuimarisha taratibu za ununuzi, na kuhakikisha utekelezaji wa miradi kwa wakati ili kuongeza thamani ya fedha na hivyo kuongeza imani ya wananchi.

Aidha, napendekeza tathmini ya kina ya mikakati ya uwekezaji ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ifanyike ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinazatoa manufaa halisi na endelevu ya kijamii na kiuchumi. Kipaumbele maalum kinapaswa kutolewa katika masuala ya kujenga uwezo, kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuhakikisha uzingatiaji madhubuti wa kanuni za kifedha na matakwa ya kisheria.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali inaendelea kuwa thabiti katika dhamira yake ya kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa uhuru na weledi, kwa lengo la kuhimiza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mwisho, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa weledi wao, bidii na juhudi kubwa zilizowezesha ukaguzi huu kukamilika kwa mafanikio makubwa.



Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI

Muhtasari huu unawasilisha matokeo muhimu ya ukaguzi, hitimisho, na mapendekezo. Ukaguzi ulifanyika katika taasisi 220, zikiwemo Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na taasisi zilizo chini yake, Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184.

Malengo makuu ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini uadilifu wa kifedha kwa kutathmini iwapo mifumo ya uhasibu ilitumika ipasavyo na kutathmini uzingatiaji wa sheria mbalimbali.

Tathmini hii ilibaini mapungufu katika mfumo wa udhibiti wa ndani, masuala ya kiutendaji, changamoto za kiutawala bora na kutokuzingatiwa kwa matakwa ya kisheria. Kwa kuzingatia matokeo haya, ukaguzi unahitimisha kuwa hatua za haraka zinahitajika ili kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani, kuongeza uwazi na kuboresha uwajibikaji katika utoaji wa taarifa za fedha.

## Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, taasisi zote 220 zilizokaguliwa zilipata hati zinazoridhisha.

## Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kutoka miaka iliyopita inaonesha kuwa kati ya mapendekezo 8,366 yaliyosalia, 3,471 (42%) yametekelezwa kikamilifu, 3,215 (38%) yapo katika hatua za utekelezaji, 498 (6%) hayajatekelezwa, 848 (10%) yamerudiwa na 334 (4%) yamepitwa na wakati.

## Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

Mamlaka za Serikali za Mitaa 156 na Sekretarieti za Mikoa 20 zilifanya malipo ya jumla ya Sh. bilioni 118.21 kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Hata hivyo, kufikia tarehe 30 Juni 2024, miamala hiyo ilirejeshwa au kukataliwa, ikimaanisha kuwa miamala husika haikukamilika. Tarehe 18 Novemba 2024, Wizara ya Fedha iliielekeza OR - TAMISEMI kutumia bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25 kugharamia malipo hayo yaliyokwama. Kushindwa kukamilisha malipo hayo kumesababisha kucheleweshwa kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na kutolipwa kwa madai ya wazabuni. Aidha, maelekezo yaliyotolewa na Hazina tarehe 18 Novemba 2024 yanaweza kusababisha uchepushwaji wa fedha kutoka kwenye shughuli

zilizopangwa, jambo ambalo litasababisha ukiukwaji wa udhibiti wa bajeti.

Kwa upande mwingine, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 29 na Sekretarieti za Mikoa mbili zilirudisha Sh. Bilioni 10.85 kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) kutokana na ukosefu wa muda wa kufanya matumizi ya fedha hizo zilizopokelewa kati ya mwezi Mei na Juni 2024. Zaidi ya hayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa 27 zilirudisha Sh. Bilioni 19.98 zilizokuwa zimepokelewa kati ya mwezi Septemba 2023 na Januari 2024, ambapo Halmashauri ya Wilaya Mbeya, Halmashauri ya Mji Tunduma na Halmashauri ya Wilaya Buchosa walirudisha jumla ya Sh. Bilioni 4.92 kutokana na kuchelewa kwa maamuzi ya matumizi ya fedha hizo. Kutokana na hayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa zinaweza kupata changamoto katika kutekeleza shughuli za kiuendeshaji, na baadhi ya taasisi kushindwa kutekeleza mikataba kutokana na ukosefu wa fedha.

Katika mwaka wa fedha wa 2023/24, kiasi cha Sh. bilioni 127.50 chini ya mfuko wa jimbo zilitengwa kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya barabara, lakini hakuna fedha zilizotolewa. Licha ya hili, TARURA ilifanikiwa kusaini mikataba 303 chini ya mradi wa Mfuko wa Jimbo, na kufikia utekelezaji wa kazi za ujenzi wa barabara kwa 64% bila kupokea fedha. Ucheleweshaji wa utoaji wa fedha umesababisha kusimama kwa miradi ya ujenzi wa barabara hizo.

TARURA ilitengewa kiasi cha Sh. bilioni 251.50 kutoka kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara, ambapo Sh. bilioni 229.14 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Sh. bilioni 22.36 kwa ajili ya maendeleo kama ilivyoainishwa katika Makubaliano ya Utendaji ya Mwaka (APA). Hata hivyo, kufikia Juni 2024, ni 40% sawa na Sh. Bilioni 99.84 tu ya kiasi kilichotengwa kilitolewa. Fedha za matengenezo ya barabara zilitolewa kwa kiasi pungufu cha Sh. bilioni 137.40, na fedha za maendeleo zilikuwa pungufu kwa Sh. bilioni 14.26. Hali hii inasababisha ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi, migogoro na wakandarasi, madeni yasiyo ya lazima, na kutofikiwa kwa malengo ya uboreshaji wa miundombinu, hivyo kuathiri vibaya utoaji wa huduma za umma na ukuaji wa uchumi.

Pia nilibaini kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 hazikutenga kiasi cha Sh. bilioni 3.95 kwa ajili ya sekta muhimu kama kilimo, mifugo, na uvuvi, ambapo zilikuwa ni 20%, 15% na 5% mtawalia ya mapato yatokanayo na sekta hizo kwa mujibu wa aya 116 ya Miongozo ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/24. Zaidi ya hayo, Halmashauri 21 zilishindwa kuhamisha kiasi cha Sh. bilioni 15.35 kwenda TARURA kwa ajili ya kazi za barabara.

Kuhusiana na kutenga fedha za mapato ya ndani yasiyolindwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 hazikutenga Sh. bilioni 28.25 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, huku Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 zikishindwa kutenga Sh. bilioni 1.43 kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa ofisi za vijiji na mitaa.

### Usimamizi wa Mapato na Matumizi

Jumla ya Sh. bilioni 3.45 zilizokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 31 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato hazikuwasilishwa benki, jambo linaloashiria uwezekano wa matumizi mabaya au upotevu wa fedha za umma.

Pia niliweza kubaini kwamba, jumla ya Sh. bilioni 44.96 hazikukusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 158 hususani kutoka kwenye ada za pango za maduka na vibanda vya soko, leseni za biashara na vileo, na uuzaji wa viwanja. Kushindwa kukusanya mapato haya kulitokana na juhudi zisizoridhisha za uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika katika ufuatiliaji wa ukusanyaji wa fedha zinazodaiwa.

Kufikia Desemba 2024, jumla ya Sh. bilioni 7.25, ikiwa ni 20% ya Sh. bilioni 36.26 zilizokusanywa kutokana na kodi za majengo, hazikuwasilishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, jambo linaloathiri mipango yao ya kifedha na utoaji wa huduma.

Kwa upande mwingine, niliweza kubaini kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa 41, Sekretarieti za Mikoa miwili na TARURA hazikuweza kuwasilisha kwa ukaguzi, stakabadhi za kielektroniki zenye thamani ya Sh. bilioni 12.84. Pia, malipo ya Sh. milioni 279.11 yaliyofanywa na TARURA kwa wakandarasi na wazabuni yalithibitishwa kwa stakabadhi za kielektroniki zisizo halali. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilithibitisha kwamba stakabadhi za kielektroniki zenye thamani ya Sh. milioni 61.93 hazikuweza kuonekana kwenye mfumo wao wa kodi, wakati stakabadhi za kielektroniki za Sh. milioni 217.18 zilionesha kiasi cha Sh. milioni 18.98 tu kwenye mfumo wa TRA.

Wakati wa mchakato wa ukaguzi, wakandarasi na wazabuni waliwasilisha stakabadhi halali zenye thamani ya Sh. milioni 226.87 ili kubadilisha stakabadhi zisizo halali zilizowasilishwa awali, hivyo kubakiwa na stakabadhi za kielektroniki zisizo halali zenye thamani ya Sh. milioni 52.23. Kutokutoa stakabadhi halali za kielektroniki na matumizi ya stakabadhi zisizo halali kuthibitisha malipo kulifanywa ili kukwepa kodi.

Aidha, tathmini ilionesha kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 48 na Sekretarieti za Mikoa miwili zilichepusha Sh. bilioni 13.99 kugharamia shughuli zisizopangwa, ikimaanisha kwamba shughuli zilizotengewa bajeti hazikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, Halmashauri 42, Sekretarieti za Mikoa mbili, na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) walichepusha jumla ya Sh. bilioni 16.03 kwenda kufadhili shughuli nyingine zisizokusudiwa. Kati ya kiasi hiki, Sh. bilioni 13.99 zilitolewa na Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa, huku Sh. bilioni 2.04 zikitolewa na DART, ambazo awali zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya fidia na mfuko wa usafiri wa umma. Mwelekeo huu wa kuhamisha fedha kinyume na malengo yake unakiuka kanuni za fedha na kuathiri utoaji wa huduma, hali inayosababisha miradi kutotekelezwa au kutokuwa na ufanisi.

### Usimamizi wa Ununuzi

Uhakiki wa shughuli za ununuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24 umebaini kuwa taasisi 12 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 20.08 nje ya mipango yao ya ununuzi iliyoidhinishwa. Ununuzi wa bidhaa na huduma nje ya mipango na bajeti za mwaka unaweza kusababisha matumizi yasiyopangwa, kuvuruga usimamizi wa fedha, na kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Pia, nilibaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 na Sekretarieti za Mikoa tatu zilifanya ununuzi wa thamani ya Sh. bilioni 6.99 bila ushindanishi wa zabuni. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 na Sekretarieti za Mikoa tatu zilifanya ununuzi wa thamani ya Sh. bilioni 4.88 bila kupata idhini kutoka kwa bodi husika za zabuni. Ukosefu wa ushindani unadhoofisha imani ya umma na kuongeza uwezekano wa vitendo vya rushwa au upendeleo, kwani maslahi binafsi yanaweza kuathiri maamuzi. Vilevile, ununuzi bila idhini ya bodi za zabuni unadhoofisha usimamizi, na kuongeza hatari zinazohusiana na uwajibikaji, ubora na thamani ya fedha.

Kwa upande mwingine, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa sita na Sekretarieti ya Mkoa moja zililipa jumla ya Sh. bilioni 1.25 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kabla ya kupokelewa. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa nne na Sekretarieti ya Mkoa moja, na TARURA zilikuwa na madai ya wakandarasi yasiyolipwa yenye thamani ya Sh.

bilioni 40.36, kwa kipindi cha kati ya siku 38 na 521 tangu madai hayo yalipothibitishwa. Malipo kwa wazabuni kabla ya kupokea bidhaa au huduma yanasababisha uwezekano wa upotevu wa fedha endapo wazabuni watashindwa kuwasilisha bidhaa zilizoagizwa, pamoja na changamoto za kurejesha fedha au kubadilisha bidhaa zisizokidhi viwango. Vilevile, ucheleweshaji wa malipo unaweza kusababisha adhabu au gharama za riba, jambo linaloongeza gharama kwa serikali na kudhoofisha imani ya umma katika mfumo wa ununuzi wa umma.

Aidha, tathmini ya usimamizi wa mikataba ilionesha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 na Sekretarieti ya Mkoa moja zilisaini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 5.38 bila kufanyiwa uhakiki wa kisheria. Kutofanyika uhakiki sahihi wa mikataba kunahatarisha maslahi ya umma na kuongeza uwezekano wa migogoro au ukiukwaji wa masharti ya mikataba. Jambo linaloongeza hatari ya usimamizi mbaya wa fedha, ukiukwaji wa taratibu za ununuzi, uwezekano wa matumizi nje ya bajeti, na kudhoofisha mfumo wa utawala kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.

### Usimamizi wa Rasilimali Watu

Ukaguzi wa taarifa za mishahara ulibaini kuwa taasisi 45 zilishindwa kuwasilisha makato ya mishahara yenye jumla ya Sh. bilioni 3.39 kwa taasisi husika, ikiwa ni pamoja na Sh. bilioni 2.63 zilizotakiwa kupelekwa kwenye mifuko ya pensheni. Ucheleweshaji huu umesababisha adhabu ya jumla ya Sh. bilioni 6.53 kwa taasisi 40, jambo linalosababisha matumizi yasiyo ya lazima kwa Serikali. Aidha, kushindwa kuwasilisha makato kwenye mifuko ya pensheni kunaathiri ukwasi wa mifuko hiyo na kuchelewesha mchakato wa malipo ya mafao ya wastaafu.

Pia, katika taasisi 52, nilibaini madai yasiyolipwa ya watumishi yenye jumla ya Sh. bilioni 24.55, huku baadhi ya madai hayo yakiwa hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12, jambo linasababisha kuongezeka kwa madeni na kuwa na hatari ya kuathiri ari ya watumishi, hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa ufanisi.

Vile vile, nilibaini uwepo wa wafanyakazi 724 katika taasisi 22 wanaopokea mishahara halisi baada ya makato chini ya kiwango cha chini kinachotakiwa cha theluthi moja ya mishahara yao ya jumla kutokana na uwepo wa makato makubwa kupita kiasi. Makato ya mshahara yanayozidi kiwango yanaweza kuwashawishi watumishi

kujihusisha na vitendo vya ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za umma kwa manufaa binafsi. Pia inaweza kushusha morali hivyo kuathiri utendaji wao, ustawi na utoaji wa huduma kwa ujumla.

### Tathmini ya Uwekezaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mkoa wa Dar es Salaam ziliwekeza jumla ya Sh. bilioni 26.84 katika benki ya DCB (Dar es Salaam Commercial Bank); hata hivyo thamani ya hisa imeshuka kutoka Sh.1,000 mwaka 2002 hadi Sh. 110 kufikia Juni 2024. Licha ya changamoto hizi za kifedha, Mamlaka husika hazijachukua hatua za kurekebisha hali hiyo au kutekeleza sera madhubuti ya uwekezaji.

Aidha, katika mapitio yangu ya uwekezaji kwenye masoko, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa tatu hazikuandaa mpango mzuri au kufanya tathmini ya maeneo sahihi kwa ajili ya ujenzi wa masoko. Kukosekana kwa maelewano baina ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na jamii kuhusu vibanda vilivyojengwa kumeathiri matumizi sahihi ya maeneo ya soko. Mapungufu katika upangaji na ushirikishwaji hafifu wa wadau umesababisha kutotumika ipasavyo kwa maduka na vibanda, hali inayosababisha upotevu wa mapato na kudhoofisha shughuli za biashara za ndani.

Zaidi ya hayo, tathmini ya hali ya masoko ilibaini mapungufu ya miundombinu na usimamizi, ikiwemo ukosefu wa maji safi, vyoo vinavyofanya kazi, kutokuwepo kwa mfumo thabiti wa kutupa taka, mifumo duni ya mifereji ya maji, na kutokuwepo kwa njia za watembea kwa miguu zilizoboreshwa, ambazo ni muhimu hususani kipindi cha mvua. Changamoto hizi za miundombinu na usimamizi usioridhisha zimeathiri ufanisi wa masoko, kusababisha hali isiyozingatia usafi, na kuleta hatari za kiafya, jambo linaloweza kusababisha upotevu wa fursa za kiuchumi na mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Vilevile, mapitio yangu ya uendeshaji wa vituo vya mabasi yalionesha kutokutumika ipasavyo na changamoto za usimamizi, jambo lililosababisha upotevu wa mapato na utoaji wa huduma usiokuwa na ufanisi. Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nne, vituo vya mabasi havifanyi kazi kikamilifu kutokana na ukosefu wa vibanda vya abiria wakati wa kusubiri huduma ya usafiri, maeneo ya ndani ya vituo kutoboreshwa na huduma ya vyoo isiyoridhisha, hali ambayo imesababisha vituo hivi kutotumika kwa urahisi. Upungufu huu

unachangia Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kuvitumia vituo vya mabasi kwa ufanisi.

Kwa upande mwingine, mradi wa majengo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni wenye thamani ya Sh. bilioni 2.69 umeendelea kutokodishwa tangu kufanyika kwa makabidhiano na mshirika wa biashara mwezi Mei 2019 kutokana na kutosuluhishwa kwa mgogoro unaohusiana na hati ya umiliki wa pamoja wa eneo la mradi. Vilevile, mradi wa Uwekezaji wa Kiwanda cha kuzalisha gesi asilia (Biogas) katika Halmashauri ya Mji Geita uliogharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.88 haujaanza kufanya kazi tangu kukamilika kwake Januari 2020 kutokana na ukosefu wa mashine ya matumizi ya nishati hiyo. Ucheleweshaji huu umesababisha upotevu wa mapato, kushuka kwa thamani ya mali, na uwezekano wa wizi, ukiashiria matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali. Mradi wa Kinondoni unakumbana na mgogoro wa umiliki, wakati mradi wa Geita ukiwa katika hali ya kutofanya kazi kwa muda mrefu, jambo linalosababisha kutopatikana kwa manufaa yaliyokusudiwa. Hali hizi zinaonesha mapungufu katika usimamizi wa miradi, hivyo kuathiri faida za kiuchumi na uthabiti wa kifedha wa halmashauri.

Baada ya kupitia Mradi wa Umwagiliaji wa Malenge katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama wenye thamani ya Sh.bilioni 2.58, ulio kamilika mwezi Machi 2024, ilibainika kuwa eneo hili linakosa mto, na bwawa haliwezi kuhifadhi maji kutokana na ubora hafifu wa udongo, jambo linaloathiri uwezo wake wa kutumika katika shughuli za umwagiliaji. Vilevile, mradi wa umwagiliaji wa Inala katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, uliokamilika mwaka 2017/18 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.66, unatumika kwa 29% tu, licha ya kuchukua eneo la ekari 400. Migogoro ya ardhi imezuia kuongezeka kwa uzalishaji wa kilimo kama ilivyokusudiwa. Mapungufu haya yanaonesha kutofanyika kwa upembuzi wa kina kuhusiana na kufanikiwa kwa miradi hii, na kuibua wasiwasi kuhusiana na uwezekano wa hasara za kifedha bila kupatikana kwa manufaa ya kilimo yaliyotarajiwa.

Halmashauri ya Jiji Dodoma iliwekeza kiasi cha Sh. bilioni 78.34 katika miradi ya maegesho ya malori, vituo vya mabasi, na shughuli nyingine za kuzalisha mapato. Hata hivyo, ukusanyaji wa mapato umeendelea kupungua, ambapo Sh. bilioni 1.84 pekee zilikusanywa kati ya Sh. bilioni 3.82 zilizokadiriwa, hivyo kusababisha upungufu wa 52%.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Sh. milioni 340.17 zilitumika kama fidia ya ardhi kati ya mwaka 2019/20 na 2021/22 kwa ajili ya

maeneo ya uwekezaji, yaliyokusudiwa kwa miradi ya kuzalisha mapato kama masoko na vituo vya usafiri. Licha ya kupata vyeti vya umiliki wa ardhi mwaka 2022, hakuna eneo lolote kati ya haya ambalo limeendelezwa au kutumika kama ilivyopangwa. Kushindwa kuendeleza maeneo ya uwekezaji yaliyolipiwa fidia kumekuwa na matokeo ya kupoteza fursa za kiuchumi, kukwamisha maendeleo ya miji na kupunguza uwezo wa halmashauri kuongeza mapato kutoka vyanzo vyake vya ndani.

Kiasi cha Sh. bilioni 9.77 kilitolewa na halmashauri 176 kwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), lakini uwekezaji huu haujaonesha faida yoyote kwa zaidi ya muongo mmoja. Uchambuzi wa hali ya kifedha ya LGLB unaonesha kuwa Sh. milioni 285.92 pekee zilitolewa kama mikopo, wakati Sh. milioni 686.40 zipo katika uwekezaji wa hisa. Vilevile imebainika kuwa na nakisi ya Sh. bilioni 74.95, ikiashiria changamoto za kifedha kutokana na usimamizi usioridhisha au wingi wa madeni. Kadhalika, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. milioni 817.89 kinachotokana na Akiba ya Lazima (Minimum Compulsory Reserve), zilizokusudiwa kwa uwekezaji na mikopo, zilitumiwa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kiuendeshaji. Kwa matokeo hayo, mpango wa uwekezaji (MCR) haukuchangia katika kudumisha ustawi wa kifedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na pia unaonesha usimamizi mbovu wa LGLB ambapo fedha hizo zimewekezwa.

## Tathmini ya Ufanisi wa Uendeshaji

UDART ilitakiwa kuendesha mabasi 210 chini ya makubaliano ya mtoa huduma wa mpito na DART. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 22 Novemba 2024, mabasi 111 pekee ndiyo yaliyo katika hali ya kufanya kazi. Mabasi 99 yaliyosalia hayapo katika utoaji wa huduma kutokana na baadhi ya mabasi hayo kuhitaji matengenezo. Upungufu huu wa 49% umesababisha msongamano, ucheleweshaji, na huduma za usafiri zisizo za uhakika hivyo kuathiri ufanisi wa utoaji huduma ya usafiri.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mapitio ya miradi ya ujenzi yalionesha kuwa miradi 45 ya sekta ya afya na elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 11, yenye thamani ya Sh. bilioni 5.64, haijaanza kutumika kutokana na upungufu wa watumishi, ukosefu wa samani, na kukosekana kwa miundombinu ya uendeshaji. Aidha , miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 77.33 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 33 haijakamilika au inatekelezwa kwa kasi ndogo licha ya kumalizika kwa muda wa utekelezaji. Ucheleweshaji huu umeathiri

utoaji wa huduma kwa jamii, hatari ya uchakavu wa mali, na inaweza kusababisha ongezeko la gharama za matengenezo.

Pia, nilibaini kuwa miradi 216 yenye thamani ya Sh. bilioni 14.30 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 ilitelekezwa ikiwa katika hatua mbalimbali za kukamilika kwa vipindi vinavyotofautiana kuanzia miaka 3 hadi 25. Kutelekeza miradi ya maendeleo baada ya uwekezaji mkubwa wa kifedha kunasababisha upotevu wa rasilimali na kukwamisha ufikiaji wa malengo yaliyokusudiwa.

Kwa upande mwingine, miradi ya barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 91.81 ilikumbwa na dosari za usanifu, zikiwemo michoro isiyokamilika, tofauti kati ya makadirio ya gharama (BOQ) na michoro, marekebisho yasiyopangwa na ukosefu wa vipengele vya kiufundi. Matatizo kama vile madaraja yenye vipimo vifupi (bridge spans), mifereji ya maji isiyotosheleza, na makalvati yasiyokamilika yalisababisha uharibifu wa mapema, hatari ya mmomonyoko wa udongo na hatari za kiusalama. Hali hii inaonesha upungufu katika udhibiti wa ubora na nyaraka za miradi, jambo ambalo linadhoofisha uimara wa miundombinu na kuongezeka kwa gharama za matengenezo.

### Sekta ya Afya

Baada ya mapitio ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ilibainika madai ya Sh. bilioni 1.34 yaliyowasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 35 yalikataliwa kutokana na makosa kwenye fomu za madai. Kati ya madai ya Sh. bilioni 8.27, Sh. bilioni 6.93 zilirejeshwa, na kiasi kilichokataliwa hakikulipwa. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa 8 zilikumbana na ucheleweshaji wa zaidi ya siku 60 kupokea kiasi cha Sh. milioni 660.17, jambo lililoathiri utoaji wa huduma za afya kutokana na upungufu wa fedha.

Kwa upande mwingine, Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 zilihifadhi dawa zilizokwisha muda wake kwa miezi 3 hadi miaka 10, zikiwa na thamani ya Sh. bilioni 1.73, bila kuziteketeza. Kutokuteketeza dawa hizi kunasababisha hatari ya usalama wa umma ikiwa zitatumika kwa bahati mbaya au kutumika vibaya na watu wasio waaminifu.
Tathmini ya usimamizi wa mfuko wa uchangiaji wa gharama (Cost Sharing Fund) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 ilibaini kuwa Sh. bilioni 17.55 zilikusanywa na vituo vya kutolea huduma za afya. Kanuni zinataka kuwa 50% ya fedha hizi sawa na Sh. bilioni 8.78, zitumike kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Hata hivyo kiasi cha Sh. bilioni 4.75

kilichepushwa na kutumika kwenye malipo ya posho na matumizi ya kiuendeshaji. Uchepushaji wa fedha umesababisha upungufu wa fedha ya ununuzi wa madawa na vifaa tiba na kudhoofisha juhudi za Serikali za kuboresha huduma za afya, na kusababisha kuathirika kwa utoaji wa huduma.

Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilitakiwa kusambaza vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 14.39 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 31. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.70 vilinunuliwa na kusambazwa, huku vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 7.69 vikiwa bado havijasambazwa. Vilevile, Wizara ya Afya iliweka Sh. bilioni 6.40 kwenye akaunti ya MSD kwa ajili ya bidhaa za afya kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nne. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, MSD ilisambaza bidhaa za afya zenye thamani ya Sh. bilioni 4.65 (73%) huku ikishindwa kusambaza bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.75 (27%), hali iliyopelekea upungufu wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya, jambo linaloathiri ubora wa huduma za afya.

Vile vile, nilibaini kuwa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.85 katika vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 havitumiki kutokana na ukosefu wa wataalamu wabobezi, miundombinu isiyotosheleza, majengo yasiyokamilika na ukosefu wa mafunzo na vifaa vya maabara, ikimaanisha kuwa, thamani na faida zinazotarajiwa kutokana na matumizi ya vifaa hivyo hazijapatikana.

Aidha, nilibaini kuwa, Sekretarieti za Mikoa 17 ziliandikisha kaya 159,773 katika mfumo wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) na kufikia 13% tu ya lengo la kaya 1,247,474. Zaidi ya hayo, Sh. bilioni 1.37 zilikusanywa kutoka kwenye kaya katika Sekretarieti za Mikoa sita kupitia mfumo wa CHF-IMIS. Hata hivyo, Serikali Kuu haikutoa fedha sawa na kiasi kilichokusanywa, hali ambayo iliathiri ustawi wa kifedha wa programu na kupunguza uwezo wake wa kutoa huduma za afya zinazokidhi mahitaji.

### Usimamizi wa Mali

Mapitio ya usimamizi wa mali katika taasisi 59 yalibaini kwamba magari 482 yalikuwa yametelekezwa kutokana na ucheleweshaji wa matengenezo na kutoyaondoa/kutoyauza magari yasiyotengenezeka. Kushindwa kutengeneza au kuyaondoa magari hayo kunachangia

uchakavu wa haraka, kupunguza muda wao wa matumizi na kuzuia kupata manufaa yaliyotarajiwa.

Pia, nilibaini kuwa taasisi 16 zinamiliki majengo au zilianzisha miradi mipya yenye thamani ya Sh. bilioni 13.09 bila kupata vyeti vya umiliki wa ardhi. Ukosefu wa hati miliki unasababisha mali hizi kuwa hatarini kwa ufikiwaji holela, uvamizi na hasara inayoweza kutokea endapo kutatokea migogoro ya umiliki.

Nilibaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 29 zilikuwa na migogoro ya ardhi 44 ambayo bado haijatolewa uamuzi yenye madai ya jumla ya Sh. bilioni 74.04. Pia, kulikuwa na mgogoro uliokuwa haujatatuliwa kuhusiana na umiliki wa ardhi ya kiwanja namba 322 Ruvu Road Oysterbay kati ya Halmashauri ya Manispaa Kinondoni na Oysterbay Villas Ltd, huku kukiwa na uwekezaji wenye thamani ya Sh. bilioni 2.69. Endapo uamuzi utakuwa kinyume na maslahi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa unaweza kusababisha madhara hasi ya kifedha.

01



# SURA YA KWANZA

## Maelezo ya Awali

## 1.0 Utangulizi

Ripoti hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi na mapendekezo kutoka kwa ukaguzi wa Fungu Na. 56 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024.

Ukaguzi huo ulihusisha taasisi 220, ikiwamo Fungu Na. 56 – Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) – pamoja na taasisi zilizozo chini yake ambazo ni Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa - Hombolo (LGTI), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), Fungu Na. 2 – Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), na Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT); Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 (MSM) na kampuni mbili tanzu ambazo ni Arusha Meat Company Ltd (AMCL) na Shirika la Maendeleo la Jiji la Dar es Salaam (DDC).

## 1.1 Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) ilianzishwa tena na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia (Tangazo la Kugawa Majukumu ya Wizara) Tangazo la Serikali Na. 385 la tarehe 7 Mei 2021. OR - TAMISEMI ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera zinazohusiana na Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi, Utawala wa Mikoa, Utawala wa Serikali za Mitaa, pamoja na Maendeleo ya Vijijini na Mijini.

Wizara hii pia inawajibika kusimamia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuratibu utoaji wa huduma vijijini na mijini kama vile usafiri, afya, maji, na usafi wa mazingira, pamoja na kusimamia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Majukumu mengine ni kusaidia wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara, kutambua na kukuza vipaji, kusimamia elimu ya msingi na sekondari, kuboresha utendaji kazi na maendeleo ya rasilimali watu, pamoja na kusimamia idara, mashirika, wakala, miradi, na programu mbalimbali za wizara.

Idara, mashirika, na wakala za wizara zinajumuisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA), iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Utendaji, Sura ya 245, ikiwa na jukumu la matengenezo, maendeleo, na usimamizi wa mtandao wa barabara za vijijini na mijini katika Tanzania Bara. Nyingine ni Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) iliyoanzishwa chini ya sheria hiyohiyo na ina jukumu la kuanzisha na kuendesha Mtandao wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) jijini Dar es Salaam. Pia, kuna Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB)

iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 56 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, inayotoa mikopo kwa mamlaka za serikali za mitaa.

Taasisi nyingine ni Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa – Hombolo (LGTI) kilichoanzishwa kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kitaalamu yanayozingatia mahitaji, utafiti, na huduma za ushauri katika nyanja za fedha, utawala, na usimamizi wa serikali za mitaa. Vilevile, kuna Jumuiya ya Tawala za mitaa Tanzania (ALAT) iliyoanzishwa mwaka 1984 kama jumuiya ya wanachama inayolenga kulinda haki na maslahi ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kuziwakilisha katika ngazi za kitaifa na kimataifa.

## 1.2 Sekretarieti za Mikoa

Sekretarieti za Mikoa zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Mikoa, Sura ya 97. Jukumu lao msingi ni kuzisaidia MSM katika kuimarisha ustawi wa jamii na maendeleo ya taifa kupitia usimamizi, uratibu, msaada wa kitaalamu, na ujenzi wa uwezo kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa malengo ya maendeleo pamoja na utekelezaji wa sera za kitaifa na kisekta katika ngazi ya mitaa huku ikidumisha amani na utulivu.

Kama wasimamizi wa majukumu ya serikali za mitaa ndani ya mkoa, sekretarieti za mikoa zina jukumu muhimu katika kudumisha sheria na utulivu pamoja na kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya mkoa husika. Mkuu wa shughuli za kila siku za sekretarieti ya mkoa ni Katibu Tawala wa Mkoa (RAS).

## 1.3 Mamlaka za Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) zilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Jumla ya mamlaka za wilaya ni 137, huku mamlaka za miji zikijumuisha halmashauri za majiji 6, halmashauri za manispaa 20, na halmashauri za miji 21. MSM zipo chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Utawala wa MSM umekabidhiwa kwa Baraza la Madiwani, linalojumuisha madiwani wakuteuliwa au wakuchaguliwa.

Shughuli za kila siku za MSM zinasimamiwa na mkurugenzi wa Halmashauri wa Wilaya, Mji, manispaa, au Jiji husika.

## 1.4 Mamlaka ya Ukaguzi

Ibara ya 143(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi kuhusu hesabu za Serikali angalau mara moja kwa mwaka.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kuwasilisha taarifa hizo kwa Rais, ambaye baadaye huzipeleka katika Bunge, kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 143(4) ya Katiba ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418.

## 1.5 Malengo ya Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa lengo kuu la kutoa tathmini huru na mahususi ya taarifa za kifedha ili kubaini iwapo taarifa hizo ziliandaliwa kulingana na mfumo wa kuripoti taarifa za kifedha unaokubalika, na kuhakikisha kuwa vipengele vyote muhimu vya kifedha vilizingatiwa ipasavyo.

Mbali na kutathmini ufanisi wa kuzingatia viwango vya kuripoti kifedha, pia ukaguzi ulitathmini iwapo sheria za ununuzi wa umma zilizingatiwa na kuhakikisha michakato ya ununuzi ilifanywa kwa njia ya haki, wazi, na inayokubalika kisheria.

Zaidi ya hayo, nilikagua uzingatizi wa Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na miongozo mingine ya bajeti ili kubaini iwapo usimamizi wa kifedha unaendana na bajeti zilizoidhinishwa, sheria, na sera zilizowekwa.

Matokeo ya ukaguzi yanatoa mwanga juu ya hatari za kifedha zinazoweza kutokea, matukio ya kutozingatia sheria, na maeneo ya kuboresha katika utawala na usimamizi wa kifedha.

## 1.6 Mawanda ya Ukaguzi

Ripoti hii inatoa matokeo muhimu na mapendekezo kulingana na mapitio yaliyofanywa kwa taasisi 220 katika mwaka wa fedha 2023/24.

Katika mapitio haya, nilikagua ufanisi katika utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa mapato na matumizi, ununuzi na usimamizi wa mikataba, pamoja na usimamizi wa mali za Serikali. Ukaguzi wangu ulijumuisha maeneo mengine kama vile ufanisi wa mifumo ya uhasibu, mfumo wa udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na utawala, ukaguzi wa taarifa za kifedha, ripoti za utendaji na taratibu nyingine muhimu kwa ajili ya kupata hitimisho za uhakika ili niweze kutoa ushauri kwa watunga sera na wadau wengine kuweza kufanya maamuzi sahihi.

Pia, nilikagua utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma na maagizo yaliyotolewa na Kamati za Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ili kutathmini hatua zilizochukuliwa na uongozi wa taasisi zilizokaguliwa kwa lengo la kukuza uwajibikaji na kuboresha utendaji wa sekta ya umma.

Mapitio yalifanyika kwa kuzingatia vihatarishi na ukubwa wake ili kuhakikisha kuwa mawanda ya ukaguzi yalikuwa ya kutosha kutengeneza msingi wa kuaminika wa matokeo ya ukaguzi.

Ni muhimu kutambua kuwa matokeo na mapendekezo yanategemea taarifa, na nyaraka zilizotolewa wakati wa ukaguzi.

## 1.7 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha kupitia taarifa za uhasibu na kutumia taratibu za ukaguzi ili kufanikisha malengo ya ukaguzi, ikiwamo kutathmini vihatarishi za upotoshaji wa taarifa za kifedha, kukusanya ushahidi wa ukaguzi, na kutathmini utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma.

Mchakato wa ukaguzi ulifuata mbinu shirikishi, ukihusisha wadau wakuu katika mzunguko wa ukaguzi kama vile Maafisa Masuuli, Menejimenti ya taasisi, na Kamati za Ukaguzi ili kutoa majibu na maoni kuhusu masuala yaliyoibuliwa

02



# SURA YA PILI

## Hati za Ukaguzi

## 2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi hutolewa kulingana na hitimisho linalotokana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, katika kutathmini kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (IPSAS) katika masuala yote muhimu. Tathmini hufanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

## 2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi zinazoweza kutolewa kulingana na upatikanaji wa ushahidi wa kutosha na unaofaa wa kuthibitisha taarifa zinazoonyeshwa moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja katika taarifa ya fedha. Hati hizo ni kama ifuatavyo:

**Hati Inayoridhisha** hutolewa pale ninapopata ushahidi wa kutosha na unaofaa, na kuridhika kuwa taarifa za fedha zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika vya kimataifa vinavyohusu uandaaji wa taarifa za fedha.

**Hati Yenye Shaka** hutolewa pale ninaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa kutoa maoni ya ukaguzi, lakini nikahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika lakini haziathiri taarifa za fedha kwa ujumla wake. Pia hati isiyoridhisha inaweza kutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa kuwapo kwa dosari katika eneo moja au mambo mengine. Hii inaweza kutokea pale unapopatikana ushahidi wa kutosha na unaofaa kuniwezesha kuhitimisha kwamba kasoro hizo mojamoja au kwa pamoja zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika ingawa hazikuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha kwa ujumla wake.

**Hati Mbaya** hutolewa wakati ninapopata ushahidi wa kutosha na unaofaa na kuridhika kuwa kuna makosa kwenye taarifa za kifedha na kuwa, makosa hayo ama kwa kuyaangalia mojamoja au kwa ujumla wake ni makubwa na yenye athari kwa taarifa zote za kifedha; hivyo, kuhitimisha kuwa taarifa hizo hazikuzingatia viwango vinavyokubalika vya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha.

**Kushindwa Kutoa Maoni** hutokea pale ninaposhindwa kupata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi ili kutoa maoni kuhusu taarifa za fedha. Katika hali hii, ninahitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na

yenye athari kwa maeneo yote ya taarifa hiyo. Katika hali nadra sana zinazohusisha kutokuwa na uhakika wa kutosha, ninaweza kushindwa kutoa maoni, hata kama ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kutokuwa na uhakika kwenye eneo mojamoja umepatikana. Hii ni kwa sababu mwingiliano wa kutokuwa na uhakika unaweza kuwa na athari jumuifu kwenye taarifa za fedha, hivyo kufanya kuwa vigumu kutoa maoni.

## 2.2 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa

Katika mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya hati 220 zilitolewa kwa taasisi zilizo chini ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hati zote zilizotolewa ni hati zinazoridhisha. Hakukuwa na hati zenye shaka, hati mbaya na kushindwa kutoa maoni.

Uchambuzi wa maoni ya ukaguzi yaliyotolewa kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2023/24 umeoneshwa katika **Jedwali Na.1 na Kiambatisho 1.**

**Jedwali Na.1: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

| Mwaka wa fedha | Taasisi | Hati za Ukaguzi | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Inayoridhisha | Yenye shaka | Mbaya | Kushindwa kutoa maoni | |
| 2023/24 | Halmashauri | 184 | 0 | 0 | 0 | 184 |
| | Kampuni Tanzu | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | 26 |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | | **220** | **0** | **0** | **0** | **220** |
| | | | | | | |
| 2022/23 | Halmashauri | 181 | 3 | 0 | 0 | 184 |
| | Kampuni Tanzu | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | 26 |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | | **217** | **3** | **0** | **0** | **220** |
| | | | | | | |
| 2021/22 | Halmashauri | 170 | 13 | 1 | 0 | 184 |
| | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | 26 |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | | **204** | **13** | **1** | **0** | **218** |
| | | | | | | |

| Mwaka wa fedha | Taasisi | Hati za Ukaguzi | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Inayoridhisha | Yenye shaka | Mbaya | Kushindwa kutoa maoni | |
| 2020/21 | Halmashauri | 176 | 8 | 1 | 0 | 185 |
| | Sekretarieti za mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | 26 |
| | OR-TAMISEMI | 7 | 1 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | | 209 | 9 | 1 | 0 | 219 |
| | | | | | | |

*Chanzo:* Ripoti za ukaguzi

## 2.3 Hitimisho Kuhusu Usimamizi wa Ununuzi na Bajeti

Zaidi ya hayo, nilitoa hitimisho kuhusu utekelezaji wa ununuzi wa bidhaa, kazi na huduma kwa taasisi 220, ambapo 20 zilizingatia kikamilifu na 200 zilizingatia na baadhi ya mapungufu yanayohitaji maboresho, kama ilivyoelezwa kwa kina katika **Jedwali 2 na Kiambatisho Na.1**

**Jedwali Na.2: Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya manunuzi na kanuni zake**

| Mwaka wa fedha | Taasisi | Hitimisho Kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Kanuni Zake | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya upungufu | |
| 2023/24 | Halmashauri | 9 | 175 | 184 |
| | Kampuni Tanzu | 2 | 0 | 2 |
| | Sekretarieti za mikoa | 7 | 19 | 26 |
| | OR- TAMISEMI | 2 | 6 | 8 |
| **Jumla** | | **20** | **200** | **220** |

*Chanzo:* Ripoti za ukaguzi 2023/24

Vivyo hivyo, nilifanya tathmini ya uundaji na utekelezaji wa bajeti kwa taasisi 220 na kubaini kuwa taasisi 42 zilizingatia sheria za bajeti, na taasisi 178 zilizingatia kwa mapungufu yanayohitaji maboresho, kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali 3** na **Kiambatisho Na.1**

**Jedwali Na.3: Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti**

| Mwaka wa fedha | Taasisi | Hitimisho Kuhusu Uzingatia wa Sheria na Kanuni za Bajeti | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Imezingatia | Imezingatia na baadhi ya upungufu | |
| 2023/24 | Halmashauri | 20 | 164 | 184 |
| | Kampuni Tanzu | 1 | 1 | 2 |
| | Sekretarieti za mikoa | 17 | 9 | 26 |
| | OR- TAMISEMI | 4 | 4 | 8 |
| **Jumla** | | **42** | **178** | **220** |

***Chanzo:*** Ripoti za ukaguzi 2023/24

03



# SURA YA TATU

## Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Miaka Iliyopita

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Pia, inatoa tathimini kama hatua zilizochukuliwa zimeweza kushughulikia kwa ufanisi upungufu uliyojitokeza katika kaguzi zilizopita.

Kifungu Na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, [Sura ya 418] kinanipa mamlaka ya kujumuisha hali ya utekelezaji wa mpango kazi ambao huandaliwa na maafisa masuuli na kuunganishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika ripoti ya mwaka ya ukaguzi.

Ifuatayo ni hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita, pamoja na maagizo ya LAAC na PAC:

## 3.1 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita katika OR-TAMISEMI pamoja na taasisi zake, sekretarieti za mikoa 26 na mamlaka za serikali za mitaa 184 pamoja na kampuni tanzu 2, imeoneshwa katika **Jedwali Na.4 na** **Kiambatisho Na.2** cha ripoti hii.

**Jedwali Na.4: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita**

| Taasisi | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Hayajatekelezwa | Yaliyojirudia | Yaliyopitwa na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| OR-TAMISEMII | 19 | 18 | 3 | 2 | 1 | 43 |
| Taasisi za OR-TAMISEMI | 59 | 126 | 39 | 25 | 3 | 252 |
| sekretarieti za Mikoa | 228 | 213 | 37 | 65 | 36 | 579 |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | 3,151 | 2,833 | 412 | 753 | 291 | 7,440 |
| Kampuni Tanzu | 14 | 25 | 7 | 3 | 3 | 52 |
| **Jumla** | **3,471** | **3,215** | **498** | **848** | **334** | **8,366** |
| % | **42** | **38** | **6** | **10** | **4** | **100** |

***Chanzo:*** Taarifa za ukaguzi za taasisi husika

Kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ni ya kuridhisha. Kwa kiasi kikubwa, hii inatokana na juhudi za Serikali zilizoongezeka katika kushughulikia udhaifu uliobainika. Hata hivyo,

bado kuna mapendekezo ambayo hayajatekelezwa na yanahitaji juhudi zaidi kutoka kwa Serikali ili kuyashughulikia.

Kushindwa kufanyia kazi mapendekezo kwa wakati kunaweza kusababisha udhaifu kama huo kujirudia katika miaka inayofuata na kuathiri ufanisi na tija katika uendeshaji wa OR – TAMISEMI pamoja na taasisi zake, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninasisitiza kuwa Serikali ihakikishe taasisi husika zinafanya juhudi zaidi kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ili kuimarisha uwajibikaji na kuzuia kujirudia kwa udhaifu uliobainishwa.**

## 3.2 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Bunge za LAAC na PAC

Kifungu Na. 38 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma [Sura ya 418] kilichorekebishwa na kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2021(sheria Na.3 2021) kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali na maafisa masuuli, baada ya majadiliano na Kamati za Bunge, kuandaa mpango wa utekelezaji wa hatua za marekebisho zinazokusudiwa na kuwasilisha kwa waziri mwenye dhamana, ambaye atawasilisha ripoti hiyo bungeni.

Tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC na PAC kwa mwaka wa fedha 2023/24 inaonesha kuwa maagizo mengi hayajatekelezwa kwa muda mrefu bila hatua zozote kuchukuliwa na menejimenti husika za mamlaka za serikali za mitaa, sekretarieti za mikoa, OR–TAMISEMI pamoja na taasisi zake.

Kati ya maagizo 1,285 yaliyotolewa, maagizo 323 (25%) yalitekelezwa, maagizo 709 (55%) yapo katika utekelezaji, maagizo 226 (18%) hayajatekelezwa, maagizo 11 (0.8%) yamejirudia na maagizo 16 (1.2%) yamepitwa na wakati kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 5 na Kiambatisho Na.3** cha ripoti hii.

**Jedwali Na.5: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati za Bunge za LAAC na PAC**

| Taasisi | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Hayajatekelezwa | Yaliyojirudia | Yaliyopitwa na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| OR-TAMISEMI | 4 | 1 | 0 | 0 | 2 | 7 |
| Taasisi za OR-TAMISEMI | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 8 |

| Taasisi | Yaliyotekelezwa | Yanayoendelea kutekelezwa | Hayajatekelezwa | Yaliyojirudia | Yaliyopitwa na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sekretarieti za Mikoa | 35 | 18 | 1 | 0 | 4 | 58 |
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | 281 | 686 | 224 | 11 | 10 | 1,212 |
| **Jumla** | **323** | **709** | **226** | **11** | **16** | **1,285** |
| **%** | **25** | **55** | **18** | **0.8** | **1.2** | **100** |

***Chanzo:*** Taarifa za ukaguzi za taasisi husika

Kushindwa kutekeleza kwa wakati maagizo ya kamati za bunge za LAAC na PAC kunaashiria kuwa upungufu uliobainika haujashughulikiwa ipasavyo, hivyo kuziweka taasisi husika katika hatari ya kifedha, kutokuwa na ufanisi na kushindwa kufikia malengo yaliyotarajiwa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe mamlaka husika zinachukua hatua stahiki kutekeleza maagizo yote ambayo hayajatekelezwa.**

04




# SURA YA NNE

## Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inachambua mwenendo wa bajeti ya OR-TAMISEMI na taasisi zinazohusiana, sekretarieti za mikoa, na mamlaka za serikali za mtaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Uchambuzi unahusisha ukusanyaji wa mapato, upokeaji wa fedha kutoka Hazina na mwenendo wa fedha. Pia, inatathmini utekelezaji wa bajeti za serikali za mitaa dhidi ya vipaumbele vikuu ikiwamo mgao wa ruzuku na ukusanyaji wa mapato ya ndani ikionesha makadirio ya bajeti dhidi ya makusanyo halisi ili kutathmini ufanisi wa upande wa fedha na uzingatizi wa sheria.

Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 iliandaliwa na kutekelezwa kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa, ambao ni mpango wa mwisho katika kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025. Lengo ni kuongeza ufanisi na tija katika uzalishaji viwandani kwa kutumia rasilimali nyingi za nchi katika kufanikisha uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Nimetathmini iwapo utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 ulizingatia Sera ya Bajeti ya Serikali, Taarifa ya Mfumo wa Fedha wa Serikali, Sheria ya Matumizi, na mifumo mingine muhimu ya mipango ya kitaifa pamoja na miongozo ya bajeti iliyotolewa.

Nawasilisha matokeo ya ukaguzi uliofanyika kuhusu bajeti ya 2023/24 kama ifuatavyo:

## 4.1 Mapitio ya Bajeti

### 4.1.1 Tathimini ya Mwenendo wa Ruzuku za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida

Katika mwaka wa fedha 2023/24, bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, Tume ya Utumishi ya Walimu na Mamlaka za serikali za Mitaa, ilifikia jumla ya Sh. trilioni 8.83 kwa matumizi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Kati ya kiasi hicho, Sh. trilioni 8.41 zilitolewa, sawa na 95% ya makadirio yaliyoidhinishwa, ikiwa ni upungufu wa Sh. bilioni 419.03. Utoaji huo wa fedha uliongezeka kwa Sh. bilioni 803.67 ikilinganishwa na Sh. trilioni 7.61 zilizotolewa mwaka wa fedha 2022/23.

Tathmini ya mwenendo wa bajeti kwa miaka mitano iliyopita unaoneshwa katika **Jedwali Na. 6 na** Kiambatisho Na.4**.**

**Jedwali Na.6: Tathimini ya mwenendo wa bajeti kwa miaka mitano**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.) | Fedha Halisi Zilizotolewa (Sh.) | Tofauti (Sh.) | Asilimia ya utendaji |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 8,829,191,309,932 | 8,410,165,492,410 | (419,025,817,522) | 95 |
| 2022/23 | 8,819,148,246,175 | 7,606,495,440,875 | (1,212,652,805,299) | 86 |
| 2021/22 | 8,819,148,246,175 | 7,521,709,076,085 | (727,561,059,894) | 85 |
| 2020/21 | 6,946,188,944,481 | 5,792,751,665,853 | (1,153,437,278,628) | 83 |
| 2019/20 | 6,805,675,947,122 | 5,458,401,067,527 | (1,347,274,879,595) | 80 |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za taasisi, 2023/24*

### (i) Mapitio ya Fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida

Bajeti ya ruzuku za matumizi ya kawaida kwa OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa 26, na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 katika mwaka wa fedha 2023/24 ilikuwa Sh. trilioni 6.01. Serikali ilitoa Sh. trilioni 5.79 ambayo ni sawa na 96% ya bajeti iliyoidhinishwa, ikionesha upungufu wa Sh. bilioni 219.09 (tazama **Kiambatisho Na.5**).

Nilibaini kuwa ruzuku za matumizi ya kawaida zilizotolewa ziliongezeka kwa Sh. bilioni 588.47, kutoka Sh. trilioni 5.20 mwaka wa fedha 2022/23 hadi Sh. trilioni 5.79 mwaka wa fedha 2023/24, ikionesha ongezeko la 11%. Mwenendo wa ruzuku ya matumizi ya kawaida kwa miaka mitano umeoneshwa katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na 7: Fedha za ruzuku za matumizi ya kawaida**

| Mwaka wa fedha | Makisio ya bejeti (Sh.) (A) | Kiasi kilichotolewa (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C =(B-A) | Asilimia (%) =B/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 6,013,449,302,041 | 5,794,362,070,001 | (219,087,232,040) | 96 |
| 2022/23 | 5,550,172,280,648 | 5,205,891,865,384 | (344,280,415,263) | 94 |
| 2021/22 | 4,912,836,455,163 | 4,807,125,959,060 | (105,710,496,103) | 98 |
| 2020/21 | 5,349,085,836,370 | 4,760,974,162,598 | (588,111,673,772) | 89 |
| 2019/20 | 5,289,377,847,806 | 4,551,253,607,566 | (738,124,240,240) | 86 |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha na utoaji wa ruzuku 2023/24*

Kutokutoa ruzuku kama ilivyoidhinishwa kunasababisha kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa.

### (ii) Mapitio ya Fedha za Ruzuku za Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2023/24, bajeti ya ruzuku za maendeleo kwa OR-TAMISEMI , Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilikuwa Sh. trilioni 2.81. Kiasi kilichotolewa ni Sh. trilioni 2.62 pekee, hivyo kusababisha nakisi ya Sh. bilioni 199.94, sawa na asilimia 7 ya upungufu (tazama **Jedwali Na.8** na **Kiambatisho Na.6**).

Jedwali Na.8: Mapitio ya Fedha za Ruzuku za Maendeleo

| Mwaka wa Fedha | Makisio ya bajeti (Sh.) (A) | Kiasi kilichotolewa (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%)=B/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 2,815,742,007,891 | 2,615,803,422,409 | (199,938,585,482) | 93 |
| 2022/23 | 3,268,975,965,527 | 2,400,603,575,491 | (868,372,390,036) | 73 |
| 2021/22 | 3,336,433,680,816 | 2,714,583,117,025 | (621,850,563,791) | 81 |
| 2020/21 | 1,597,103,108,111 | 1,031,777,503,255 | (565,325,604,856) | 65 |
| 2019/20 | 1,516,298,099,316 | 907,147,459,961 | (609,150,639,355) | 60 |

***Chanzo:*** *Taarifa za mgao wa fedha na hesabu*

Utoaji wa ruzuku pungufu unaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Licha ya upungufu huu, jumla ya Sh. bilioni 215.19 zimetolewa zaidi katika mwaka wa fedha 2023/24, ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka wa fedha 2022/23.

**Narudia mapendekezo yangu ya awali kwamba Serikali itoe ruzuku sawa na bajeti iliyopitishwa ili kutekeleza shughuli zilizopangwa. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuziba mapengo endapo ruzuku inatolewa pungufu pia kuwezesha mipango ya maendeleo.**

### 4.1.2 Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mamlaka za serikali za mitaa

Kifungu cha 6, 7, 8 na 9 vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, vinabainisha vyanzo vya mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambavyo ni: ushuru wa mazao ya kilimo, ada, faini na adhabu, ada za leseni, vibali vya ujenzi, pamoja na vyanzo vingine vya mapato.

Nilibaini kuwa mamlaka hizo zilikusanya jumla ya Sh. trilioni 1.23 zaidi ya makadirio ya bajeti ya Sh. trilioni 1.14. Hii inaonesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa Sh. bilioni 87.75 (sawa na ongezeko la 8%). Uboreshaji huu unatokana na uwezo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuboresha fursa za mapato zilizopo **(Rejea Kiambatisho Na.7)**

Kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiasi cha Sh. bilioni 319.49, kutoka Sh. bilioni 912.12 katika mwaka wa fedha 2022/23 hadi Sh. trilioni 1.23 mwaka wa fedha 2023/24.

Jedwali Na.9: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa miaka mitano

| Mwaka wa fedha | Makisio (Sh.) (A) | Makusanyo halisi (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C=(B-A) | Asilimia (%) =C/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 1,143,871,207,000 | 1,231,616,905,758 | 87,745,698,758 | 8 |
| 2022/23 | 911,863,338,484 | 912,123,865,087 | 260,526,603 | 0.03 |
| 2021/22 | 873,898,493,691 | 891,836,133,308 | 17,937,639,617 | 2 |
| 2020/21 | 822,375,950,562 | 769,422,329,061 | (52,953,621,501) | (6) |

| Mwaka wa fedha | Makisio (Sh.) (A) | Makusanyo halisi (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C=(B-A) | Asilimia (%) =C/A *100 |
|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 759,907,423,938 | 709,573,567,541 | (50,333,856,397) | (7) |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za taasisi husika*

Ukusanyaji wa mapato unaonesha kwa mwaka wa fedha 2023/24 halmashauri 110 zilizidi malengo yao kwa kiasi cha Sh. bilioni 155.39, huku halmashauri 72 zikiwa hazikufikia malengo yao kwa Sh. bilioni 74.82. Rejea **Jedwali Na 10** na **Na 11. Pia Kiambatisho Na.8 na Kiambatisho Na.9.**

**Jedwali Na.10: Halmashauri zenye makusanyo zaidi ikilinganishwa na bajeti**

| Mwaka wa fedha | Makisio ya bajeti (Sh.) (A) | Makusanyo halisi (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%) =B/A *100 | Idadi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 669,180,373,162 | 824,570,001,432 | 155,389,628,270 | 123 | 110 |
| 2022/23 | 327,986,323,174 | 444,127,705,034 | 116,141,381,860 | 135 | 79 |
| 2021/22 | 413,871,167,926 | 479,401,407,535 | 65,530,239,610 | 116 | 102 |

**Jedwali Na.11: Halmashauri ambazo hazikufikia malengo ya makusanyo**

| Mwaka wa fedha | Makisio ya bajeti (Sh.) (A) | Makusanyo halisi (Sh.) (B) | Tofauti (Sh.) C=(B-A) | Ufanisi (%) =B/ A *100 | Idadi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 474,386,375,377 | 399,561,564,925 | (74,824,810,452) | 84 | 72 |
| 2022/23 | 575,028,005,691 | 459,147,150,434 | (115,880,855,257) | 80 | 103 |
| 2021/22 | 460,027,325,765 | 412,434,725,772 | (47,592,599,993) | 90 | 82 |

***Chanzo:*** Taarifa za fedha za mwaka 2023/24

Makusanyo yanayozidi malengo yanaashiria juhudi za Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato, zikichochewa na mbinu bora na ufanisi katika kukusanya mapato. Hata hivyo, yanaweza pia kuashiria kuwa makadirio ya bajeti hayakuwa halisi. Kinyume chake, mamlaka hizo ambazo hazikufanikisha malengo yao ya makusanyo zinaweza kuonesha ukosefu wa uchunguzi wa kina wa vyanzo vya mapato vilivyopo au juhudi na mikakati isiyotosheleza kufanikisha matokeo yanayotarajiwa ya mapato.

**Ninatoa wito kwa Serikali kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaandaa mikakati sahihi ya ukusanyaji wa mapato kwa kubaini vyanzo vinavyoaminika na kuanzisha vyanzo vipya ndani ya maeneo yao ya mamlaka. Pia, mamlaka hizo zinapaswa kuandaa**

**bajeti zinazoendana na uhalisia ili kuongeza makusanyo ya mapato na kuhakikisha uendelevu wa kifedha.**

## 4.2 Mchakato wa Malipo Ambayo Haukukamilika Sh. Bilioni 118.21

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Halmashauri za Mamlaka za Serikali za Mitaa 156 na Sekretarieti za Mikoa (RS) 20 zilifanya michakato ya malipo yenye jumla ya Sh. bilioni 118.21 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na kawaida. Hata hivyo, malipo haya hayakukamilika, hali iliyosababisha ucheleweshaji wa utoaji wa fedha.

Mnamo tarehe 18 Novemba 2024, Wizara ya Fedha iliielekeza OR-TAMISEMI kutumia bajeti ya mwaka 2024/25 kugharamia shughuli zilizoathirika kutokana na malipo ambayo hayakukamilika. Maelezo ya malipo haya yasiyokamilika yanaoneshwa katika **Kiambatisho Na.10.**

Kushindwa kukamilisha mchakato wa malipo pamoja na ukosefu wa mawasiliano kuhusu hali ya malipo hayo kumesababisha kuchelewesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Taasisi husika kulazimika kutumia bajeti mpya ya mwaka 2024/25, hali inayoweza kusababisha uchepushaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli nyingine.

**Ninapendekeza kwamba Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, ihakikishe kuwa michakato ya malipo inakamilika kwa wakati ili kuepuka usumbufu katika utoaji wa huduma. Aidha, inapaswa kuanzishwa mfumo wa uwazi wa mawasiliano ili kutoa taarifa kwa wakati kuhusu hali ya malipo, marejesho, na kukataliwa kwa malipo, hivyo kuhakikisha usimamizi bora wa fedha na kuzuia ucheleweshaji wa aina hii katika siku zijazo.**

## 4.3 Fedha Zilizorejeshwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kutokana na Ucheleweshaji wa Utoaji na Matumizi Sh. Bilioni 30.73

Kulingana na Aya ya 4(B) ya Waraka Na. 4 (2023/24) na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Bajeti [Sura ya 439], fedha ambazo hazijatumika zinapaswa kurejeshwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Shughuli zozote ambazo hazijatekelezwa zinapaswa kupangwa upya kwenye bajeti ya mwaka unaofuata.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 29 na Sekretarieti za Mikoa mbili zilirejesha jumla ya Sh. bilioni 10.75 mfuko mkuu kutokana na ukosefu wa muda wa kutosha wa kutumia fedha hizo, kwani zilipokelewa kati ya mwezi Mei na Juni 2024. Aidha, mamlaka za Serikali za Mitaa 27 zilirejesha jumla ya Sh. bilioni 19.98 baada ya kupokea fedha hizo kati ya Septemba 2023 na Januari 2024. Kati ya Sh. bilioni 19.98, Halmashauri ya H/W Mbeya, H/Mji Tunduma, na H/W

Buchosa zilirejesha jumla ya Sh. bilioni 4.92 kutokana na ucheleweshaji wa maamuzi. Fedha hizo zilirejeshwa kwa mujibu wa waraka na kifungu kilichorejelewa. **Rejea** Kiambatisho Na.11 na 12

Kurejeshwa kwa fedha kulisababishwa na Hazina kuchelewa kutoa fedha na ucheleweshaji wa maamuzi kutoka kwenye taasisi husika. Kasoro hizi zimesababisha kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa, hivyo manufaa yaliyokusudiwa hayakufikiwa.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha kuziruhusu Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kuhamishia katika akaunti ya amana fedha zote zilizopokelewa mwishoni mwa mwaka ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Pia Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa zinashauriwa kuboresha michakato ya ufanyaji maamuzi ili kuepuka ucheleweshaji wa matumizi ya fedha zilizopokelewa.**

## 4.4 Kutotolewa kwa Fedha za Miradi Wakati Mikataba Tayari Imesainiwa

Aya ya 3.2 ya Mkataba wa Utendaji wa Kila Mwaka (Annual Performance Agreement - APA) kati ya OR-TAMISEMI na TARURA inaeleza kuwa wajibu wa Wizara ni kuipatia TARURA fedha kulingana na mpango wa mtiririko wa fedha wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/24.

### (i) Fedha za Barabara za Mfuko wa Majimbo Sh. bilioni 127.50

Kiasi cha fedha za mfuko wa majimbo kilichoidhinishwa kwenye makubaliano hayo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara kwenye majimbo kwa mwaka wa fedha 2023/24 kilikuwa Sh. bilioni 127.50.

Tathmini ilibaini kuwa TARURA haikupokea fedha hizo, licha ya kusaini mikataba 303, huku utekelezaji wa miradi hiyo ukiwa umefikia 64% ya kazi. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 49(4) cha Sheria ya Bajeti ambacho kinakataza taasisi kuingia mikataba bila uhakika wa fedha.

### (ii) Fedha za Mfuko wa Bodi ya Barabara Sh. Bilioni 151.67

TARURA ilipokea Sh. bilioni 99.84 (sawa na 40%) ya Sh. bilioni 251.50 zilizotarajiwa kutolewa na Bodi ya Mfuko wa Barabara, huku fedha za matengenezo na maendeleo zikiwa zimetolewa pungufu kwa Sh. bilioni 137.41 na Sh. bilioni 14.26, mtawalia kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.12**

**Jedwali Na.12: Fedha ambazo hazikupelekwa**

| Na | Maelezo | Kiasi kwenye mkataba (Sh.) | Kiasi kilichopokelewa (Sh.) | Kiasi ambacho hakijapokelewa (Sh.) | asili mia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa matengenezo | 229,141,137,184 | 91,735,755,657 | 137,405,381,526 | 40% |
| 2. | Mfuko wa maendeleo | 22,360,126,354 | 8,099,260,050 | 14,260,866,303 | 36% |
| | **Jumla** | **251,501,263,538** | **99,835,015,707** | **151,666,247,829** | **40%** |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha*

Hali ya Hazina kutotoa fedha pamoja na kuwapo kwa kifungu cha APA kinachoruhusu Mkurugenzi Mtendaji wa TARURA kuanzisha mchakato wa ununuzi kabla ya kupokea fedha vimesababisha kusimama kwa miradi ya barabara. Matokeo yake, 99% ya mikataba iliyosainiwa haina ufadhili wa kifedha, licha ya 64% ya kazi kufanyika. Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshaji wa miradi, migogoro na wakandarasi, madeni, na kutotimizwa kwa malengo ya miundombinu, jambo ambalo linaweza kuathiri utoaji wa huduma za umma na ukuaji wa uchumi.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha ipeleke fedha za barabara kama zilivokusudiwa.**

## 4.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa Kutotenga Fedha za Miradi ya Maendeleo na Uendeshaji wa Vijiji/Mitaa Sh. bilioni 48.99

Aya ya 116 ya Miongozo ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 kuhusu makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa, ilitoa maelekezo yafuatayo kwa kwa maafisa masuuli:

i. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye mapato yasiyolindwa yanayozidi Sh. bilioni 5 zinapaswa kutenga angalau 60% kwa maendeleo, ikijumuisha 10% kwa mikopo ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, na 10% kwa miundombinu ya barabara inayoendeshwa na TARURA.

ii. Mamlaka zilizo na mapato kati ya Sh. bilioni 2 na Sh. bilioni 5 zinapaswa kutenga angalau 40% kwa maendeleo, ikiwamo 10% kwa mikopo ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

iii. Mamlaka zilizo na mapato chini ya Sh. bilioni 2 zinapaswa kutenga angalau 20% kwa maendeleo, ikijumuisha 10% kwa mikopo ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

iv. Kiasi cha angalau Sh. 200,000 kwa kila robo mwaka kinapaswa kutengwa kwa shughuli za vijiji/mitaa. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa zinazokusanya chini ya Sh. bilioni 1.5 zimetakiwa kutenga angalau Sh. 100,000 kwa kila kijiji/mtaa kwa kila robo mwaka; na kuendelea kutenga Sh.100,000 kila mwezi kwa ajili ya posho za majukumu kwa maafisa watendaji wa kata.

v. Kuhakikisha kuwa mapato kutoka kilimo (20%), mifugo (15%), na uvuvi (5%) yanatengwa na kutumika katika sekta husika ili kuboresha na kuendeleza mazao ya kimkakati.

Kinyume na hayo, katika mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini: Mamlaka za Serikali za Mitaa 65 zilishindwa kutenga sh. bilioni 28.26 kwa ajili ya shughuli za maendeleo; Mamlaka 23 hazikutenga sh. bilioni 1.43 kwa ajili ya shughuli za mitaa na vijiji; Mamlaka 17 zilishindwa kutenga Sh. bilioni 3.95 kwa kilimo; na Mamlaka 21 zilishindwa kutenga Sh. bilioni 15.35 kwa TARURA inayohusika na usimamizi wa miundombinu ya barabara. Rejea **Kiambatisho Na.13** na **Jedwali Na.13** hapa chini.

**Jedwali Na.13: Shughuli ambazo hazikupelekewa fedha**

| Na | Shughuli | Idadi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kutokupelekwa kwenye shughuli za maendeleo | 65 | 28,255,235,529 |
| 2. | Kutopelekwa kwa fedha kwenye ofisi za mitaa na vijiji | 23 | 1,428,252,500 |
| 3. | Kutokupelekwa kwenye shughuli za kilimo | 17 | 3,950,333,615 |
| 4. | Kutopekwa kwa fedha TARURA | 21 | 15,354,626,707 |
| **5.** | **Jumla** | | 48,988,448,351 |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha na uchambuzi wa kikaguzi*

Kushindwa kutenga fedha kama inavyotakiwa na miongozo ya bajeti kulitokana hasa na kuchepusha mapato yaliyokusanywa kwenda kwenye matumizi mengine ya kawaida ambayo hayakukusudiwa. Pia, yalisababishwa na ukosefu wa usimamizi madhubuti ya utekelezaji kutoka OR-TAMISEMI. Matokeo yake, huduma muhimu katika sekta hizi ziliathirika, ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa barabara kutokana na ukosefu wa matengenezo na ucheleweshaji wa maendeleo ya kilimo. Hali hii inaweza kusababisha gharama kubwa zaidi za matengenezo siku za usoni, kupungua kwa ufanisi wa usafirishaji, kuleta athari mbaya kwa uchumi wa maeneo husika, na kuathiri usalama wa umma.

**Ninapendekeza kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zifuate maelekezo ya Serikali kwa kutenga sehemu inayotakiwa ya mapato yao ya ndani kwa miradi ya maendeleo na shughuli za vijiji/mitaa.**

**Aidha, OR-TAMISEMI inashauriwa kuimarisha usimamizi na mifumo ya utekelezaji ili kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazingatia mgawanyo wa lazima wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.**

## 4.6 Dosari Zilizobainika Katika Matumizi ya Fedha za Bakaa

### 4.6.1 Matumizi ya Fedha za bakaa Bila Idhini - Sh. Bilioni 11.79

Tathmini ya taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ilibaini kuwapo kwa fedha za bakaa kiasi cha Sh. bilioni 11.44 katika Halmashauri 5. Kufikia robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25, kiasi cha Sh bilioni 5.81 kilikuwa kimetumika, na kuacha bakaa ya Sh. bilioni 5.62. Wilaya husika zilikuwa katika mchakato wa kupata vibali vya matumizi ya fedha za bakaa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, kama inavyotakiwa na Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Bajeti (Jumla), 2015, lakini mchakato huo haukukamilika hadi Januari 2025.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi ilitumia Sh. milioni 350 za mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali bila idhini kutoka Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipago na Baraza la Madiwani la Halmashauri. Hii ni kinyume na Agizo la 18 (1)-(2) la Mwongozo wa Fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 linalosisitiza kuwa iwapo halmashauri inataka kutumia fedha ambazo hazikubainishwa katika bajeti ya awali au iwapo mgao wa bajeti ya mwaka haukutosha, inapaswa kuwasilisha bajeti ya nyongeza kwa Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango ambayo baadaye inapaswa kuwasilishwa katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani kwa ajili ya kuidhinishwa.

**Jedwali Na.14: Matumizi ya Fedha za Bakaa bila Idhini kutoka kwa**

| Jina la Halmashauri | Salio la Fedha za bakaa (Sh.) | Kiasi Kilichotumika Kufikia Oktoba 2024 (Sh.) | Salio la Fedha Kufikia Robo ya Kwanza ya 2024/25 (Sh.) |
|---|---|---|---|
| H/M Iringa | 1,161,670,236 | 622,026,007 | 539,644,230 |
| H/W Iringa | 5,142,134,528 | 1,441,585,032 | 3,700,549,497 |
| H/W Kilolo | 1,651,904,987 | 935,286,350 | 716,618,637 |
| H/W Mufindi | 2,621,530,012 | 1,955,183,861 | 666,346,151 |
| H/Mji Mafinga | 859,530,104 | 859,530,104 | 0 |
| **Jumla** | **11,436,769,868** | **5,813,611,353** | **5,623,158,515** |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za mwaka 2023/24*

Kutokuzingatia miongozo ya bajeti kulitokana na shinikizo la kukamilisha miradi, jambo ambalo linaweza kusababisha upungufu katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka ujao na utekelezaji wa miradi isiyokusudiwa.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa Sekretarieti za Mikoa zinasimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa kanuni za bajeti kwa kuhakikisha kuwa halmashauri zinapata idhini kabla ya kutumia fedha za bakaa. Wizara ya Fedha inapaswa kuongeza usimamizi na mawasiliano na Halmashauri ili kuzielekeza matumizi sahihi ya fedha.**

### 4.6.2 Kuchelewa Kutumia Fedha za Bakaa - Sh. bilioni 35.92

Nilibaini ongezeko la idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazoshindwa kutumia fedha za bakaa ndani ya muda uliopangwa. Katika mwaka wa fedha 2023/24, Mamlaka 19 hazikutumia Sh. bilioni 35.92 ikilinganishwa na Sh. bilioni 19.97 katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, ikiwa ni ongezeko la 57%.

Hii ni kinyume na Kanuni ya 21 (1) na (2) ya Kanuni za Bajeti, 2015 inayotaka fedha zote za matumizi ambazo hazijatekeleza miradi mwishoni mwa mwaka wa fedha zitumike ndani ya robo ya kwanza ya mwaka unaofuata. **Jedwali Na.15** linaonesha mchanganuo.

**Jedwali Na.15: Fedha za bakaa ambazo hazikutumika**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kibiti | 1,807,384,398 | 11. | H/Mji Tarime | 499,047,479 |
| 2. | H/W Mafia | 2,912,922,782 | 12. | H/W Morogoro | 1,352,727,531 |
| 3. | H/W Rufiji | 260,917,669 | 13. | H/M Morogoro | 1,095,908,424 |
| 4. | H/W Ilala | 15,757,968,470 | 14. | H/Mji Makambako | 1,194,586,665 |
| 5. | H/W Bahi | 150,473,117 | 15. | H/W Njombe | 189,041,014 |
| 6. | H/W Chamwino | 69,494,800 | 16. | H/W Handeni | 454,492,062 |
| 7. | H/W Bukombe | 233,215,582 | 17. | H/W Kilindi | 926,510,187 |
| 8. | H/W Mbogwe | 1,015,228,291 | 18. | H/W Muheza | 366,051,284 |
| 9. | H/W Mtama | 6,847,000,000 | 19. | Sekretrieti ya Mkoa Manyara | 333,794,735 |
| 10. | H/W Tarime | 448,781,422 | | **Jumla** | **35,915,545,912** |

***Chanzo:*** *Taarifa za bejeti*

Ucheleweshaji wa matumizi ya fedha za bakaa ulisababishwa hasa na ucheleweshaji wa urejeshaji wa fedha na taratibu za malipo zilizocheleweshwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Kushindwa kutumia fedha ndani ya muda uliopangwa kunakwamisha utekelezaji wa shughuli za kawaida na za maendeleo.

**Serikali inapaswa kuimarisha uratibu kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Hazina ili kuharakisha utoaji wa fedha.**

## 4.7 Mpango na Bajeti Hafifu kwa Ajili ya Kulipa Madeni - Sh bilioni 70.20

Nilifanya tathmini ya bajeti ya mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya kulipa madeni yaliyosalia kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini kuwa halmashauri 43 na sekretarieti za mikoa 2 hazikutenga bajeti au zilitenga kiasi pungufu kulipa madeni ya wazabuni na madai ya watumishi yenye jumla ya Sh. bilioni 70.20. Hii ni kinyume na Aya ya 1.7 (94) ii-iv cha Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 uliotolewa na Wizara ya Fedha, ambacho kinawataka maafisa masuuli kutenga bajeti kwa ajili ya madai ya watumishi, watoa bidhaa na huduma, na kuepuka malimbikizo ya madeni ili kupunguza gharama zinazotokana na riba na faini **(Rejea Kiambatisho Na.14)**

Malimbikizo ya madeni yanaongeza mzigo kwa mamlaka za serikali za mitaa kutokana na gharama za riba na faini. Watoa huduma na bidhaa kukabiliwa na matatizo ya kifedha, jambo linaloweza kuchelewesha au kusitisha utoaji wa huduma. Pia, malipo yaliyocheleweshwa kwa watumishi yanaweza kushusha morali ya kazi, kupunguza ufanisi wa utendaji na kusababisha migogoro sehemu ya kazi. Pia, malimbikizo ya madeni kwa muda mrefu yanaathiri uaminifu wa mamlaka za serikali za mitaa kwa wadau wake.

**Ninasisitiza mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba menejimenti ya mamlaka ya serikali za mtaa, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha (MoF), ifanye tathmini ya kina ya madeni yaliyosalia na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuyalipa.**

## 4.8 Kuendelea Kuchepusha Fedha kwa Shughuli Zisizokusudiwa - Sh. bilioni 16.03

Kifungu cha 27(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kinaelekeza kwamba mara baada ya bajeti za Serikali na taasisi za umma kupitishwa, zinapaswa kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Aidha, Agizo la 18(4) la Mwongozo wa Fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009, linaelekeza kuwa hakuna ruhusa ya kuhamisha fedha kati

ya bajeti ya maendeleo na matumizi ya kawaida bila idhini ya Baraza la Madiwani. Hata hivyo, michango ya matumizi ya kawaida kutoka kwenye mapato ya ndani ya halmashauri inaweza kuhamishiwa kwenye bajeti ya maendeleo.

tathmini yangu kwa mwaka wa fedha 2023/24 imebaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 42 na sekretarieti za mikoa 2, zilihamisha jumla ya Sh. bilioni 13.99 kugharamia shughuli nyingine za maendeleo na matumizi ya kawaida. Fedha hizo zilitumika kinyume na bajeti, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Kuchepusha fedha kunaashiria kuwa shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa **(Rejea Kiambatisho Na.15)**

Zaidi ya hayo, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) ulitumia Sh. bilioni 2.04 ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya fidia na mfuko wa usafiri wa abiria kwa shughuli nyingine zisizokusudiwa. Hii ni kinyume na Kanuni ya 5.2.1 (d) ya DART ya mwaka 2014 ambayo inamtaka mtendaji mkuu wa wakala kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na masharti yote yanayohusiana na fedha hizo yanazingatiwa. Hadi tarehe 30 Juni 2024, ilibaki kiasi cha Sh. milioni 1.8 tu, wakati madai ya fidia yalikuwa ni Sh. bilioni 1.94.

Jumla ya Sh. bilioni 16.03 zilichepushwa na DART, sekretarieti za mikoa na mamlaka za serikali za mitaa katika mwaka wa fedha 2023/24, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 3.20 ikilinganishwa na Sh. bilioni 12.83 zilizochepushwa mwaka wa fedha 2022/23. Hali hii inaonesha kuwa kuna mwendelezo wa uchepushaji wa fedha, ambapo fedha zinatumika kinyume na bajeti iliyopangwa.

Uchepushwaji wa fedha unaweza kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii, kwa miradi iliyokusudiwa kutotekelezwa. Aidha, kuchepusha fedha kwa miradi mingine ya maendeleo kunaweza kusababisha utekelezaji wa miradi isiyo na manufaa kwa jamii.

**Ili kuzuia uchepushaji fedha na kuhakikisha utoaji wa huduma bora, Wizara ya Fedha na mamlaka husika zinapaswa kuimarisha ufuatiliaji wa bajeti, kusimamia utekelezaji madhubuti wa kanuni za fedha, na kuongeza uwazi katika matumizi ya fedha. Vilevile, mabadiliko yote ya bajeti yanapaswa kupitishwa kwa taratibu sahihi za kibajeti, kwa kuzingatia utoaji wa fedha kwenye miradi inayotekelezeka na inayokidhi mahitaji ya jamii.**

05



# SURA YA TANO

## Usimamizi wa Mapato na Matumizi

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inabainisha matokeo ya ukaguzi wa mapato na matumizi katika OR-TAMISEMI, sekretarieti za mikoa na pamoja na taasisi zilizo chini yake, mamlaka za serikali za mitaa, pamoja na usimamizi wa akaunti za amana.

## 5.1 Usimamizi wa Mapato

Usimamizi madhubuti wa mapato huwezesha mamlaka ya serikali za mitaa kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii, na ukuaji endelevu wa mamlaka hizo. Mamlaka ya serikali za mitaa zina vyanzo mbalimbali vya mapato, kama vile ushuru, leseni, ada, tozo za adhabu, na mapato kutoka kwenye vyazo vingine.

Takwimu za miaka mitatu iliyopita zinaonesha kuwa mamlaka ya serikali za mitaa zilikusanya mapato zaidi kutoka katika vyanzo vyake kwa mwaka wa fedha 2023/24, ambayo ni Sh. trilioni 1.23. Hii inaonesha kuwa kuna ongezeko la bilioni 319.49 ikilinganishwa na mwaka uliyopita, kama ilivyoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na.1** na kufananuliwa kwenye **Kiambatisho Na.16**.

**Kielelezo Na. 1:Mwenendo wa makusanyo ya mapato**




***Chanzo:*** *Taarifa kutoka kwenye mfumo wa MUSE*

Nilipitia menejimenti ya mapato katika halmashauri, nikihusisha mchakato wa ukusanyaji wa mapato na uzingatiaji wa sheria, kanuni na maelekezo ya Serikali na kubaini mapungufu yafuatayo:

### 5.1.1 Udhaifu Ulioonekana Katika Ukusanyaji wa Ushuru wa Huduma Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

#### (i) Mapato Yatokanayo na Ushuru wa Huduma Ambayo Hayajakusanywa Sh. bilioni 8.10

Kifungu 6(1)(u) na 7 (1) (y) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kinaitaka halmashauri kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwa taasisi au mtu anayefanya biashara ambaye mauzo yake ya kila mwaka yanazidi shilingi milioni 4 kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya ushuru kwa mauzo baada ya kutoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.

Katika mapitio ya ukusanyaji wa ushuru wa huduma kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 28 hazikukusanya ushuru wa huduma kiasi cha Sh. bilioni 8.10 kutoka taasisi 1164 zinazofanya kazi ndani ya mamlaka hizo kutokana na kutokuwapo kwa jitihada za kutosha za kuhakisha taasisi hizo zinalipa ushuru wa huduma. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.16** hapa chini.

**Jedwali Na.16: Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma**

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya taasisi | Kiasi kisichokusanywa (Sh. ) | Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya taasisi | Kiasi kisichokusanywa (Sh. ) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Tarime | 1 | 738,636,772 | 15 | H/ Jiji Arusha | 314 | 179,210,037 |
| 2 | H/M Morogoro | 1 | 2,791,362,704 | 16 | H/Mji Babati | 18 | 42,277,997 |
| 3 | H/W Serengeti | 83 | 2,439,904,216 | 17 | H/M Bukoba | 5 | 7,765,362 |
| 4 | H/W Geita | 19 | 19,872,341 | 18 | H/W Kishapu | 1 | 38,277,079 |
| 5 | H/M Tabora | 2 | 37,560,455 | 19 | H/W Mafia | 22 | 29,011,493 |
| 6 | H/Mji Geita | 1 | 91,000,296 | 20 | H/W Rorya | 6 | 10,698,923 |
| 7 | H/M Kahama | 166 | 270,298,201 | 21 | H/W Biharamulo | 13 | 22,659,889 |
| 8 | H/ Mji Mafinga | 5 | 8,900,193 | 22 | H/Mji Mbinga | 51 | 62,492,605 |
| 9 | H/W Msalala | 6 | 31,305,419 | 23 | H/W Namtumbo | 13 | 23,055,263 |
| 10 | H/Jiji Dodoma | 146 | 355,285,404 | 24 | H/M Songea | 14 | 95,272,934 |
| 11 | H/M Kinondoni | 50 | 242,169,397 | 25 | H/Jiji Mwanza | 146 | 146,279,304 |

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya taasisi | Kiasi kisichokusanywa (Sh. ) | Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya taasisi | Kiasi kisichokusanywa (Sh. ) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12 | H/W Ngorongoro | 12 | 247,827,564 | 26 | H/M Ubungo | 34 | 133,738,448 |
| 13 | H/W Meru | 23 | 21,959,486 | | | | |
| 14 | H/W Chato | 12 | 11,556,114 | | **Jumla** | **1164** | **8,098,377,896** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukusanyaji, ankara na rejista kwa mwaka 2023/24*

### (ii) Kutokukusanywa kwa Ushuru wa Huduma Kutoka kwa Taasisi 29,432

Kifungu cha 6(1)(n) na 7(1) (aa) cha Sheria ya Fedha ya mamlaka za serikali za mitaa, Na. Sura ya 290 kinaeleza kuwa ushuru wa huduma unatozwa kwa taasisi zote zinazofanya shughuli zao ndani ya mamlaka ya serikali za mitaa. Ushuru wa huduma ni fedha zinazotokana na tozo ya huduma inayolipwa na mashirika ya kibiashara kwa kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mapato ya mauzo baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.

Nilifanya tathmini ya ukusanyaji wa ushuru wa huduma kwenye mamlaka ya serikali za mitaa na ilibainika kuwa mamlaka 7 za serikali za mitaa hazikutoa ankara za malipo kwa ajili ya kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwenye taasisi 29,432 zinayofanya kazi ndani ya mamlaka zake.

Hata hivyo, sikuweza kubainisha kiasi cha ushuru wa huduma ambao ulitakiwa kukusanywa kutoka kwenye taasisi hizo. Hii ilitokana na kutowasilishwa kwa mauzo ghafi na fomu za ithibati ya mauzo ya taasisi husika wakati wa ukaguzi. Idadi ya taasisi ambazo hazijalipa ushuru wa huduma kwa mamlaka ya serikali za mitaa imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.17.**

**Jedwali Na.17: Orodha ya Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma**

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Taasisi |
|---|---|---|
| 1 | H/M Kinondoni | 27,663 |
| 2 | H/M Kigamboni | 389 |
| 3 | H/W Kigoma | 49 |
| 4 | H/W Kishapu | 3 |
| 5 | H/ Mji Kondoa | 1300 |
| 6 | H/W Magu | 12 |
| 7 | H/W Mufindi | 16 |
| | **Jumla** | **29,432** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya taasisi zisizolipa ushuru wa huduma na rejista*

Kutokusanywa kwa ushuru wa huduma kutoka kwa taasisi zinazoendesha shughuli ndani ya mamlaka za serikali za mitaa kunasababisha upotevu wa mapato ya ndani, jambo ambalo linaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

### (iii) Ushuru wa Huduma Uliokusanywa Bila Kuwapo kwa Msingi wa Ukokotoaji Sh. bilioni10.37

Aya ya 6.6.1(iii na iv) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 inabainisha mkakati na taratibu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma, ambazo ni pamoja na utoaji wa fomu ya kuthibitisha mauzo ghafi inayojazwa na walipa ushuru wa huduma. Fomu hii hutumika kama msingi wa kutoza ushuru wa huduma kwa usahihi na kwa ufanisi.

Wakati wa tathmini ya makusanyo ya mapato yaliyokusanywa kupitia mifumo ya ukusanyaji mapato ya LGRCIS na TAUSI, nilibaini kuwa mamlaka 24 za serikali za mitaa zilikusanya kiasi cha Sh. billioni 10.37 kutokana na ushuru wa huduma kutoka kwa taasisi zinazofanya kazi ndani ya mamlaka hizo bila ya msingi wa ukokotoaji wa ushuru huo ambapo ni asilimia 0.3 ya mauzo ghafi. Taarifa hizo za mauzo ghafi zinapatikana kutoka Mamlaka ya mapato Tanzania au mamlaka zingine ili kujiridhisha usahihi wa kiasi kilichokusanywa.

Hali hii ilichangiwa na kukosekana kwa utaratibu mzuri wa kupata taarifa za mauzo kwa njia ya kielekitroni kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) na mamlaka zingine kama vile Ofisi za Tume ya Madini na kutotunza kanzidata ya walipaji wa ushuru wa huduma, hivyo kusababisha ukusanyaji wa ushuru wa huduma bila kuwapo kwa msingi wa ukokotoaji wa ushuru huo. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimekusanya ushuru wa huduma bila ya msingi wa ukokotoaji imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.18** hapa chini.

**Jedwali Na.18: Mamlaka za serikali za mitaa ambazo zimekusanya ushuru wa huduma bila msingi wa ukokotoaji**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh. ) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh. ) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Rufiji | 78,951,936 | 14. | H/W Simanjiro | 338,725,616 |
| 2. | H/M Kahama | 171,792,714 | 15. | H/W Nsimbo | 76,236,350 |
| 3. | H/W Kilosa | 595,428,703 | 16. | H/M Shinyanga | 72,187,410 |
| 4. | H/M Lindi | 134,803,073 | 17. | H/W Ukerewe | 219,163,224 |
| 5. | H/W Msalala | 54,705,233 | 18. | H/W Uvinza | 15,810,312 |
| 6. | H/W Ulanga | 189,583,141 | 19. | H/W Uyui | 245,704,947 |
| 7. | H/Jiji | 3,621,732,640 | 20. | H/M Iringa | 27,614,551 |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh. ) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh. ) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dodoma | | | | |
| 8. | H/W Kyela | 157,592,929 | 21 | H/W Mbarali | 432,034,934 |
| 9. | H/W Mpimbwe | 10,757,779 | 22 | H/W Rungwe | 261,081,173 |
| 10. | H/W Muheza | 259,031,780 | 23 | H/M Ubungo | 868,810,107 |
| 11. | H/W Bunda | 202,719,254 | 24 | H/W Kilindi | 221,045,570 |
| 12. | H/W Kigamboni | 2,074,442,960 | | **Jumla** | **10,374,351,948** |
| 13. | H/W Kishapu | 44,395,612 | | | |

***Chanzo:*** Taarifa ya makusanyo ya mwaka 2023/24

Hata hivyo, kukusanya ushuru wa huduma bila msingi wa ukokotoaji (mauzo ghafi) kumefanya iwe vigumu kuthibitisha usahihi wa kiasi kilichokusanywa. Hii ni kwa sababu kilichokusanywa kinaweza kuwa pungufu ya kiasi halisi kilichotakiwa kukusanywa.

Pia, kushindwa kutunza kanzidata ya walipaji wa ushuru wa huduma kumefanya iwe vigumu kukusanya ushuru huo kikamilifu kwa mamlaka ya serikali za mitaa kwa mwaka husika.

**Ninapendekeza OR - TAMSIEMI, kupitia Malaka za Serikali za Mitaa husika, iweke na ihuishe kanzidata ya wafanya biashara ili kuboresha ukusanyaji wa ushuru wa huduma. Ili kuimarisha uzingatiaji wa taratibu na ukusanyaji wa mapato, Serikali ifikirie uwezekano wa kuhamisha jukumu la ukusanyaji wa ushuru wa huduma kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa niaba ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwakuwa TRA inaweza kuthibitisha taarifa za mauzo halisi, kwa kupitia za taarifa za kifedha za makampuni na kuhakikisha ukokotoaji sahihi wa kodi ya 0.3%.**

### 5.1.2 Kutokusanywa kwa Mapato Kutoka Vyanzo Mbalimbali kiasi cha Sh. bilioni 44.96

Agizo la 38(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa la mwaka 2009 linaeleza kuwa litakuwa jukumu la mweka hazina wa halmashauri kuweka taratibu za kifedha na kihasibu zitakazowezesha kuhakikisha kuwa fedha zote ambazo halmashauri inadai zinakusanywa na kupelekwa benki kwa wakati.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 44.96 hakikukusanywa na mamlaka 158 za serikali za mitaa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, vikiwamo kodi ya pango ya maduka na vibanda, leseni za biashara, meza za sokoni, uuzaji wa viwanja, na leseni za vileo kama ilivyoorodheshwa kwenye rejista za madai.

Kutokukusanywa kwa mapato kutoka vyanzo mbalimbali kulitokana na udhaifu wa mfumo wa udhibiti wa ndani na mbinu zinazotumiwa na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa katika kukusanya mapato kutoka vyanzo vilivyopo na vipya. Hii ni pamoja na kutokuwapo kwa taratibu madhubuti za kukusanya madai yaliyokaa muda mrefu, mawasiliano dhaifu na mikakati ya kuwafikia wafanyabiashara na umma kwa ujumla kuhusu wajibu wao wa kulipa mapato, na kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha.

Muhtasari wa mapato yasiyokusanywa kutoka kwa kila chanzo umeonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 19.**

**Jedwali Na.19: Kutokusanywa kwa Mapato kutoka kwa vyanzo mbalimbali**

| Na. | Chanzo cha mapato | Idadi ya mamlaka ya serikali ya Mitaa | Kiasi ambacho hakijakusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Uuzaji wa viwanja | 38 | 30,635,881,559 |
| 2 | Pango la vibanda na maduka | 45 | 6,113,434,753 |
| 3 | Ushuru wa vibanda vya soko na soko | 13 | 2,070,292,493 |
| 4 | Leseni za biashara | 28 | 1,978,101,189 |
| 5 | Ada za Maegesho | 7 | 1,185,643,600 |
| 6 | Ushuru wa hoteli | 6 | 968,881,090 |
| 7 | Ada ya uchimbaji wa madini | 2 | 941,855,323 |
| 8 | Ada ya mabango | 3 | 476,771,831 |
| 9 | Ada za Shule | 4 | 313,168,000 |
| 10 | Mrahaba wa misitu | 4 | 222,693,899 |
| 11 | Ushuru wa Nyenzo za ujenzi | 3 | 20,486,000 |
| 12 | Leseni za pombe kali | 3 | 19,940,000 |
| 13 | Ada ya kibali cha ujenzi wa ghala | 2 | 10,200,000 |
| | **Jumla** | **158** | **44,957,349,737** |

***Chanzo:*** Taarifa ya makusanyo na bajeti, 2023/24

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa, iweke mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vilivyopo na vipya. Pia, ihakikishe mapato yote yanakusanywa bila kuchelewa na iweke taratibu madhubuti za ukusanyaji wa madai ya muda mrefu. Aidha, iwe na mawasiliano na wamiliki wa biashara kuhusu wajibu wao na kuhakikisha rasilimali za kutosha kwa ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi.**

### 5.1.3 Mapato Yalikusanywa na Kutowasilishwa Benki Kiasi cha Sh. bilioni 3.45

Kifungu cha 42(2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kinaelekeza kuwa, mapato yote ya mamlaka za serikali za mtaa yatalipwa kwenye akaunti ya benki au akaunti nyingine yoyote inayomilikiwa na mamlaka hizo isipokuwa kama itakavyoelezwa vinginevyo katika memoranda ya fedha. Aidha, Agizo la 50(5) la LGFM, 2009 linataka fedha zote zinazopokelewa na mamlaka za serikali za mitaa zipelekwe kwenye akaunti za benki za mamlaka ya serikali za mitaa kila siku au siku inayofuata ya kazi. Kuzingatia agizo hili husaidia kupunguza vishawishi vya kutumia fedha za mamlaka za serikali za mitaa kwa shughuli zisizotarajiwa.

Wakati wa mapitio ya mifumo ya LGRCIS na TAUSI nilibaini kwamba kiasi cha Sh. bilioni 3.45 zilikusanywa katika mamlaka 31 za serikali za mitaa lakini hazikuwasishwa benki. Muhtasari wa mapato yaliyokusanywa bila kupelekwa benki yameonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 20** na kufafanuliwa kwenye **Kiambatisho Na.17.**

**Jedwali Na.20: Muhtasari wa mapato yaliyokusanywa pasipo kupelekwa benki**

| Na | Mfumo uliotumika kukusanya mapato | Idadi ya taasisi (Taasisi moja inaweza tokea kwenye mfumo zaidi ya mmoja) | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | LGRCIS | 23 | 2,921,158,937 |
| 2 | TAUSI | 20 | 442,197,792 |
| 3 | GoTHoMIS | 3 | 87,008,120 |
| **Jumla** | | **46** | **3,450,364,849** |

***Chanzo :*** *Taarifa za makusanyo kutoka kwenye mifumo na taarifa za kibenki 2023/24*

Hali hii imetokana na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani, kutofanyika kwa usuluhishi wa mara kwa mara pamoja na kutokuwapo kwa ufuatiliaji wa karibu wa wakusanyaji ili kuhakikisha makusanyo yote yanawasilishwa benki. Kutoweka benki mapato yaliyokusanywa kunaashiria usimamizi mbovu wa fedha, hivyo kuathiri uwezo wa kifedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani na taratibu nyingine, ikijumuisha kuwepo makubaliano ya kipengele cha adhabu kwa wakusanya mapato kwa kuchelewa kuwasilisha benki fedha za makusanyo. Pia kufanya usuluhishi wa mara kwa mara na ufuatiliaji wa karibu kwa wakusanya mapato.**

### 5.1.4 Ukosefu wa Ufanisi Katika Kukokotoa Bei ya Mazao na Ukusanyaji wa Ushuru wa Mazao ya Sh. bilioni 4.75

Kifungu cha 7(1)(g) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kinataka fedha zote zinazotokana na ushuru unaolipwa kwa chanzo cha mazao yoyote ya kilimo au mazao mengine yanayozalishwa katika eneo la halmashauri ya wilaya, chini ya sheria hii au sheria nyingine yoyote iliyoandikwa, isipokuwa mazao makuu ya mauzo ya nje, iwe kati ya sifuri hadi asilimia tano ya bei ya mazao; na itakatwa kutoka kwenye chanzo.

Mapitio ya makusanyo ya mapato kwa mwaka husika yalionesha kuwa kiasi cha Sh. bilioni 4.75 kitokanacho na ushuru wa mazao hakikukusanywa katika mamlaka 19 za serikali za mitaa. Mapato hayo hayakukusanywa kutokana na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kutokuwa na ufuatiliaji wa kutosha kwa taasisi na vyama vya ushirika (AMCOS) vilivyonunua mazao katika mamlaka hizo. Pia, kiasi hicho cha fedha hakikukusanywa kwa kuwa ukokotoaji wa bei ya mazao haukuwa sahihi; hivyo kusababisha bei za mazao kuwa chini ya bei elekezi. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa mazao kwa ufanisi ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.21**.

**Jedwali Na.21: Mamlaka ya serikali za mitaa ambazo hazikukusanya ushuru wa mazao**

| Na. | Aina ya ushuru wa mazao | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh. ) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mazao mchanganyiko | H/W Songea | 1,430,054,876 |
| 2. | Ushuru wa kahawa | H/W Mbinga | 723,672,080 |
| 3. | Ushuru wa tumbaku | H/W Urambo | 693,002,006 |
| 4. | Ushuru wa Alizeti | H/W Mkalama | 624,708,420 |
| 5. | Ushuru wa ufuta | H/W Tunduru | 335,735,728 |
| 6. | Ushuru wa Tumbaku | H/W Ushetu | 262,200,336 |
| 7. | Ushuru wa Tumbaku | H/W Kaliua | 134,060,386 |
| 8. | Ushuru wa mazao mchanganyiko | H/W Nyasa | 123,077,580 |
| 9. | Ushuru wa chai | H/W Busokelo | 76,507,588 |
| 12. | Ushuru wa mazao mchanganyiko | H/M Songea | 71,617,842 |
| 13. | Ushuru wa chai | H/W Chunya | 69,892,630 |
| 14. | Ushuru wa Ufuta | H/W Mtwara | 60,249,232 |
| 15. | Ushuru wa Kahawa | H/ Mji Mbinga | 39,714,168 |
| 16. | Ushuru wa pareto | H/W Mbeya | 24,115,748 |
| 17. | Ushuru wa Tumbaku | H/W Serengeti | 23,786,962 |

| Na. | Aina ya ushuru wa mazao | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh. ) |
|---|---|---|---|
| 18. | Ushuru wa mazao mchanganyiko | H/W Kibiti | 19,978,380 |
| 19. | Ushuru wa kahawa | H/W Kigoma | 17,081,333 |
| 20. | Ushuru wa tumbaku | H/W Nzega | 8,730,093 |
| 21. | Ushuru wa korosho | H/W Newala | 7,381,316 |
| | **Jumla** | | **4,745,566,704** |

***Chanzo:*** *Rejista za ushuru wa mazao*

Kushindwa kukusanya mapato yatokanayo na ushuru wa mazao kumesababisha upotevu wa mapato yaliyotarajiwa. Pia, hali hii inaweza kusababisha shughuli za utendaji katika mamlaka za serikali za mitaa kutofanyika, na miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa kwa

mapato ya ndani kutotekelezwa; hivyo kuathiri utoaji wa huduma kwa jamii kwa ujumla.

**Ninapendekeza kwamba, menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa mapato yatokanayo na ushuru wa mazao yanakusanywa kwa wakati kutoka kwa taasisi na vyama vya ushirika (AMCOS) vinavyonunua mazao ndani ya mamlaka zao. Pia, inapaswa kuanzisha mikataba yenye ukomo wa muda wa malipo ya ushuru wa mazao kwa mamlaka za serikali za mitaa, yenye kipengele cha adhabu kwa ucheleweshaji wowote wa ulipaji ushuru wa mazao. Vilevile, ihakikishe kuwa bei za mazao zinazingatia bei elekezi.**

### 5.1.5 Kuhama Kutoka Mfumo wa LGRCIS kwenda TAUSI Bila Kuwapo kwa Mpango wa Ukusanyaji Madeni kiasi cha Sh. Bilioni 12.20

Agizo la 38(1) na (6) la Memoranda ya Fedha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa la Mwaka 2009 linaelekeza mweka hazina wa halmashauri kuandaa taratibu za kifedha na kihasibu ili kuhakikisha kumbukumbu sahihi za fedha zote ambazo halmashauri inadai zinakusanywa na kupelekwa benki kwa wakati. Aidha, Kamati ya Fedha inapaswa kueleza wazi taratibu za ufuatiliaji wa madeni yaliyobaki na mbinu ambazo zitatumika kukusanya madai hayo.

Tarehe 31 Januari 2023 OR-TAMISEMI ilitoa barua yenye Na.Kumb.EB.151/297/02/108 kuziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha uwekaji kamili wa mfumo wa TAUSI kabla ya tarehe 31 Machi 2023 na kusitisha shughuli zote za ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS.

Tathmini yangu ya mfumo wa LGRCIS na TAUSI ilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa na madai kwenye mfumo wa LGRCIS kiasi cha Sh. bilioni 12.20. Hali hii inahusianishwa na juhudi ndogo zilizowekwa na uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kufuatilia mapato kwa wanaodaiwa na ukosefu wa mpango wa urejeshaji wa madeni kwa wadaiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo bado zina madai kwenye mfumo wa LGRCIS inaonekana kwenye **Jedwali Na. 22.**

**Jedwali Na.22: Orodha ya mamlaka ya serikali za mitaa zenye madai**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | 6,238,826,657 | 14 | H/W Kyerwa | 176,133,801 |
| 2 | H/W Chamwino | 1,143,429,317 | 15 | H/W Nzega | 139,146,414 |
| 3 | H/W Kilindi | 920,958,029 | 16 | H/W Chemba | 136,177,892 |
| 4 | H/Jiji Dar es salaam | 804,057,050 | 17 | H/W Nyasa | 103,293,561 |
| 5 | H/W Ngara | 365,369,382 | 18 | H/W Mbulu | 62,907,842 |
| 6 | H/W Karatu | 346,216,475 | 19 | H/W Bumbuli | 52,984,927 |
| 7 | H/W Rufiji | 287,910,607 | 20 | H/Mji Geita | 51,013,761 |
| 8 | H/W Korogwe | 209,154,829 | 21 | H/W Bagamoyo | 42,475,900 |
| 9 | H/W Muheza | 208,804,669 | 22 | H/W Madaba | 40,201,265 |
| 10 | H/M Lindi | 196,631,982 | 23 | H/W Kondoa | 37,479,900 |
| 11 | H/W Karagwe | 196,600,922 | 24 | H/W Nsimbo | 36,309,941 |
| 12 | H/M Kahama | 190,649,700 | 25 | H/W Ngorongoro | 20,597,134 |
| 13 | H/W Handeni | 183,519,555 | 26 | H/Mji Kondoa | 11,589,131 |
| | | | | **Jumla** | **12,202,440,643** |

***Chanzo:*** Orodha ya wadaiwa kutoka kwenye mfumo, 2023/24

Kutokuweza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato yaliyobaki kutoka kwa wadai kunaonekana kusababishwa na ukosefu wa ufuatiliaji na utekelezaji wa taratibu za ukusanyaji. Vilevile, hakuna ulinganifu wa mara kwa mara wa wadai (angalau kila mwezi) ili kupunguza hatari zilizoainishwa na kuhakikisha usimamizi bora wa mapato. Hali hii imesababisha kushindwa kukusanya mapato, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ambazo zilikuwa zitafadhiliwa na vyanzo vya fedha vya ndani kutokana na upungufu wa fedha.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, waanzishe mpango wa ukusanyaji wa madeni kwa wadaiwa ambao bado wapo katika LGRCIS wakati wa kipindi cha mpito kuelekea mfumo wa TAUSI. Vilevile, wafanye ulinganifu wa mara kwa mara wa wadaiwa (angalau kila**

**mwezi) ili kupunguza hatari zilizoainishwa na kuhakikisha usimamizi bora wa mapato.**

### 5.1.6 Mapato Yaliyokusanywa Kupitia Mfumo wa LGRCIS Badala ya TAUSI Sh. bilioni 6.68

Kifungu cha 17A cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kutumia mfumo wa kielekitroni wa kukusanya mapato. Aidha, aya ya 5.2.1 ya Mwongozo Usimamizi wa Mapato wa Mamlaka za Mitaa wa mwaka 2019 inazitaka mamalaka za serikali za mitaa zote kukusanya vyanzo vyote vya mapato kwa kutumia mfumo rasmi wa ukusanyaji wa mapato.

Tarehe 31 Januari 2023, OR-TAMISEMI ilitoa agizo lenye nambari ya kumbukumbu EB.151/297/02/108 kuziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha usimikwaji na utumiaji kamili wa mfumo wa TAUSI ifikapo tarehe 31 Machi 2023. Maagizo haya yaliamuru usajili wa mashine zote za kukusanyaji wa mapato (POS) na kufanya uwianishaji wa madai yaliyopo kwenye mfumo wa LGRCIS na kusitisha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS.

Baada ya mapitio ya makusanyo ya mapato kupitia mifumo ya TAUSI na LGRCIS, ilibainika kuwa mamlaka 16 za serikali za mitaa zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 6.68 kupitia LGRCIS badala ya mfumo wa TAUSI, ikiwa ni kinyume na maelekezo ya barua iliyorejewa hapo juu.

Tatizo hili lilihusishwa na kushindwa kusajili vyanzo fulani vya mapato kama vile ushuru wa hoteli, ada za huduma za machinjio, ada za leseni za uchimbaji wa vifaa vya ujenzi, na vibali vya ujenzi ndani ya mfumo wa TAUSI, hali iliyozuia ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi kupitia TAUSI. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) ziliendelea kutumia mfumo wa LGRCIS kukusanya mapato kutoka kwa vyanzo ambavyo havijasajili kwenye mfumo wa TAUSI.

Kuendelea kutumia mfumo uliositishwa kutumika katika ukusanyaji mapato kunasababisha ugumu wa upatikanaji wa taarifa wakati wa mapitio ya mfumo hivyo kupunguza uwazi. Zaidi ya hayo, mapato yanayokusanywa nje ya mfumo ulioidhinishwa yanahatari zaidi ya kupotea au kuchepushwa, kwani kuna udhibiti mdogo au ukaguzi wa kuhakikisha kuwa fedha hizo zinakusanywa na kuwekwa benki kwa usahihi. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato kupitia LGRCIS badala ya mfumo wa TAUSI zimeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.23.**

**Jedwali Na.23: Mapato ya Ndani Yaliyokusanywa LGRCIS badala ya TAUSI**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi kilichokusanywa (Sh.) | Na | Halmashauri | Kiasi kilichokusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Tunduma | 1,152,923,098 | 9 | H/M Kigoma/Ujiji | 266,755,233 |
| 2 | H/Mji Nzega | 1,065,752,850 | 10 | H/W Kaliua | 266,755,233 |
| 3 | H/W Ukerewe | 833,617,222 | 11 | H/W Kondoa | 226,537,984 |
| 4 | H/Jiji Tanga | 688,474,988 | 12 | H/W Karagwe | 164,747,566 |
| 5 | H/W Misungwi | 685,871,620 | 13 | H/W Mlimba | 77,481,010 |
| 6 | H/W Kilindi | 616,112,347 | 14 | H/W Bahi | 32,039,329 |
| 7 | H/Mji Korogwe | 275,662,777 | 15 | H/W Sumbawanga | 29,202,000 |
| 8 | H/W Rombo | 275,318,741 | 16 | H/Mji Handeni | 22,887,981 |
| | | | | **Jumla** | **6,680,139,979** |

***Chanzo:*** Taarifa ya makusanyo kutoka kwenye mfumo wa LGRCIS, 2023/24

Hii inadhoofisha uadilifu na ufanisi wa mchakato wa ukusanyaji mapato na inaweza kusababisha upotevu wa mapato na kuziathiri mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI, ihakikishe vyanzo vyote vya mapato vinasajiliwa katika mfumo wa TAUSI ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato.**

### 5.1.7 Mapato Yasiyokusanywa na Mawakala Sh. bilioni 26.12

Kifungu cha 29 (c) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kinawataka mawakala kulipa fedha zote walizokusanya kwa Mamlaka husika za Serikali za Mitaa.

Nilibaini mamlaka za serikali za mitaa 14 zilikusanya Sh. bilioni 19.49 kupitia mawakala wa kukusanya mapato. Hata hivyo, baada ya kupitia mikataba ya mawakala na taarifa za makusanyo, nilibaini kuwa mapato yaliyokusanywa yalikuwa chini ya kiwango kilichokubaliwa kwenye mikataba. Kwa mujibu wa mikataba, kiasi kilichotakiwa kukusanywa ni Sh. bilioni 45.61, wakati kiasi cha Sh. bilioni 19.49 pekee ndicho kilichokusanywa, hivyo kusababisha kiasi cha Sh. bilioni 26.12 ambacho hakijakusanywa.

Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zinazokusanya mapato kwa kutumia mawakala ambao hawakuzingatia matakwa ya mkataba inaonekana kwenye **Jedwali Na. 24** na kufafanuliwa zaidi kwenye **Kiambatisho Na.18.**

**Jedwali Na.24: Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato bila kuzingatia matakwa ya mkataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi kilichotakiwa kukusanywa (Sh.) | Kiasi kilichokusanywa (Sh.) | Kiasi ambacho hakijakusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 15,000,000,000 | 3,479,778,733 | 11,520,221,267 |
| 2 | H/M Kinondoni | 9,306,336,000 | 5,516,784,717 | 4,739,951,283 |
| 3 | H/M Ubungo | 3,120,000,000 | 909,779,440 | 2,210,220,560 |
| 4 | H/Jiji Mwanza | 3,652,299,719 | 1,643,585,916 | 2,008,713,803 |
| 5 | H/W Kibondo | 2,191,250,000 | 635,604,400 | 1,555,645,600 |
| 6 | H/W Babati | 2,500,975,000 | 1,447,145,753 | 1,053,829,247 |
| 7 | H/M Songea | 1,935,000,000 | 1,129,023,600 | 805,976,400 |
| 8 | H/W Kaliua | 2,600,864,000 | 1,873,923,308 | 726,940,692 |
| 9 | H/M Singida | 716,400,000 | 331,482,866 | 384,917,134 |
| 10 | H/W Korogwe | 545,223,463 | 176,796,047 | 368,427,416 |
| 11 | H/W Muheza | 1,451,761,678 | 1,109,190,545 | 342,571,133 |
| 12 | H/Jiji Dodoma | 421,320,056 | 198,923,205 | 222,396,851 |
| 13 | H/W Songea | 1,102,000,000 | 986,926,133 | 115,073,867 |
| 14 | H/Mji Korogwe | 111,745,500 | 48,120,000 | 63,625,500 |
| | **Jumla** | **45,605,575,416** | **19,487,064,663** | **26,118,510,753** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya makusanyo na mikataba ya mawakala*

Kutozingatia matakwa ya mikataba na mawakala wa kukusanya mapato kumetokana na usimamizi dhaifu wa mikataba ya mapato na kushindwa kufanya tathmini ya upembuzi yakinifu au tafiti kuhusu mapato yatakayo kusanywa kutoka katika vyanzo husika.

Ukusanyaji pungufu wa mapato hayo unaweza kusababisha kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa kutokana na ukosefu wa fedha. Pia, inaweza kusababisha upotevu wa mapato endapo mapato hayato kusanywa kutoka kwa mawakala hao.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa husika zihakikishe kunakuwa na usimamizi wa karibu wa mikataba ya mapato na kuweka kipengele kwenye mikataba kinachoainisha dhamana ambayo itachukuliwa kama fidia pale mawakala watakaposhindwa kukusanya mapato kwa mujibu wa mkataba au wanaposhindwa kutekeleza matakwa ya mikataba hiyo.**

### 5.1.8 Mapato Yaliyokusanywa Nje ya Mfumo wa GoT-HoMIS na TAUSI, Sh. bilioni 3.74

Tarehe 17 Oktoba 2016, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI aliandika barua yenye nambari ya kumbukumbu CEB.151/297/02/N/61, akiagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha vituo vyote vya afya vinafunga mfumo wa kielekitroni wa kukusanya mapato (Government of Tanzania Hospital Management Information System-GoT-HoMIS) kwa madhumuni ya ufuatiliaji na udhibiti wa mapato.

Pia, tarehe 31 Januari 2023, agizo lingine (Na. Kumb. EB.151/297/02/108) lilitolwea kuziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha mfumo wa TAUSI unasimikwa na kutumika kikamilifu ifikapo tarehe 31 Machi 2023. Maagizo haya yaliamuru usajili wa mashine zote za ukusanyaji wa mapato (POS) na kufanya uwianishaji wa madai yaliyopo kwenye mfumo wa LGRCIS, kutumia moduli zote za mfumo wa TAUSI na kusitisha ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mfumo wa LGRCIS.

Mfumo huu uliundwa ili kuboresha ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa kwa kuboresha ufanisi katika mchakato wa ukusanyaji, usimamizi wa fedha taslimu, utunzaji kanzidata za walipakodi, utayarishaji na uwasilishaji wa ripoti, utoaji wa stakabadhi za kielekitroni, na udhibiti katika mifumo ya mapato.

Baada ya mapitio ya taarifa za makusanyo ya mapato kutoka katika mfumo wa GoT-HoMIS, ilibainika kuwa mamlaka za serikali za mitaa 12 zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 3.74 nje ya mifumo. Hali hii ilichangiwa na kukosekana kwa mtandao mara kwa mara na kutofungwa kwa mifumo wa GoT-HoMIS hasa katika vituo vya afya. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato nje ya mfumo imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.25**.

**Jedwali Na.25: Mamlaka za serikali za mitaa zilizokusanya mapato nje ya mfumo**

| Na | Jina la Halmashauri | Aina ya Mifumo | Kiasi (Sh. ) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Nzega | TAUSI | 1,065,752,850 |
| 2 | H/M Kigamboni | TAUSI | 1,048,972,072 |
| 3 | H/W Kaliua | TAUSI | 266,755,233 |
| 4 | H/W Mlimba | TAUSI | 77,481,010 |
| | **Jumla ndogo** | | **2,458,961,165** |
| 5 | H/W Kilolo | GOT-HOMIS | 402,657,175 |
| 6 | H/Mji Kondoa | GOT-HOMIS | 302,837,842 |
| 7 | H/W Kondoa | GOT-HOMIS | 226,537,984 |
| 8 | H/W Mufindi | GOT-HOMIS | 198,361,978 |
| 9 | H/WBiharamulo | GOT-HOMIS | 51,024,375 |
| 10 | H/W Missenyi | GOT-HOMIS | 47,481,242 |
| 11 | H/M Bukoba | GOT-HOMIS | 33,326,540.88 |
| 12 | H/W Morogoro | GOT-HOMIS | 17,153,039 |
| | **Jumla ndogo** | | **1,279,380,175** |
| | **Jumla Kuu** | | **3,738,341,341** |

***Chanzo:*** Taarifa ya makusanyo ya kila mwezi kwa mwaka 2023/24

Kutokana na kukosekana kwa mifumo madhubuti, mamlaka za serikali za mitaa hazitaweza kufuatilia ukusanyaji wa mapato kikamilifu.

**Ninapendekeza kwamba, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zitenge bajeti kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa mifumo ya kielekitroni ya ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia mfumo huoa. Vingineyo, juhudi za serikali kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato zitapotea bure.**

### 5.1.9 Ankara Zilizotolewa Kupitia TAUSI na GoTHoMIS Hazijalipwa, Sh. bilioni 1.16

Kifungu cha 6.7 cha Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato wa Serikali za Mitaa wa 2019 kinaeleza kwamba, kwa kuzingatia ankara zinazotolewa kwenye mfumo, mlipakodi (watu binafsi na wafanyabiashara) atalipa kiasi cha kodi anayostahili kulipa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki inayomilikiwa na mamlaka ya serikali za mitaa au malipo ya kielekitroni na rekodi za mlipakodi katika mfumo na ankara zitahuhishwa mara mlipakodi atakapofanya malipo. Pia, kutoka kwenye malimbikizo ya ankara yaliyoko kwenye mfumo mamlaka ziandae mchanganuo wa umri wa madeni kwa ajili ya kutambua wadai sugu ili ziweke usimamizi bora wa ufuatiliaji madeni na walipakodi wanaodaiwa wataarifiwe mapema kuhusu madeni yao.

Tathmini ya ankara zote zilizotolewa kupitia mfumo wa TAUSI na GoTHoMIS, ilibaini kuwa ankara zenye thamani ya Sh. Bilioni 1.16 zilizotolewa na mamlaka 9 za serikali za mitaa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2024, zilikuwa hazijalipwa, kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.26**.

**Jedwali Na.26: Ankara zilizotolewa kupitia TAUSI na GoTHoMIS hazijalipwa**

| Na | Jina la Halmashauri | Aina ya mfumo uliotumika | Kiasi (Sh. ) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | GoTHoMIS | 529,096,333 |
| 2. | H/Jiji Arusha | TAUSI | 417,613,513 |
| 3. | H/M Singida | TAUSI | 63,567,181 |
| 4. | H/W Ileje | TAUSI | 41,375,046 |
| 5. | H/W Busega | TAUSI | 33,872,945 |
| 6. | H/W Itilima | TAUSI | 24,763,123 |
| 7. | H/W Igunga | TAUSI | 19,130,007 |
| 8. | H/W Karatu | TAUSI | 18,631,743 |
| 9. | H/W Shinyanga | TAUSI | 12,388,775 |
| | **Jumla** | | **1,160,438,666** |

***Chanzo:*** Orodha ya ankara ambazo hazijalipwa kwenye TAUSI na GoTHoMIS

Hali hii imechangiwa na kuwapo kwa utaratibu na mikakati dhaifu ya kukusanya ankara ambazo hazijalipwa zilizopo kwenye mfumo. Hii ni pamoja na kutokuwapo kwa vikumbusho vya mfumo vinavyotumwa kwa

wadaiwa kupitia meseji za simu, baruapepe, au mfumo wa TAUSI. Pia, hakuna mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa madai hayo. Hata hivyo, hakuna adhabu wala riba kwa ankara zilizochelewa kulipwa ili kuhimiza malipo yafanyike kwa wakati.

Kutokusanya mapato kiasi cha Sh. bilioni 1.16 kunaweza kuathiri kazi za utendaji wa kila siku wa mamlaka za serikali za mitaa, na kunaweza kusababisha upotevu wa mapato kama mapato yatokanayo na ankara hizo hayatokusanywa.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa, ikusanye mapato ya ankara zote ambazo hazijalipwa ya thamani ya Sh. bilioni 1.16 bila kuchelewa. Pia, ziimarishe udhibiti wa mfumo wa ndani katika ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha mikakati madhubuti inawekwa katika ukusanyaji wa mapato ankara zinapotolewa.**

### 5.1.10 Kutokusanywa kwa Mapato Yatokanayo na Kodi ya Ardhi na Ada za Mabango, Sh. milioni 363.62

Kifungu cha 7(1)(x) na (y) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura.290, kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 41 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 (Sheria Na.8 ya 2023), kinaziagiza halmashauri za wilaya kukusanya 20% ya kodi ya ardhi inayokusanywa na Serikali Kuu chini ya Sheria ya Ardhi na 20% ya kodi ya majengo inayokusanywa chini ya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 289. Pia, kifungu cha 31A cha sheria hiyohiyo, kilichorekebishwa na kifungu cha 43 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, kinaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kusimamia viwango vya kodi ya majengo hadi tarehe 31 Desemba 2023; baada ya hapo mamlaka za serikali za mitaa zitachukua jukumu hili na kushughulikia ada za matangazo ya mabango.

Nilifanya tathmini ya makabidhiano ya vyanzo vya mapato vilivyokuwa vikisimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ambavyo ni ada za mabango na kodi ya ardhi mtawalia. Nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 5 hazikukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vilivyotajwa, kiasi cha Sh. milioni 363.62. Hii ni kutokana na kukosekana kwa mwongozo kutoka Wizara ya Fedha na utaratibu mzuri wa makabidhiano ya madai na kanzidata ya walipakodi kati ya mamlaka ya serikali za mitaa, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Hakuna jitihada zozote zilizofanywa na mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha kuwa ada ya mabango na kodi ya ardhi inakusanywa kwa

mujibu wa sheria. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikukusanya mapato ya kodi ya ardhi na mabango imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.27**.

**Jedwali Na.27: Mapato yasiyokusanywa kutoka kwa kodi ya ardhi na ada za mabango**

| Na | Jina la Halmashauri | Chanzo cha mapato | Kiasi kilichokusanywa na Wizara (Sh.) | Kiasi kilichatakiwa kukusanywa lakini Hakijakusanywa na Halmashauri(Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Tarime | Kodi ya Ardhi | 408,361,465 | 81,672,293 |
| | | Ada ya mabango | - | 70,500,000 |
| 3 | H/W Kilosa | Ada ya mabango | - | 81,915,552 |
| 4 | H/Jiji Dar es salaam | Ada ya mabango | - | 127,034,631 |
| 5 | H/W Rorya | Kodi ya Ardhi | 12,476,475 | 2,495,295 |
| | **Jumla** | | **420,837,940** | **363,617,771** |

***Chanzo:*** Taarifa za makusanyo, rejista, 2023/24

Hali hii inachangiwa na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato; kutokuwapo kwa kanzidata ya vyanzo vya mapato tajwa hapo juu; na ukosefu wa mfumo ulioanzishwa wa madai. Pia kunakosekana uratibu wa kutosha kati ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) na wadau wengine, kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika ukusanyaji wa ada za mabango, na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHS) katika ukusanyaji wa kodi ya ardhi.

Hali hii inazikosesha Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) fedha muhimu zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali na huduma zinazolenga kuboresha ustawi wa jamii.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa, kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na wadau wengine iweke mfumo bora wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo hivyo na kukamilisha uundaji wa kanzidata kwa ajili ya vyanzo vya mapato husika.**

### 5.1.11 Kasoro Zilizobainika Katika Usimamizi wa Kodi za Majengo

Kifungu cha 31A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kama ilivyorekebishwa na Kifundu cha 43 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2023, kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kutathmini, kukusanya, na kutolea taarifa kodi ya majengo kuanzia mwezi Januari 2024. Ili kutekeleza hili, OR-TAMISEMI ilisaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU)

na TANESCO mwezi Februari 2024 ili kurahisisha ukusanyaji wa kodi ya majengo kupitia ada za mita za umeme.

Nilikagua utaratibu uliopo wa tathmini kwenye kodi ya majengo, ukusanyaji na uwajibikaji katika mwaka wa fedha 2023/24 na kubaini changamoto zifuatazo:-

(i) **Upungufu Katika Uhakiki na Ugawaji:** Kati ya mwezi Februari hadi Agosti 2024, TANESCO iliwasilisha jumla ya Sh. bilioni 36.26 kwa OR-TAMISEMI kama kodi ya majengo zilizokusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/24. Hata hivyo, nilibaini kuwa hakukuwa na kanzidata ya kidijiti ya walipakodi ya majengo, hali iliyoleta ugumu katika kuthibitisha usahihi wa makusanyo na ukosefu wa usimamizi ulioimarishwa ulisababisha kuchelewesha ugawaji wa fedha zilizokusanywa kwa mamlaka za serikali za mitaa;

(ii) **Ucheleweshaji wa Ankara na Uhamishaji wa Fedha:** Kifungu cha 8 cha MoU kinahitaji OR-TAMISEMI kutuma kiasi kilichokusanywa kwa Mfuko Mkuu wa Serikali kabla ya tarehe 8 ya kila mwezi. Hata hivyo, ankara za OR-TAMISEMI kwa TANESCO zilicheleweshwa kwa siku 2 hadi 36, wakati malipo ya TANESCO kwa OR-TAMISEMI yalicheleweshwa kwa siku 16 hadi 42. Aidha, hadi Disemba 2024, Sh. bilioni 7.25 (20% ya Sh. bilioni 36.26 zilizokusanywa) hazikuwa zimetumwa kwa mamlaka za serikali za mitaa, jambo ambalo linakiuka Kifungu cha 6(1)(t) na Kifungu cha 7(1)(y) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, na Kifungu cha 16(3) cha Sheria ya mamlaka za serikali za mitaa (Tozo), Sura ya 289; na

(iii) **Kutokamilika kwa Moduli ya Kodi ya Majengo kwenye Mfumo wa TAUSI:** OR-TAMISEMI ilitekeleza moduli ya kodi ya majengo kwenye mfumo wa TAUSI katika mamlaka za serikali za mitaa (MSM) 47 pekee; hivyo mamlaka za serikali za mitaa 137 zilibaki kutegemea ukusanyaji wa TANESCO. Matokeo yake, majengo yasiyo na umeme hayakulipiwa kodi.

Kutokuwapo kwa muunganiko kati ya mfumo wa TAUSI na mfumo wa ukusanyaji wa TANESCO kumesababisha OR-TAMISEMI kutopata taarifa za moja kwa moja za makusanyo ya kodi ya majengo, hivyo kuhitaji uwianishaji wa taarifa kabla ya kupokea fedha iliyokusanywa. Ukosefu wa usimamizi wa kutosha umechangia ucheleweshaji wa ankara na uhamishaji wa 20% inayohitajika kwa mamlaka za serikali za mitaa, hivyo kuathiri mipango yao ya kifedha na utoaji wa huduma. Aidha, kutokuwapo kwa bajeti ya utekelezaji wa mfumo katika mamlaka za serikali za mitaa 137 kumekwamisha matumizi ya mfumo wa kidijitali

wa ukusanyaji, jambo linalopunguza ufanisi na kuleta hatari ya upotevu wa mapato.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ifanye uratibu wa muunganiko wa mifumo ya ukusanyaji ya TAUSI na TANESCO ili kuwezesha ufuatiliaji kwa wakati halisi na kuondoa makosa ya ulinganifu wa taarifa. Aidha, OR-TAMISEMI inapaswa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuharakisha kutuma Sh. bilioni 7.25 kwenda mamlaka za serikali za mitaa na kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mfumo katika mamlaka za serikali za mitaa zote 184, ikiwa ni pamoja na uratibu wa kifedha na shughuli za ufuatiliaji ili kuongeza ufanisi na uzingatiaji wa sheria.**

### 5.1.12 Malipo ya Wanachama Yasiyolipwa Kutoka kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa - Sh. bilioni 4.90

Ibara ya 6 ya Katiba ya ALAT (1985), iliyorekebishwa mwaka 2014, inatamka kuwa mamlaka zote za serikali za mitaa nchini Tanzania Bara ni wanachama wa ALAT na zinatakiwa kulipa ada ya uanachama ya kila mwaka.

Nilibaini kwamba, mamlaka za serikali za mitaa 172 zilikuwa na madeni ya ada ya uanachama jumla ya Sh. bilioni 4.90 tangu mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2023/24. Aidha, 91% ya ada ya uanachama, mahsusi kwa mwaka wa fedha 2023/24, inayofikia Sh. 620.22 milioni, haijalipwa na mamlaka za serikali za mitaa husika.

Kutokulipwa kwa kiasi kikubwa cha ada, kunaonesha upungufu wa ALAT katika utekelezaji wa mikakati ya ufuatiliaji na kusimamia utekelezaji wa malipo, jambo ambalo linaweza kusababisha kuongezeka kwa deni hili. Kushindwa kukusanya ada hizi kunaweza kuathiri uwezo wa ALAT kutekeleza shughuli zake zilizopangwa na kufikia malengo yake.

**Ninapendekeza kwamba, menejimenti ya ALAT itekeleze mikakati madhubuti ya kuhakikisha ukusanyaji wa ada na kuzikumbusha mara kwa mara mamlaka za serikali za mitaa kulipa ada zao kwa wakati. Aidha, ninapendekeza kwamba menejimenti ya ALAT ifanye tathmini ya hali ya kukusanyika kwa madeni ya tangu mwaka wa fedha 2018/19 na kuchukua hatua stahiki kulingana na matokeo ya tathmini hiyo.**

### 5.1.13 Kupoteza Mapato Yanayoweza Kupatikana kwa Sababu ya Mpangaji Kuweka Matangazo Yasiyo Idhinishwa kwenye Kadi ya Mteja

Mamlaka ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) iliingia mkataba na mpangaji tarehe 26 Oktoba 2023 kwa ajili ya kusimamia na kuweka mfumo wa maegesho ya magari wa kiotomatiki kwenye eneo la

maegesho la Gerezani. Kifungu cha 1 cha mkataba kinabainisha mgawanyo wa mapato, ambapo 70% ya mapato yatakwenda kwa mmiliki (DART) na 30% kwa mpangaji kwa kipindi cha miaka mitano, huku kukiwa na uwezekano wa kuhuisha mkataba kwa masharti mapya baada ya miaka mitatu. Kifungu cha 31(c) kinaeleza kwamba mmiliki anaweza kuvunja mkataba ikiwa mpangaji atautumia mfumo kwa madhumuni mengine tofauti na yale yaliyotajwa kwenye mkataba.

Baada ya kutembelea eneo la maegesho tarehe 16 Novemba 2024, ilibainika kuwa mpangaji alikuwa ameweka tangazo kwenye kadi ya mteja kwa huduma iitwayo "Affordable HR & Payroll System Today" bila idhini ya mmiliki. Pia, nilibaini kuwa hakukuwa na makubaliano rasmi kuhusu tangazo hili, na DART haikupokea mapato yoyote kutokana na tangazo hilo, jambo linalokiuka masharti ya mkataba wa upangaji.

Ukosefu wa mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mikataba ulisababisha matumizi yasiyoruhusiwa ya mfumo, hivyo kusababisha kupoteza mapato ya matangazo na kutokuzingatia masharti ya mkataba wa upangaji. Pia, ukosefu wa idhini kwa tangazo na kushindwa kuweka makubaliano rasmi kuhusu mgawanyo wa mapato unadhihirisha kutokuzingatia masharti ya mkataba.

**Ninapendekeza kuwa uongozi wa DART ushughulikie tangazo lisiloidhinishwa lililowekwa na mpangaji au kuingia katika makubaliano rasmi na mpangaji kuhusu tangazo hilo.**

## 5.2 Usimamizi wa Matumizi

Usimamizi wenye ufanisi wa matumizi ya fedha za umma ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria na udhibiti uliowekwa. Hii inasaidia kuongeza uwajibikaji na kuhakikisha kuwa rasilimali zilizopo zinatumika kwa maslahi ya umma.

Matokeo ya ukaguzi yamebainisha upungufu mbalimbali katika usimamizi wa fedha kwenye mamlaka za serikali za mitaa nchini Tanzania. Upungufu huo unajumuisha kutokuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa fedha za umma, jambo linalosababisha kuwapo kwa usimamizi usioridhisha wa fedha na kusababisha kuwepo kwa matumizi yasiyo na tija ya rasilimali za umma.

Sura hii inaelezea kwa undani masuala yaliyobainika na ambayo yanayohitaji kushughulikiwa kwa haraka, na ikiwa hayatatatuliwa, yanaweza kuathiri vibaya matumizi sahihi ya fedha za umma katika mamlaka za serikali za mitaa na kudhoofisha utoaji wa huduma pamoja na uwajibikaji katika masuala ya kifedha.

### 5.2.1 Malipo Yasiyo na Stakabadhi za Kielekitroni Sh. bilioni 12.85

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi [Sura ya 438], kinamtaka kuwa mtu yeyote anayefanya biashara ya kusambaza bidhaa, kutoa huduma, au kupokea malipo kwa bidhaa alizotoa au huduma alizotoa kutoa stakabadhi ya kielekitroni.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 41, sekretarieti za mikoa mbili (2), na taasisi ya TARURA zilifanya malipo ya bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 12.85 bila kudai stakabadhi za kielekitroni. Orodha ya taasisi hizo imeainishwa kwenye **Jedwali Na. 28** hapa chini.

**Jedwali Na.28: Malipo Yasiyo na Stakabadhi za Kielekitroni**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/ Jiji Mwanza | 8,258,118,176 | 25 | H/W Mkinga | 52,800,500 |
| 2 | H/W Musoma | 895,889,372 | 26 | H/W Liwale | 43,103,457 |
| 3 | H/W Kaliua | 409,740,872 | 27 | H/W Hai | 42,368,203 |
| 4 | H/W Longido | 328,635,926 | 28 | H/W Meatu | 40,710,670 |
| 5 | H/W Pangani | 228,170,853 | 29 | H/W Muheza | 40,664,205 |
| 6 | H/W Mpwapwa | 209,742,185 | 30 | H/Mji Nzega | 38,501,460 |
| 7 | H/M Shinyanga | 201,572,864 | 31 | H/M Mtwara/Mikindani | 37,572,945 |
| 8 | H/W Mlimba | 195,316,115 | 32 | H/W Kibondo | 30,981,242 |
| 9 | H/W Tarime | 185,755,650 | 33 | H/W Chamwino | 26,476,200 |
| 10 | H/W Msalala | 157,645,139 | 34 | H/W Lushoto | 21,844,500 |
| 11 | H/W Nanyumbu D | 149,096,164 | 35 | H/M Mpanda | 18,233,660 |
| 12 | H/W Shinyanga | 131,439,120 | 36 | H/W Mpimbwe | 17,105,100 |
| 13 | H/Jiji Arusha | 125,337,552 | 37 | H/W Busega | 15,714,727 |
| 14 | H/W Ushetu | 91,180,822 | 38 | H/Mji Kondoa | 9,063,140 |
| 15 | H/W Kongwa | 90,260,159 | 39 | H/W Magu | 7,760,000 |
| 16 | H/W Maswa | 82,254,847 | 40 | H/W Newala | 5,335,429 |
| 17 | H/W Bariadi | 77,397,937 | 41 | H/W Handeni | 2,281,295 |
| 18 | H/W Madaba | 74,344,310 | **Jumla Ndogo-** | | **12,726,540,734** |
| 19 | H/W Itilima | 73,996,048 | | | |
| 20 | H/W Bumbuli | 70,951,608 | 1 | S/M Geita | 78,218,658 |
| 21 | H/W Karatu | 64,124,663 | 2 | S/M Arusha | 20,449,784 |
| 22 | H/W Mpanda | 62,702,167 | 3 | TARURA | 21,807,631 |
| 23 | H/W Manyoni | 57,950,280 | **Jumla Ndogo** | | **120,476,073** |
| 24 | H/Mji Tunduma | 54,401,172 | **Jumla Kuu** | | **12,847,016,807** |

***Chanzo:*** Hati za Malipo

Aidha, nilibaini kuwa TARURA ililipa kiasi cha Sh. milioni 279.11 kwa wakandarasi na wazabuni, lakini stakabadhi za EFD zisizo sahihi zilithibitisha malipo.

Mawasiliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalibainisha kuwa stakabadhi za kielekitroni kwa malipo yanayofikia Sh. milioni 61.93 hazikuweza kupatikana katika mfumo wa kutambua walipakodi wa TRA. Pia, stakabadhi za kielekitroni zenye thamani ya Sh. milioni 217.18 zilionekana kwenye mfumo wa TRA kuwa ni za kiasi cha Sh. milioni 18.98 badala ya kiasi halisi.

Wakandarasi waliweza kuwasilisha stakabadhi nyingine halisi za kielekitroni kufidia na kusahihisha stakabadhi za awali zenye jumla ya Sh. milioni 226.87.Hivyo kubaki na stakabadhi zisizo sahihi za kielekitroni zenye thamani ya Sh. milioni 52.23. Kitendo hiki kinakiuka matakwa ya Kanuni ya 17(2) ya Kanuni za Kodi ya Mapato (Matumizi ya Vifaa vya Kielekitroni vya Kodi) za mwaka 2012, ambayo inakataza mtumiaji kubadilisha taarifa zilizohifadhiwa katika Vifaa vya Kielekitroni vya Kodi.

Kutokutoa stakabadhi za kielekitroni na kutoa stakabadhi zisizosahihi za kielekitroni ili kuthibitisha malipo yaliyofanyika kunatokana na ukwepaji kodi wa makusudi unaofanywa na watu wasio waaminifu; pamoja na upungufu katika ufuatiliaji na utekelezaji wa sheria na mamlaka husika. Hali hii inachochea ukwepaji wa kodi miongoni mwa wazabuni na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

**Ninaishauri kuwa Serikali kuwa OR-TAMISEMI, Wizara ya Fedha na TRA, iimarishe ushirikiano wao katika kutekeleza kikamilifu sheria za kodi kwa kwa kuzitaka taasisi za umma kudai stakabadhi za kielekitroni kutoka kwa wazabuni pindi wanapofanya malipo ya bidhaa na huduma.**

**Vilevile, TRA inapaswa kuchunguza na kuchukua hatua stahiki dhidi ya matukio ya watu kutoa stakabadhi zisizo sahihi za kielekitroni ili kuzuia kujirudia kwa matukio kama hayo na wahusika wanapaswa kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria za kodi zilizopo.**

### 5.2.2 Malipo Yaliyofanyika kwa Fedha Taslimu Sh. bilioni 4.22

Kwa mujibu wa Kanuni ya 93(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, malipo yanapaswa kufanywa tu kwa watu waliotajwa kwenye hati za malipo au mawakala wao waliothibitishwa. Kwa vyovyote iwezekanavyo, malipo hayo yafanywe kupitia uhamisho wa moja kwa moja kwa kupitia benki au hundi zilizofungwa. Vivyo hivyo, Aya ya 6.7.3 ya Mwongozo wa Uhasibu wa mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inazitaka halmashauri kufanya malipo yote kwa njia ya kielekitroni katika akaunti za benki za walipwaji, na kwa hali yoyote ile, halmashauri isilipe kwa fedha taslimu.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 13 na Sekretarieti za Mkoa mbili zilifanya malipo ya jumla ya Sh. bilioni 4.22 kwa wazabuni na watumishi mbalimbali kwa njia ya fedha taslimu, kinyume na matakwa ya kanuni na mwongozo uliotajwa hapo juu. Orodha ya taasisi zilizofanya malipo kwa fedha taslimu imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 29**.

**Jedwali Na.29: Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslimu**

| Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/ Jiji Dar es Salaam | 2,512,349,250 | 10 | H/Mji Ifakara | 39,780,000 |
| 2 | H/ Jiji Dodoma | 431,895,597 | 11 | H/W Iramba | 34,186,600 |
| 3 | H/ W Shinyanga | 261,507,000 | 12 | H/W Chamwino | 18,963,520 |
| 4 | H/W Mlimba | 249,456,948 | 13 | H/W Manyoni | 10,580,000 |
| 5 | H/Mji Kahama | 145,716,183 | **Jumla ndogo-Halmashauri** | | **3,976,830,972** |
| 6 | H/W Igunga | 78,625,428 | 14 | S/M Mwanza | **151,307,640** |
| 7 | H/M Singida | 72,614,000 | 15 | S/M Shinyanga | 89,559,500 |
| 8 | H/M Kigamboni | 64,611,750 | **Jumla ndogo-S/M** | | **240,867,140** |
| 9 | H/W Kilosa | 56,544,696 | **Jumla Kuu** | | **4,217,698,112** |

***Chanzo:*** *Hati za Malipo*

Hoja hii imechangiwa na upungufu wa mfumo wa udhibiti wa ndani katika uidhinishwaji wa malipo kwenye taasisi husika na kukosekana kwa dhamira ya dhati ya kuzingatia matakwa ya kanuni na mwongozo husika. Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu huongeza hatari ya matumizi mabaya ya fedha; kukosekana kwa uwajibikaji, na uwezekano wa upotevu wa mapato ya serikali kutokana na ukwepaji kodi unaofanywa na wazabuni.

**Ninaishauri Serikali kupitia OR TAMISEMI na menejimenti ya taasisi husika kuimarisha udhibiti wa malipo kwa kutekeleza sheria inayokataza malipo ya fedha taslimu. Aidha, kuimarisha jukumu la kitengo cha ukaguzi wa awali katika kupitia malipo kabla hayajafanyika, pamoja na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kupitia kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kubaini upungufu na kuhakikisha kanuni husika zinazingatiwa.**

### 5.2.3 Kodi ya Zuio Iliyokatwa Kutowasilishwa TRA Sh. bilioni 1.11

Kifungu cha 83 (A) na Aya ya 4(c) (v) cha Jedwali la 1 la Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332) kinataka kila taasisi kukatwa 2% kwa bidhaa

zinazotolewa kwa taasisi za Serikali na kiasi kilichozuiliwa kutumwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 49, sekretarieti ya mkoa moja, na Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) walikuwa na deni la kodi ya zuio ya Sh. bilioni 1.11 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024. Kiasi hiki kilikatwa kwa wazabuni bila kuwasilishwa TRA, na kuripotiwa kama deni katika taarifa za fedha. Mchanganuo wa kina umeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.19**.

Upungufu wa mfumo wa udhibiti wa ndani katika taasisi husika umesababisha kushindwa kuhakikisha kuwa kodi zilizokatwa zinawasilishwa TRA kwa wakati na kwa usahihi. Kutowasilisha kodi ya zuio iliyokatwa kunapunguza mapato ya serikali, hivyo kuathiri uwezo wa serikali kugharamia huduma muhimu na kudhoofisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia OR TAMISEMI na menejimenti ya taasisi husika, iimarishe udhibiti wa makato na uwasilishaji wa kodi ya zuio. Pia, ihakikishe zinawasilisha kwa wakati kodi zilizokatwa TRA. Kuimarisha mifumo hii ya udhibiti kutasaidia kuepuka adhabu kutokana na ucheleweshaji wa masilisho ya kodi, kuimarisha uzingatiaji wa sheria za kodi na kuongeza mapato ya serikali.**

## 5.3 Usimamizi wa Akaunti ya Amana

Akaunti ya amana ni kwa ajili ya kutunza fedha za walioweka amana ili zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Hivyo, matumizi ya fedha zilizopo katika akaunti hiyo yanapaswa kuendana na lengo kuu la amana hizo.

Usimamizi usioridhisha wa fedha hizo huwazuia wawekaji kupata fedha zao pindi zinapohitajika, huchelewesha malipo muhimu, hupunguza imani katika usimamizi wa kifedha wa taasisi, na huiweka taasisi katika hatari ya kupoteza sifa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Tathmini yangu ya usimamizi wa akaunti za amana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa ilibaini kasoro kadhaa kama ilivyoelezwa hapa chini:

### (i) Fedha zilizokopwa akaunti ya Amana bila kurejeshwa Sh. bilioni 3.79

Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 inamtaka ofisa anayeidhinisha marejesho ya madai ya amana kujiridhisha kwamba

amana imetumika kwa lengo lililokusudiwa. Pia, lazima ofisa huyo ajiridhishe kwa kurejea stakabadhi ya awali iliyotolewa ili kuthibitisha mtu anayedai amana ndiye mwekaji halali wa amana au ana haki ya kurejeshewa.

Nilibaini malipo yenye jumla ya Sh. bilioni 3.79 yaliyofanyika na mamlaka za serikali za mitaa 26 na sekretarieti za mikoa nne kutoka katika akaunti za amana kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizokuwa, kinyume na malengo yaliyokusudiwa na fedha hazikurejeshwa kwenye akaunti husika. Mchanganuo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 30**.

**Jedwali Na.30: Fedha zilizokopwa akaunti ya amana bila kurejeshwa**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dodoma | 552,479,435 | 18 | H/W Muleba | 45,417,027 |
| 2 | H/ Jiji Dar es Salaam | 546,606,100 | 19 | H/W Karagwe | 33,984,950 |
| 3 | H/W Tarime | 219,344,208 | 20 | H/W Rorya | 32,459,260 |
| 4 | H/W Kalambo | 217,169,016 | 21 | H/W Nsimbo | 29,978,200 |
| 5 | H/Mji Makambako | 209,455,200 | 22 | H/W Ruangwa | 25,966,958 |
| 6 | H/ Mji Kahama | 199,213,443 | 23 | H/Mji Masasi | 25,208,560 |
| 7 | H/W Bunda | 198,869,141 | 24 | H/M Kigamboni | 21,825,000 |
| 8 | H/W Shinyanga | 161,680,921 | 25 | H/W Ngara | 17,460,000 |
| 9 | H/Mji Bariadi | 146,229,501 | 26 | H/W Bukoba | 13,790,670 |
| 10 | H/Jiji Tanga | 126,092,464 | **Jumla Ndogo** | | **3,368,282,476** |
| 11 | H/M Musoma | 113,790,931 | 1 | S/M Geita | 284,586,054 |
| 12 | H/M Shinyanga | 104,926,312 | 2 | S/M Kagera | 52,502,457 |
| 13 | H/Mji Babati | 89,764,219 | 3 | S/M Shinyanga | 48,677,550 |
| 14 | H/W Butiama | 66,816,023 | 4 | S/M Mwanza | 40,200,100 |
| 15 | H/W Madaba | 60,552,992 | **Jumla Ndogo** | | **425,966,161** |
| 16 | H/W Kishapu | 55,569,644 | **Jumla Kuu** | | **3,794,248,637** |
| 17 | H/W Rungwe | 53,632,301 | | | |

***Chanzo:*** *Daftari la Fedha na Hati za Malipo*

### (ii) Malipo zaidi ya Kiasi kilichowekwa kwenye Akaunti ya Amana Sh. bilioni 2.59

Nilipitia usimamizi wa akaunti ya amana na kubaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 20 na sekretarieti za mkoa mbili zilifanya malipo na kuvuka viwango vilivyowekwa kwenye akaunti kwa kiasi cha Sh. bilioni 2.59, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.31** hapa chini. Kitendo hiki kinakiuka matakwa ya Kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001, hivyo huathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Jedwali Na.31: Malipo zaidi ya kiasi kilichowekwa akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Ngorongoro | 549,633,044 | 14 | H/W Makete | 62,666,890 |
| 2 | H/M Kigamboni | 325,330,508 | 15 | H/W Longido | 59,370,602 |
| 3 | H/Mji Ifakara | 287,521,763 | 16 | H/W Mkalama | 29,732,658 |
| 4 | H/Mji Babati | 162,602,704 | 17 | H/W Missenyi | 27,198,830 |
| 5 | H/W Magu | 152,371,101 | 18 | H/W Arusha | 24,086,610 |
| 6 | H/W Mbinga | 144,501,844 | 19 | H/W Kyerwa | 22,858,508 |
| 7 | H/W Muheza | 118,880,048 | 20 | H/W Bukoba | 21,058,664 |
| 8 | H/W Bunda | 105,664,119 | **Jumla Ndogo** | | **2,489,278,652** |
| 9 | H/W Monduli | 95,539,505 | 1 | S/M Kigoma | 57,372,966 |
| 10 | H/W Hanang' | 88,244,073 | 2 | S/M Mtwara | 44,745,000 |
| 11 | H/M Ilemela | 79,391,793 | **Jumla Ndogo** | | **102,117,966** |
| 12 | H/W Siha | 69,520,559 | **Jumla Kuu** | | **2,591,396,618** |
| 13 | H/Mji Njombe | 63,104,829 | | | |

*Chanzo: Daftari la Fedha na Hati za Malipo*

Vilevile, nilibaini malipo ya Sh. bilioni 1.91 yaliyofanywa kutoka kwenye akaunti za amana katika mamlaka za serikali za mitaa 19, pamoja na sh. milioni 464.84 yaliyofanywa na sekretarieti za mikoa nne, bila uthibitisho wa fedha hizo kupokelewa akaunti ya amana, kinyume na kanuni ya 132 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 32.**

**Jedwali Na.32: Malipo bila uthibitisho wa fedha kupokelewa akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/M Kinondoni | 603,531,258 | 14 | H/W Kakonko | 32,836,939 |
| 2 | H/W Shinyanga | 215,587,998 | 15 | H/W Nsimbo | 24,932,000 |
| 3 | H/W Kishapu | 202,469,960 | 16 | H/W Bumbuli | 21,480,000 |
| 4 | H/W Kibondo | 163,120,778 | 17 | H/Mji Babati | 20,526,316 |
| 5 | H/W Mkuranga | 142,279,814 | 18 | H/W Buchosa | 12,871,000 |
| 6 | H/W Kwimba | 89,123,743 | 19 | H/W Biharamulo | 12,104,800 |
| 7 | H/Mji Handeni | 75,186,900 | **Jumla Ndogo** | | **1,905,353,081** |
| 8 | H/W Newala | 64,510,318 | 1 | S/M Shinyanga | 205,816,345 |
| 9 | H/Jiji Mwanza | 62,183,600 | 2 | S/M Mwanza | 162,876,920 |
| 10 | H/W Monduli | 48,474,137 | 3 | S/M Geita | 59,319,230 |
| 11 | H/W Simanjiro | 40,307,520 | 4 | S/M Kagera | 36,829,863 |
| 12 | H/W Tunduru | 38,826,000 | **Jumla Ndogo** | | **464,842,358** |
| 13 | H/W Musoma | 35,000,000 | **Jumla Kuu** | | **2,370,195,439** |

*Chanzo: Daftari la Fedha na Hati za Malipo*

### (iii) Uhamisho usioruhusiwa wa Mapato ya Ndani kwenda Akaunti ya Amana Sh. bilioni 1.06

Aya ya 3 ya Sehemu ya 2 ya Mwongozo uliotolewa na OR-TAMISEMI Septemba 2017 inaelekeza jinsi ya fedha za mapato ya ndani zitahamishwa kwenda akaunti ya mfuko wa pamoja na akaunti ya miradi ya maendeleo.

Hata hivyo, nilibaini mamlaka za serikali za mitaa tano zilihamisha kiasi cha Sh. bilioni 1.06 kutoka kwenye akaunti za mapato ya ndani kwenda akaunti za amana kwa ajili ya matumizi yasiyoidhinishwa. Rejea **Jedwali Na. 33**.

**Jedwali Na.33: Uhamisho wa Mapato ya Ndani kwenda akaunti ya Amana**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Chamwino | 328,900,000 |
| 2 | H/W Kigoma | 305,701,950 |
| 3 | H/W Longido | 209,719,711 |
| 4 | H/W Arusha | 138,349,780 |
| 5 | H/W Ngorongoro | 79,160,000 |
| **Jumla** | | **1,061,831,441** |

***Chanzo:*** *Daftari la Fedha*

Ufinyu wa bajeti katika taasisi husika, hususani katika mamlaka za serikali za mitaa, na upungufu wa mfumo wa udhibiti wa ndani imara katika usimamizi wa fedha kwenye akaunti za amana ni miongoni mwa sababu zinazochangia usimamizi usioridhisha na ukopaji usiodhibitiwa kutoka kwenye akaunti za amana.

Kutumia fedha za akaunti za amana kutekeleza shughuli zisizoendana na malengo ya fedha hizo kunawazuia wenye amana hizo kupata fedha zao, na kusababisha madeni makubwa kwa taasisi, hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

Vilevile, kuhamisha fedha za mapato ya ndani kwenda kwenye akaunti za amana kinyume na maagizo husika kunasababisha matumizi yasiyoidhinishwa kwenye bajeti na inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo.

**Ninaihimiza Serikali, kupitia OR-TAMISEMI, ishirikiane na menejimenti ya taasisi husika kutafuta suluhisho la tatizo hili kwa kuimarisha udhibiti wa usimamizi wa ndani wa akaunti za amana. Hii inapaswa kujumuisha utekelezaji wa taratibu thabiti za ufuatiliaji, usuluhishi wa taarifa za fedha na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na miongozo husika. Vilevile,**

**juhudi zinapaswa kuelekezwa katika kurejesha kiasi cha fedha kilichotumika kwenye shughuli zisizoendana na malengo yaliyokusudiwa, kuhakikisha kuwa fedha za akaunti za amana zinatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa pekee, na kuhakikisha uzingatiaji wa mwongozo unaozuia uhamisho wa fedha za mapato ya ndani kwenda kwenye akaunti za amana.**

### 5.3.1 Bakaa katika Akaunti ya Amana inayotunzwa na OR-TAMISEMI haikugawiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika Sh. Bilioni 3.85

Kanuni ya 130 ya Kanuni za Fedha za Umma (PFR) ya mwaka 2001 inawataka maafisa masuuli kutunza akaunti ya udhibiti kwa kila aina ya amana, ikionesha salio linalodaiwa. Aidha, kumbukumbu za kila mwenye amana zinapaswa kutunzwa, zikionesha miamala iliyofanyika na salio la fedha.

Tathmini ya taarifa ya salio la amana kwenye akaunti ya amana ya MSM (Akaunti Na. 9921169787 inayotunzwa na OR-TAMISEMI) mnamo tarehe 30 Juni 2024 ilionesha salio la Sh. bilioni 66.82. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 38.92 zilielekezwa kwenye akaunti ndogo za mamlaka za serikali za mitaa, huku Sh. bilioni 27.90 zikibaki. OR-TAMISEMI haikuwa na mchanganuo unaoeleza vyanzo, wanaotakiwa kupewa, na shughuli zinazokusudiwa kwa fedha hizi. Kwa kuwa akaunti hii ni ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, kiasi hicho ambacho hakikugawiwa hakikuripotiwa katika taarifa zozote za fedha.

Mpaka mwezi Desemba 2024, uchambuzi ulikuwa umefanywa kwa Sh. bilioni 24.18, na kiasi hicho kiligawiwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa , ikiacha salio la Sh. bilioni 3.85 halijagawiwa.

Tatizo hili linatokana na kuchelewa kupokea taarifa kutoka kwa walioweka fedha kuhusu madhumuni yake. na kutokuwapo kwa mfumo sahihi wa kuripoti salio la fedha hizo. Hii inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha kwa kuwa fedha zisizogawiwa haziwi kwenye taarifa za kifedha, jambo linalopunguza uwazi na uwajibikaji wake.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, iweke utaratibu mzuri wa kuripoti na kusimamia fedha zisizogawiwa zinazobakia kwenye akaunti ya Amana ya mamlaka. Aidha, ninashauri OR-TAMISEMI ianzishe mfumo wa kuripoti wa kiotomatiki ili kurahisisha utambuzi wa fedha na ugawaji wake pindi zinapopokelewa. Pia, ninashauri OR-TAMISEMI iharakishe ugawaji wa fedha zilizosalia ili kuboresha uwazi na kuimarisha utoaji wa huduma.**

# 06

# SURA YA SITA

## Usimamizi wa Ununuzi

## 6.0 Utangulizi

Kifungu cha 48(1)(b) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma (Sura ya 410) kinawaelekeza maofisa masuuli wa taasisi nunuzi kuzingatia taratibu zilizowekwa za ununuzi na mikataba. Zaidi ya hayo, kama chombo cha uhakikisho, ofisi yangu imepewa mamlaka chini ya Kifungu cha 48(3) cha Sheria hiyohiyo kutathmini kama taasisi zinazofanya ununuzi zimezingatia masharti ya Sheria ya Ununuzi wa umma na taratibu zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA).

Kwa miaka mingi, nimekuwa nikisisitiza mara kwa mara umuhimu wa ununuzi na usimamizi mzuri wa mikataba katika kuhakikisha matumizi bora na ya wazi ya rasilimali za umma. Hata hivyo, pamoja na maendeleo ya kisheria na kuanzishwa kwa mfumo wa ununuzi wa kielekitroni kwenye sekta za serikali (NeST), ukaguzi wangu kwa mwaka wa fedha 2023/24 umebaini kasoro mbalimbali zinazoambatana na ukiukwaji wa sheria za ununuzi na taratibu zilizowekwa.

Sura hii inabainisha masuala muhimu kama vile matumizi ya njia zisizo za ushindani, ukosefu wa uangalizi mzuri, na utendaji duni wa vitengo vya usimamizi wa ununuzi. Masuala haya yanazuia serikali kupata thamani bora ya fedha katika mchakato wa ununuzi wa umma.

## 6.1 Ununuzi Uliofanywa Nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kielekitroni Sh. bilioni 31.81

Kanuni ya 342(1) (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi kutekeleza ununuzi ya kielekitroni ndani ya mfumo wa ununuzi wa umma. Aidha, tarehe 23 Julai 2023, Wizara ya Fedha ilitoa Waraka Na. 2 unaozitaka taasisi zinazofanya ununuzi kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Kielekitroni unaojulikana kama NeST, kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023.

Ukaguzi wangu wa miamala inayohusiana na ununuzi ulibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 88 zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 31.81 nje ya mfumo wa ununuzi ya kielekitroni kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na.20**

Kushindwa kutumia kwa ufanisi mfumo wa kielekroniki (NeST) kulitokana na sababu kadhaa ambazo ni watumiaji wengi hawakuwa wamepatiwa mafunzo kamili au hawakuwa na uzoefu wa kutosha na mfumo, hali ambayo ilisababisha makosa, kasoro na kutokuwa na ufanisi katika mchakato wa manunuzi; mfumo kukutana na changamoto za kiufundi mara kwa mara kama vile uwezo mdogo wa "sever" na muundo

usiofaa, jambo lililosababisha mfumo kutopatikana, hivyo kuzuia matumizi sahihi ya mfumo.

Utaratibu huu unakwenda kinyume na kanuni zilizotajwa hapo juu ambazo husababisha kushindwa kwa lengo serikali la kuboresha ufanisi, kuongeza kasi ya ununuzi na kupunguza vihatarishi. Pia, hali hiyo hukwamisha juhudi za kuboresha uwazi na haki katika ununuzi wa umma.

**Ninatoa wito kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa watumishi wa vitengo vya Ununuzi na TEHAMA wanapata mafunzo yanayofaa na ya mara kwa mara kuhusu mfumo wa ununuzi wa kielekitroni. Ustadi wao ni muhimu kwa uendeshaji mzuri wa mfumo. Pia, washirikiane na mamlaka husika kufanya mafunzo ya kina na uhamasishaji kwa wadau wote.**

**Aidha, ninaishauri serikali kuimarisha mafunzo ya watumiaji na kuhakikisha uboreshaji wa mara kwa mara wa uwezo na uboreshaji wa mfumo ili kuzuia kuelemewa na kazi kupita uwezo wake. Kuboresha uaminifu na utendaji wa mfumo kutahakikisha kuwapo kwa michakato ya ununuzi yenye ufanisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

## 6.2 Ununuzi Nje ya Mpango wa Ununuzi wa Mwaka Sh. bilioni 20.08

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuakisi mahitaji yao ya bidhaa, huduma na kazi kwa usahihi iwezekanavyo. Hii ni muhimu kwa ajili ya kuandaa mipango bora na bajeti sahihi ili kuhakikisha kuwa rasilimali zimetengwa ipasavyo kwa miradi na shughuli zijazo.

Mipango ya kila mwaka hujumuisha makadirio ya kifedha ambayo yanaelezea matumizi yanayotarajiwa kwa mwaka, yakiwiana na mpango kazi. Makadirio haya yanapaswa kutoa ufahamu wa kiasi cha fedha kinachotengwa kwa kila mradi au shughuli, na kuhakikisha kuwa mchakato wa ununuzi unawiana na upangaji wa kifedha wa taasisi.

Hata hivyo nilibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 11 na Sekretariati ya Mkoa moja zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 20.08 nje ya mipango yao ya mwaka ya ununuzi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 34**.

**Jedwali Na.34: Ununuzi nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka**

| Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Monduli | 1,107,500,000 | 7 | H/Mji Babati | 354,999,282 |
| 2 | H/W Ngorongoro | 2,105,169,844 | 8 | H/W Morogoro | 313,874,500 |
| 3 | H/W Kibiti | 71,285,702 | 9 | H/M Kahama | 1,252,200,000 |
| 4 | H/W Iringa | 184,251,083 | 10 | H/Mji Bariadi | 2,794,633,982 |
| 5 | H/W Kilolo | 11,492,980,952 | 11 | H/W Iramba | 194,779,900 |
| 6 | H/W Ruangwa | 40,952,980 | 12 | S/Mkoa Manyara | 171,408,995 |
| | | | | **Jumla** | **20,084,037,220** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na mpango wa manunuzi wa mwaka*

Hali hii ya taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI kutotumia ipasavyo mfumo wa udhibiti wa ndani uliopo pamoja na kushindwa kuhuisha mipango ya mwaka ya ununuzi kwa fedha zilizopokelewa nje ya bajeti iliyoidhinishwa ilisababisha ununuzi kufanyika nje ya mipango ya mwaka.

Ununuzi nje ya mipango na bajeti ya mwaka unaweza kusababisha matumizi yasiyopangwa na kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa.

**Ninapendekeza kuwa taasisi husika kuhakikisha shughuli zao za ununuzi zinaendana na mipango yao ya manunuzi ya kila mwaka iliyoidhinishwa na mipango hiyo hupaswa kuhuishwa kila mara inapopatikana fedha za ziada. Aidha, nashauri kufuatwa kwa mchakato wa upangaji wa bajeti ili kuhakikisha maamuzi ya manunuzi ni ya kweli, sahihi, na yenye uendelevu wa kifedha.**

## 6.3 Ununuzi Uliofanywa bila Zabuni Shindanishi Sh. Bilioni 6.99

Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka nukuu za bei zipatikane kutoka kwa wazabuni wasiopungua watatu.

Ukaguzi wangu wa ununuzi uliofanyika katika taasisi 26 ulibaini kuwa ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 6.99 ulifanywa bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 35.**

**Jedwali Na.35: Ununuzi yaliyofanywa bila nukuu za ushindani**

| Na | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | S/M Kigoma | 3,039,637,160 | 15 | H/M Kasulu | 81,089,404 |
| 2 | H/W Tunduru | 975,567,301 | 16 | H/W Kongwa | 80,242,160 |
| 3 | H/M Tarime | 329,222,455 | 17 | H/W Tarime | 79,297,500 |
| 4 | S/ Shinyanga | 313,271,422 | 18 | H/W Longido | 72,297,264 |
| 5 | H/W Geita | 299,616,632 | 19 | H/W Butiama | 68,390,000 |
| 6 | H/M Handeni | 295,778,800 | 20 | H/Mji Bunda | 64,756,250 |
| 7 | H/W Kishapu | 221,904,000 | 21 | H/W Mkinga | 46,307,190 |

| Na | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | S/M Manyara | 208,179,574 | 22 | H/W Liwale | 34,134,800 |
| 9 | H/W Shinyanga | 141,563,791 | 23 | H/M Mpanda | 10,878,944 |
| 10 | H/W Madaba | 135,110,640 | 24 | H/J Mwanza | 16,304,828 |
| 11 | H/M Temeke | 131,224,257 | 25 | H/W Korogwe | 22,430,920 |
| 12 | H/M Musoma | 117,816,384 | 26 | H/M Iringa | 6,071,545 |
| 13 | H/W Mufindi | 106,197,864 | **Jumla** | | **6,988,595,526** |
| 14 | H/W Ushetu | 91,304,441 | | | |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na viambatisho vyake*

Ununuzi usio na zabuni shindani unaweza kutokana na mambo kama vile shinikizo linalotokana na dharura za kukimbizana na wakati, uangalizi dhaifu, na upendeleo kwa wasambazaji wa ndani.

Kutofuatwa ipasavyo kwa sheria na taratibu za ununuzi kwa taasisi 26 kumesababisha taratibu za ununuzi zisizo na ushindani; hivyo kupunguza uwazi na haki kwa walengwa. Ukosefu huu wa ushindani hudhoofisha uaminifu wa umma na huongeza hatari ya rushwa, ujamaa au upendeleo, kwa kuwa maamuzi yanaweza kuathiriwa na maslahi ya kibinafsi badala ya vigezo vya lengo.

**Ninaishauri Serikali kupitia OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa taasisi zote zinazingatia kwa ukamilifu sheria na kanuni zinazohusika. Hii itasaidia kufikia thamani ya fedha katika ununuzi na kuweka mazingira ya haki na ya ushindani kwa wazabuni wote wanaotarajiwa.**

## 6.4 Utekelezaji wa chini ya kiwango wa mpango wa ununuzi wa mwaka kwa Sh. bilioni 29.06

Kifungu cha 49 cha Sheria ya Ununuzi wa umma, Sura ya 410 na Kanuni ya 69 ya Kanuni za Ununuzi wa umma za mwaka 2013 zinaitaka taasisi nunuzi kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka kwa njia ya kimantiki; na kwamba, uakisi wa ununuzi yake lazima uwe sahihi na unaotekelezeka.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi saba hazikuzingatia shughuli za ununuzi zilizopangwa na muda uliopangwa. Maelezo yapo kwenye **Jedwali Na. 36**.

**Jedwali Na.36:Taasisi za TAMISEMI zilizotekeleza mpango wa ununuzi chini ya kiwango**

| Na | Jina la Taasisi | Kiasi cha Makisio (Sh.) | Kiasi Kilichotekelezwa (Sh.) | Kiasi Kisichotekelezwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| | **Mamlaka Serikali za Mitaa** | | | |
| 1 | H/W Kilosa | 29,083,728,183 | 7,187,008,357 | 21,896,719,825 |
| 2 | H/W Mbogwe | 4,980,583,294 | 2,347,340,926 | 2,633,242,368 |
| 3 | H/W Kibiti | 602,600,000 | 0 | 602,600,000 |
| | **Jumla ndogo** | | | |
| | **Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa** | | | |
| 4 | S/M Njombe | 5,065,872,486 | 3,376,872,736 | 1,688,999,750 |
| | **Jumla ndogo** | | | |
| | | | | |
| 4 | LGTI | 630,412,856 | 0 | 630,412,856 |
| | **Jumla ndogo** | | | |
| | **Kampuni Tanzu** | | | |
| 6 | Arusha Meat Co. | 2,242,541,317 | 1,863,489,271 | 379,052,046 |
| 7 | DDC | 1,928,900,000 | 696,872,426 | 1,232,027,574 |
| | **Jumla ndogo** | | | |
| | **Jumla Kuu** | **44,534,638,136** | **15,471,583,716** | **29,063,054,419** |

***Chanzo:*** *Mpango wa mwaka wa ununuzi na hati za malipo*

Hali hii imechangiwa na ucheleweshaji wa kutolewa kwa bajeti ambayo inaathiri utekelezaji wa ununuzi uliopangwa kwa wakati. Aidha, kukosekana kwa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji wa kufuatilia maendeleo dhidi ya mpango wa ununuzi kunaweza kusababisha ucheleweshaji usiojulikana au mikengeuko; na hatimaye kusababisha vikwazo vya utekelezaji wa mradi, uzembe na mahitaji ya umma kutokidhiwa.

**Ninaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mipango ya ununuzi inazingatia ubashiri halisi na sahihi wa mahitaji ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi. Mpango wa ununuzi lazima ulingane na mpangokazi wa mwaka, bajeti, na makadirio, kwa kuzingatia mambo kama vile muda wa mradi na upatikanaji wa fedha.**

## 6.5 Ununuzi uliofanywa bila kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni Sh. bilioni 4.88

Kanuni za 55 (2), 163 (4), na 185 (1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 zinakataza taasisi kutoa zabuni isipokuwa kama tuzo hiyo imeidhinishwa na bodi ya zabuni inayohusika. Kanuni hizi kwa pamoja zinaweka ulinzi muhimu katika mfumo wa ununuzi wa umma kwa kuhitaji kwamba maamuzi yote kuhusu utoaji wa kandarasi yatasimamiwa na bodi ya zabuni inayofaa.

Kinyume na kanuni hizo tajwa, nilibaini kuwa taasisi 22 zilinunua bidhaa mbalimbali zenye thamani ya sh. bilioni 4.88 bila kupata kibali kutoka kwa bodi za zabuni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.37.**

**Jedwali Na.37: Ununuzi bila idhini ya bodi ya zabuni**

| Na | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Longido | 33,139,678 | 13 | H/W Maswa | 1,175,640,230 |
| 2 | H/M Temeke | 378,868,446 | 14 | H/W Ikungi | 104,513,110 |
| 3 | H/W Chamwino | 355,146,097 | 15 | H/W Ileje | 93,045,350 |
| 4 | H/W Mpwapwa | 252,376,760 | 16 | H/W Bumbuli | 163,559,279 |
| 5 | H/M Iringa | 21,380,620 | 17 | H/Mji Handeni | 79,074,250 |
| 6 | H/Mji Mafinga | 32,697,940 | 18 | H/W Kilindi | 218,651,267 |
| 7 | H/W Mpimbwe | 55,195,120 | 19 | H/W Mkinga | 358,918,251 |
| 8 | H/Mji Kasulu | 62,258,687 | | **Jumla ndogo** | **3,738,212,403** |
| 9 | H/W Uvinza | 132,284,106 | | **Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa** | |
| 10 | H/W Mtama | 17,330,000 | 20 | S/M Morogoro | 773,708,257 |
| 11 | H/M Morogoro | 49,146,120 | 21 | S/M Shinyanga | 297,759,300 |
| 12 | H/M Songea | 154,987,092 | 22 | S/M Iringa | 69,571,680 |
| | | | | **Jumla ndogo** | **1,141,039,237** |
| | | | | **Jumla kuu** | **4,879,251,640** |

*Chanzo: Hati za malipo na majalada ya bodi ya zabuni*

Aidha, Kanuni ya 166 (7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka manunuzi yote madogo (micro procurements) yaripotiwe kwenye bodi ya zabuni kila mwezi na mamlaka iliyokasimiwa kwa kutumia fomu ya kiutaratibu iliyotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Serikali(PPRA). Hii inahakikisha kwamba hata ununuzi mdogo, ambao huenda usipitie mchakato kamili wa zabuni, bado unasimamiwa na kuwajibika.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi 17 zilifanya ununuzi mdogo wenye thamani ya Sh. bilioni 2.42 bila kuripotiwa kwenye Bodi za Zabuni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 38**.

**Jedwali Na.38: Ununuzi mdogo usioripotiwa kwa Bodi za Zabuni**

| Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Moshi | 895,654,380 | 10 | H/W Mufindi | 56,321,580 |
| 2 | H/M Kigamboni | 271,371,682 | 11 | S/M Manyara | 56,315,608 |
| 3 | H/Mji Handeni | 227,800,000 | 12 | H/W Ukerewe | 52,537,997 |
| 4 | H/W Singida | 215,293,000 | 13 | H/W Kilosa | 42,108,250 |
| 5 | H/W Songea | 168,672,573 | 14 | H/W Nsimbo | 28,870,450 |
| 6 | H/Mji Njombe | 104,935,586 | 15 | H/Mji Korogwe | 25,686,000 |

| Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | H/W Kakonko | 95,419,700 | 16 | H/W Mpwapwa | 20,150,000 |
| 8 | H/W Mwanga | 77,164,172 | 17 | H/W Babati | 14,724,000 |
| 9 | H/W Bahi | 68,652,441 | | **Jumla** | **2,421,677,419** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na majalada ya bodi ya zabuni*

Kutokuwepo kwa mifumo ya mapitio ya kutosha na kutokuzingatia kanuni zilizowekwa kumepelekea kufanyika kwa manunuzi bila idhini ya Bodi husika ya Manunuzi, kunadhoofisha uadilifu wa mchakato wa manunuzi.

Manunuzi yaliyofanywa bila idhini ya Bodi za Manunuzi yanazuia bodi kutekeleza majukumu yao ya usimamizi, hivyo kuundaa mazingira hatarishi katika uwajibikaji, ubora, na thamani kwa fedha zinaweza kuathiriwa.

Aidha, kushindwa kuripoti manunuzi madogo kwa Bodi za Manunuzi, kumeongeza zaidi upungufu katika usimamizi. Masuala haya si tu yanakiuka mahitaji ya kisheria bali pia yanaanzisha fursa za kutokufanya kazi kwa ufanisi, usimamizi usiofaa, na matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa taasisi husika zinachukua hatua stahiki, ikiwa ni pamoja na kuongeza udhibiti wa usimamizi na mapitio ya taratibu ya ununuzi na miamala kwa wakati. Pia Serikali inapaswa kutekeleza kusimamia taratibu na kuzuia kufanya manunuzi bila kupitia Bodi za Zabuni.**

## 6.6 Mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa bila kukaguliwa na kupimwa ubora Sh. bilioni 3.07

Kanuni za 244(1) na 245 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 zinataka taasisi zinazopokea bidhaa kukagua bidhaa zilizopokelewa kutoka kwa wazabubi na kukubali iwapo tu zinakidhi masharti ya mkataba.

Hata hivyo, nilibaini kuwa taasisi 34 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 3.07 kutoka kwa wazabuni bila kufanyiwa uhakiki unaohitajika na kamati za ukaguzi na kupokea bidhaa. Orodha ya taasisi zilizoshindwa kukagua na kupima bidhaa zilizonunuliwa zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 39**.

**Jedwali Na.39: Bidhaa zilizopokelewa bila kukaguliwa**

| Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mpwapwa | 402,836,890 | 19 | H/W Newala | 53,122,747 |
| 2 | H/W Mufindi | 283,488,610 | 20 | S/M Shinyanga | 48,230,192 |
| 3 | H/Mji Ifakara | 197,490,090 | 21 | H/W Mkalama | 47,610,319 |
| 4 | H/W Muheza | 187,768,387 | 22 | H/W Madaba | 47,520,200 |
| 5 | H/W Rufiji | 160,817,422 | 23 | H/M Temeke | 41,242,143 |
| 6 | H/Jiji Tanga | 158,773,447 | 24 | S/M Geita | 36,513,450 |
| 7 | H/W Mlimba | 151,966,495 | 25 | H/W Kishapu | 30,090,000 |
| 8 | H/W Karatu | 146,000,000 | 26 | H/Mji Bunda | 28,890,890 |
| 9 | H/W Bariadi | 132,203,395 | 27 | H/W Mpanda | 28,785,194 |
| 10 | H/W Kongwa | 112,571,767 | 28 | S/M Manyara | 28,376,995 |
| 11 | H/M Musoma | 110,038,543 | 29 | H/W Kibondo | 24,326,323 |
| 12 | H/M Shinyanga | 92,869,601 | 30 | H/W Lushoto | 23,270,000 |
| 13 | H/W Tunduru | 84,105,686 | 31 | H/W Manyoni | 21,342,861 |
| 14 | H/M Kigamboni | 83,527,489 | 32 | H/W Itilima | 20,851,116 |
| 15 | H/W Meatu | 67,366,143 | 33 | H/W Bumbuli | 18,900,000 |
| 16 | H/W Korogwe | 63,470,798 | 34 | H/W Mbulu | 14,563,081 |
| 17 | H/W Mkuranga | 63,199,567 | | | |
| 18 | H/W Pangani | 56,552,668 | | **Jumla** | **3,068,682,509** |

**Chanzo: Hati za malipo za Halmashauri na viambatisho vyake**

Ukosefu wa usimamizi na uwajibikaji wa bidhaa zilizopokelewa ulitokana na kushindwa kukagua kwa kamati zinazohusika kama inavyotakiwa. Kutokufanya ukaguzi kabla ya kufanya malipo kunahatarisha ubora na uzingatiaji wa vipimo ambavyo vinaweza kusababisha ununuzi wa bidhaa zilizo chini ya kiwango na kupunguza ufanisi na thamani ya matumizi ya fedha za umma.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe taasisi husika zinazingatia sheria za ununuzi kwa kukagua ubora na idadi kwa bidhaa zilizonunuliwa kabla ya kupokea na kufanya malipo kwa wazabuni.**

## 6.7 Ununuzi wa bidhaa bila kubainisha vipimo sahihi vya mahitaji kwa wasambazaji yenye thamani ya Sh. bilioni 1.16

Kanuni ya 164 (2) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013) inataka barua ya mwaliko wa nukuu na viambatisho vyovyote iwe na maelezo kamili ya bidhaa, kazi au huduma zitakazonunuliwa; ikijumuisha sifa za kiufundi au ubora zinazohitajika, vipimo, miundo, mipango na michoro, inavyostahili. Pia, Aya ya 24.2 ya mwongozo wa kufanya kazi chini ya nguvukazi shirikishi wa mwaka 2020 kinataka vifaa

vya ujenzi vitakavyonunuliwa viendane na orodha ya mahitaji na maelezo yaliyotajwa yaliyoidhinishwa na meneja wa mradi.

Katika ukaguzi wangu wa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya miradi inayotekelezwa kupitia nguvukazi shirikishi, nilibaini kuwa ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 1.16 katika mamlaka za serikali za mitaa 17 ulifanyika bila kuwepo maelezo ya kiufundi. Ununuzi huo ulihusisha vifaa kwa ajili ya ufungaji wa mtandao wa eneo mzunguko (LAN), fremu za milango, vifaa vya jumla, marumaru, madirisha ya alumini, meza za ofisi na viti kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 40.**

**Jedwali Na.40: Halmashauri zilizo na vitu vilivyonunuliwa bila maelezo maalumu**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Longido | 8,724,610 | 10 | H/Mji Bariadi | 160,512,946 |
| 2 | H/W Mufindi | 153,619,538 | 11 | H/W Busega | 17,326,846 |
| 3 | H/W Siha | 49,740,610 | 12 | H/W Itigi | 16,641,000 |
| 4 | H/W Butiama | 30,400,000 | 13 | H/W Singida | 41,643,138 |
| 5 | H/W Ludewa | 127,300,984 | 14 | H/W Handeni | 77,050,441 |
| 6 | H/W Kalambo | 53,305,607 | 15 | H/W Kilindi | 67,397,000 |
| 7 | H/W Nkasi | 28,355,931 | 16 | H/W Muheza | 33,395,499 |
| 8 | H/W Mbinga | 226,100,000 | 17 | H/W Pangani | 36,839,220 |
| 9 | H/M Kahama | 27,776,968 | | **Jumla** | **1,156,130,338** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo za Halmashauri pamoja na viambatisho vyake*

Tathmini ya jumla ilionesha kuwa kulikuwa na ushirikiano hafifu kati ya watumishi wa kitengo cha usimamizi wa ununuzi na idara za watumiaji katika kubainisha vipimo vya kujumuishwa katika nyaraka za nukuu. Kutokuwepo bayana kwa vipimo kwenda kwa mzabuni inaweza kupelekea bei iliyolipwa isilingane na ubora wa bidhaa, vile vile bidhaa zilizopokelewa huenda zisiendane na mahitaji ya mtumiaji.

**Ninapendekeza uboreshaji wa ufuatiliaji na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa maafisa masuuli wanazingatia kanuni za ununuzi kwa kuzingatia maelezo ya kiufundi. Hii itasaidia, kuzuia kupokea bidhaa zisizo na ubora, kuepuka gharama zisizo za lazima, na kuhakikisha thamani ya fedha inakuwepo.**

## 6.8 Ununuzi ya vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji ya mradi Sh. milioni 586.82

Aya ya 11.1 ya mwongozo wa kufanya kazi kwa kutumia nguvukazi shirikishi kwa taasisi nunuzi za nchini Tanzania iliyotolewa na Mamlaka

ya Usimamizi wa Manunuzi ya Serikali(PPRA) inahitaji idara ya mtumiaji au idara ya kiufundi kuelezea kazi za ujenzi au matengenezo zinazohitajika kutekelezwa. Pia, Aya ya 24.2 ya Mwongozo huo huo inahitaji vifaa vya ujenzi kununuliwa kwa kuzingatia mahitaji yaliyoainishwa katika orodha ya vifaa vya ujenzi na viwango vilivyoidhinishwa na meneja wa mradi.

Katika tathmini yangu ya ununuzi na uhakiki wa utekelezaji wa mradi, nilibaini kuwa taasisi sita zilinunua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh. milioni 586.82 zaidi ya kiasi kinachohitajika kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na.41** hapa chini.

**Jedwali Na.41: Taasisi zenye Ununuzi ya Vifaa vya Ujenzi Zaidi ya mahitaji**

| Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dodoma | 209,577,356 |
| 2 | H/W Mbinga | 128,592,468 |
| 3 | H/W Nzega | 83,498,800 |
| 4 | S/M Manyara | 60,180,000 |
| 5 | H/W Chunya | 55,372,600 |
| 6 | H/W Lindi | 49,596,167 |
| **Jumla** | | **586,817,391** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na mahitaji yaliyoainishwa katika orodha ya vifaa vya ujenzi*

Tathmini yangu ilibaini kuwa baadhi ya vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa vilibaki kwenye stoo za taasisi tajwa hapo juu bila kutumika. Suala hili liliibuka kutokana na makadirio yasiyo ya kweli katika miundo wa mradi na michoro. Makadirio hayo hayakuambatana na mahitaji halisi kulingana na mchoro wa mradi.

Ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji halisi ya miradi hiyo unaweza kutumiwa vibaya au kutumika kwa manufaa ya kibinafsi. Aidha, vifaa vilivyohifadhiwa kwenye stoo kwa muda mrefu vinaweza kuharibika na hatimaye kutotumika, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

**Ninahimiza Serikali kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa taasisi husika zinaandaa orodha sahihi ya mahitaji ya vifaa vya ujenzi ili kuzuia manunuzi ya vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji. Aidha, taasisi husika zinahimizwa kuhakikisha matumizi bora na madhubuti ya vifaa vyovyote vya ujenzi vya ziada.**

## 6.9 Ununuzi uliofanywa kabla ya kutoa hati ya agizo la ununuzi wa ndani Sh. bilioni 1.20

Kanuni ya 233(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 75 (a)(1) ya Kanuni za Ununuzi wa umma(Iliyorekebishwa) ya mwaka 2016 inataka pale zabuni

inapokubaliwa na afisa masuuli husika, taasisi ya ununuzi na mtu ambaye zabuni yake inakubaliwa kuingia katika mkataba wa ugavi wa bidhaa au huduma ndani ya siku 14 za kazi, baada ya kutimiza masharti yote kabla ya kusainiwa kwa mkataba. Pia, Agizo Na. 69(1) la LGFM la mwaka 2009 linahitaji bidhaa, vifaa, huduma au vifaa vyote kwa ajili ya kufanya kazi vilivyotekelezwa kwa wakala kuagizwa au kuthibitishwa kwa maandishi na Agizo rasmi la Ununuzi wa Ndani (LPO).

Ukaguzi wangu wa ununuzi uliofanywa katika mamlaka za serikali za mitaa 12 na Sekretarieti za Mikoa mbili ulibaini kuwa Sh. bilioni 1.20 zililipwa kwa wazabuni wa bidhaa na huduma bila kutoa maagizo ya mkataba wa ununuzi wa ndani(LPO) kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 42**.

**Jedwali Na.42: Ununuzi Yanayofanywa bila LPOs**

| Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mbinga | 334,406,254 | 9 | H/M Mpanda | 29,687,348 |
| 2 | H/W Tarime | 304,257,890 | 10 | S/M Morogoro | 28,332,910 |
| 3 | H/W Handeni | 110,162,394 | 11 | S/M Katavi | 22,693,854 |
| 4 | H/W Nanyumbu | 89,790,080 | 12 | H/W Nsimbo | 14,913,640 |
| 5 | H/W Meatu | 72,396,330 | 13 | H/W Itilima | 14,179,694 |
| 6 | H/W Mpimbwe | 67,321,123 | 14 | H/W Pangani | 13,652,081 |
| 7 | H/W Mlele | 57,373,592 | | | |
| 8 | H/W Bariadi | 36,361,820 | | **Jumla** | **1,195,529,010** |

**Chanzo: Hati za malipo**

Upangaji na usimamizi usiofaa katika michakato ya ununuzi umesababisha kushindwa kuhakikisha kuwa nyaraka za maagizo ya ununuzi wa ndani (LPOs) zinatolewa kabla ya kununua bidhaa na huduma. Kununua bila LPO kunaweza kusababisha hasara kubwa endapo kutakuwa na ukiukaji wa mkataba, kwani hakutakuwa na makubaliano ya kisheria kati ya wahusika.

**Ninapendekeza kwamba Serikali isimamie uzingatiaji wa kanuni za ununuzi zinazofanywa na mamlaka za serikali za mitaa na sekretarieti za mikoa na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wanaohusika na kutozingania sheria na kanuni za manunuzi.**

## 6.10 Malipo ya Ununuzi wa Bidhaa kabla Hazijapokelewa Sh. bilioni 1.25

Kanuni ya 242(1) ya Kanuni zaa Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 iinataka taasisi nunuzi kupata taarifa za kupokelewa kwa bidhaa kwa mujibu wa mikataba kisha itaidhinisha malipo kwa mzabuni kwa wakati.

Kinyume na Kanuni hapo juu, nilibaini uwepo wa malipo ambayo yalifanywa kabla ya kupokea bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 1.25 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa sita na Sekretarieti ya Mkoa moja, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 43.

**Jedwali Na.43: Taasisi zilizofanya Malipo Kabla ya Kupokea Bidhaa**

| Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Chato | 708,850,620 |
| 2 | H/W Mpwapwa | 178,864,406 |
| 3 | S/M Morogoro | 169,216,255 |
| 4 | H/Mji Masasi | 116,490,000 |
| 5 | H/W Makete | 33,478,318 |
| 6 | H/M Ifakara | 20,253,600 |
| 7 | H/W Musoma | 20,157,000 |
| **Jumla** | | **1,247,310,199** |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na notisi ya kupokelea bidhaa*

Malipo kufanyika kabla ya kupokea bidhaa huchangiwa na udhibiti duni wa ndani wa ununuzi na mchakato wa malipo pamoja na usimamizi duni wa menejimenti. Malipo kwa wazabuni kabla ya kupokea bidhaa huziweka taasisi husika katika hatari ya upotevu wa fedha iwapo wazabuni watashindwa kuleta bidhaa. Aidha, ikiwa bidhaa zilizopokelewa hazikidhi viwango au kuwa na kasoro, taasisi nunuzi inaweza kupata ugumu wa kurejeshewa fedha au kubadilishiwa bidhaa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali iwatake maafisa masuuli kuidhinisha malipo ya bidhaa baada ya kupokea bidhaa, kukaguliwa na kukubalika.**

## 6.11 Mikataba ya thamani ya Sh. bilioni 5.38 iliyosainiwa na kutekelezwa bila kuhakikiwa

Kanuni za 59(2) na (5), na 60 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 2 na 3 kwa mtiririko huo wa Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 121/2016) zinasisitiza kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ahakiki mkataba rasmi ambao thamani yake ni ya shilingi bilioni moja unafanywa kupitia zabuni za ushindani wa kimataifa. Pia, maafisa wa sheria wa taasisi nunuzi wanatakiwa kuhakiki mkataba ambao thamani yake ni chini ya shilingi bilioni moja kabla ya kusainiwa na wahusika.

Aidha, Kanuni ya 59(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 iliyofanyiwa marekebisho na Kanuni ya 2 ya Kanuni za Ununuzi wa umma ya mwaka 2016 inaeleza kuwa mikataba ambayo haijapitiwa na kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali inachukuliwa kuwa ni batili.

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa mikataba ulibaini kuwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa 18 na Sekretarieti ya Mkoa moja zilisaini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 5.38 bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au maafisa wa sheria wa taasisi husika. Rejelea maelezo katika **Jedwali Na. 44**.

**Jedwali Na.44: Orodha ya mikataba ambayo haijahakikiwa**

| Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kaliua | 2,600,864,000 | 11 | H/W Mufindi | 83,000,000 |
| 2 | S/M Morogoro | 480,407,018 | 12 | H/W Mtama | 76,835,000 |
| 3 | H/W Ulanga | 339,030,000 | 13 | H/W Korogwe | 74,350,000 |
| 4 | H/M Tabora | 314,633,882 | 14 | H/W Karatu | 63,050,000 |
| 5 | H/M Lindi | 286,117,851 | 15 | H/W Biharamulo | 58,202,000 |
| 6 | H/M Temeke | 212,302,660 | 16 | H/W Mkinga | 45,850,000 |
| 7 | H/W Namtumbo | 203,725,600 | 17 | H/W Masasi | 41,411,000 |
| 8 | H/W Morogoro | 173,870,900 | 18 | H/W Kisarawe | 35,083,857 |
| 9 | H/M Kigamboni | 164,545,000 | 19 | H/W Bumbuli | 33,735,100 |
| 10 | H/W Babati | 96,120,000 | | **Jumla** | **5,383,133,868** |

*Chanzo: Majalada ya mikataba*

Kushindwa kuzingatia matakwa ya kisheria inadhoofisha uadilifu wa mchakato wa usimamizi wa mikataba, na kuziweka taasisi kwenye hatari zinazoweza kutokea za kisheria, ikiwa ni pamoja na kubatilishwa kwa mikataba hii. Ukosefu wa mapitio sahihi ya kisheria huhatarisha ulinzi wa maslahi ya umma na huongeza uwezekano wa migogoro au kutozingatia matakwa ya kimkataba.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ichukue hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa taasisi husika zinazingatia sheria za ununuzi na kubuni upya taratibu za ufuatiliaji zitakazohakikisha kuwa sheria za ununuzi zinafuatwa.**

## 6.12 Manunuzi Yaliyocheleweshwa na Kutotekelezwa kwa Mkataba wa Makubaliano (MOU) Kutokana na OR-TAMISEMI Kutofanya Malipo Sh. bilioni 17.20 bilioni

Kanuni ya 69 (3) ya Sheria ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuakisi kwa usahihi mahitaji yao ya bidhaa, huduma na kazi, hasa kwa shughuli ambazo tayari zimepangwa katika mpangokazi wa mwaka na makadirio. Aidha, Kanuni ya 69(4) inahitaji makisio yawe na tathmini ya muda muafaka wa utekelezaji na kumalizika kwa huduma, na muda huo kuwekwa kwa mwezi unaokaribia.

Mchakato wa ununuzi wa vitabu na miongozo ya walimu wenye thamani ya sh. bilioni 17.20 kwa ajili ya elimu ya awali, msingi na sekondari chini ya OR-TAMISEMI ulikabiliwa na ucheleweshaji mkubwa. Ingawa makubaliano(MOU) na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) yalitiwa saini tarehe 15 Aprili 2024 kwa ajili ya kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Aprili hadi 30 Agosti 2024, mchakato huo ulicheleweshwa kwa miezi minne toka mpango wa awali wa ununuzi uliowekwa mwezi Januari 2024.

Licha ya kupokea fedha tarehe 6 Desemba 2023, OR-TAMISEMI ilishughulikia malipo tarehe 8 Aprili 2024, lakini haikufanikiwa kuhamishiwa kwa mtoa huduma kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha, na kusababisha kughairi. Wizara ya Fedha iliombwa kuhamisha fedha hizo kwenye Akaunti ya Amana, lakini badala yake zilirejeshwa Hazina. Kufikia tarehe 10 Oktoba 2024, mtoa huduma alikuwa hajapokea malipo, na hivyo kushindwa kutekeleza mkataba.

Kushindwa kusambaza vitabu vya kiada na miongozo ya walimu kutokana na kutolipwa kwa mtoa huduma huleta matokeo yafuatayo: hutatiza ujifunzaji wa wanafunzi, haswa katika masomo ya msingi; huzuia uwezo wa walimu wa kutoa elimu kwa ufanisi; huharibu sifa na uhusiano wa OR-TAMISEMI na watoa huduma na wadau; na huweza kusababisha migogoro ya kisheria na adhabu za kifedha.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe taratibu za ununuzi zinakamilika mara moja na malipo yafanyike mara moja baada ya kupokea fedha ili kuepusha ucheleweshaji wa malipo kwa siku zijazo. Aidha, ni muhimu kupata fedha zinazohitajika ili kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati kwa mtoa huduma.**

## 6.13 Malipo yanayofanyika bila kuchukua vipimo wala kuthibitishwa na wasimamizi wa miradi Sh. bilioni 1.19

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba; na kwamba, asilimia kadhaa ya thamani ya kazi zilizotekelezwa kutoka kila cheti cha malipo inaweza kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matazamio hadi mkataba utakapohitimishwa.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa taasisi 14 zililipa kiasi cha Sh. bilioni 1.19 kwa mafundi wataalam(Local Fundi) bila kuwapo kwa nyaraka za vipimo vya kazi zilizofanyika kuhusiana na miradi ya ujenzi ili kuhalalisha wingi wa kazi zilizotekelezwa, kama inavyooneeshwa kwenye **Jedwali Na.45** hapa chini.

**Jedwali Na.45: Malipo bila Kipimo na Uidhinishaji wa Mhandisi**

| Na | Jina la Halmashauri/Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri/ Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | S/M Lindi | 345,595,026 | 8 | H/W Rorya | 48,424,000 |
| 2 | H/W Mbozi | 156,619,600 | 9 | H/M Mpanda | 47,305,170 |
| 3 | H/W Bariadi | 132,924,972 | 10 | H/W Itilima | 40,564,050 |
| 4 | H/Mji Mbulu | 105,744,492 | 11 | H/W Meatu | 37,654,470 |
| 5 | S/M Shinyanga | 79,701,774 | 12 | H/W Mkuranga | 31,258,063 |
| 6 | H/W Gairo | 72,844,000 | 13 | H/Mji Bariadi | 16,721,000 |
| 7 | H/W Rungwe | 65,073,985 | 14 | H/W Handeni | 9,624,795 |
| | | | | **Jumla** | **1,190,055,397** |

***Chanzo:*** Hati na vyeti vya malipo

Malipo yanayofanywa bila kupima kiasi na bila kuthibitishwa na wasimamizi wa mradi kwa mafundi wataalam(Local Fundi) yanaweza kusababishwa na: uangalizi usiofaa, ukosefu wa utaratibu mzuri wa ufuatiliaji, na kutofuatwa ipasavyo kwa taratibu zilizowekwa za ununuzi na usimamizi wa mradi.

Hii inaweza kusababishwa na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani, ukosefu wa mafunzo ya kutosha kwa wafanyakazi, au kushindwa kutekeleza matakwa ya kisheria, hatimaye kupelekea malipo yasiyofaa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Kidhihirisha malipo bila kukagua na kupima kazi zilizotekelezwa kunaweza kusababisha malipo ya ziada au malipo ya kazi ambazo hazikutekelezwa, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe taasisi husika zinapatiwa wahandisi wa kutosha watakao kuwa wanafanya tathmini ya kazi zilizokamilika, na maafisa masuuli wahakikishe kazi zinathibitishwa kabla ya malipo kufanyika.**

## 6.14 Kutojumuishwa kwa Ununuzi ya Ngazi ya Chini Katika Ripoti za Ununuzi za Robo Mwaka Zenye Thamani ya Sh. Bilioni 25.23

Kifungu cha 38(0) cha Sheria ya Ununuzi wa umma Sura ya 410, kinataka Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kuandaa taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa mwaka na kuwasilisha kwenye vikao vya utawala.

Aidha, Kanuni ya 87 (2) (c) na (d) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi nunuzi kuandaa taarifa za utekelezaji wa ununuzi ya kila mwezi na robo mwaka na kuwasilisha kwa mamlaka ndani ya siku saba baada ya kumalizika kwa mwezi au robo na taarifa

za utekelezaji wa ununuzi ya mwaka husika ndani ya siku thelathini baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha husika.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa ripoti za robo mwaka Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 hazikujumuisha taarifa za manunuzi katika ngazi  za chini. Manunuzi haya yalihusisha vifaa huduma na kazi zenye thamani ya Sh. bilioni 25.23, kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 46**. Hivyo basi, ununuzi kama huu, kwa kawaida, hutarajiwa kuripotiwa katika ripoti hizi za robo mwaka kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji.

**Jedwali Na.46: Kutojumuishwa kwa ununuzi wa ngazi za chini katika ripoti za robo mwaka**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Kaliua | 11,570,019,169 |
| 2 | H/W Mufindi | 7,100,756,412 |
| 3 | H/W Nkasi | 3,492,698,536 |
| 4 | H/W Kibiti | 949,873,872 |
| 5 | H/M Morogoro | 790,409,126 |
| 6 | H/W Gairo | 685,019,542 |
| 7 | H/W Bagamoyo | 502,424,393 |
| 8 | H/W Bumbuli | 79,013,525 |
| 9 | H/W Mkuranga | 53,275,990 |
| 10 | H/W Lushoto | 7,516,920 |
| | **Jumla** | **25,231,007,485** |

***Chanzo:*** Taarifa za ununuzi za Halmashauri za kila robo

Kutojumuishwa kwa ununuzi ya ngazi cha chini ya kiutendaji kunachangiwa na ufuatiliaji duni wa taarifa za ununuzi kutoka ngazi ya chini na vitengo vya ununuzi kwa ajili ya kuunganishwa kwa ripoti ya robo mwaka iliyowasilishwa kwa kamati ya fedha na baraza la Madiwani.

Maoni yangu ni kwamba, kutokuwapo kwa taarifa hizi muhimu za fedha kunaweza kusababisha kuwapo kwa pengo katika uwekaji wa kumbukumbu au taratibu sahihi za utoaji taarifa ndani ya halmashauri hizi. Thamani ya ununuzi huu, uliojumuisha vifaa vya ujenzi, huduma za kandarasi, na kazi mbalimbali, ilipaswa kuwa wazi ili kutoa picha kamili ya shughuli za kifedha na kuhakikisha uangalizi mzuri.

**Ninapendekeza kwamba mamlaka za serikali za mitaa husika zijumuishe taarifa za ununuzi za ngazi ya chini kwa kila robo mwaka na kuwasilisha kwenye vikao vya menejimenti na kwa mamlaka husika kila mwezi na robo mwaka ili kuhakikisha uwajibikaji na thamani ya fedha. Pia, wanapaswa kuimarisha udhibiti kwa kufanya**

**usuluhishi wa kila wiki na mwezi ili kuhakikisha taarifa sahihi za robo mwaka zinatayarishwa na kutolewa.**

## 6.15 Matumizi Yasiyotosheleza ya Njia za Ununuzi kwa Mikataba Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 15.61

Kanuni ya 152 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 kama ilivyorekebishwa na kanuni ya 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (marekebisho), 2016 (G.N. Namba 333/2016), taasisi nunuzi ina mamlaka ya kutumia busara katika kizuizi cha kutoa hati za zabuni kwa wachaguliwa wachache tu, ikiwa wamethibitishwa awali; bidhaa, kazi, au huduma zinazohitajika ni maalum na zinapatikana kutoka vyanzo vichache; kuna hitaji la dharura la bidhaa au huduma ambazo haziruhusu muda wa zabuni wazi, au dharura hiyo haikuweza kutarajiwa na haikusababishwa na ucheleweshaji wa taasisi husika, au lengo ni kufikia malengo ya kijamii kwa kushirikisha jamii za mitaani, vikundi maalum, au mashirika.

Ukaguzi wangu wa mikataba katika mikoa ya Morogoro, Rukwa, na Singida ulibainisha kuwa TARURA ilitoa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 5.14 kwa kutumia njia ya ukomo wa zabuni bila uhalali. Katika Mkoa wa Morogoro, njia ya zabuni ya chanzo kimoja zilitumika kwa zabuni 14 zenye thamani ya Sh. bilioni 2.63. Katika Mkoa wa Rukwa, mkataba No. S10/019/2023/2024/W/66 wenye thamani ya Sh.milioni 348.03 ulitolewa kwa njia ya ukomo wa zabuni. Vilevile, katika Mkoa wa Singida, zabuni kwa njia ya ukomo ilitumika kwa mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 2.15. Licha ya uongozi kudai dharura, hakukuwa na nyaraka zinazothibitisha dai hili. Miradi hii haikuwa na dharura wala utaalamu maalum, na hivyo kuibua wasiwasi kuhusu uhalali wa kupuuziliwa mbali kwa njia za manunuzi za ushindani. Maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye **Jedwali 47** na **Kiambatisho Na.21**

**Jedwali Na.47: Mikataba iliyotolewa kwa kikwazo na TARURA Mkoa wa Singida pasipo uhalali**

| Na | Namba ya Mkataba | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | S10/023/2023/2024/W/92 | 291,113,000 |
| 2 | S10/023/2023/2024/W/96 | 290,914,500 |
| 3 | S10/023/2023/2024/W/94 | 396,290,000 |
| 4 | S10/023/2023/2024/W/105 | 211,675,875 |
| 5 | S10/023/2023/2024/W/106 | 963,157,200 |
| | **Jumla** | **2,153,150,575** |

***Chanzo:*** Daftari la Mikataba la TARURA Mkoa wa Singida

Audha, Kanuni ya 161 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inakataza taasisi nunuzi kutumia njia ya chanzo kimoja cha ununuzi bila uhalali wa kutosha wa mradi unaotekelezwa ili kuepusha ushindani wa zabuni.

Kinyume chake, katika mapitio ya mchakato wa ununuzi, nilibaini kuwa Ofisi za TARURA katika mikoa ya Njombe, Kagera na Tanga zilitumia njia moja ya utoaji zabuni kwenye ununuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 10.47 bila kuzingatia matakwa ya kanuni iliyotajwa hapo juu. Zabuni husika zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 48** na **49** na **Kiambatisho Na.22**

**Jedwali Na.48: Mikataba ambayo chanzo kimoja na utoaji wa zabuni uliozuiliwa ulitumika**

| Na | Namba ya Mkataba | Kiasi cha Mkataba (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | S10/017/2023/2024/W/83 | 150,000,000 |
| 2. | S10/017/2023/2024/W/94 | 200,000,000 |
| 3. | S10/017/2023/2024/W/101 | 499,782,197 |
| 4. | S10/017/2023/2024/W/80 | 77,650,000 |
| 5. | S10/017/2023/2024/W/81 | 400,000,000 |
| 6. | S10/017/2023/2024/W/100 | 597,209,700 |
| | **Jumla** | **1,924,641,897** |

***Chanzo:*** Rejesta ya Mikataba wa TARURA Mkoa wa Njombe

**Jedwali Na.49: Kandarasi nyingi kwa Mzabuni mmoja kabla ya kukabidhi kandarasi nyingine kupitia njia ya chanzo kimoja**

| Na. | Namba ya Mkataba | Kiasi cha Mkataba (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | S10/006/2023/2024/W/09 | 849,235,120 |
| 2 | S10/006/2023/2024/W/157 | 371,304,000 |
| 3 | S10/006/2023/2024/W/31 | 500,879,000 |
| 4 | S10/006/2023/2024/W/26 | 939,643,632 |
| 5 | S10/006/2023/2024/W/129 | 1,541,196,750 |
| | **Jumla** | **4,202,258,502** |

***Chanzo:*** Daftari la Mikataba la TARURA Mkoa wa Kagera

Utumiaji usio na msingi wa mbinu za kuchagua chanzo kimoja bila ushindani na wenye vikwazo kwenye ununuzi unaonesha pengo katika usimamizi wa TARURA kuhusu uelewa wa kina wa kanuni za ununuzi na uzingatiaji wa usimamizi.

Hali hii inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uwazi, kupungua kwa ushindani, upendeleo, na kupuuzwa kwa uadilifu katika mchakato wa ununuzi. Hii inaweza kusababisha kutokuwa na ufanisi, gharama kubwa, na ukosefu wa uwajibikaji. Zaidi ya hayo, inaweza kuhatarisha shirika katika hatari za kisheria, ikiwa ni pamoja na changamoto za maamuzi ya ununuzi, ufisadi unaoweza kutokea, na uharibifu wa sifa ya Taasisi.

**Nashauri kwamba Menejimenti ya TARURA iboreshe Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi (PMU) na kuboresha mifumo ya uangalizi, ambayo ni muhimu katika kuhakikisha uwazi na uzingatiaji wa sheria katika manunuzi.**

## 6.16 Upungufu Katika Uhakiki wa Kisheria na Utiaji Saini wa Mikataba Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 7.35

Kanuni 59 na 60 za Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013, kama ilivyorekebishwa na kanuni 2 na 3 za Kanuni za Manunuzi ya Umma (Iliyorekebishwa), ya mwaka 2016 (GN. Namba 121/2016) zinahitaji mkataba wowote rasmi kukaguliwa kabla ya kusainiwa. Mikataba iliyo chini ya shilingi bilioni moja lazima ipitiwe upya na afisa sheria, huku ile yenye thamani ya shilingi bilioni moja au zaidi ikihitaji kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Afisa sheria lazima pia atoe maoni kwa ajili ya kujumuishwa na afisa masuuli kabla ya mikataba kusainiwa.

Mapitio yangu ya usimamizi wa mikataba katika TARURA yalibaini kuwa maoni ya uhakiki wa mikataba kutoka kwa maafisa wa sheria hayakuingizwa kikamilifu katika mikataba mingi katika mikoa ya Singida na Mtwara, ambayo ni jumla ya thamani ya sh. bilioni 6.30. Baadhi ya upungufu uliobainika ni: vifungu visivyokamilika, vyeti vinavyokosekana, na kutozingatia miundo ya kisheria, kama vile kuachwa kwa mahali pa kuapisha. Rejelea maelezo katika **Kiambatisho Na.23.**

Aidha, kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu, katika TARURA Mkoa wa Tanga, nilibaini kuwapo kwa mkataba Na. S10/026/2023/2024/W/56 wenye thamani ya Sh. bilioni 1.05 kwa ajili ya matengenezo na uboreshaji wa barabara muhimu katika mkoa wa Tanga ulisaniwa bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Usimamizi usiojitosheleza wa mikataba ikiwa ni pamoja na utekelezaji hafifu wa mahitaji ya uhakiki na kutotii masharti ya kisheria, pamoja na upungufu wa mfumo na ukosefu wa ufahamu wa kutumia mfumo wa NeST, ulisababisha upungufu katika utayarishaji wa mkataba na kuachwa kwa hati na miundo muhimu.

Kushindwa kuzingatia matakwa ya kisheria inadhoofisha uadilifu wa mchakato wa usimamizi wa kandarasi. Aidha, huweka taasisi kwenye hatari zinazoweza kutokea za kisheria, ikiwa ni pamoja na kubatilishwa kwa mikataba hii. Ukosefu wa mapitio sahihi ya kisheria huhatarisha ulinzi wa maslahi ya umma. Pia, huongeza uwezekano wa migogoro au kutozingatia majukumu ya kimkataba.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI ichukue hatua stahiki ili kuhakikisha kuwa TARURA inazingatia sheria za ununuzi na kubuni upya taratibu za ufuatiliaji zitakazohakikisha kuwa sheria za ununuzi**

**zinafuatwa, ikiwa ni pamoja na kuzingatia maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au afisa sheria katika mikataba kabla ya kusainiwa.**

## 6.17 Ucheleweshaji wa Malipo ya Madai ya Vyeti vya Wakandarasi Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 40.37

Kanuni 44(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inasema kwamba, kwa madhumuni ya kusaidia ukuaji wa kampuni za ndani na kuwapa kampuni hizo uwezo wa kutimiza majukumu yao ya mkataba, taasisi zinazofanya manunuzi zitahakikisha kwamba malipo yanafanywa kwa wakati kwa watoa zabuni. Pia, Kipengele cha 53.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba ya Hati za Zabuni za Kawaida kinataka waajiri kulipa wakandarasi kiasi kilichothibitishwa na meneja wa mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila cheti.

Mapitio yangu ya hati za malipo za TARURA na nyaraka zinazohusiana yalionesha ucheleweshaji katika kulipa wakandarasi kwa kazi zilizoidhinishwa zenye thamani ya Sh. bilioni 21.92. Ucheleweshaji huo ulikuwa kati ya siku 38 hadi 521, kinyume na masharti ya mkataba. Pia, nilibaini vyeti vyenye thamani ya Sh bilioni 14.03 ambavyo havijalipwa kwa kipindi cha siku 46 hadi 434 hadi tarehe ya ukaguzi. Maelezo zaidi yanaoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.24 na 25.**

Aidha, nilibaini Mamlaka nne za Serikali za Mitaa na Sekretariati ya Mkoa mmoja zikiwa na madai ya wakandarasi yasiyolipwa ya Sh. bilioni 4.42, kwa kipindi cha siku 49 hadi 294 tangu tarehe madai hayo yalipopitishwa. Maelezo zaidi yanaonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 50.**

**Jedwali Na.50:Taasisi zilichelewesha malipo kwa kazi zilizotekelezwa na wakandarasi**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Idadi ya siku zilizochelewa |
|---|---|---|---|
| 1 | H/M Nzega | 2,109,367,036 | 49 hadi 294 |
| 2 | H/M Tarime | 1,175,500,703 | 125 |
| 3 | S/M Rukwa | 525,615,228 | 180 |
| 4 | H/M Geita | 377,719,579 | 125 |
| 5 | H/W Mtama | 227,967,272 | 210 |
| | **Jumla** | **4,416,169,818** | |

***Chanzo:*** *Hati za malipo na vyeti vya malipo*

Ucheleweshaji wa malipo kwa madai ya wakandarasi kwa kiasi kikubwa ulisababishwa na kushindwa kwa Hazina kutoa fedha kwa taasisi husika.

Ucheleweshaji huu unaweza kudhuru uthabiti wa kifedha wa wakandarasi, kuathiri ratiba za utekelezaji wa miradi, na hata kuzuia zabuni zijazo kutokana na wasiwasi kuhusu uaminifu wa malipo. Aidha, ucheleweshaji wa malipo unaweza kusababisha adhabu au malipo ya

riba, na hivyo kuongeza gharama kwa Serikali na kudhoofisha uaminifu wa mfumo wa manunuzi.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha wahakikishe fedha za miradi zinatolewa kwa wakati. Hii itasaidia utekelezaji mzuri wa miradi hiyo na kuepusha riba na adhabu zisizo za lazima.**

07




# SURA YA SABA

## Tathmini ya Utawala Bora na Usimamizi wa Vihatarishi

## 7.0 Utangulizi

Utawala bora wenye ufanisi huhakikisha maamuzi sahihi, uwajibikaji na mikakati elekezi, wakati mbinu za usimamizi wa vihatarishi, hutambua, kutathmini na kupunguza madhara. Kwa pamoja, vinaunda mfumo imara unaowezesha taasisi kufanikisha malengo yake kwa ufanisi

Muongozo wa Wizara ya Fedha (uliorekebishwa Julai 2023) kwa ajili ya kuandaa na kutekeleza mfumo wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi na usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu katika taasisi za umma unazitaka taasisi zote za sekta ya umma kuandaa, kutekeleza na kuendelea kuboresha mfumo wa usimamizi wa vihatarishi na vihatarishi vya ubadhirifu.

Taasisi hizi zinapaswa kuandaa mchakato wa kufuatilia, kukagua, kuripoti, na kuboresha mbinu za usimamizi wa vihatarishi vya Ubadhirifu. Zaidi ya hayo, zinatakiwa kudumisha mifumo ya utawala inayojumuisha sheria, taratibu, na miundo inayoongoza mwelekeo, usimamizi, na uangalizi wa shughuli zao.

Tathmini ya mfumo wa utawala, udhibiti wa ndani, na usimamizi wa vihatarishi imebaini maeneo kadhaa yanayohitaji kutiliwa mkazo ili kuimarisha utawala bora miongoni mwa wale waliokabidhiwa majukumu kama ilivyoorodheshwa hapa chini:

## 7.1 Utendaji Usioridhisha na Mgao wa Rasilimali kwa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Kanuni ya 33 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 inaelezea ukaguzi wa ndani kama kitengo muhimu kwa ajili ya kupitia na kutathmini ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani katika taasisi, pamoja na kufanya ukaguzi wa kiutendaji na tathmini ya thamani ya fedha, ili kuhakikisha kuwapo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani na mifumo ya kihasibu

Nilikagua utendaji kazi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na kubaini upungufu ufuatao:

i. Kwa mwaka wa fedha 2023/24, vitengo vya ukaguzi wa ndani katika mamlaka za serikali za mitaa 24, sekretarieti za mikoa tatu, na Tume ya Utumishi ya Walimu, vilikuwa na upungufu wa wakaguzi wa ndani 71.

ii. Mamlaka za serikali za mitaa 14 na sekretarieti za mikoa mbili zilipata changamoto za bajeti kwa 44% (bajeti ya Sh. milioni 588.88 huku mapato halisi yakiwa Sh. milioni 329.70) kutoka kwenye bajeti iliyoidhinishwa, hali iliyosababisha kupunguza mawanda ya ukaguzi. Pia, Mamlaka za serikali za mitaa 18 na sekretarieti za mikoa tatu, zina upungufu wa rasilimali muhimu kama vile magari, vichapishi, mashine za kudurufu, na kompyuta mpakato. Hali hii ni kinyume na Aya ya 2.7.2 (iv) ya Muongozo ya Kamati ya Ukaguzi kwa Taasisi za Umma wa mwaka 2019, ambayo inaitaka Kamati ya Ukaguzi kushauri menejimenti kuhusu rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya kitengo cha ukaguzi wa ndani.

Kushindwa kuviwezesha vitengo vya ukaguzi wa ndani kunadhoofisha mfumo wa udhibiti wa ndani, huongeza vihatarishi, hupunguza ufanisi wa ukaguzi, husababisha kutokuzingatiwa kwa sheria, na husababisha maamuzi yasiyo sahihi, hivyo kuhatarisha utawala na uwajibikaji kwa mamlaka za serikali za mitaa na sekretarieti za mikoa. Maelezo yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.26.**

**Ninahimiza Serikali ihakikishe kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani vinapewa rasilimali za kutosha na mafunzo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Hii itasaidia kufanya tathmini huru ya mifumo ya udhibiti wa ndani, kuchunguza na kutathmini ufanisi na utoshelevu wa udhibiti ili kuhakikisha uwajibikaji katika taasisi husika.**

## 7.2 Upungufu katika Mfumo wa Udhibiti wa Ndani na Usimamizi wa Vihatarishi

Miongozo ya kuandaa na kutekeleza mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu katika Taasisi za Sekta ya Umma iliyoboreshwa Julai 2023 inazitaka taasisi zote za sekta ya umma kuandaa, kutekeleza, na kuboresha mfumo na mchakato wa usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu na kuhakikisha kuwa kuna mchakato uliowekwa wa kufuatilia, kukagua, kuripoti, na kuboresha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na vihatarishi vya ubadhirifu pamoja na utawala.

Katika tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini dosari zifuatazo:

i. Mamlaka za serikali za mitaa 12 na sekretarieti za mikoa nne hazikufanya tathmini yoyote rasmi ya vihatarishi.
ii. Mamlaka za serikali za mitaa nne hazina sera rasmi zilizoidhinishwa za usimamizi wa vihatarishi.
iii. Mamlaka za serikali za mitaa nne na sekretarieti za mkoa mbili hazina sera ya usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu.
iv. Mamlaka za serikali za mitaa nane na sekretarieti ya mkoa moja, hazikuwa na regista ya vihatarishi, kinyume na Aya ya 4.4.5.1 ya Muongozo wa Usimamizi wa vihatarishi kwenye Taasisi za Umma ya mwaka 2023.
v. Mamlaka za serikali za mitaa nne na sekretarieti ya mkoa moja hazikufanya tathmini ya vihatarishi vya ubadhirifu, hivyo kuzifanya taasisi hizo kuwa katika hatari za ubadhirifu.
vi. Mamlaka za serikali za mitaa tatu na sekretarieti za mikoa mbili hazikufanya mafunzo ya mara kwa mara kuhusu maadili na uelewa wa ubadhirifu kwa wafanyakazi na wadau wake kinyume na Aya ya 3.4.2 ya Miongozo ya Usimamizi wa Vihatarishi ya Ubadhirifu katika taasisi za Umma ya mwaka 2023. Mafunzo haya yanatoa uelewa kuhusu ubadhirifu, jinsi ya kuushughulikia, namna ya kutoa taarifa, na utambuzi wa viashiria vya ubadhirifu. Maelezo yameonyeshwa katika
vii. **Kiambatisho Na.27.**

**Ninapendekeza kwamba mamlaka za serikali za mitaa na sekretarieti za mikoa kuandaa na kuidhinisha sera za usimamizi wa vihatarishi na vihatarishi vya ubadhirifu, mara kwa mara kufanya tathmini za vihatarishi vya ubadhirifu na kuhuisha rejista ya vihatarishi kwa mujibu wa miongozo ya usimamizi wa vihatarishi katika sekta za umma.**

## 7.3 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Kuchelewa Kutatua Malalamiko

Kanuni ya 62(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022 inahitaji malalamiko yashughulikiwe na kukamika ndani ya siku 90. Hata hivyo, nilibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ilichelewa kutatua malalamiko 85 ya walimu, ambapo ucheleweshaji ulikuwa kati ya siku 100 hadi 409.

Ucheleweshaji huu ulisababishwa na kutokuwepo kwa Mwenyekiti wa Tume kutoka Mei 2023 hadi Juni 2024, hali iliyoathiri uwezo wa Tume kufanya kazi kwa ufanisi. Katika kipindi hiki, Katibu Mkuu - OR-TAMISEMI alitekeleza majukumu ya Mwenyekiti wa Tume. lakini kutokana na ratiba yake ngumu, kikao kimoja tu cha malalamiko kilifanyika katika kipindi hicho. Hali hii ilisababisha ucheleweshaji wa kutatua malalamiko, kupungua kwa imani katika ufanisi wa TSC, na athari zinazoweza kujitokeza katika hari ya kazi ya walimu na utendaji wao.

**Ninapendekeza kuwa, kwa nyakati zijazo uongozi wa OR-TAMISEMI uharakishe uteuzi wa Mwenyekiti wa Tume ili kuhakikisha muendelezo wa uongozi na kuepuka usumbufu katika utendaji wa Tume. Aidha, ninashauri menejimenti ya TSC kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuwa na mfumo wa ufuatiliaji wa muda wa kutatua malalamiko ili kuhakikisha kanuni ya siku 90 inafuatwa.**

## 7.4 Kazi Zinazoshabihiana Kati ya Tume ya Utumishi wa Walimu na Bodi ya Walimu Tanzania

Nilifanya tathmini ya Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, 2015 na Sheria ya Bodi ya Walimu Tanzania (TTPB), 2018, na kubaini kuwepo kwa kazi zinazoshabihiana kati ya TSC na TTPB, hasa katika usajili wa walimu, kusimamia maendeleo endelevu ya kitaaluma (CPD) na kushughulikia taratibu za kinidhamu. Hali hii inasababisha uwezekano wa kurudia kupandana kwa majukumu na kukinzana kwa utendaji kwenye usimamizi wa walimu.

Ushabihiano huu unatokana na kutokuwa wazi kwa mgawanyo wa majukumu katika mifumo ya sheria zilizoanzisha taasisi hizi. Ukosefu huu wa ufanisi unaweza kusababisha mkanganyiko wa kiutawala na mzigo mkubwa kwa walimu, na kupunguza ufanisi wa sera zinazolenga kuboresha taaluma ya ualimu.

**Ninapendekeza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Bodi ya Walimu Tanzania kwa kushiriaka na OR-TAMISEMI na mamlaka nyingine zinazohusika, kupitia sheria zinazosimamia taasisi hizi mbili kwa lengo la kubainisha kwa uwazi na kupangilia majukumu na madaraka ya kila taasisi ili kuondoa muingiliano na kuboresha ufanisi.**

## 7.5 Kumalizika kwa Kipindi cha Uongozi cha Bodi ya Wadhamini

Kifungu cha 5 (1-3) cha Sheria ya Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) inaeleza kwamba, Bodi ya Wadhamini inajukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli za Taasisi hiyo. Wanajumbe wanateuliwa na Waziri kwa muda wa miaka mitatu, isipokuwa kama itaainishwa vinginevyo.

Bodi ya Wadhamini ya LGTI ilianzishwa tarehe 5 Novemba 2021, na kipindi chake kilikamilika Oktoba 2024.

Mkuu wa Chuo alimtumia barua Katibu Mkuu - OR-TAMISEMI yenye kumb. namba CBA.36/198/01/24 tarehe 27 Mei 2024 kuhusu kumalizika kwa muda wa uongozi wa wanachama wa Bodi, akiomba ama kuongeza muda au uteuzi wa wanachama wapya. Hata hivyo, hadi tarehe 24 Desemba 2024, Bodi haikuwa imehuishwa.

Ukosefu wa Bodi ya Wadhamini unaleta changamoto kubwa katika utawala bora, usimamizi wa kimkakati, na udhibiti wa kifedha, kama ilivyosisitizwa katika maelekezo ya Msajili wa Hazina (Kumb. Na. CBC.165/191/01B/387 ya Februari 2024). Hali hii inahatarisha ufanisi wa shughuli za Taasisi na michakato ya maamuzi.

**Ninapendekeza kwamba, mamlaka ya uteuzi ifanye jitihada za haraka ili kuhuisha Bodi ya Wadhamini kwa ajili ya kurejesha utawala na usimamizi bora Chuoni.**

## 7.6 Kukosekana kwa Sera ya Uwekezaji kwa Uwekezaji Uliofanywa katika Mfuko wa UTT

Sera ya uwekezaji ni waraka rasmi unaoelezea miongozo, kanuni, na mikakati inayotumiwa na taasisi ya sekta ya umma katika kusimamia uwekezaji wa fedha zake. Sera hii inahakikisha uwazi, uwajibikaji, na matumizi sahihi ya rasilimali za umma, huku ikihakikisha maamuzi ya uwekezaji yanaendana na malengo ya taasisi na kulinda rasilimali dhidi ya hatari zisizostahili. Hii ni muhimu katika kujenga imani ya umma na kuhakikisha uzingatiaji wa mifumo ya kisheria na ya udhibiti.

Uchambuzi wa taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 umebaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 1.44 kiliripotiwa kama “rasilimali nyingine za kifedha”, ikiwa ni uwekezaji uliofanywa na Wakala wa mabasi yaendayo haraka Dar es Salaam (DART) katika Mfuko wa Uwekezaji wa Tanzania (UTT). Hata hivyo, DART haina sera rasmi ya uwekezaji inayoongoza uwekezaji wake katika UTT. Kutokana na hali hiyo, hakuna mfumo uliopangiliwa wa mikakati ya uwekezaji, hali inayosababisha ufanisi duni na kuhatarisha uendelevu wa shughuli za kifedha za Wakala.

Aidha, matumizi yanayohusiana na mapato yanayotokana na uwekezaji wa UTT hayakutambuliwa, hivyo kuongeza hatari ya usimamizi usiofaa wa fedha. Kutegemea taratibu zisizo rasmi na ukosefu wa sera ya uwekezaji kumechangia changamoto hii. Bila mfumo rasmi, tathmini ya uwekezaji na uangalizi wa kina hauwezi kufanyika ipasavyo.

Vilevile, ukosefu wa nyaraka na mchakato wa idhini ulio wazi unadhoofisha mfumo wa udhibiti wa ndani, kupunguza uwazi, na kuathiri maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Ninapendekeza Menejimenti ya DART iandae sera rasmi ya uwekezaji inayoainisha wazi taratibu, malengo ya kimkakati, viwango vya uvumilivu wa hatari, na vigezo vya kutathmini uwekezaji. Sera hii inapaswa kuendana na malengo ya kifedha ya DART na kujumuisha mfumo madhubuti wa uthibitishaji na uidhinishaji wa maamuzi ya uwekezaji. Pia, naishauri menejimenti kutambua na kuidhinisha matumizi yote yanayofadhiliwa na mapato yanayotokana na uwekezaji huo.**

08



# SURA YA NANE

## Usimamizi wa Rasilimali Watu

## 8.0 Utangulizi

Usimamizi wa malipo ya mishahara na rasilimaliwatu ni sehemu muhimu ya mfumo wa usimamizi wa ajira na utoaji wa huduma kwa watumishi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs). Usimamizi mzuri wa rasilimaliwatu, ikiwamo malipo ya mishahara pamoja na stahiki mbalimbali kwa watumishi wa umma, ni muhimu katika kuhakikisha ustawi wa watumishi na kuogeza ari ya ufanyaji kazi, ufanisi na tija katika utoaji wa huduma kwa jamii.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi katika usimamizi wa rasilimaliwatu, ikilenga usimamizi wa mishahara, posho, mafao, malimbikizo, na michakato ya malipo inayohusiana na ajira, vyeo, uhamisho, na kuachishwa kazi. Mbali na umuhimu wake katika kuhakikisha ufanisi na utoaji wa huduma bora, usimamizi wa rasilimaliwatu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

## 8.1 Michango ya Watumishi Isiyowasilishwa Yenye Thamani ya Sh. Bilioni 3.39

Mishahara ya watumishi wa umma hukatwa makato ya kisheria na yasiyo ya kisheria. Makato haya yanajumuisha michango kwenye taasisi kama vile Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), malipo ya kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), pamoja na marejesho ya mikopo kwa taasisi za kifedha na vyama vya akiba na mikopo (SACCOS) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Kifungu cha 7.4.6 (a-d) cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (LAAM) wa mwaka 2019 kinazitaka halmashauri kufanya makato ya fedha ya lazima au ya hiari kutoka mishahara ya wafanyakazi na kuwasilisha fedha hizo kwa taasisi husika. Aidha, Kifungu cha 19(1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ya mwaka 2018 (Sheria ya PSSSF) na Kifungu cha 14(3) cha Sheria ya NSSF (Sura ya 50) vinatoa adhabu kwa waajiri

wanaoshindwa kuwasilisha michango kamili na kwa wakati. Chini ya Sheria ya PSSSF, waajiri wanapaswa kulipa nyongeza ya 1.5% ya kiasi kisicholipwa, huku Sheria ya NSSF ikitoza adhabu ya 5% kwa kila mwezi au sehemu ya mwezi baada ya tarehe ya mwisho ya malipo.

Nilibaini taasisi 45 zilishindwa kuwasilisha jumla ya Sh. bilioni 3.39, ikiwa ni pamoja na Sh. bilioni 2.63 ambazo zilipaswa kupelekwa kwenye mifuko ya mafao na bilioni 755.50 za makato mengine. Kuchelewa kuwasilisha makato imesababisha adhabu ya Sh. bilioni 6.53 kwa taasisi 40. Mchanganuo wa kiasi cha makato yasiyowasilishwa kwa mwaka wa fedha 2023/24 umetolewa katika **Jedwali Na. 51,** huku maelezo zaidi yakiwa katika **Kiambatisho Na.28** cha ripoti hii.

**Jedwali Na.51: Muhtasari wa Michango katika taasisi mbalimbali**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Adhabu (Sh.) | Jumla (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PSSSF | 2,621,121,600 | 6,364,023,951 | 8,985,145,551 |
| 2 | NSSF | 12,698,255 | 164,314,332 | 177,012,587 |
| **Jumla Ndogo** | | **2,633,819,855** | **6,528,338,283** | **9,162,158,138** |
| 3 | NHIF | 13,129,772 | - | 13,129,771 |
| 4 | TRA | 704,564,620 | - | 704,564,620 |
| 5 | NMB | 37,806,079 | - | 37,806,079 |
| **Jumla Ndogo** | | **755,500,471** | **-** | **755,500,471** |
| **Jumla Kuu** | | **3,389,320,326** | **6,528,338,283** | **9,917,658,609** |

***Chanzo:*** *Taarifa za mishahara na za watumishi*

Malipo ya adhabu yanasababisha matumizi yasiyo na tija kwa serikali, ambayo yangeweza kuepukwa na fedha hizo zingeweza kutumika kutekeleza miradi ya maendeleo au kutoa huduma kwa umma. Aidha, kushindwa kwa mamlaka za serikali za mitaa kuwasilisha makato haya, hasa kwa mifuko ya mafao, kumeathiri ukwasi wa mifuko hiyo, jambo ambalo linaweza kuathiri ulipaji wa mafao kwa wastaafu kwa wakati.

**Ninapendekeza kwamba mamlaka husika za serikali za mitaa zihakikishe makato yanawasilishwa kwa taasisi husika na kwa wakati. Hii itasaidia kuepuka gharama zisizo za lazima kutokana na adhabu. Pia, itasaidia kuhakikisha kwamba mafao ya kisheria yanapatikana kwa wakati mara baada ya wafanyakazi kustaafu.**

## 8.2 Madai ya Watumishi Ambayo Hayajalipwa, Sh. Bilioni 24.55

Agizo E.23 la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma la mwaka 2009 linataka mtumishi wa umma anapopandishwa cheo au kuteuliwa kushika wadhifa wa juu, alipwe malimbikizo ya mshahara anayostahili, huku posho ya kukaimu aliyolipwa awali ikisitishwa kwa kuwa hastahili tena kuanzia tarehe halali ya uteuzi au kupandishwa kwake cheo.

Nilifanya mapitio ya mafaili binafsi ya watumishi, nyaraka mbalimbali zinazohusu madai ya watumishi na mahojiano na maafisa rasilimaliwatu katika taasisi 52, na kubaini madai ya watumishi ya jumla ya Sh. bilioni 24.55 ambayo hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

Madai haya ni pamoja na Sh. bilioni 10.01 za malimbikizo ya mishahara, Sh. milioni 543.65 za gharama za usafiri kwa watumishi waliostaafu, na Sh. bilioni 13.99 kwa ajili ya stahiki nyingine kama vile posho za kisheria kwa wakuu wa idara, vitengo na watumishi wengine. Maelezo zaidi yametolewa katika Kiambatisho Na.29.

Ugawaji wa fedha usiotosheleza kwa ajili ya vyeo vinavyotarajiwa, posho za kisheria, na madai mengine ya wafanyakazi umechangia mapungufu yaliyobainika. Madai ambayo hayajalipwa huongeza madeni kwa taasisi husika na kuathiri motisha ya wafanyakazi, hivyo kupunguza ufanisi wao katika utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza kuwa serikali kuhakikisha halmashauri husika kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Hazina, zinatenga bajeti na kutoa fedha kwa ajili ya kulipa madai ya watumishi ili kuepusha malimbikizo ya madeni.**

## 8.3 Wafanyakazi Wenye Tarehe Tofauti za Kuzaliwa Kati ya Mfumo wa Mamlaka za Vitambulisho na Mfumo wa Mishahara

Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009 zinahitaji utunzaji sahihi wa kumbukumbu za watumishi wa umma. Kutofautiana kwa taarifa kunadhoofisha uaminifu wa rekodi za wafanyakazi na kuathiri ufanisi wa taasisi katika kusimamia taarifa ya rasilimaliwatu.

Hata hivyo, katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa wafanyakazi 6,364 katika taasisi 43 walikuwa na tofauti katika taarifa za tarehe ya kuzaliwa kati ya kumbukumbu za malipo katika Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali Watu (HCMIS) na kanzidata ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).

Hali hii imesababishwa na makosa wakati wa kuingiza taarifa za watumishi katika mfumo wa usimamizi wa rasilimaliwatu au kanzidata ya mamlaka ya vitambulisho vya taifa, kutofanya uhakiki wa kutosha wakati wa ukusanyaji na uhuishaji wa taarifa, au matumizi ya tarehe za kuzaliwa zilizokadiriwa badala ya zilizo kwenye vyeti rasmi.

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini kuwa taasisi 184 zilikuwa na wafanyakazi 76,536 waliokuwa na kasoro hiyohiyo. Ingawa kumekuwa na maboresho katika eneo hilo, juhudi zaidi zinahitajika ili kuondoa kabisa tofauti hizi na kuhakikisha kumbukumbu

sahihi za watumishi zinatunzwa. Orodha ya taasisi imeoneshwa kwenye **Jedwali na. 52.**

### Jedwali Na.52: Taasisi Zenye Wafanyakazi Wenye Utofauti wa Tarehe za Kuzaliwa

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Wafanyakazi | Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Wafanyakazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Bukombe | 295 | 23 | H/Mji Kasulu | 216 |
| 2 | H/W Bumbuli | 114 | 24 | H/W Kibiti | 52 |
| 3 | H/W Geita | 56 | 25 | H/W Kibondo | 50 |
| 4 | H/W Handeni | 83 | 26 | H/Manispaa Kigoma-Ujiji | 321 |
| 5 | H/W Kasulu | 172 | 27 | H/W Kilindi | 114 |
| 6 | H/W Kibaha | 90 | 28 | H/Mji Korogwe | 179 |
| 7 | H/Mji Kibaha | 155 | 29 | H/W Madaba | 19 |
| 8 | H/W Kisarawe | 14 | 30 | H/W Mafia | 45 |
| 9 | H/W Lushoto | 223 | 31 | H/W Mbinga | 51 |
| 10 | H/W Mkuranga | 25 | 32 | H/Mji Mbinga | 40 |
| 11 | H/W Moshi | 40 | 33 | H/Mji Mbulu | 117 |
| 12 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 8 | 34 | H/W Meru | 139 |
| 13 | Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani | 11 | 35 | H/Manispaa Moshi | 9 |
| 14 | H/W Rufiji | 82 | 36 | H/W Nkasi | 334 |
| 15 | H/W Pangani | 135 | 37 | H/W Nyasa | 18 |
| 16 | H/Jiji Arusha | 671 | 38 | H/W Siha | 34 |
| 17 | H/W Arusha | 488 | 39 | H/W Sumbawanga | 203 |
| 18 | H/W Buhigwe | 62 | 40 | H/Manispaa Sumbawanga | 425 |
| 19 | H/W Chato | 172 | 41 | H/Jiji Tanga | 230 |
| 20 | H/Mji Handeni | 32 | 42 | H/W Tunduru | 61 |
| 21 | H/W Kakonko | 133 | 43 | H/W Uvinza | 308 |
| 22 | H/W Kalambo | 338 | | **Jumla** | **6,364** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Mifumo ya HCMIS na NIDA*

Kutofautiana huku kunatia mashaka kuhusu usahihi na kuaminika kwa taarifa kuhusu tarehe ya kuzaliwa kati ya mifumo hii miwili, jambo ambalo linaweza kusababisha makosa katika malipo ya mishahara, utambulisho usio sahihi wa wafanyakazi, na changamoto katika kukokotoa mafao ya wastaafu.

**Ninapendekeza kwamba serikali ihakikishe taasisi husika, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO-PSM), zinalinganisha taarifa za tarehe za kuzaliwa kati ya mifumo ya HCMIS na kanzidata ya NIDA ili kuboresha usimamizi wa rasilimali watu na kuongeza ufanisi wa utendaji.**

## 8.4 Uboreshaji Usio Kamili wa HCMIS kwa Watumishi 1914 Waliohamishwa

**Kifungu cha 79(1) cha Muongozo wa Fedha za Serikali za Mitaa wa mwaka 2009 kinamtaka afisa rasilimaliwatu au mkuu wa idara husika kuweka rejista ya watumishi wote na taarifa zao ikiwa imehuishwa kwa wakati wote na kumjulisha mhasibu haraka kuhusu masuala yote yanayoathiri malipo ya stahili zao, yakiwamo:**

(a) Uteuzi, kujiuzulu, kufukuzwa, kusimamishwa, kuhamishiwa kwa muda au kuhamishwa; (b) Mabadiliko ya malipo ya mshahara, isipokuwa nyongeza za kawaida na ongezeko la mshahara kwa mujibu wa mikataba ya jumla;(c) Kutokuwapo kazini kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine, isipokuwa likizo iliyoidhinishwa; na (d) Taarifa hizi ni muhimu kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu za utumishi zinazohusiana na kodi ya mapato na michango ya mfuko wa hifadhi ya jamii.

Ukaguzi wangu wa taarifa za malipo ya mishahara, faili za wafanyakazi, na rejista za uhamisho wa wafanyakazi katika taasisi 57 ulibaini kwamba wafanyakazi 1,914 walihamishiwa katika taasisi nyingine za serikali lakini bado walikuwa wanapokea mishahara kupitia vituo vyao vya awali. Maelezo yameonyeshwa katika **Kiambatisho Na.30**

Kucheleweshwa kwa uidhinishaji wa uhamisho katika mfumo wa HCMIS na ukosefu wa ufuatiliaji wa kutosha wa taarifa za mishahara ya wafanyakazi na menejimenti ya halmashauri za serikali za mitaa (LGAs) zilionekana kuwa sababu kuu za upungufu huu. Kushindwa kuhuisha taarifa za wafanyakazi katika mfumo wa HCMIS kuhusu uhamisho wao kwenda vituo vipya vya kazi kunaweza kusababisha malipo ya mishahara na mafao mengine kuendelea kulipwa kwa watumishi waliokwishajiuzulu au kutokuwapo kazini. Aidha, iwapo kuna utovu wa nidhamu kwa mtumishi husika, kituo kipya cha kazi kinaweza kushindwa kusitisha mishahara ya mfanyakazi huyo wakati wa kusubiri maamuzi ya kinidhamu.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhuisha taarifa za uhamisho wa**

**watumishi kwa wakati kwenye mfumo wa usimamizi wa rasilimaliwatu.**

## 8.5 Wafanyakazi Kupokea Mishahara Chini ya Kiwango kinachotakiwa kutokana na Makato Makubwa

Sehemu ya 3 ya Sheria ya Maofisa Maalumu (Urejeshaji wa Madeni) Na.7 ya 1970 kama ilivyoonyeshwa katika Mzunguko na Rejeo Na.CE.26/46/01/1/66 ya tarehe 28 Novemba 2012 inahitaji wafanyakazi kufanyiwa makato yasiyozidi theluthi mbili ya mishahara yao ya msingi ya kila mwezi.

Wakati wa ukaguzi wa orodha ya mishahara, nilibaini watumishi 724 katika taasisi 22 wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachotakiwa cha theluthi moja ya mishahara yao kutokana na makato makubwa kama invyoonekana kwenye **Jedwali Na. 53.**

**Jedwali Na.53: Taasisi Zenye Watumishi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika**

| Na | Majina ya Taasisi | Idadi | Na | Majina ya Taasisi | Idadi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | S/M Arusha | 7 | 13 | H/W Mpanda | 16 |
| 2 | H/Mji Bariadi | 52 | 14 | H/Manispaa Mpanda | 33 |
| 3 | H/W Bumbuli | 26 | 15 | H/W Mpwapwa | 41 |
| 4 | S/M Dar es Salaam | 8 | 16 | H/W Nkasi | 22 |
| 5 | H/Mji Geita | 82 | 17 | H/W Pangani | 10 |
| 6 | S/M Iringa | 5 | 18 | H/W Sumbawanga | 10 |
| 7 | H/W Kalambo | 46 | 19 | H/W Ukerewe | 71 |
| 8 | H/W Kibiti | 17 | 20 | H/W Geita | 82 |
| 9 | H/W Korogwe | 26 | 21 | H/W Mtama | 15 |
| 10 | H/Mji Korogwe | 18 | 22 | H/Manispaa Temeke | 88 |
| 11 | H/W Maswa | 32 | **Jumla** | | **724** |
| 12 | H/W Mlele | 17 | | | |

***Chanzo:*** Taarifa za Mishahara

Ongezeko la makato linasababishwa na nyongeza ya makato kwa wadaiwa wa mikopo ya elimu ya juu, makato ya mishahara kama hatua za kinidhamu kwa mtumishi, na wafanyakazi kuchukua mikopo bila kushirikisha uongozi.

Makato makubwa ya mishahara kwa wafanyakazi yanaweza kuwaletea hatari ya kuvutiwa na kufanya vitendo vya udanganyifu, ufujaji wa fedha za umma au matumizi mabaya ya ofisi za umma kwa manufaa

binafsi. Aidha, inawashusha morali wafanyakazi na kuathiri utendaji wao, ustawi na utoaji huduma kwa ujumla.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe taasisi husika zinatekeleza udhibiti madhubuti ili kuzuia makato mapya yatakayopelekea wafanyakazi kupokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika.**

09




# SURA YA TISA

## Uwekezaji Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

## 9.0 Utangulizi

Katika sura hii, nimebainisha uwekezaji wa kimkakati uliofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha mapato yao ya ndani, ustawi wa maendeleo ya jamii, kuchochea ukuaji wa uchumi, na kuboresha utoaji wa huduma. Kifungu namba 41 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290) kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kwa ajili ya uwekezaji wenye tija kulingana na vigezo vilivyowekwa, kuhakikisha ufanisi na matumizi sahihi ya rasilimali.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa mamlaka kadhaa za serikali za mitaa zimewekeza katika taasisi za fedha, viwanda vya kutengeneza matofali, vituo vya mabasi, masoko, na miradi mingine. Pia, nilifanya tathmini ya uzingatizi wa sheria, kanuni, sera, na miongozo inayoongoza maamuzi ya uwekezaji wa fedha za umma.

Tathmini hiyo ilihusisha uchambuzi wa faida za uwekezaji na ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya miaka ya iliyopita, hasa vituo vya mabasi na masoko. Lengo lilikuwa kutathmini ufanisi wa miradi hiyo katika kufikia malengo yaliyowekwa kama vile kuchochea uchumi, kuongeza mapato, na kuimarisha utoaji wa huduma.

Kulingana na matokeo ya ukaguzi, sura hii inatoa mapendekezo ya kina, yakiwamo hatua za muda mfupi na mrefu, ili kushughulikia udhaifu uliobainika na kuimarisha mbinu za uwekezaji ndani ya mamlaka za serikali za mitaa.

## 9.1 Uwekezaji katika Hisa

Kifungu cha 41 cha Sheria ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa, Sura ya 290, kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuwekeza sehemu yoyote ya fedha zilizopo kwenye akaunti zake katika uwekezaji ulioidhinishwa.

### 9.1.1 Kuendelea Kushuka kwa Thamani ya Uwekezaji katika Hisa za Benki ya DCB

Mwaka 2001, Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mkoa wa Dar es Salaam zilifanya maamuzi ya pamoja ya kuanzisha Benki ya Jamii ya Dar es Salaam (DCB), ambayo ilianza rasmi shughuli zake mwaka 2002. Mnamo mwezi Februari mwaka 2012, benki hiyo ilibadilisha jina na kuwa "DCB

Commercial Bank Plc" na kufikia mwezi Julai mwaka 2012, ilipatiwa leseni ya ya kujiendesha kama benki ya biashara nchini kote.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoshiriki ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, na Ubungo, kwa pamoja ziliwekeza jumla ya Sh. bilioni 26.84 katika hisa 31,923,990.

Hata hivyo, thamani ya hisa hizo imeendelea kushuka kwa kasi na kwa kiwango kikubwa mwaka hadi mwaka. Mnamo mwaka 2002, hisa moja ilikuwa na thamani ya Sh. 1,000, lakini hadi tarehe 30 Juni 2023, thamani yake ilipungua hadi Sh. 140. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kiwango cha uwekezaji katika hisa hizo imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 54**.

**Jedwali Na.54: Uwekezaji uliofanywa na Kila Halmashauri**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Hisa | Thamani ya Hisa mwaka 2001 @ Sh. 1,000 na Sh. 250 mwaka 2018/19 | Thamani ya Hisa kufikia tarehe 30 Juni 2023 @ Sh. 140 (A) | Thamani ya Hisa kufikia tarehe 30 Juni 2024 @ Sh. 110 (B) | Hasara ya Mwaka 2023/24 (Sh.) (A-B) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar | 6,832,094 | 6,832,094,000 | 956,493,160 | 751,530,340 | 204,962,820 |
| | | 3,396,254 | 849,063,500 | 475,475,560 | 373,587,940 | 101,887,620 |
| 2 | H/M Ilala | 6,357,426 | 6,357,426,000 | 890,039,640 | 699,316,860 | 190,722,780 |
| | | 1,509,434 | 377,358,500 | 211,320,760 | 166,037,740 | 45,283,020 |
| 3 | H/M Kinondoni | 3,750,013 | 3,750,013,000 | 525,001,820 | 412,501,430 | 112,500,390 |
| | | 1,875,006 | 468,751,500 | 262,500,840 | 206,250,660 | 56,250,180 |
| 4 | H/M Temeke | 3,422,252 | 3,422,252,000 | 479,115,280 | 376,447,720 | 102,667,560 |
| 5 | H/M Kigamboni | 2,281,502 | 2,281,502,000 | 319,410,280 | 250,965,220 | 68,445,060 |
| 6 | H/M Ubungo | 2,500,009 | 2,500,009,000 | 350,001,260 | 275,000,990 | 75,000,270 |
| **Jumla** | | **31,923,990** | **26,838,469,500** | **4,469,358,600** | **3,511,638,900** | **957,719,800** |

***Chanzo:*** *Tovuti ya Benki ya DCB na Ripoti ya Uwekezaji*

Mapitio ya taarifa za fedha niliofanya kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 yamebainisha kupungua zaidi kwa thamani ya hisa hadi Sh. 110. Hii imepelekea kupungua kwa thamani ya uwekezaji kwa Sh. milioni 957.72, ikilinganishwa na mwaka uliopita, kutokana na kupungua kwa thamani ya uwekezaji kutoka Sh. bilioni 4.47 mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 3.51 mwaka 2023/24. Matokeo yake, hasara zilizokusanywa zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 22.37 mwaka 2022/23 hadi Sh. bilioni 23.33 mwaka 2023/24, hivyo kuendelea kupunguza mizania ya uwekezaji. Mwenendo wa kushuka kwa thamani ya hisa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo umeoneshwa kwenye grafu katika **Kielelezo Na. 2**.

**Kielelezo Na. 2:Kushuka kwa thamani ya uwekezaji wa hisa**




Aidha, nimebaini kuwa benki hiyo imeendelea kutokulipa gawio kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, jambo ambalo limepelekea kuendelea kwa hasara inayotokana na mapato ya gawio kutoka kwenye uwekezaji.

Licha ya kuendelea kushuka kwa thamani ya uwekezaji katika hisa, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa mamlaka husika za serikali za mitaa zimechukua hatua za kurekebisha hali hiyo ili kupunguza hasara zaidi au kubuni mikakati mbadala ya uwekezaji, hata baada ya mapendekezo niliyotoa katika ripoti zangu za ukaguzi zilizopita. Zaidi ya hayo, kukosekana kwa sera madhubuti ya uwekezaji kunazidisha hatari ya kuzorota zaidi kwa hali ya kifedha, hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza kwamba, Serikali ihakikishe kuwa uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa husika unafanya tathmini ya kina ya uwekezaji wao katika Benki ya DCB na kufanya maamuzi sahihi kuhusu kuendelea na uwekezaji huo, kuuza au kuubadilisha uwekezaji ili kupunguza hasara zaidi.**

**Aidha, ninashauri Serikali kujadiliana na Menejimenti ya Benki ya DCB kuhusu hatua za kimkakati kama vile uundaji upya wa shirika na uwekezaji wa mapato ya gawio. Vilevile, ninapendekeza menejimenti ya Benki ya DCB ishirikiane na wataalamu wa masuala ya kifedha ili kubaini njia mbadala endelevu za uwekezaji na kuandaa sera shirikishi ya uwekezaji itakayotoa muongozo wa maamuzi ya baadaye ili kuepuka hasara zaidi.**

## 9.2 Uwekezaji katika Masoko

Uwekezaji wa fedha za umma katika miundombinu ya masoko unapaswa kupangwa, kuendelezwa, na kusimamiwa ipasavyo ili kuhakikisha matumizi bora, kuongeza tija ya kiuchumi, na kuboresha utoaji wa huduma. Nilipitia masuala ya uwekezaji katika masoko ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubaini yafuatayo: -

### 9.2.1 Ukosefu wa Mipango Madhubuti na Ushirikishwaji Duni wa Wadau katika Uwekezaji Kwenye Masoko Uliosababisha Matumizi Hafifu katika Masoko Yaliyokamilika na Upotevu wa Mapato

Mwongozo wa Kitaifa wa Kuandaa na Kufadhili Uwekezaji wa Miundombinu Inayozalisha Mapato uliotolewa na OR-TAMISEMI mwezi Julai 2021, unaeleza kuwa mamlaka za serikali za mitaa huandaa mapendekezo ya miradi bila mipango madhubuti, mara nyingi zikisahau kufanya upembuzi yakinifu, kutambua wadau muhimu, na kubaini hatari pamoja na mbinu za kuzidhibiti. Hali hii husababisha changamoto wakati wa utekelezaji. Uwekezaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika masoko unakutana na ufanisi mdogo kutokana na mipango duni, jambo linalosababisha masoko kutotumika ipasavyo. Usimamizi na uangalizi mzuri ni muhimu katika kuongeza mapato na kuzuia hasara.

Nilipitia uwekezaji wa masoko katika mamlaka tatu za Serikali za Mitaa, ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, na kubaini kutotumika ipasavyo kwa masoko yaliyokamilika, hivyo kusababisha kupoteza mapato na utoaji duni wa huduma. Masoko yaliyokamilika kwa kiasi kikubwa hayajapangishwa. Baadhi ya wafanyabiashara bado wanaendelea kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi, huku majengo ya masoko yaliyojengwa yakibaki wazi. hali inayoonesha tofauti kati ya maamuzi ya uwekezaji na mahitaji halisi ya biashara.

Aidha, nilibaini kuwa baadhi ya masoko yametelekezwa kutokana na kuchagua maeneo yasiyofaa na ushindani kutoka kwa masoko mengine ya jirani, huku migogoro kati ya wawekezaji na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikichelewesha uendeshaji wa miundombinu iliyokamilika. Aidha, ukosefu wa mifumo madhubuti ya usimamizi wa fedha na mipangilio ya usimamizi wa kiutendaji inaibua walakini kuhusu uwazi, uwajibikaji na uwekezaji endelevu na wa muda mrefu katika masoko. Iwapo changamoto hizi hazitatatuliwa, zinaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato na kukua kiuchumi katika mamlaka za serikali za

mitaa husika. Maelezo ya upungufu katika mipango na ushirikishwaji wa wadau yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.31**.

Kutotumika ipasavyo kwa masoko kunasababishwa na ukosefu wa tafiti za awali zilizofanywa vizuri, upangaji usiofaa wa maeneo, ushirikishwaji duni wa wadau, na migogoro ya umiliki isiyotatuliwa. Maamuzi yenye ushawishi wa kisiasa na tathmini dhaifu ya mahitaji yamesababisha miundombinu isiyolingana na uhitaji halisi, huku usimamizi dhaifu na ushiriki mdogo wa mamlaka za serikali za mitaa vikichangia kuendelea kwa hali hiyo. Matokeo yake ni upotevu wa mapato, upungufu wa fedha kwa ajili ya huduma, na kutokupata manufaa ya kiuchumi yaliyokusudiwa. Iwapo hali hii haitashughulikiwa ipasavyo, kuendelea kutotumika kwa masoko hayo kutachochea uharibifu wa miundombinu, na hivyo kushindwa kutimia kwa malengo ya kupata thamani ya fedha.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kupitia mamlaka husika ikiwamo OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha iwezeshe na kufuatilia mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha zinafanya tafiti za kina na kupanga maeneo ya kimkakati kwa ajili ya masoko, kuwezesha matumizi bora ya ardhi na ufanisi wa uwekezaji.**

**Aidha, ninaishauri Serikali kuimarisha ushirikishwaji wa wadau ili kutatua migogoro ya umiliki na kuboresha mifumo ya usimamizi wa masoko, zikilenga matumizi sahihi ya masoko yaliyojengwa na kuboresha upangaji na usimamizi ili kuepuka kutotumika ipasavyo kwa masoko hayo.**

### 9.2.2 Miundombinu Isiyojitosheleza na Usimamizi Usioridhisha wa Masoko Vinasababisha kutokuwapo kwa Ufanisi Kiuchumi

Masoko ya umma ni muhimu kwa uchumi wa ndani, lakini ufanisi wake unategemea usimamizi mzuri na miundombinu inayojitosheleza.

Ukaguzi wangu wa hali za masoko ulibaini upungufu katika miundombinu na changamoto za usimamizi katika mamlaka sita za serikali za mitaa, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa maji safi na vyoo vinavyotumika, hali iliyosababisha mazingira kuwa machafu. Nilibaini kuwa masoko kadhaa yamekuwa yakifanya kazi kwa muda mrefu bila vyoo, hali inayowalazimu wafanyabiashara na wateja kutumia njia mbadala zisizo salama kiafya.

Aidha, ukosefu wa mifumo ya kutupa taka, mifereji duni ya maji, na njia zisizopitika wakati wa mvua umefanya masoko kuwa na mazingira yasiyo rafiki kwa biashara. Upungufu huu wa miundombinu na usimamizi duni umeathiri ufanisi wa masoko, kusababisha upotevu wa fursa za kiuchumi na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na miundombinu ya masoko husika na changamoto za usimamizi katika masoko imeoneshwa katika **Kiambatisho Na.32**

**Ninapendekeza kuwa, OR-TAMISEMI ifanye tathmini ya kina ya miundombinu na usimamizi wa masoko ili kushughulikia changamoto hizi. Kipaumbele kiwe kwenye ukarabati wa miundombinu iliyochakaa na kuweka huduma muhimu kama maji safi na vyoo bora.**

**Aidha, ninaishauri OR-TAMISEMI kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa taka, kuimarisha ulinzi, na kuweka utaratibu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kudumisha viwango vya usafi na kuboresha mvuto wa masoko.**

## 9.3 Uwekezaji katika Vituo vya Mabasi

Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Fedha kwa Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kinatoa mamlaka kwa serikali za mitaa kutoza ada katika vituo vya mabasi kama chanzo cha mapato, kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na waziri na jedwali chini ya kifungu hicho kinachotaja vituo vya mabasi kama sehemu zinazostahili kutozwa ada. Ada hizi zinapaswa kutekelezwa kupitia sheria ndogo zinazobainisha viwango vya ada na makundi ya watu wanaopaswa kulipa ili kuhakikisha utekelezaji wake kwa mujibu wa sheria.

### 9.3.1 Matumizi Hafifu ya Vituo vya Mabasi na Changamoto za Uendeshaji katika Vituo Hivyo

Uwekezaji wa fedha za umma katika vituo vya mabasi unapaswa kusimamiwa ipasavyo na kuendeshwa na kufanya kazi kikamilifu ili kuboresha utoaji wa huduma, kuongeza makusanyo ya mapato, na kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inapatikana. Mipango madhubuti, matengenezo, na usimamizi makini ni muhimu katika kuimarisha matumizi yake na kuzuia upotevu wa fedha.

Ukaguzi wa uendeshaji wa vituo vya mabasi ulibaini kwa kiasi kikubwa kutokutumika ipasavyo na upungufu katika uendeshaji wa vituo, jambo linalosababisha upotevu wa mapato na utoaji wa

huduma hafifu. Vituo vya mabasi katika halmashauri nne havifanyi kazi ipasavyo, huku idadi ndogo ya mabasi ikivitumia kutokana na ukosefu wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji. Aidha, vituo vingi vya mabasi vinakabiliwa na changamoto za miundombinu, kama vile ukosefu wa sehemu za abiria kujikinga jua na mvua, barabara zisizo na vibamba (*pavements*), na uhaba wa vyoo, hali inayofanya mazingira ya vituo hivyo kutokuwa rafiki kwa watumiaji.

Ukosefu wa rejista za kufuatilia mabasi yanayoingia na kutoka, na ukosefu wa walinzi, vinauweka uwekezaji huu katika vituo vya mabasi katika hatari ya kutoendeshwa kwa ufanisi na upotevu wa mapato. Mchanganyiko wa changamoto hizo unaonesha haja ya usimamizi thabiti, mifumo madhubuti ya uendeshaji, na uchukuaji wa hatua stahiki ili kuhakikisha matumizi sahihi ya uwekezaji wa fedha umma katika vituo vya mabasi. Orodha ya serikali za mitaa ambazo mapupungufu yake katika uendeshaji wa vituo vya mabasi yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.33**.

**Ninapendekeza kuwa, OR-TAMISEMI isimamie utekelezaji wa miongozo ya uendeshaji ili kuhakikisha vituo vya mabasi vinatumika kikamilifu; iweke mifumo ya ufuatiliaji wa mabasi yanayoingia na kutoka vituoni; na iboreshe miundombinu kama vile sehemu za abiria kukaa, barabara katika vituo vya mabasi, na huduma za usafi. Aidha, mamlaka za serikali za mitaa husika zinapaswa kuimarisha usalama ili kulinda mapato na kuzuia uharibifu wa miundombinu na wizi.**

**Aidha, ninaishauri Serikali, kupitia OR-TAMISEMI na mamlaka nyingine husika za usafiri na afya kuwezesha na kusimamia uwekaji wa mazingira rafiki katika vituo vya mabasi. Hatua hii haitaboresha tu utoaji wa huduma bali pia itaimarisha ukusunyaji wa mapato.**

## 9.4 Uwekezaji katika Miradi Mingine

### 9.4.1 Utelekezaji wa Majengo ya Kupangisha na Kiwanda cha Biogesi yenye Thamani ya Sh. Bilioni 4.57

Agizo la 52(1) la Memoranda ya Fedha kwa Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka uwekezaji wa fedha za ziada kufanyika kwa kuzingatia sera ya mamlaka husika na maelekezo ya waziri ili kupata manufaa bora ya kiuchumi. Kifungu cha 52(2) pia kinataka uwekezaji wote ufanywe na afisa masuuli kwa niaba ya mamlaka husika. Uwekezaji

wa fedha za umma katika rasilimali za halmashauri unapaswa kusimamiwa kwa ufanisi ili kuhakikisha matumizi bora, ongezeko la mapato, na utoaji mzuri wa huduma.

Ukaguzi wangu wa mradi wa uwekezaji wa mali isiyohamishika katika Kiwanja Namba 322, Barabara ya Ruvu, Oysterbay, katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, wenye thamani ya Sh. bilioni 2.69, ulibaini changamoto kubwa zilizochangia kuachwa kwa mradi huo. Ingawa mradi huu ulikabidhiwa kwa Halmashauri na mbia tarehe 8 Mei 2019 lakini bado haujaendelezwa, hususani katika suala la upangaji, hali iliyotokana na kuwepo kwa mgogoro wa muda mrefu kuhusu hati miliki ya pamoja. Shauri hili lilifikishwa mahakamani, na kuamuliwa chini ya Shauri la Utendaji wa Kibiashara Namba 14283 la mwaka 2024, kati ya Oysterbay Villas Limited na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Hukumu hiyo ilimtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kuandaa hati miliki ya pamoja kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeandaa hati ya uhamisho kwa majina ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Oysterbay Villas Limited, ikisubiri idhini kutoka kwa Kamishna wa Ardhi.

Vile vile, nilibaini mradi wa uwekezaji wa Kiwanda cha Biogas kilichotelekezwa katika Halmashauri ya Mji wa Geita, ambapo Halmashauri ilijenga mtambo wa usimamizi wa taka kwa ajili ya machinjio ya kisasa kwa Sh. bilioni 1.88. Mradi ulikamilika mwezi Januari mwaka 2020; hata hivyo, haujaanza kufanya kazi kutokana na ukosefu wa mashine ya matumizi ya biogas inayohitajika kwa uzalishaji wa umeme. Kutotumika kwa mtambo kwa muda mrefu kwa zaidi ya miaka minne kunaongeza hatari ya uharibifu wa mtambo, wizi wa vifaa vya mtambo, na uchakavu wa thamani yake katika taarifa za fedha, ikiashiria matumizi yasiyo bora ya rasilimali za umma na kupunguza manufaa yaliyotarajiwa ya uwekezaji.

Utelekezaji wa mradi wa uwekezaji wa mali isiyohamishika katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni umetokana na kutokuelewana kati ya Halmashauri na mwekezaji katika miliki ya hati ya pamoja, huku pande zote mbili zikishindwa kutimiza masharti ya mkataba. Matokeo yake, Halmashauri imepoteza mapato ya uwezekezaji, na kuathiri hali yake ya kifedha na kupunguza fedha kwa ajili ya miradi na huduma nyingine.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI ifanye mazungumzo yenye tija na mwekezaji ili kutatua masuala ya mkataba na kuhakikisha inatekeleza majukumu yaliyoainishwa. Pia, ni vyema kupitia upya na kurekebisha baadhi ya vipengele vya mkataba ili kuja na makubaliano yatakayowezesha mradi kutumika na kuwezesha kukusanywa kwa mapato**

**Aidha, ninaishauri OR-TAMISEMI kupitia mamlaka husika kuzisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa miongozo na rasilimali kwa ajili ya usimamizi wa mikataba wenye ufanisi na kusaidia uwekezaji ili kuimarisha matokeo ya miradi na kuhakikisha uendelevu wake.**

### 9.4.2 Kutokuwapo kwa Uhakika wa Tija katika Uwekezaji wa Skimu za Umwagiliaji zenye Thamani ya Sh. Bilioni 4.24

Agizo la 10(2)(c) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 kinamtaka afisa mwenye dhamana kuhakikisha matumizi ya fedha yanafanywa kwa ufanisi wa kiuchumi na thamani ya fedha inapatikana.

Ukaguzi niliofanya katika uwekezaji wa skimu za umwagiliaji ulibaini kuwa miradi miwili ya umwagiliaji yenye thamani ya jumla ya Sh. bilioni 4.24 haijazalisha tija kama ilivyotarajiwa kutokana na upungufu wa tathmini yakinifu kabla ya utekelezaji wake. Miradi hii ambayo ililenga kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri, imebaki kutotumika, hali iliyopelekea uwekezaji wa fedha za umma usio na tija na kushindwa kufikia malengo ya kimkakati kama inavyoelezewa hapa chini"

Ukaguzi wa nyaraka za mkataba ulibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama iliingia mkataba wa Sh. bilioni 2.58 kwa ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Malenge. Mradi huo uliokamilika tarehe 14 Machi 2024 ulilenga kuboresha shughuli za umwagiliaji na uimarisha uzalishaji wa kilimo. Kutokana na andiko la mradi, skimu ya umwagiliaji ilitarajiwa kutegemea mto ya msimu ili kuvuna maji na kuyaelekeza kwenye bwawa kwa ajili ya umwagiliaji.

Hata hivyo, ukaguzi katika eneo la mradi ulibaini kuwa hakuna mto wa msimu, kinyume na andiko la mradi. Aidha, kutokana na asili ya udongo, bwawa lililojengwa haliwezi kuhifadhi maji kwa muda mrefu, hivyo kuathiri shughuli za umwagiliaji. Matokeo yake,

uzalishaji wa mazao ya kilimo uliokusudiwa huenda usifikie matarajio.

Vilevile, Mradi wa Umwagiliaji wa Inala katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora uliokamilika mwaka wa fedha 2017/18 kwa gharama ya Sh. bilioni 1.66 unatumika kwa 29% pekee licha ya kuwa na eneo kwa ajili ya kilimo la hekta 400. Tatizo kuu linaloathiri mradi huu ni migogoro ya ardhi ambayo haijapatiwa ufumbuzi, hali inayosababisha mradi kushindwa kufanikisha malengo yake ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Kasoro hizi zinaashiria kuwa upembuzi yakinifu haukufanyika ipasavyo kabla ya uamuzi wa uwekezaji, jambo linaloibua mashaka kuhusu uendelevu wa mradi na matumizi bora ya fedha za umma. Iwapo skimu hizi za umwagiliaji zitashindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa, halmashauri itakuwa katika hatari ya kupoteza fedha bila kufanikisha manufaa ya kiuchumi yaliyotarajiwa.

**Ninapendekeza kwamba OR-TAMISEMI, na mamlaka za serikali za mitaa husika zitathmini upya uhalisia wa miradi na kuchukua hatua stahiki za marekebisho. Vilevile, ofisi za makatibu tawala wa mikoa na mamlaka za serikali za mitaa zishughulikie migogoro ya ardhi ili kuzuia matumizi mabaya ya fedha na kuhakikisha kuwa miradi ya umwagiliaji inasaidia kilimo na kukuza uchumi.**

**Aidha, ninaishauri OR-TAMISEMI ihakikishe kuwa uwekezaji wa miundombinu katika siku zijazo unafanyiwa upembuzi yakinifu wa kina ili kutathmini uhalisia wake wa kiufundi na kiuchumi kabla ya utekelezaji, hivyo kuboresha uendelevu wa miradi na kuongeza manufaa ya uwekezaji wa umma.**

### 9.4.3 Utekelezaji Duni wa Uwekezaji wa Kimkakati na Kupoteza Fursa Muhimu

Agizo la 52(1) la Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 inataka uwekezaji wa fedha za ziada kufanyika kwa mujibu wa sera ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na maelekezo ya Waziri ili kufanikisha manufaa ya juu zaidi kifedha. Usimamizi madhubuti wa uwekezaji wa umma katika mamlaka za serikali za mitaa ni muhimu ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, kuongeza mapato, na kuboresha utoaji wa huduma.

Katika tathmini ya uwekezaji wa kimkakati, nilibaini kuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliwekeza jumla ya Sh. bilioni 78.34 katika miradi mbalimbali, ikiwamo maegesho ya malori, vituo vya mabasi, na miradi mingine ya uwekezaji inayozalisha mapato. Licha ya uwekezaji huu, makusanyo ya mapato yameendelea kuwa chini ya makadirio ya bajeti. Uchambuzi unaonesha kuwa, kati ya makusanyo yaliyotarajiwa ya Sh. bilioni 3.82, miradi sita ya kimkakati iliingiza mapato ya Sh. bilioni 1.84 pekee, na kusababisha upungufu wa Sh. bilioni 1.98, sawa na 52% ya mapato yaliyotarajiwa.

Aidha, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo halisi ya mapato kutoka miradi miwili ya uwekezaji wa kimkakati (Soko la Ndugai na Mtumba Complex) kwa kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2023/24 unaonesha mtiririko usio imara wa mapato, kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3**). Katika miradi hii makusanyo yalishuka zaidi katika mwaka wa 2023/24 kutokana na ufanisi duni wa uendeshaji, udhaifu katika usimamizi wa ada za watumiaji, na miundombinu isiyokidhi mahitaji. Maelezo kuhusu mapato yaliyotarajiwa dhidi ya mapato halisi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 55**.

**Kielelezo Na. 3:Mtiririko wa Ukusanyaji Mapato kwa Miradi ya Kimkakati**



**Jedwali Na.55: Mapato Tarajiwa dhidi ya Makusanyo Halisi kwa Miradi ya Uwekezaji**

| Na. | Jina la Mradi | Kiasi cha Uwekezaji (Sh.) | Makusanyo Yaliyotarajiwa (Sh.) | Makusanyo Halisi (Sh.) | Tofauti (Sh.) | Tofauti (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Maegesho ya Malori Nala | 5,925,928,105 | 234,071,835 | 63,043,757 | 171,028,078 | 73 |
| 2 | Soko la Ndugai | 14,648,625,050 | 443,261,513 | 101,500,029 | 341,761,484 | 77 |
| 3 | Eneo la Maegesho Chinangali | 2,907,688,337 | 230,865,372 | 15,545,000 | 215,320,372 | 93 |
| 4 | "Mtumba Complex" | 18,875,665,010 | 1,134,710,369 | 241,514,000 | 893,196,369 | 79 |
| 5 | Hoteli ya Jiji Dodoma | 11,945,995,953 | 641,292,699 | 550,000,000 | 91,292,699 | 14 |
| 6 | Kituo Kikuu cha Mabasi Nanenane | 24,033,456,298 | 1,136,710,369 | 866,408,471 | 270,301,898 | 24 |
| **Jumla** | | **78,337,358,753** | **3,820,912,157** | **1,838,011,257** | **1,982,900,900** | **52** |

**Chanzo**: Bajeti na Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato

Vilevile, katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, nilibaini kuwa malipo ya Sh. milioni 340.17 yalifanyika kwa ajili ya kulipia fidia katika ununuzi wa ardhi katika maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji kati ya mwaka wa fedha 2019/20 na 2021/22. Maeneo haya yalilenga kutekeleza miradi ya kuzalisha mapato kama vile masoko, vituo vya mabasi, na makazi ya kupangisha. Hata hivyo, licha ya kupata hati za umiliki mnamo mwaka 2022, hakuna eneo lolote kati ya haya ambalo limeendelezwa au kutumiwa kwa madhumuni ya kiuchumi kama ilivyokusudiwa.

Kukosekana kwa upembuzi yakinifu kabla ya kuanzisha miradi, ukosefu wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji, miongozo ya kufanya tathmini, pamoja na usimamizi mdogo na mwitikio duni kunakwamisha ufanisi wa uwekezaji katika mamlaka za serikali za mitaa na hivyo kusababisha makusanyo duni. Aidha, kushindwa kutumia maeneo ya uwekezaji yaliyolipiwa fidia kumesababisha kupoteza fursa muhimu za kiuchumi, jambo linalokwamisha maendeleo ya miji na kupunguza uwezo wa halmashauri katika kukusanya mapato yake ya ndani.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha, iandae muongozo wa viwango vya tathmini ya uwekezaji, iongeze mifumo ya usimamizi wa ufuatiliaji wa uwekezaji wa miradi ya kuzalisha mapato. Pia, itoe msaada wa kitaalamu na**

**kifedha kwa mamlaka za serikali za mitaa halmashauri ili kuboresha ufanisi wa uwekezaji wa kimkakati. Kupitia utekelezaji wa hatua hizi, mamlaka za serikali za mitaa zitaweza kuimarisha tija katika uwekezaji wa miradi ya kimkakati na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa ufanisi katika kukuza mapato na maendeleo ya kiuchumi ya maeneo husika.**

### 9.4.4 Uwekezaji Usio na Tija wa Sh. Bilioni 9.79 Uliofanywa na Halmashauri katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

Aya 20.3(a) ya Mwongozo wa Uhasibu wa mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuweka fedha kama Akiba ya Lazima ya Kima cha Chini katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa.Aidha, Kifungu cha 60(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kinaainisha kuwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa inawajibika kusimamia, kuwekeza, na kukopesha fedha zake kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Katika kupitia taarifa za fedha za mamlaka za serikali za mitaa, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 9.77 zimewekwa kama amana na halmashauri 176 katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kuoneshwa kama uwekezaji katika taarifa zao za fedha lakini fedha hizo hazijawahi kutoa faida yoyote kwa zaidi ya miaka kumi. Katika hali hii, licha ya uwekezaji ulioorodheshwa, uchambuzi wa taarifa ya kifedha ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa unaonesha kuwa kiasi cha Sh. milioni 285.92 pekee ndicho kimekopesha, Sh. Milioni 686.4 kimewekezwa katika hisa, na Sh. bilioni 1 kipo katika mali za kifedha.

Aidha, Bodi imetengeneza upungufu mkubwa wa mali za jumla ya Sh. bilioni 74.95, unaoashiria hali ya kifedha ngumu. Kwa kuzingatia ugumu huu wa kifedha, inawezekana kwamba fedha za uwekezaji za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeelekezwa kwenye shughuli zisizohusiana na madhumuni yaliyokusudiwa, kwani nimebaini kwamba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Bodi imetumia Sh. milioni 817.89 kutoka katika fedha za Hifadhi ya Sharti la Chini (MCR) kwa matumizi ya ofisi. Hii ni kinyume na kifungu cha 60(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa kinachotaka fedha hizi zitumike pekee kwa shughuli za uwekezaji na mikopo. Jukumu la kisheria la kuwekeza fedha katika mpango usio na tija wa Hifadhi ya Sharti la Chini (MCR) linaonesha uamuzi usiofaa wa uwekezaji uliofanywa na Serikali. Hii inajumuisha pia kukosekana kwa hatua za kibunifu na

mipango ya kifedha kutoka kwa Bodi ili kuboresha uwekezaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Matokeo yake, mpango wa uwekezaji wa Hifadhi ya Sharti la Chini (MCR) haukuchangia tu katika uendelevu wa kifedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, bali pia unaonesha usimamizi usiofaa wa fedha uliofanywa na Bodi ambapo fedha hizo zimehifadhiwa. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na uwekezaji wao katika Bodi umeoneshwa katika **Kiambatisho Na.34**.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha ifanye tathmini kuona uwezekano wa kurekebisha muundo wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ili kuongeza wigo wa majukumu yake na kuhakikisha kuwa inatekeleza malengo yake kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.**

**Aidha, ninashauri OR-TAMISEMI iimarishe udhibiti katika usimamizi wa kifedha na miundo ya utawala ili kulinda fedha za Mikopo ya Serikali za Mitaa dhidi ya usimamizi usiofaa na kuboresha usimamizi wa rasilimali fedha**

10




# SURA YA KUMI

## Utendaji wa Kisekta

## 10.0 Utangulizi

Tathmini ya utendaji wa kisekta ilifanyika katika maeneo ya afya, miundombinu, majukumu ya usimamizi na utawala, usimamizi wa miradi, usimamizi wa ardhi, pamoja na usimamizi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Lengo lilikuwa kutathmini ufanisi, tija, na uzingatizi wa sheria, ili kutoa ushauri utakaowezesha kuboresha uwajibikaji serikalini, uwazi, na utoaji wa huduma bora.

Matokeo ya ukaguzi yalibainisha upungufu wa ufanisi katika maeneo kadhaa, ikiwa ni pamoja na utekelezaji duni wa baadhi ya majukumu ya kisekta kama vile usimamizi wa fedha na utekelezaji usioridhisha wa miradi. Masuala haya yanaathiri utawala bora, utoaji wa huduma endelevu, na imani ya umma kwa serikali.

Sura hii inaangazia mwenendo, vihatarishi, na changamoto zinazoathiri utoaji endelevu wa huduma, ikisisitiza maeneo yanayohitaji maboresho ili kuimarisha nidhamu ya kifedha, ufanisi wa uendeshaji, na usimamizi wa miradi.

## 10.1 Usimamizi na Utawala

### 10.1.1 Utambuzi na Uendelezaji Usioridhisha wa Wafanyabiashara Wadogo

Tarehe 25 Januari 2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikutana na viongozi wa wafanyabiashara wadogo jijini Dar es Salaam na kusisitiza dhamira ya serikali ya kuwatambua rasmi kama kundi maalum linalohitaji usimamizi wa kisheria. Kufuatia hilo, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ilipewa jukumu la kusimamia wafanyabiashara wadogo kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na wizara nyingine husika ili kuboresha mazingira ya biashara na kuwawezesha kukua hadi kuwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa.

Mwezi Aprili 2024, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI walitengeneza miongozo ya uratibu na usajili wa wafanyabiashara wadogo. Tathmini yangu ya utekelezaji wa jukumu la OR-TAMISEMI ilibaini masuala yafuatayo:

i. Hakukuwa na kanzidata (database) iliyoundwa ili kufuatilia na kusimamia wafanyabiashara wadogo, licha ya sensa ya 2022

kubaini uwepo wa zaidi ya wafanyabiashara milioni 1.1 Tanzania Bara.

ii. Hakukuwa na programu za kujengea uwezo au mipango ya kuzisaidia Sekretarieti za Mikoa (RSs) na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kinyume na mahitaji ya mwongozo.

iii. Hakukuwa na ripoti ya ufuatiliaji na tathmini ambayo ingewezesha kutathmini ugawaji wa maeneo ya biashara na miundombinu.

iv. Hakukuwa na mikakati yoyote iliyotekelezwa kuzuia ukatili wa kijinsia (GBV) dhidi ya wafanyabiashara wanawake.

v. Hakukuwa na tathmini za mara kwa mara zinazofanyika ili kufuatilia wafanyabiashara wadogo wanaopiga hatua kwenda kuwa wafanyabiashara wa kati na wakubwa; na

vi. Viashiria Muhimu vya Utendaji (KPIs) havikuwa vimeainishwa ili kupima ufanisi wa mipango ya maendeleo ya wafanyabiashara wadogo.

Changamoto hizi zinatokana na uratibu, ufuatiliaji, na tathmini isiyoridhisha kutoka OR-TAMISEMI, hali inayopunguza uwezo wa serikali kusaidia na kutathmini maendeleo ya wafanyabiashara wadogo. Aidha, kutokuwepo kwa mikakati ya kuzuia ukatili wa kijinsia kunawaweka wafanyabiashara wanawake katika mazingira hatarishi, jambo linaloweza kuathiri ukuaji wa biashara zao na kusababisha upotevu wa fursa za kiuchumi.

**Napendekeza kuwa, OR-TAMISEMI iunde kanzidata ya kidijidali ya wafanyabiashara wadogo na kutekeleza programu za mafunzo kuhusu usimamizi wa fedha, masoko, huduma kwa wateja, na mikakati ya biashara. Vilevile, mifumo ya mara kwa mara ya ufuatiliaji na tathmini ianzishwe, ili kufuatilia mgawanyo wa maeneo ya biashara na kutathmini maendeleo ya wafanyabiashara kwa kutumia viashiria kama vile ukuaji wa mapato, faida, na kupanuka kwa biashara. Aidha, OR-TAMISEMI inapaswa kushirikiana na wadau ili kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia kupitia programu za uhamasishaji na mifumo salama ya utoaji wa taarifa, huku ikianzisha viashiria vya utendaji (KPIs) ili kutathmini ufanisi wa jitihada za maendeleo ya wafanyabiashara.**

### 10.1.2 Dosari katika Uhamisho wa Mali, Madeni na Fedha Baada ya Kuvunjwa kwa Iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

Ukaguzi ulibaini dosari katika mchakato wa ugawaji wa mali kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC), jambo linaloibua wasiwasi kuhusu uzingatiaji wa taratibu, uwazi, na uwajibikaji. Kwa mujibu wa Miongozo ya Usimamizi wa Mali ya mwaka 2019, uhamisho wa mali unapaswa kurekodiwa rasmi kwa kutumia Fomu ya Uhamisho Na. 7, lakini utaratibu huu haukuzingatiwa. Mapitio ya Tangazo la Serikali (GN) Na. 86 la Januari 2024 yalibaini kuwa mgawanyo wa mali ulifanyika bila uthamini, na taarifa za kifedha zilizotumika zilikuwa za tarehe 30 Juni 2020 badala ya taarifa sahihi zaidi za Februari 2021. Aidha, salio la wadaiwa na wadai lilihamishwa bila nyaraka za uthibitisho wa wadau husika, hali iliyosababisha sintofahamu kuhusu usahihi wa taarifa hizo.

Vilevile, mali za Kampuni ya Soko la Kariakoo (KMC) ziligawiwa kwa DCC, kana kwamba KMC imevunjwa, ingawa kisheria bado ni taasisi inayojitegemea inayomilikiwa kwa asilimia 51 na DCC. Aidha, mradi wa mbolea unaotekelezwa kwa kushirikiana na Jiji la Hamburg ulioko chini ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ulihamishiwa DCC ingawa mpangilio rasmi wa mgao haukuonesha hivyo.

Zaidi ya hayo, kati ya Sh. bilioni 1.44 ambao ni mgao wa DCC mpya, ni Sh. milioni 772 pekee zilizohamishwa na Sh. milioni 669 bado hazijakabidhiwa kwa DCC. Mapitio ya barua yenye Kumb. Na. CA.74/90/01D/42 ya tarehe 28 Juni 2021 yalithibitisha kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es Salaam iliomba kuhamishwa kwa Sh. bilioni 2.42 kutoka akaunti mbalimbali kwenda akaunti ya amana mbalimbali ya Serikali za Mitaa iliyopo BOT. Hata hivyo, licha ya ombi la Sekretarieti ya Mkoa kwa Hazina tarehe 20 Septemba 2024 (Kumb. Na. CGA.82/218/01/113) la kuhamisha kiasi cha Sh. milioni 260 kwenda Halmashauri ya Manispaa ya Ilala (ambayo sasa ni DCC), Hazina haikuhamisha fedha hizo na haikutoa uthibitisho wowote wa uwepo wa fedha hizo. Baadaye, Hazina ilieleza kuwa fedha hizo bado zipo katika akaunti za amana ya hazina ndogo, hali inayozua mashaka kuhusu uhalali na uwajibikaji kwa fedha hizo.

Dosari hizi zilitokana na ukosefu wa uratibu wa kutosha, kwani mchakato wa usambazaji wa mali ulifanyika bila mashauriano na

wadau muhimu, wakiwemo wamiliki wa mali na wataalamu wa uthamini. Ukosefu huu wa usimamizi umeleta sintofahamu kuhusu ugawaji wa mali, msingi wa kisheria wa uhamisho wa fedha, na upatikanaji wa salio la fedha zilizobaki, hali inayohitaji hatua thabiti za utawala bora na uwajibikaji.

**Ninapendekeza kuwa uhamisho wote wa mali baada ya kuvunjwa kwa taasisi uzingatie kikamilifu Miongozo ya Usimamizi wa Mali, kwa kuhakikisha kuwa nyaraka sahihi zinatumiwa, hususani Fomu ya Uhamisho Na. 7 na nyaraka za kuthibitisha madeni na madai. Aidha, Hazina kwa kushirikia na Sekretarieti ya Mkoa inapaswa kuthibitisha uwepo wa fedha na kukamilisha uhamisho wa fedha hizo ikiwa ni pamoja na Sh. milioni 669 zinazotakiwa kuhamishiwa kwenye akaunti ya DCC.**

**Zaidi ya hayo, mali zilizogawiwa vibaya zinapaswa kurekebishwa. Shirika la Soko la Kariakoo (KMC) linapaswa kubaki kama tawi la DCC mpya, ambapo umiliki utaendelea kuwa chini yake lakini mali zake zisihamishwe. Mradi wa Mbolea wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni unapaswa kubaki chini ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, na uhamishaji wake kwenda DCC unapaswa kubatilishwa. Katika siku zijazo, ugawaji wa mali unapaswa kufanywa kwa kushirikiana na wadau husika na wataalamu wa tathmini ili kuhakikisha usahihi na utekelezaji wa masharti ya kisheria.**

## 10.2 Usimamizi wa Miundombinu

### 10.2.1 Miradi ya Ujenzi Iliyokamilika Lakini Haitumiki Sh. bilioni 5.64

Ukaguzi wangu wa miradi ya ujenzi, kwa mwaka wa fedha 2023/24 umebaini miradi 45 ya sekta ya afya, elimu na utawala katika mamlaka 11 za serikali za mitaa yenye thamani ya Sh. bilioni 5.64 ilikamilika lakini haitumiki. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi iliyokamilika lakini haitumiki imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 56.**

**Jedwali Na.56: Halmashauri zenye miradi iliyokamilika lakini haijatumika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miradi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mkuranga | 12 | 2,486,907,918 |
| 2 | H/M Temeke | 2 | 449,293,900 |
| 3 | H/Mji Mbulu | 5 | 108,000,000 |
| 4 | H/Mji Geita | 2 | 95,000,000 |
| 5 | H/W Mvomero | 1 | 100,000,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miradi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 6 | H/W Misungwi | 7 | 728,661,050 |
| 7 | H/W Ileje | 2 | 608,000,000 |
| 8 | H/W Mkinga | 2 | 114,400,000 |
| 9 | H/W Chemba | 5 | 230,000,000 |
| 10 | H/W Itigi | 3 | 500,000,000 |
| 11 | H/W Mbulu | 4 | 215,115,740 |
| **Jumla** | | **45** | **5,635,378,608** |

***Chanzo*:** Taarifa za Utekelezaji na Ukaguzi wa Miradi

Miundombinu hii haitumiki kutokana na sababu mbalimbali. Miongoni mwazo ni: upungufu wa watumishi, ukosefu wa samani, vifaa vya maabara za shule, na miundombinu mingine ya uendeshaji kama vile mahali pa kuchomea taka na vyoo.

Kushindwa kutumia miundombinu iliyokamilika kutaathiri sekta za elimu na afya kwa kuchelewesha utoaji wa huduma, kunyima jamii manufaa yaliyokusudiwa, na kusababisha uchakavu wa mali. Hali hii itaongeza gharama za matengenezo na hatari ya miundombinu hiyo kuchakaa kabla ya kutumiwa.

**Ninaishauri kila mamlaka ya serikali za mitaa ihakikishe kuwa miundombinu iliyokamilika inatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa, na kuhakikisha samani na vifaa vya maabara vinakuwapo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Vilevile, ninapendekeza Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ipange watumishi wa kutosha kulingana na mahitaji ya muundo wa mamlaka ya serikali ya mitaa husika.**

### 10.2.2 Kasi Ndogo ya Ujenzi wa Miradi Sh. bilioni 77.33

Kanuni ya 243(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inataka taasisi nunuzi kusimamia utendaji wa mkandarasi au mtoahuduma katika mikataba inayohusisha huduma zisizo za ushauri au kazi za ujenzi. Usimamizi huu unapaswa kufanyika kwa kulinganisha kazi zinazotekelezwa na mahitaji maalumu au ratiba ya kazi hiyo kama ilivyobainishwa katika mkataba, kwa kutumia ripoti za kila siku, kila wiki, au kila mwezi zinazoandaliwa na msimamizi aliyeteuliwa kwa ajili ya huduma au kazi husika.

Nilibaini kuwa miradi kadhaa yenye thamani ya Sh. bilioni 77.33 iliyotekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa 33 katika mwaka wa fedha uliokaguliwa haijakamilika, huku miradi mingine ikiendelea

kufanyika kwa kasi ndogo licha ya kuisha kwa muda wa mikataba husika. Maelezo mahususi yametolewa katika **Kiambatisho Na.35**.

Kucheleweshwa kukamilika kwa miradi hii kunatokana na utoaji usiotosheleza au ucheleweshaji wa fedha, usimamizi na ufuatiliaji hafifu kutoka kwa menejimenti ya serikali za mitaa, pamoja na ushirikishwaji mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi.

Matokeo yake, ucheleweshaji wa miradi na kutokamilika kwake kunaweza kusababisha kurejewa kwa makadirio ya gharama (BOQ) ili kuendana na mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na gharama nyingine za uendeshaji zinazosababishwa na mfumuko wa bei. Aidha, jamii zilizolengwa zinakosa kwa muda mrefu kufaidika na huduma zilizokusudiwa kutoka kwa miradi hii.

**Ninahimiza OR-TAMISEMI, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuanzisha mifumo madhubuti ya kusimamia miradi isiyokamilika. Hii inapaswa kujumuisha tathmini ya miradi yote inayoendelea, kufanya makadirio ya rasilimali zinazohitajika ili kuikamilisha, na kuhakikisha utolewaji wa fedha kwa wakati ili kuepuka ongezeko la gharama na kuwezesha kukamilika miradi hiyo.**

**Aidha, ninapendekeza kuwa mamlaka za serikali za mitaa ziweke kipaumbele cha kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kutathmini kazi zilizobaki katika miradi hiyo, kuandaa mikakati mahususi ya kuikamilisha, kuboresha upangaji wa miradi, ufuatiliaji na usimamizi, pamoja na kuongeza ushiriki wa jamii ili kuhakikisha utekelezaji wa haraka wa miradi inayoanzishwa.**

### 10.2.3 Fedha za Miradi Zisizotumika Sh. bilioni 9.42

Kifungu cha 27(4) cha Sheria ya Bajeti, [sura ya 439] kinataka pale ambapo matumizi ya fedha za serikali na taasisi za umma yamepitiswa, zitatumika tu kwa madhumuni yaliyoainishwa.

Mapitio yangu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya maendeleo yalibaini kuwa kiasi cha Sh. bilioni 9.42 kilihamishiwa kwa mamlaka za ngazi za chini (shule na vituo vya afya). Hata hivyo, fedha hizi hazikutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2023/24.

**Jedwali Na.57: Orodha ya MSM zenye Fedha za Miradi ambazo Hazikutumika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi Kisichotumika (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Karatu | 20,000,000 |
| 2 | H/W Longido | 26,600,000 |
| 3 | H/W Kisarawe | 351,754,484 |
| 4 | H/W Tandahimba | 1,182,154,800 |
| 5 | H/W Kaliua | 938,940,731 |
| 6 | H/M Tabora | 92,000,000 |
| 7 | H/W Korogwe | 4,160,209,825 |
| 8 | H/W Mkinga | 2,386,576,946 |
| 9 | H/W Chemba | 259,761,029 |
| **Jumla** | | **9,417,997,815** |

**Chanzo: Taarifa za Mapato na Matumizi ya Fedha**

Fedha za miradi hazikutumika hadi mwisho wa mwaka kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo ugumu wa kufanya malipo kupitia mfumo wa kiuhasibu wa FFARS, ucheleweshaji wa michakato ya ununuzi, na utolewaji wa fedha kwa kuchelewa kutoka Hazina. Kushindwa kutumia fedha kwa wakati kunaweza kusababisha ongezeko la gharama kutokana na mfumuko wa bei na mabadiliko ya bei ya bidhaa, hali inayochelewesha utoaji wa manufaa kwa jamii iliyokusudiwa.

**Ninaishauri OR-TAMISEMI kushughulikia changamoto za kiufundi katika mfumo wa malipo FFARS ili kurahisisha mtiririko wa malipo na kuzuia ucheleweshaji usio wa lazima na kuoanisha ratiba za utoaji wa fedha na muda wa utekelezaji wa miradi ili kuboresha ufanisi na kupunguza hatari ya fedha kutotumika.**

### 10.2.4 Miradi Iliyotelekezwa kwa Kipindi cha Hadi Miaka 25 yenye Thamani ya Sh. Bilioni 14.30

Kifungu cha 111 (b na c) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinazitaka serikali za mitaa kuhamasisha ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi kwa wakazi wote ndani ya maeneo yao ya utawala, kwa kuzingatia sera na mipango ya kitaifa ya maendeleo ya vijijini na mijini.

Nilibaini kuwa miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 14.30 ilitekelezwa na mamlaka za serikali za mitaa 13 kwa vipindi kati ya mwaka 3 hadi miaka 25 ikiwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

**Jedwali Na.58: Orodha ya Halmashauri zenye Miradi Iliyotelekezwa**

| Na | Jina la Halmashauri | Muda wa Kutelekezwa | Idadi ya Miradi | Thamani ya Miradi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Shinyanga | Hadi miaka 25 | 20 | 1,204,760,659 |
| 2 | H/W Moshi | Hadi miaka 23 | 73 | 1,297,099,800 |
| 3 | H/M Kigoma Ujiji | Hadi miaka 22 | 11 | 1,308,000,000 |
| 4 | H/W Butiama | Hadi miaka 15 | 20 | 1,623,000,000 |
| 5 | H/W Mwanga | Hadi miaka 10 | 11 | 228,423,115 |
| 6 | H/W Nzega | Hadi miaka 10 | 5 | 308,499,408 |
| 7 | H/W Pangani | Hadi miaka 7 | 13 | 1,118,929,283 |
| 8 | H/W Mlele | Hadi miaka 6 | 8 | 185,000,000 |
| 9 | H/Mji Geita | Hadi miaka 5 | 14 | 1,080,000,000 |
| 10 | H/W Meru | Hadi miaka 3 | 35 | 2,432,664,888 |
| 11 | H/W Rufiji | Hadi miaka 3 | 4 | 3,368,338,000 |
| 12 | H/W Chemba | Hadi miaka 3 | 1 | 45,012,000 |
| 13 | H/M Singida | Hadi miaka 3 | 1 | 100,000,000 |
| **Jumla** | | | **216** | **14,299,727,153** |

***Chanzo:*** Ripoti za Utekelezaji na Ukaguzi wa Miradi

Utelekezaji wa miradi hii umetokana na ukosefu wa bajeti za kutosha na kutoweka kipaumbele cha kukamilisha miradi ya awali, hasa kwa miradi iliyoanzishwa kupitia michango ya jamii. Kutelekeza miradi ya maendeleo baada ya uwekezaji mkubwa wa fedha husababisha upotevu wa rasilimali na kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI ihakikishe mamlaka ya serikali za mitaa zinatenga upya bajeti ya miradi hii iliyoachwa kwa muda mrefu ili kuhakikisha inakamilika na kufanikisha malengo yake. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuweka kipaumbele katika upangaji wa fedha na matumizi kwa kuzingatia miradi michache inayoweza kukamilika kwa wakati uliopangwa ili kuepuka kutelekeza miradi katika siku zijazo.**

### 10.2.5 Upungufu katika Miradi ya Ujenzi Yaliobainika Wakati wa Ukaguzi Sh. bilioni 6.26

Kanuni ya 114(c) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inataka taasisi nunuzi kuwajibika kusimamia kikamilifu ununuzi wa bidhaa, huduma, au kazi anayotekeleza na kuchukua hatua za kurekebisha au kuwajibisha ukiukwaji wa masharti ya mkataba.

Nilibaini kasoro mbalimbali nyufa kwenye kuta/kuta kuanguka, vyoo kutokuwa na mzunguko wa hewa n.k katika miradi ya maendeleo yenye thamani ya Sh. 6.26 bilioni iliyotekelezwa katika mamlaka za serikali za mitaa nane.

Kasoro hizi zilichangiwa zaidi na usimamizi dhaifu wa mafundi wa ndani (mafundi mchundo) na kutowashirikisha wataalamu katika tathmini na uteuzi wa mafundi. Maelezo ya kina ya kasoro hizo yameoneshwa katika **Kiambatisho Na.36.**

Kutokana na changamoto hizi, mamlaka za serikali za mitaa husika zitakabiliwa na gharama za ziada za kurekebisha kasoro katika miradi hiyo, huku miundombinu muhimu kama mabweni, majengo ya hospitali, madarasa, na mifumo ya usafi ikibaki bila kutumika, hivyo kuwanyima wananchi huduma za msingi.

**Ninashauri OR-TAMISEMI iimarishe usimamizi wa mikataba ili kuepuka kazi zenye upungufu mwingi. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuweka vipengele katika mikataba ya ujenzi na usambazaji ambavyo vitahakikisha uwekaji upya wa vifaa visivyokuwa na ubora au kurudiwa kufanywa kwa kazi ziliyofanywa chini ya viwango vinavyokubalika bila malipo ya ziada.**

### 10.2.6 Upungufu katika Usimamizi wa Mikataba na Udhibiti wa Ubora katika Miradi ya Barabara za TARURA yenye Thamani ya Sh. bilioni 21.89

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaitaka TARURA kusimamia mikataba ya kazi kwa ufanisi kwa kuhakikisha ufuatiliaji wa utekelezaji, ukamilishaji kwa wakati, uzingatiaji wa viwango vya ubora, na utekelezaji wa masharti ya mkataba.

Uhakiki wa miradi ya barabara yenye thamani ya Sh. bilioni 21.89 ulionesha upungufu kadhaa, ikiwamo ujenzi usiozingatia viwango, ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi, na ujenzi usiozingatia masharti ya mkataba kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho Na.37.**

Ujenzi usioridhisha, mipango na usimamizi wa ujenzi usio na ufanisi, pamoja na udhaifu katika utekelezaji wa masharti ya mikataba, vimesababisha matengenezo ya mara kwa mara na yenye gharama kubwa, kupungua kwa muda wa matumizi wa miundombinu, na kuongezeka kwa hatari za usalama.

**Ninapendekeza TARURA isimamie kwa uthabiti utekelezaji wa viwango vya usanifu, kanuni za usalama, na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ubora na usalama wa miundombinu ya bara bara.**

### 10.2.7 Kutozingatia Kanuni na Dosari za Usanifu katika Miradi ya Barabara za TARURA yenye Thamani ya Sh. bilioni 91.81

Kanuni ya 10(1)(c) ya Kanuni za Ushuru wa Barabara na Mafuta za mwaka 2016 inamtaka wakala mtekelezaji kuhakikisha kazi yoyote iliyopangwa inatekelezwa ndani ya muda, gharama, na viwango vya ubora vilivyoainishwa kwenye mkataba husika. Vilevile, kifungu cha 39(1)(k) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, sura ya 410, kinaitaka idara husika kusimamia utekelezaji wa mikataba, ikijumuisha kupitia na kuidhinisha taarifa za kiufundi, usanifu, au matokeo yoyote kulingana na mkataba.

Ukaguzi wa miradi ya barabara ya TARURA kwa mwaka wa fedha 2023/24 yenye thamani ya Sh. bilioni 91.81 ulibaini dosari nyingi za usanifu, zilizochangia ujenzi duni na kuongezeka kwa gharama. Changamoto zilizobainika ni pamoja na utekelezaji wa miradi bila usanifu wa kina, tofauti kati ya makadirio ya gharama (BoQ) na michoro, mabadiliko ya kazi yasiyopangwa, na kutokamilika kwa vipimo vya kiufundi.

Upungufu uliojitokeza ni pamoja na madaraja yenye ukubwa uliopungua, miundombinu duni ya kupitisha maji, ukosefu wa usanifu wa tabaka la barabara, na makalavati yasiyokamilika. Upangaji dhaifu na usimamizi usiokuwa wa ufanisi husababisha uchakavu wa mapema wa barabara, hatari ya mmomonyoko wa udongo, na ukiukwaji wa viwango vya usanifu katika mikoa mbalimbali. Dosari hizi zinaonesha upungufu katika udhibiti wa ubora, utunzaji wa nyaraka za miradi, na uzingatiaji wa viwango vya uhandisi. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Kiambatisho Na.38**.

Kwa maoni yangu, upungufu huu unaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za matengenezo, miundombinu duni ya barabara, hatari za usalama, na ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi.

**Ninapendekeza kuwa TARURA ihakikishe inafanya tafiti za kina na kuandaa usanifu wa kina unaojumuisha vipengele vyote muhimu. Hatua hii inapaswa kuambatana na utekelezaji madhubuti wa viwango vya ujenzi, kuimarisha hatua za udhibiti wa ubora, na kutenga bajeti ya kutosha ili kuhakikisha maendeleo ya miundombinu salama inayozingatia kanuni na yenye gharama nafuu.**

### 10.2.8 Dosari katika Utekelezaji wa Miradi ya Majaribio ya Barabara kwa Kutumia Teknolojia Mbadala Sh. bilioni 24.99

Katika mwaka wa fedha 2023/24, TARURA iliendelea na utekelezaji wa miradi ya majaribio ya ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia mbadala ya uimarishaji wa udongo. Mikataba minne yenye thamani ya Sh. bilioni 24.99 ilitekelezwa kwa kutumia teknolojia hizi mpya kama ilivyobainishwa kwenye **Jedwali Na. 59**.

**Jedwali Na.59: Utekelezaji wa Miradi ya Barabara kwa Teknolojia Mbadala**

| Na | Eneo | Namba ya Mkataba | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Teknolojia Iliyotumika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma-Chamwino | AE/092/2022/2023/HQ/W/29 | 7,874,965,401 | ECOROADS |
| 2 | Barabara ya Iringa-Kilolo Sawala - Mkonga - Iyegeya | AE/092/2022/2023/HQ/W/19 | 9,015,416,000 | ECOROADS |
| 3 | Barabara ya Pwani-Rufiji Utete – Kingupira | S10/2023/2024/W/17 | 4,769,050,000 | Enzymic Compound |
| 4 | Barabara ya Simiyu Itilima Oil - Ikindilo | S10/2023/2024/W/10 | 3,329,570,000 | Ecozyme |
| **Jumla** | | | **24,989,001,401** | |

**Chanzo:** Rejesta ya Mikataba

Uhakiki wa kitaalamu na kufuata vipengele vya mikataba miwili, Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/19 wenye thamani ya Sh. bilioni 9.01 kwa ajili ya ukarabati wa Barabara ya Sawala-Mkonga-Iyegeya iliyopo H/W ya Kilolo - Mkoa wa Iringa kwa kutumia ECOROADS, na mkataba Na. S10/2023/2024/W/10 wenye thamani ya Sh. bilioni 3.32 kwa ajili ya uboreshaji wa Barabara ya Itilima Oil-Ikindilo (km 5.2) katika H/W Itilima - Mkoa wa Simiyu kwa kutumia kemikali ya Ecozyme, ulibaini changamoto zifuatazo:

#### i) Kutokuwapo kwa Kibali cha Kutumia Teknolojia Mbadalaa kutoka Wizara ya Ujenzi

Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 385 la tarehe 5 Mei 2021, Wizara ya Ujenzi inawajibika kuweka viwango na kufuatilia uzingatiaji wa ubora katika ujenzi, ukarabati, na matengenezo ya barabara. Nilibaini TARURA inatekeleza miradi kwa kutumia technolojia mbadala bila kupata kibali kutoka Wizara ya Ujenzi, jambo ambalo linaweza

kusababisha kutozingatia viwango vya ujenzi, kuathiri uimara wa barabara, na kusababisha matatizo ya uzingatiaji wa sheria na uwezekano wa teknolojia hii kutodumu.

### ii) Ukosefu wa Viwango vya Mchanganyiko na Muda wa Ufanisi kwa Teknolojia ya ECOROADS

Sehemu ya 1.4.3 ya Mwongozo wa Usanifu wa Barabara za Lami (1999) inataka usanifu wa barabara ya lami unapaswa kulinda tabaka la msingi wa barabara na kuhakikisha uimara wake kwa kufanikisha kiwango cha chini cha CBR cha 15%. Katika ukaguzi wa barabara ya Sawala-Mkonge-Iyegeya-Lulanda (km 10) na nyaraka zake uliofanyika tarehe 18 Oktoba 2024 ilibainika kuwa ECOROADS haikuwa na viwango vilivyobainishwa kwa ajili ya mchanganyiko wala muda wa ufanisi wake. Jambo hili linaweza kuathiri uimara wa barabara, kupunguza muda wake wa matumizi, na kuongeza gharama za matengenezo.

### iii) Kutokufanyika kwa Uchambuzi wa Gharama kwa Matumizi ya ECOROADS

Ukaguzi ulibaini kuwa gharama za kushindilia udongo kwa kutumia ECOROADS ni nafuu kwa Sh. 14,400 kwa kila mita ya ujazo ikilinganishwa na njia ya jadi ya kutumia tabaka la C2 lililowekwa saruji. Hata hivyo, bila tathmini kamili ya gharama za muda mrefu, uchambuzi huu wa gharama za awali hauwezi kuhalalisha matumizi yake. Mchanganuo wa ulinganisho wa gharama umeoneshwa katika **Jedwali Na. 60.**

**Jedwali Na.60: Ulinganisho wa Gharama kati ya ECOROADS na Njia za Kawaida**

| Kipengele | Maelezo | Kitengo | Kiasi | Kiwango (Sh.) | Tofauti ya Gharama (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Kiasi cha Kemikali ya ECOROADS kinachotakiwa kwa mita ya ujazo | $M^3$ | 1 | 65,600 | |
| B | Tabaka lililowekwa saruji (C2) kwa mita ya ujazo | $M^3$ | 1 | 80,000 | 14,400 |

***Chanzo:*** *Makadirio ya gharama ya mkataba AE/092/2022/2023/HQ/W/19*

### iv) Ufanisi Mdogo wa Kemikali ya Ecozyme kwenye Mchanga na Udongo wa Changarawe

Kemikali za kuimarisha udongo zinapaswa kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwenye aina tofauti za udongo, au maboresho yafanyike ili kuendana na utofauti wa udongo. Miradi ya ujenzi wa barabara hutegemea miongozo ya udongo, kama vile AASHTO (American Association of State Highway and Transportation Officials) ili kuhakikisha kuwa kiimarisha udongo kilichochaguliwa kinastahili kulingana na hali ya udongo.

Hata hivyo, Mwongozo wa Matumizi wa Ecozyme unaonesha kuwa mfumo wa kipimo unahitaji udongo uwe na mfinyanzi wa kutosha ili kufikia kiwango cha plastiki (*Plasticity Index* - PI) iliyobainishwa. Kwa hiyo, uchanganyaji mzuri wa punjepunje za udongo pamoja na mfinyanzi unahitajika ili kufanikisha kiwango cha plastiki cha 15 au zaidi. Ikiwa udongo hauna mfinyanzi wa kutosha, kiwango cha uimarishaji wa udongo kinachotakiwa kinaweza kisifikiwe, hivyo kuhatarisha ubora wa miundombinu, kuongezeka kwa gharama za matengenezo, au kuharibika kwa barabara mapema. Hii inafanya utumiaji wa kemikali ya Ecozyme kuwa na mipaka katika aina za udongo.

### v) Kipengele cha Mazingira: Uharibifu wa Taratibu wa Tabaka la Barabara kwa Sababu ya Kuoza kwa Ecozyme

Viwango vya Vipimo vya Kazi za Barabara vya mwaka 2000 vinataka changarawe ziwe na viwango vilivyowekwa kabla na baada ya kuimarishwa, ambapo Kifungu cha 3802(a) kinataja viambata vinavyokubalika kwa ajili ya kuimarisha udongo kuwa ni chokaa ya barabara, saruji, au majivu mepesi. Uchaguzi wa kiambata cha kuimarisha udongo unapaswa kuzingatia vipimo maalumu au maelekezo ya mhandisi. Udongo ulioimarishwa unapaswa kubaki katika uimara wake kwa muda mrefu. Kutokana na asili yake ya kuoza, kemikali ya Ecozyme inaweza kuvunjwa polepole na vimelea, jambo ambalo linaweza kudhoofisha safu ya barabara, hivyo kuathiri uimara wa muda mrefu na ufanisi wa gharama katika mzunguko wa maisha ya barabara husika.

### vi) Kipengele cha Uendeshaji: Ukosefu wa Udhibiti wa Utengamano wa Ecozyme

Ukaguzi wa kemikali ya kuimarisha udongo (Ecozyme) umebaini changamoto kama vile kuwapo kwa mwongozo wa mtumiaji usiokamilika na udhibiti duni wa ubora. Mwongozo huo unakosa maelekezo muhimu kuhusu upimaji wa udongo, ikiwa ni pamoja na vigezo muhimu kama njia ya upangaji wa ubora wa udongo (*grading modulus*), kiwango cha juu cha plastiki (PI) baada ya uimarishwaji, na uimara wa changarawe (TFV-dry). Upungufu huu unazuia tathmini sahihi ya ufanisi wa uthabiti wa udongo na ufuatiliaji wa mchanganyo wake.

Masuala haya, pamoja na mwongozo duni wa mtumiaji na udhibiti usioridhisha wa uendeshaji, yanahatarisha uthabiti na uendelevu wa miradi ya majaribio.

**Ninapendekeza kuwa, TARURA ihakikishe inapata idhini rasmi kutoka Wizara ya Ujenzi kabla ya kutekeleza teknolojia mbadala ili kuhakikisha inakidhi viwango vya kitaifa vya ujenzi wa barabara. Vilevile, ninaishauri TARURA kufanya upimaji wa kina wa kimaabara kwa viambata vya uimarishaji wa udongo ili kubaini vigezo muhimu vinavyohitajika kama vile, viwango vya uchanganyaji na muda wa matumizi, pamoja na kufanya uchambuzi wa kina wa gharama na faida za teknolojia mbadala.**

**Ninashauri TARURA, kwa miradi ya baadaye, ihakikishe inafanya tathmini sahihi ya utangamano wa udongo na kutekeleza hatua mahususi za udhibiti wa ubora, ikiwamo upimaji ulio wazi. Mwisho, ninaishauri TARURA kufanya uchunguzi wa kina ili kutathmini uimara wa muda mrefu wa Ecozyme na viambata vingine vya uthabiti ili kuhakikisha miradi ya majaribio inazingatia viwango vya kiufundi na kimazingira.**

### 10.2.9 Upungufu Katika Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya Barabara yenye Thamani ya Sh. Bilioni 22.99

Ukaguzi wangu ulibaini upungufu mkubwa katika usimamizi wa mikataba, ikiwa ni pamoja na taarifa za kuvunjwa kwa mikataba kutopelekwa kwenye mamlaka husika, kushindwa kuwatoza wakandarasi fidia ya ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa miradi, kutoa

nyongeza ya muda wa mkataba bila sababu za msingi na kutotekeleza masharti ya mikataba kwa ufanisi.

TARURA katika Mkoa wa Tabora ilivunja mikataba minne yenye thamani ya Sh. bilioni 1.58 lakini haikupeleka taarifa ya kuvunjwa kwa mikataba hiyo kwa PPRA na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kama inavyotakiwa na Kanuni 113(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, hivyo kuzuia mamlaka hizo kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwafungia wakandarasi husika. Maelezo ya mikataba iliyovunjwa yanapatikana kwenye **Jedwali Na. 61.**

### Jedwali Na.61: Mikataba Iliyovunjwa Lakini Taarifa Zake Hazikupelekwa PPRA na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| Wilaya | Namba ya Mkataba | Tarehe ya Kuvunjwa | Thamani ya Mkataba (Sh.) |
|---|---|---|---|
| H/W Nzega | S10/025/2023/2024/W/79 | 26/8/2024 | 445,403,314 |
| H/W Nzega | S10/025/2023/2024/W/80 | 26/8/2024 | 441,800,271 |
| H/Mji Nzega | S10/025/2023/2024/W/52 | 26/8/2024 | 243,945,476 |
| H/W Uyui | S10/025/2023/2024/W/27 | 14/7/2024 | 458,118,000 |
| **Jumla** | | | **1,589,267,061** |

***Chanzo:*** *Majalada ya mikataba*

Katika Mkoa wa Mara, fidia ya ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa miradi kiasi cha Sh. milioni 283.59 hakikutozwa kwa wakandarasi waliocheleweshа kukamilisha miradi kwa kipindi cha kati ya siku 43 hadi 100, kinyume na Kanuni 112(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.

### Jedwali Na.62: Fidia ya Hasara Haikutolewa

| Namba ya Mkataba | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Siku za Ucheleweshaji | Kiasi cha Fidia ya Ucheleweshwaji (Sh.) | Fidia iliyotozwa (Sh.) | Kiasi cha Fidia Kisicholipwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| AE/092/2021/2022/MAR/W/50 | 459,509,322 | 100 | 68,926,398 | 37,909,515 | 31,016,883 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/60 | 358,412,085 | 76 | 40,858,978 | 0 | 40,858,978 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/68 | 305,855,537 | 100 | 45,878,330 | 0 | 45,878,330 |
| AE/092/2021/2022/MAR/W/89 | 199,864,000 | 100 | 29,976,600 | 0 | 29,976,600 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/53 | 152,000,000 | 100 | 22,800,000 | 0 | 22,800,000 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/51 | 474,787,800 | 43 | 30,623,813 | 0 | 30,623,813 |
| AE/092/2022/2023/MAR/W/56 | 549,627,500 | 100 | 82,444,125 | 0 | 82,444,125 |
| **Jumla** | | | | | **283,598,729** |

*Chanzo:* Majalada ya Mikataba

Vilevile, mikataba minne yenye thamani ya Sh. bilioni 1.51 ilikuwa na ukiukwaji wa masharti ya mkataba kutokana na kuchelewa kukamilisha miradi kwa kipindi cha zaidi ya siku 100, lakini mikataba hii haikuvunjwa kama ilivyoelekezwa chini ya Kifungu cha 69 cha Masharti ya Jumla ya mikataba hiyo.

### Jedwali Na.63: Mikataba iliyocheleweshwa zaidi ya muda unaokubalika na haikusitishwa

| Mkataba Na. | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Tarehe ya kumaliza iliyorekebishwa | Tarehe ya kumalizika kwa fidia ya ucheleweshaji | Tarehe halisi ya kumaliza kazi | Idadi ya siku baada ya tarehe ya kumalizika kwa fidia ya ucheleweshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| AE/092/2021/2022 /MAR/W/50 | 459,509,323 | 31/07/2023 | 08/11/2023 | 28/06/2024 | 233 |
| AE/092/2022/2023 /MAR/W/68 | 305,855,537 | 05/04/2023 | 11/07/2023 | 15/08/2024 | **401** |
| AE/092/2021/2022 /MAR/W/89 | 199,864,000 | 22/07/2023 | 13/11/2023 | 20/06/2024 | 220 |
| AE/092/2022/2023 /MAR/56 | 549,627,500 | 31/12/2023 | 09/04/2024 | Haijakamika | |
| **Jumla** | **1,514,856,360** | | | | |

*Chanzo*: Majala ya mikataba na taarifa za utekelezaji

Pia, ukaguzi ulibaini nyongeza za muda wa mikataba zilitolewa bila kuwapo sababu za msingi. Katika mikoa ya Mara, Njombe, na Mwanza, mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 4.77 ilipewa nyongeza za muda wa kukamilisha miradi bila kuwapo matukio ya kuhalalisha nyongeza za muda au sababu za msingi za kufanya hivyo. Mkoa wa Ruvuma ulibainika kuwa na nyongeza kubwa sana ambapo miradi 37 kati ya 61 yenye thamani ya Sh. bilioni 14.84 iliongezewa muda wa utekelezaji, na miradi 14 kati yake haikuwa imekamilika.

Kasoro hizi zinatokana na kutokuwapo kwa uangalizi wa kutosha na ufanisi mdogo kwenye kutekeleza masharti ya mikataba. Kuchelewa kukamilika kwa mradi kunaongeza gharama kutokana na kuchelewa kutoa huduma kwa wananchi na inaathiri maendeleo ya miundombinu. Pia, kushindwa kutekeleza masharti ya mikataba na sheria za manunuzi kunadhoofisha uwajibikaji, uwazi, na kuiweka TARURA kwenye hatari ya kuingia kwenye migogoro na kupoteza fedha.

**Ninaushauri uongozi wa TARURA kuhakikisha kuwa taarifa za mikataba yote inayovunjwa zinawasilishwa PPRA na Ofisi ya**

**Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa wakati na maafisa watakaoshindwa kufanya hivyo wachukuliwe hatua za uwajibikaji. Kuimarisha usimamizi wa mikataba kunahitaji udhibiti wa utoaji wa taarifa kwa wakati, ufuatiliaji, utunzaji wa nyaraka, pamoja na kutoza fidia pale miradi inapocheleweshwa.**

**Ili kuboresha utekelezaji wa miradi, ninashauri TARURA kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji ambao unataka kuwapo kwa sababu za kimaandishi za kuongeza muda wa mkataba. Vilevile, ninaishauri TARURA kuanzisha mafunzo na kuboresha zana za ufuatiliaji kwa watekelezaji wa miradi ili kufuatilia hatua muhimu za utekelezaji, kushughulikia ucheleweshaji mapema, na kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya mikataba na sheria za manunuzi.**

### 10.2.10 Utekelezaji wa Miradi ya Agri-Connect Nyuma ya Muda Uliopangwa

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilingia Mkataba Na. TZ/FED/039-797 na Tume ya Ulaya (European Commission) mnamo tarehe 25 Septemba 2008 kwa ajili ya mpango wa Agri-Connect, kwa kutengewa kiasi cha Euro milioni 48 (Sh. bilioni 113.85) kwa ajili ya kuboresha barabara za vijijini ili kuongeza ufikiaji wa masoko kwa bidhaa za kilimo. Mradi huu uligawanywa katika awamu tatu, ambapo awamu ya I (2016/17–2017/18) ilikua na Sh. bilioni 40.59, awamu ya II (2018/19–2019/20) ilikuwa na Sh. bilioni 38.77, na awamu ya III (2019/20–2020/21) ilikuwa na Sh. bilioni 34.48.

Hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/24, Sh. bilioni 96.61 zilikuwa zimekwishahamishiwa Bodi ya Mfuko wa Barabara, lakini utekelezaji wa awamu ya III ya mradi haukuwa umeanza. Aidha, awamu ya I ya mradi imekamilika kikamilifu kwa barabara zilizowekwa lami zenye urefu wa km 87.76, huku awamu ya II ya mradi ikiwa imekamilika kwa 71.8%, ikiwa na barabara zilizowekwa lami zenye urefu wa km 49.2.

Ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi umehusishwa na michakato ya muda mrefu ya uchaguzi wa barabara, uthibitishaji na uhakiki kutoka kwa Wizara ya Kilimo, pamoja na changamoto zilizotokana na mvua kubwa na ardhi iliyokaa vibaya. Ucheleweshaji huu unachelewesha ufikiaji wa masoko kwa wakulima na unaweza kusababisha ongezeko la gharama kutokana na mfumuko wa bei na changamoto nyingine za usafirishaji.

**Ninashauri kuwa, OR-TAMISEMI ifanye kazi kwa karibu na Wizara ya Kilimo, TARURA, na Bodi ya Mfuko wa Barabara kutatua changamoto hizi, na kwamba mapitio ya maendeleo ya mradi yafanyike ili kulinganisha matarajio na ratiba za utekelezaji.**

### 10.2.11 Kusimamishwa kwa Malipo ya Ada ya Utumiaji na Msajili wa Hazina (TR) Kinyume na Mkataba Sh. bilioni 2.009

Makubaliano yanayosimamia huduma za mwendeshaji mabasi yaendayo haraka kwa Awamu ya 1 ya Mfumo wa DART yanaelezea majukumu ya kifedha na michakato ya utatuzi wa migogoro. Kifungu cha 3.1 cha Kiambatisho Na. 4 cha Makubaliano ya Mtoahuduma wa Mpito (TSP) kati ya DART na UDART (kilichosainiwa tarehe 5 Agosti 2021) kinataka ada ya kutumia miundombinu ya Sh. milioni 20.03 kwa siku kubaki kwa Wakala (DART).

Uhakiki wa taarifa za kifedha za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ulionesha kuwa kulikuwa na kiasi cha Sh. milioni 869.93 kilichokuwa kinadaiwa kama ada ya utumiaji wa miundombinu ambacho hakikulipwa na UDART kutokana na kusitishwa kwa malipo na Msajili wa Hazina.

Nilibaini kuwa, tarehe 17 Oktoba 2024 Mtendaji Mkuu wa DART alimwandikia Msajili wa Hazina, barua yenye Kumb. Na. CDA.90/393/01-C/53 akisisitiza kuwapo kwa makubaliano ya pande mbili kutatua suala la malipo ya ada ya utumiaji wa miundombinu.

Aidha, kuanzia tarehe 9 Oktoba 2024 hadi tarehe 19 Novemba 2024, Msajili wa Hazina alisitisha kulipwa kwa jumla ya Sh. bilioni 1.14 ya ada ya kutumia miundombinu, na hivyo kufanya jumla ya ada ambazo hazijakusanywa kufikia sh. bilioni 2.009. Hali hii inahatarisha ukwasi wa kifedha wa Wakala (DART) na uendelevu wa shughuli zake.

**Nashauri kwamba DART na Msajili wa Hazina kufanya mazungumzo rasmi haraka ili kutatua kusimamishwa kwa malipo ya ada ya matumizi ya barabara, kuhakikisha makubaliano wazi na yanayoweza kutekelezeka kuhusu masharti ya malipo na utatuzi wa migogoro.**

### 10.2.12 Kutolipwa kwa Makato ya Utendaji Kutokana na Mtoahuduma wa Mpito Kushindwa Kukidhi Viwango vya Utendaji vya BRT Sh. bilioni 15.32

Kifungu cha 1.3 cha mkataba kati ya DART na UDART uliosainiwa tarehe 16 Agosti 2019 kinamtaka UDART (TSP) kuhakikisha kuwa 90% ya mabasi yanafanya kazi wakati wa masaa yenye abiria wengi, na 10% inayobaki kuwa tayari kutumika pale yatakapohitajika. Kushindwa kufikia kiwango hiki kunasababisha makato kama inavyoelezwa katika Jedwali la Kwanza (Kifungu 5(c)). Kifungu cha 1.4 kinasisitiza kuhusu kuzingatia muda, Kifungu cha 1.5 kinahitaji kudumisha ubora wa huduma na kuzuia kupakia abiria zaidi, na Kifungu cha 1.7 kinataka kuzingatia maagizo ya Afisa wa Usalama wakati wa matengenezo yasiyopangwa. Kushindwa kutimiza majukumu haya kunasababisha makato kama inavyoelezwa kwenye jedwali. Aidha, Kifungu cha 1.6 katika Jedwali Na. E kinataka makato husika yalilipwe ndani ya siku tatu za kazi baada ya kutoa ankara ya kila mwezi.

Uhakiki wa taarifa za kifedha kwa mwaka 2023/24 ulionesha kuwa mtoahuduma wa mpito alitozwa na faini zenye jumla ya Sh. bilioni 3.84 kutokana na kushindwa kutimiza viwango vya utendaji kama inavyoelezwa kwenye mkataba. Hili lilikuwa ongezeko la Sh. milioni 808.21 au 27%, ikilinganishwa na faini za mwaka uliopita za Sh. bilioni 3.033.

Kuongezeka kwa faini hizi kunahusiana na kushindwa kufikia viwango vya upatikanaji wa mabasi, uzingatiaji wa muda, na ubora wa huduma, na kusababisha malalamiko ya wateja kwa kutoridhika na huduma. Pia, hadi mnamo tarehe 30 Juni 2024, madeni ya faini za mtoahuduma wa mpito yalifikia Sh. bilioni 15.32. Hii inaashiria hatari kubwa ya kifedha ikiwa faini hizi zitaendelea kutolipwa.

Upungufu huu ulitokana na ukosefu wa ufuatiliaji na usimamizi mzuri wa utendaji wa mtoahuduma wa mpito, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa Mfumo wa Usafiri wa Kisasa (ITS) wa kufuatilia ubora wa huduma na kuzingatia viwango. Kushuka kwa ubora wa huduma kumechangia wateja kutoridhika na huduma inayotolewa. Pia, na madeni ya makato yaliyopo yanaashiria uwezo mdogo wa DART kukusanya deni hili.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti ya DART itekeleze Mfumo wa Usafiri wa Kisasa (ITS) ili kuboresha ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli; ihakikishe inazingatia kwa makini viwango vya utendaji ili**

**kufikia kiwango cha huduma kinachokusudiwa; na kuimarisha juhudi za kukusanya faini zilizotozwa.**

### 10.2.13 Upungufu wa Mabasi ya UDART Unasababisha Kudorora kwa Huduma za Usafiri

Utoaji wa usafiri ulioelezewa katika Kifungu cha 5 cha Makubaliano na Mtoahuduma wa Mpito UDART (TSP) na DART uliosainiwa tarehe 16 Agosti 2019, kinaitaka UDART itoe usafiri wa Mabasi 140 na iwe nyongeza ya mabasi 70, hivyo kufikisha jumla ya mabasi 210 yanayotakiwa kama ilivyoelekezwa chini ya kifungu cha 2.1 cha Kiambatisho Na. 4 cha makubaliano kilichosainiwa tarehe 5 Agosti 2021.

Hata hivyo, hadi tarehe 22 Novemba 2024, ni mabasi 111 tu yalikuwa yanatumika, huku mabasi 99 yakishindwa kufanya kazi kutokana na sababu mbalimbali, ambapo mabasi 88 yalikuwa hayatumiki kwa sababu ya ubovu, mabasi 2 yaliungua kwa moto na mabasi 9 yalikuwa katika matengenezo. Upungufu huu wa 49% ya mabasi yaliyotakiwa kuwapo umesababisha misongamano katika mabasi, kuchelewa kwa huduma, na kutokidhi mahitaji ya abiria, hali ambayo inaathiri ubora na uhakika wa huduma za usafiri.

Tatizo hili lilitokana na kutokuwapo kwa matengenezo ya mara kwa mara kutoka kwa mtoahuduma wa mpito, hivyo kushindwa kutimiza mahitaji ya mabasi yaliyowekwa kwenye mkataba. Kushindwa kutekeleza kifungu cha 5 cha mkataba kunaathiri uwezo wa DART kutoa huduma za usafiri wa umma zenye ufanisi na uhakika.

**Nashauri kwamba uongozi wa DART kuimarisha utekelezaji wa masharti ya matengenezo na upatikanaji wa magari kwa kuweka motisha kulingana na utendaji. Mtoahuduma anapaswa kuwasilisha na kutekeleza mpango wa matengenezo, huku ukaguzi wa mara kwa mara ukifanywa na timu huru ya kiufundi.**

**Vilevile, nashauri DART kutafuta watoa huduma mbadala ili kushughulikia upungufu na kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji wa wakati halisi wa upatikanaji wa magari na huduma. Hatua hizi zitaboresha ufanisi, kupunguza msongamano, na kuboresha huduma za usafiri wa umma.**

## 10.3 Sekta ya Afya

Sekta ya afya ni muhimu katika kukuza maendeleo ya taifa, kuhakikisha ustawi wa watu wake, na kujenga nguvu kazi imara. Ili kuimarisha huduma za afya, Serikali imetekeleza mipango kadhaa, kama vile kujenga vituo vipya vya afya, kukarabati vilivyopo, kusambaza vifaatiba na dawa muhimu, na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa muhimu vya matibabu.

Hata hivyo, wakati wa tathmini ya utoaji wa huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, nilibaini kuwa sekta ya afya bado inakabiliwa na changamoto kadhaa, zikiwamo ukosefu wa miundombinu, uhaba wa dawa na vifaatiba, upotevu wa fedha unaosababishwa na madai ya bima ya afya kukataliwa, dawa zilizoisha muda wake wa matumizi, upungufu katika usambazaji wa dawa na vifaatiba kutoka Bohari ya Dawa (MSD).

Sehemu hii inabainisha changamoto zinazoikabili sekta ya afya, ikiangazia maeneo muhimu yanayohitaji uangalizi na usimamizi, na kupendekeza hatua kwa Serikali na wadau wengine kushughulikia changamoto hizi.

### 10.3.1 Tathmini na Usimamizi wa Fedha za Sekta ya Afya

#### (i) Halmashauri kupoteza mapato kutokana na Madai ya Bima ya Afya kukataliwa Sh. bilioni 1.34

Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395, kinabainisha kuwa Mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai ya yasiyo sahihi au pale wadai wanaposhindwa kuzingatia kanuni au taratibu za malipo ya madai yaliyotolewa.

Tathmini yangu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ilionesha kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulikataa kurejesha Sh. bilioni 1.34 kwa halmashauri 35. Kukataa huko kulisababishwa na makosa mbalimbali katika fomu za madai za NHIF zilizowasilishwa. Makosa hayo ni kama vile uidhinishaji usio sahihi, alama (codes) za magonjwa zisizo sahihi, na kutozingatia miongozo ya kawaida ya matibabu. Halmashauri ziliwasilisha madai ya jumla ya Sh. bilioni 8.27, ambapo NHIF ilifanikiwa kurejesha Sh. bilioni 6.93, na kusababisha kiasi cha Sh. bilioni 1.34 kukataliwa. Hii ni sawa na 16% ya jumla ya madai yaliyowasilishwa, kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na.39**.

**Ninaishauri Serikali kupitia TAMISEMI na Wizara ya Afya kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kutoa mafunzo ya kushughulikia madai ya bima ili kuboresha usahihi wa kujaza fomu za madai ya NHIF.**

### (ii) Madai ya Muda Mrefu Ambayo Hayajarejeshwa na Mfuko wa Bima ya Afya Sh. milioni 660.17

Kifungu cha 27(1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395 kinautaka Mfuko kuingia mkataba na kila mtoahuduma ya afya ili kuhakikisha kuwa kuna mifumo ya ufuatiliaji ili kujilinda dhidi ya matumizi makubwa ya huduma za afya; matumizi duni ya huduma za afya; taratibu zisizohitajika za vipimo na matibabu; dawa zisizo idhinishwa; na rufaa zisizofuata utaratibu. Pia, mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai yasiyo sahihi au pale mdai anaposhindwa bila sababu za msingi kuzingatia sheria au kanuni zinazohusu malipo ya madai yaliyotolewa chini ya Sheria hii.

Nilibaini kuwa halmashauri 8 zilizotoa huduma kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya zilipata ucheleweshaji mkubwa wa marejesho ya fedha zinazodaiwa, kiasi cha Sh. milioni 660.17. Aidha, hapakuwa na mrejesho wowote kutoka Bima kwa zaidi ya siku 60 kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 64.**

**Jedwali Na.64: Madai yasiyorejeshwa na Mfuko wa Bima ya Afya**

| Na | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Idadi ya siku zilizochelewa |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dodoma | 309,876,892 | 80-240 |
| 2. | H/W Nanyumbu | 132,095,632 | 120 |
| 3. | H/W Longido | 44,041,736 | 240 |
| 4. | H/Jiji Arusha | 40,748,855 | 240 |
| 5. | H/W Kongwa | 34,101,711 | 120 |
| 6. | H/W Msalala | 16,830,504 | 300 |
| 7. | H/W Mtwara | 11,912,682 | 180-480 |
| 8. | H/W Bagamoyo | 70,564,535 | 240 |
| **Jumla** | | **660,172,547** | |

***Chanzo:*** Fomu za madai ya Halmashauri na fomu za marejesho ya NHIF

Kushindwa kulipa kiasi kinachodaiwa kwa wakati, kama inavyotakiwa na mkataba, kunasababisha kutotolewa kwa huduma za afya kwa jamii kutokana na uhaba wa fedha.

**Ninaishauri Serikali kupitia TAMISEMI na Wizara ya Afya kufuatilia na kuhakikisha kuwa fedha zote zinazodaiwa zinalipwa kwa muda unaotakiwa ili kuwezesha utoaji bora wa huduma za afya.**

### (iii) Hasara Iliyotokana na Dawa Zilizokwisha Muda wake Sh. bilioni 1.73

Aya ya 4.11 na 4.14 ya Mkataba wa Makubaliano kati ya Bohari ya Dawa (MSD) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaitaka MSD kupanga utaratibu wa uteketezaji wa bidhaa za afya zilizokwisha muda wake au zilizoharibika na kuiarifu Wizara ya Afya kuhusu upatikanaji wa bidhaa za afya zilizokaa kwa muda mrefu (zaidi ya miezi kumi).

Katika ukaguzi wa rejista za dawa zilizoisha muda wake wa matumizi, nilibaini halmashauri 13 zilizokuwa na dawa zilizoisha muda wake kwa muda wa kuanzia miezi mitatu hadi miaka 10 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.73 ambazo hazijateketezwa. Dawa zilizoisha muda wake zinaweza kuwa zimesababishwa na ununuzi au upokeaji wa dawa zinazokaribia kuisha muda wa matumizi kutoka Bohari ya Dawa na ukosefu wa mpangilio mzuri wa dawa zilizopokelewa ili kuhakikisha kuwa dawa zinatolewa kwa msingi wa kutoa dawa zilizotangulia kupokelewa. Halmashauri husika zilizo na dawa zilizoisha muda wake wa matumizi Pamoja na thamani yake zimeonyeshwa kwenye **Jedwali 65**.

**Jedwali Na.65: Halmashauri zenye dawa zilizoisha muda wa matumizi**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---:|
| 1 | H/W Maswa | 765,712,335 |
| 2 | H/Jiji Tanga | 239,288,938 |
| 3 | H/W Gairo | 219,126,323 |
| 4 | H/W Pangani | 175,307,677 |
| 5 | H/W Mkalama | 78,394,351 |
| 6 | H/W Longido | 66,576,983 |
| 7 | H/W Handeni | 51,905,340 |
| 8 | H/W Chalinze | 40,386,699 |
| 9 | H/W Ruangwa | 33,442,647 |
| 10 | H/W Mtwara | 18,616,601 |
| 11 | H/W Kisarawe | 18,354,164 |
| 12 | H/W Kilindi | 16,150,665 |
| 13 | H/W Tandahimba | 3,391,668 |
| | **Jumla** | **1,726,654,391** |

**Chanzo: Rejista za dawa zilizoisha muda wa matumizi**

Pamoja na hasara ya Sh. bilioni 1.73 pia uhifadhi wa dawa zilizokwisha muda wake unaweza kusababisha madhara kwa umma iwapo zitatumiwa kwa bahati mbaya au zikitua mikononi mwa watu wasio waaminifu.

**Ninaishauri Serikali kuhakikisha Halmashauri husika zenye dawa zilizoisha muda wake zinateketeza dawa hizo kwa mujibu wa matakwa ya sheria. Zaidi ya hayo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kusimamia ipasavyo uagizaji na upokeaji wa dawa kwa kuzingatia mahitaji yaliyotathminiwa vizuri ili kuepuka kupoteza rasilimali ambazo zingeweza kutumika katika maeneo yenye uhitaji zaidi.**

### (iv) Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Dawa na Vifaa vya Tiba Kuelekezwa kwenye Matumizi Mengine Sh. bilioni 4.75

Aya ya 3.2(i) ya Maelekezo ya Usimamizi wa Mfuko wa Uchangiaji wa Gharama (cost sharing) yaliyotolewa na Wizara ya Afya mwaka 2017 inataka 50% ya makusanyo ya mapato ya papo kwa papo (user fee) itengwe kwa ajili ya ununuzi wa dawa, na vifaatiba.

Katika tathmini yangu niliyoifanya kuhusu usimamizi wa fedha za uchangiaji gharama za afya zilizokusanywa katika halmashauri 10, nilibaini kuwa jumla ya Sh. bilioni 17.55 zilikusanywa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. bilioni 8.78 kilipaswa kutengwe kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Hata hivyo, nilibaini kuwa Sh. bilioni 4.44 kutoka kwenye fedha za kuchangia gharama zilielekezwa kwenye matumizi mengine, ikiwamo posho na matumizi ya kawaida kama inavyobainishwa kwenye **Jedwali Na. 66**.

**Jedwali Na.66: Fedha za uchangiaji wa gharama za dawa na vifaatiba zilizobadilishiwa matumizi**

| Na | Halmashauri | Kiasi Kilichokusanywa (Sh.) | 50% Kiasi kilichohitajika (Sh.) | Kiasi Tumika (Sh.) | Kiasi kilichobadilishiwa matumizi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/J Dar | 7,611,604,634 | 3,805,802,319 | 1,526,839,787 | 2,278,962,532 |
| 2 | H/M Ubungo | 4,462,266,117 | 2,231,133,058 | 1,416,672,879 | 814,460,179 |
| 3 | H/M Kigamboni | 1,422,353,512 | 711,176,757 | 251,793,435 | 459,383,322 |
| 4 | H/J Dodoma | 1,485,208,061 | 742,604,030 | 342,131,526 | 400,472,504 |
| 5 | H/J Mwanza | 697,197,026 | 348,598,513 | 87,360,117 | 261,238,396 |
| 6 | H/W Handeni | 549,837,850 | 274,918,925 | 47,100,592 | 227,818,333 |
| 7 | H/W Kyela | 583,527,015 | 291,763,508 | 97,685,382 | 194,078,126 |
| 8 | H/J Mbeya | 496,589,776 | 248,294,888 | 180,712,844 | 67,582,044 |
| 9 | H/W Shinyanga | 62,282,141 | 31,141,071 | 4,584,900 | 26,556,171 |
| 10 | H/W Kongwa | 183,905,180 | 91,952,590 | 76,150,832 | 15,801,758 |
| | **Jumla** | **17,554,771,312** | **8,777,385,659** | **4,031,032,294** | **4,746,353,365** |

***Chanzo***: Taarifa za makusanyo kutoka mfumo wa GoTHOMIS

Kutotengwa kwa fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa na vifaatiba kunakwamisha juhudi za serikali za kuboresha huduma za afya kwa jamii. Utaratibu huu unadhoofisha ufanisi wa utoaji huduma na kupunguza ubora wa huduma inayopatikana kwa umma.

**Ninapendekeza kwa uongozi wa halmashauri husika kuhakikisha vituo vya afya vinatenga 50% inayohitajika kutoka kwenye makusanyo ya uchangiaji wa gharama kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.**

### 10.3.2 Ukaguzi wa Huduma Zinazotolewa na MSD kwa Halmashauri

#### (i) Upungufu uliobainika kwa Bohari ya Dawa katika Usambazaji wa Vifaatiba kwa Halmashauri Sh. bilioni 9.44

Aya ya 9 (a) ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa MSD inabainisha kwamba mchakato wa agizo la maalumu ya vituo vya huduma za afya kuchukua angalau miezi miwili tangu tarehe ya kuagiza. Pia, kifungu cha 10.1 cha Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa MSD wa mwaka 2021 kinahitaji upatikanaji wa vifaatiba kwa wakati kwa bei nafuu, upatikanaji wa mahitaji ya mteja kama ilivyoombwa, na mchakato wa manunuzi kuchukua muda wa miezi mitatu tangu wakati malipo yafanyike na mteja hadi bidhaa zinapokelewa.

Nilipitia taarifa za vifaatiba vilivyonunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa Bohari ya dawa (MSD) ilipewa kazi ya kununua na kusambaza vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 14.39 katika halmashauri 31. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2024 vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.70 vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya afya. Aidha, vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 7.69 havijatolewa kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na.40**.

Pia, nilibaini kuwa halmashauri 4 zilikuwa na Sh. bilioni 6.40 kama ruzuku iliyowekwa MSD na Wizara ya Afya kwa ajili ya vifaatiba. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2024 MSD iliweza kusambaza dawa na vifaatiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.65, sawa na 73%, kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 67.**

**Jedwali Na.67: Halmashauri zenye salio la fedha MSD**

| Na. | Halmashauri | Kiasi pokelewa (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Kiasi kilichosalia (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Busega | 859,360,047 | 696,272,598 | 163,087,449 |
| 2. | H/W Karatu | 1,626,032,833 | 1,454,732,782 | 171,300,051 |

| Na. | Halmashauri | Kiasi pokelewa (Sh.) | Kiasi kilichotumika (Sh.) | Kiasi kilichosalia (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 3. | H/W Mbogwe | 1,184,861,609 | 599,148,618 | 585,712,991 |
| 4. | H/W Kilosa | 2,726,248,593 | 1,898,494,082 | 827,754,511 |
| Jumla | | **6,396,503,082** | **4,648,648,080** | **1,747,855,002** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Halmashauri kutoka Bohari ya Dawa*

Fedha zilizosalia Bohari ya Dawa sio tu kwamba zilipunguza upatikanaji wa dawa na vifaatiba katika vituo vya afya, bali pia zilipunguza utoaji wa huduma bora za matibabu. Niliripoti changamoto kama hiyo katika ripoti iliyopita kwamba Sh. bilioni 8.37 hazijatumika na Bohari ya Dawa. Hii inamaanisha kuwa menejimenti haijatekeleza ipasavyo mapendekezo yaliyotolewa.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Afya ihakikishe Bohari ya Dawa inasambaza vifaatiba na vifaa kwa wakati. Pia, katika mazingira ambayo Bohari ya Dawa haina vifaatiba, utaratibu mbadala uzingatiwe ili kuwezesha halmashauri kununua kutoka kwa wazabuni wengine kwa bei nzuri.**

### (ii) Vifaa tiba Vilivyofikishwa kwenye vituo vya Afya na havitumiki Sh. bilioni 3.85

Nilifanya uhakiki katika vituo vya afya katika halmashauri 25 na kubaini kuwa vifaatiba vilivyonunuliwa vyenye thamani ya Sh. bilioni 3.85 bado havijaanza kutumika.

Pia, nilibaini kutotumika kwa vifaatiba kumesababishwa na ukosefu wa wataalamu maalumu kama vile radiografa, pamoja na miundombinu duni ya kuwezesha vifaa hivyo kutumika; kama vile ukosefu wa umeme, uhaba wa majengo, uhaba wa nafasi ya kutunza vifaa vilivyoletwa na ukosefu wa mafunzo na upungufu wa vitendanishi. Maelezo yanaonyeshwa katika **Jedwali Na. 68.**

**Jedwali Na.68: Halmashauri zenye vifaa tiba visivyotumika**

| Na | Jina | Kiasi (Sh.) | Na | Jina | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Busoga | 684,809,300 | 14 | H/W Hai | 110,433,849 |
| 2 | H/Mji Kahama | 340,260,252 | 15 | H/W Geita | 118,943,730 |
| 3 | H/W Kaliua | 339,409,468 | 16 | H/W Msalala | 104,679,589 |
| 4 | H/W Kongwa | 222,483,183 | 17 | H/W Kibaha | 101,762,027 |
| 5 | H/W Kilindi | 213,214,539 | 18 | H/M Tabora | 100,534,000 |
| 6 | H/W Mlele | 208,893,351 | 19 | H/W Igunga | 84,000,000 |
| 7 | H/W Liwale | 204,441,854 | 20 | H/M Sumbawanga | 78,571,356 |
| 8 | H/W Lushoto | 179,999,701 | 21 | H/W Ulanga | 50,561,980 |
| 9 | H/Jiji Arusha | 168,582,107 | 22 | H/W Mpimbwe | 37,782,949 |

| Na | Jina | Kiasi (Sh.) | Na | Jina | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 10 | H/W Longido | 150,000,000 | 23 | H/W Arusha | 29,530,980 |
| 11 | H/M Moshi | 121,292,134 | 24 | H/M Handeni | 25,325,826 |
| 12 | H/W Mtwara | 139,338,506 | 25 | H/WPangani | 19,160,133 |
| 13 | H/W Ruangwa | 137,149,666 | | **Jumla** | **3,852,216,750** |

**Chanzo:** *Ziara kwenye vituo vya afya*

Thamani inayotarajiwa ya pesa na manufaa kutoka kwa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 3.85 bado haijapatikana kama ilivyotarajiwa. Zaidi ya hayo, vifaa vinaharibika kutokana na uchakavu kabla ya kuanza kutumika.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, ihakikishe vifaatiba vinavyonunuliwa kwa ajili ya halmashauri vinatumika kwa kuweka vipaumbele vya upatikanaji wa miundombinu pamoja na kuwa na wataalamu wa afya wa kutosha.**

### 10.3.3 Tathmini ya Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF)

Aya ya 2(i) na (ii) ya Mwongozo Na. 1 wa utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa wa mwaka 2018 inaeleza kuwa Katibu Tawala wa Mkoa (RAS) ana jukumu la kusimamia utekelezaji bora wa iCHF kwa kuzingatia matakwa ya kimuundo yaliyofanyiwa marekebisho katika ngazi zote. Zaidi ya hayo, Katibu Tawala ana jukumu la kuongeza ufahamu na mipango ya uhamasishaji ili kukuza ushiriki wa jamii katika iCHF. Tathmini yangu ya utekelezaji wa mwongozo huo imebaini kasoro zifuatazo:

#### (i) Kutofikiwa kwa Lengo la iCHF la Uandikishaji wa Kaya

Waraka Na. 1 (Na.CD.151/161/01''C''/46) wa tarehe 06 Aprili 2018 kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI unazitaka Sekretarieti za Mikoa kuongeza uelewa na uhamasishaji kwa jamii, kujiunga na iCHF, na kuhakikisha kila mkoa unafikia lengo la uandikishaji wa kaya mpya.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Sekretarieti za Mikoa 17 zilishindwa kufikia idadi ya kaya zilizoandikishwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024 ni kaya 159,773 tu ndizo zilizoandikishwa kati ya kaya 1,247,474 zilizolengwa. Taarifa ya uandikishaji imeonyeshwa kwenye **Jedwali Na.69**.

**Jedwali Na.69: Hali ya uandikishaji wa kaya mpya kwenye mpango wa iCHF**

| Na. | Sekretarieti | Malengo ya uandikishaji | Uandikishaji halisi | Asilimia ya uandikishaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tabora | 4,819 | 2,968 | 62% |
| 2 | Katavi | 14,950 | 8,635 | 58% |
| 3 | Kilimanjaro | 7,356 | 2,921 | 40% |
| 4 | Ruvuma | 140,047 | 31,767 | 23% |
| 5 | Pwani | 19,167 | 4,219 | 22% |
| 6 | Mwanza | 14,157 | 2,505 | 18% |
| 7 | Tanga | 146,955 | 25,569 | 17% |
| 8 | Iringa | 247,717 | 36,664 | 14% |
| 9 | Morogoro | 82,990 | 10,873 | 13% |
| 10 | Morogoro | 82,990 | 10,873 | 13% |
| 11 | Mbeya | 31,505 | 4,123 | 13% |
| 12 | Singida | 38,939 | 4,573 | 12% |
| 13 | Lindi | 52,085 | 3,378 | 6% |
| 14 | Shinyanga | 86,378 | 5,188 | 6% |
| 15 | Mtwara | 49,309 | 1,562 | 3% |
| 16 | Mara | 32,179 | 905 | 3% |
| 17 | Njombe | 195,931 | 3,050 | 2% |
| | **Jumla** | **1,247,474** | **159,773** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za uandikishaji kutoka kwenye mfumo wa IMIS*

Hali hii ya uandikishwaji hafifu katika mpango wa iCHF unahusishwa na kaya nyingi kusita kujiunga kutokana na ufinyu wa huduma za afya ikilinganishwa na bima nyingine kama Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Kadhalika, changamoto za kiufundi ndani ya mfumo wa IMIS, hasa wakati wa mchakato wa usajili, pamoja na kiwango kikubwa cha maofisa wanaoandikisha kujitoa kwenye bima katika ngazi za kata na vijiji. Changamoto hizi zinapelekea hatari kwa maendeleo endelevu na mafanikio ya Mfuko.

**Ninapendekeza kwamba uongozi wa Sekretarieti za Mikoa husika zishirikiane na Wizara ya Afya kuhamasisha jamii kuhusu manufaa ya bima ya iCHF ili kuwawezesha kuweka nia ya kujiunga, hivyo kuboresha na kupanua wigo wa utoaji huduma.**

### (ii) Kutotolewa kwa fedha pacha (matching grants) za iCHF Sh. bilioni 1.37

Waraka Na.1 wa uboreshaji wa CHF wenye Kumb. CD.151/161/01 ‘‘C’’/46 wa tarehe 06 Aprili 2018 unataka mchango wa mwanachama wa ICHF kuwa Sh.30,000 kila mwaka kwa walengwa sita wa familia/kaya, ambapo serikali itachangia kiasi hichohicho kama nyongeza ya kuwezesha utoaji wa huduma bora katika ngazi ya zahanati hadi hospitali za rufaa.

Nilibaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya mchango wa Sh. bilioni 1.37 ulikusanywa kutoka kwa kaya katika sekretarieti za mikoa

6. Hata hivyo, Serikali Kuu haikutoa fedha zinazolingana na kiasi hicho kilichokusanywa. Maelezo yanaonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 70.**

**Jedwali Na.70: Ruzuku zinazolingana ambazo hazijatolewa**

| Na. | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Kagera | 822,366,748 |
| 2 | Kilimanjaro | 226,346,384 |
| 3 | Pwani | 125,358,943 |
| 4 | Manyara | 119,490,000 |
| 5 | Mtwara | 46,860,000 |
| 6 | Mara | 27,150,000 |
| | **Jumla** | **1,367,572,075** |

*Chanzo:* Taarifa ya makusanyo kutoka mfumo wa CHF-IMIS

Ninahusisha hili na ufinyu wa bajeti na mifumo duni ya usimamizi na ufuatiliaji ili kuhakikisha uzingatiaji wa maagizo ya waraka. Matokeo haya yana athari hasi katika utoaji wa huduma za afya katika vituo husika.

**Ninapendekeza kuwa Serikali Kuu, kupitia Wizara ya Afya, iharakishe kutoa ruzuku husika. Hatua hii itawezesha utoaji wa huduma bora za afya na kuhakikisha kuwa rasilimali fedha zinazohitajika zinapatikana kwa ajili ya uendeshaji bora wa mpango wa iCHF, hivyo kunufaisha jamii.**

### (iii) Ucheleweshaji wa Malipo Ya iCHF kwa Vituo vya Afya Sh. milioni 599.07

Aya ya 2.2.2 ya mwongozo wa iCHF kuhusu usimamizi wa fedha za iCHF inaelekeza malipo kufanywa kabla ya siku ya 10 ya mwezi unaofuata.

Mapitio yangu ya ripoti za madai ya matibabu yaliyowasilishwa kutoka vituo vya afya kwa ajili ya huduma zinazotolewa kupitia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Bima (CHF-Insurance Management Information System (IMIS)) katika sekretarieti za mikoa 6, nilibaini ucheleweshaji wa hadi siku 360 katika kulipa madai ya matibabu yaliyowasilishwa na vituo vya afya, kinyume na matakwa ya aya ya 2.2.2 ya mwongozo wa iCHF kuhusu usimamizi wa mfuko kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 71**.

**Jedwali Na.71: Madai yaliyocheleweshwa**

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) | Siku zimechelewa |
|---|---|---|---|
| 1 | Tanga | 44,106,678 | 10 hadi 12 |
| 2 | Dar es Salaam | 409,583,708 | 11 hadi 283 |
| 3 | Mara | 10,254,666 | 11 hadi 90 |
| 4 | Shinyanga | 58,003,683 | 30 hadi 360 |
| 5 | Simiyu | 21,959,108 | 60 hadi 180 |
| 6 | Ruvuma | 55,158,087 | 60 hadi 180 |

| Na | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) | Siku zimechelewa |
|---|---|---|---|
| Jumla | | 599,065,930 | |

***Chanzo:*** *Taarifa za madai ya matibabu*

Ninahusisha suala hili na sekretarieti za mikoa kushindwa kushughulikia na kulipa madai kwa wakati pamoja na muda mrefu unaohitajika kuanzisha na kupata kibali cha malipo. Kucheleweshwa kwa malipo kunaweza kusababisha ukosefu wa fedha, hatimaye kuathiri uwezo wa vituo vya afya kutoa huduma bora za afya kwa jamii.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kupitia OR - TAMISEMI na Wizara ya Afya, ifuatilie na kuhakikisha malipo ya awali na idhini ya malipo yanapatikana kwa wakati. Aidha, Sekretarieti za mikoa husika zilipe madai halali ndani ya muda uliopangwa.**

## 10.4 Usimamizi wa Mali

Usimamizi wa mali ni mbinu ya kimfumo ya utawala na uboreshaji wa thamani ya mali ambazo taasisi inawajibika kuzisimamia katika mzunguko wake wote wa maisha. Mchakato huu unahusisha ununuzi, matumizi, matengenezo, uendeshaji, ufuatiliaji, na uondoaji wa mali husika kwa njia yenye tija na ya gharama nafuu, ili kuongeza ufanisi wake pamoja na kuboresha huduma zinazotolewa na taasisi.

Sehemu hii inachambua mambo muhimu ya usimamizi na matengenezo ya mali zisizohamishika kama vile magari na majengo. Aidha, inahusisha masuala ya usimamizi wa ardhi (kama vile ugawaji, matumizi, utatuzi wa migogoro, na uzingatizi wa mifumo ya kisheria). Sehemu hii pia inaangazia changamoto kama vile migogoro ya ardhi, ardhi iliyopimwa lakini haijaendelezwa, ucheleweshaji wa utaratibu wa kushugulikia na utoaji wa hatimiliki. Aidha, inapendekeza hatua mwafaka za kushughulikia changamoto hizo ipasavyo.

Ukaguzi wangu kuhusu usimamizi wa mali umebaini masuala yanayohitaji uangalizi wa Serikali kama ifuatavyo:

### 10.4.1 Usimamizi Usioridhisha wa Mali Zilizoharibika na Chakavu

Aya ya 14 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma, 2019 inamtaka kila afisa masuuli kuandaa na kufuata mpango wa matengenezo na marekebisho ya mali ili kuhakikisha kuwa mali zinabaki kuwa katika hali nzuri na zinasaidia katika utoaji wa huduma na zinatumika kwa wakati wote kwa malengo yaliyokusudiwa kwa manufaa ya taasisi husika. Aidha, Agizo la 45(1) la Randama ya Fedha kwa Serikali za Mitaa

kinahimiza utambuzi na uondoaji wa mali chakavu kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuharibika, kupitwa na wakati, kuchakaa au kutofaa kwa matumizi baada ya kupata idhini ya Kamati ya Fedha na Mipango na Baraza la Madiwani husika.

Nilibaini kuwa katika taasisi 81 kulikuwa na jumla ya magari 552, pikipiki 98 na mali nyingine za kudumu 20 kama vile matrekta, mitambo, jenereta yakiwa yameachwa bila kufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu au kuchelewa kuuzwa kwa mali ambazo ni chakavu kwa kuzingatia taratibu za uuzaji wa mali za umma. Orodha ya taasisi na idadi ya mali chakavu imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.41.**

Dosari hii imesababishwa na menejimenti za taasisi husika kutokuwa na mipango madhubuti kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya mali zilizoharibika na kushindwa kufanya maamuzi sahihi kwa wakati ya uondoshaji wa mali chakavu. Kutotengeneza mali zilizoharibika kunaweza kuongeza kasi ya uharibifu, uchakavu, kupunguza muda wake wa matumizi na manufaa yaliyotarajiwa. Aidha, hali hii inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli ambazo zilipaswa kuwezeshwa na vyombo hivi, hivyo kuathiri utendaji kazi wa taasisi husika.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa taasisi husika zinaandaa na kutekeleza mipango madhubuti ya matengenezo ili kuhakikisha mtengenezo, ukarabati au uondoshaji wa mali zilizoharibika unafanyika kwa wakati. Hii itasaidia kuongeza muda wa matumizi ya mali, kuzuia kuharibika zaidi, na kuboresha ufanisi wa jumla katika utoaji wa huduma.**

### 10.4.2 Magari na Mali Nyingine ambazo Hazijakatiwa Bima

Agizo 95(1) la Randama ya Fedha kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 linawataka maafisa usafirishaji kuhakikisha kuwa magari yote yanakatiwa bima kulingana na matakwa ya kisheria na kwamba malipo ya bima yanatakiwa kufanyika kwa wakati.

Hata hivyo, nilibaini kuwa halmashauri 34 na sekretarieti zilikuwa na jumla ya mali 389, ikijumuisha magari 306, pikipiki na mitambo 83 zilizokuwa zinatumika bila ya kuwa na bima hai. Hii ni kinyume na agizo tajwa hapo juu. Orodha ya taasisi zenye magari, pikipiki na mitambo isiyokuwa na bima imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.42.**

Kasoro hii imetokana na menejimenti ya taasisi husika kushindwa kutenga bajeti na kutoa fedha kwa ajili ya gharama za bima. Kuendesha mali bila bima kunaziweka taasisi hizi katika hatariya kupata hasara kwa kuingia gharama za matengenezo, fidia au ununuzi wa magari mapya endapo ajali itatokea.

**Ninapendekeza kwa Serikali ihakikishe taasisi zote husika zinajumusha gharama za bima kwenye bajeti zake za kila mwaka na zinakata bima kwa mali zinazohusika.**

### 10.4.3 Kutokuwekwa Nambari za Utambulisho katika Mali za Kudumu zenye Thamani ya Sh. bilioni 53.15

Agizo la 63(5) cha Randama ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya Mwaka 2009 linataka mali zote zisizohamishika ziandikwe kwenye rejista ya mali za kudumu na kupatiwa namba za msimbo kwa urahisi wa kutambulika.

Nilifanya uhakiki wa mali kwa sampuli, na kubaini kwamba mamlaka za serikali za mitaa 17 zilikuwa na mali mbalimbali za kudumu zenye thamani ya Sh. bilioni 53.15 ambazo hazikuwekwa namba za utambulisho. Halmashauri zinazohusika zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 72**.

**Jedwali Na.72: Mali Zisizokuwa na Namba za Utambulisho**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh. ) | S/N | Jina la Halmashauri ya Wilaya | Kiasi (Sh. ) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Mpwapwa | 49,223,079,586 | 10 | H/Mji Masasi | 95,905,000 |
| 2 | H/Jiji Arusha | 685,003,335 | 11 | H/W Itilima | 238,124,493 |
| 3 | H/W Kaliua | 647,563,161 | 12 | H/W Singida | 5,180,000 |
| 4 | H/W Kasulu | 106,871,500 | 13 | H/W Malinyi | 674,787,378 |
| 5 | H/Mji Mbulu | 132,695,628 | 14 | H/W Mbulu | 19,648,726 |
| 6 | H/W Mbinga | 176,000,000 | 15 | H/W Missenyi | 255,864,549 |
| 7 | H/W Kalambo | 198,507,535 | 16 | H/W Wanging'ombe | 529,053,535 |
| 8 | H/W Meru | 25,014,456 | 17 | H/W Kwimba | 123,793,686 |
| 9 | H/W Itigi | 12,203,800 | | Jumla Kuu | **53,149,296,368** |

**Chanzo**: Nyaraka za Malipo na Rejista za Mali za Kudumu

Upungufu huu umetokana na ukosefu wa bajeti. Mali zisizo na nambari za utambulisho ziko katika hatari kubwa ya kuibwa, kwani haziwezi kutambulika kwa urahisi kutokana na kufanana na mali zinazomilikiwa na taasisi nyingine au watu binafsi.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe kuwa taasisi husika zinatenga bajeti na kutoa fedha kwa ajili ya kuweka nambari za utambulisho kwenye mali zote. Aidha, ihuishe taarifa kwenye rejista ya mali za kudumu ili kuongeza uwajibikaji na kuimarisha usalama wa mali hizo.**

### 10.4.4 Matumizi Yasiyoridhisha ya Mfumo wa GAMIS kutokana na Kutosajili Mali zisizohamishika katika Mfumo

Waraka Na. 2 (Kumb. Na. JA.32/233/01) wa tarehe 15 Julai 2021 unawataka maafisa masuuli kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) kwa ajili ya usimamizi mzuri wa mali na utunzaji sahihi wa kumbukumbu. Ilielkezwa zoezi hilo kukamilika kabla ya tarehe 31 Agosti 2021. Aidha, Kifungu cha 3 cha Muongozo wa Hazina Namba 2 wa mwaka wa fedha 2021/22 kinamtaka afisa masuuli kuhakikisha mali zote za kudumu zimeingizwa kwenye GAMIS na kutumia taarifa za mfumo huo katika kuandaa taarifa za fedha. Usajili sahihi wa mali ni muhimu kwa ajili ya usahihi wa kifedha, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa mali za umma.

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha na mfumo wa GAMIS, nilibaini kuwa taasisi 41 zilishindwa kusajili mali zao katika mfumo hata baada ya kupita miaka mitatu tangu tarehe ya mwisho kupita.

Kasoro hii imetokana na: ukosefu wa dhamira ya kutosha kutoka kwa maafisa husika, upungufu wa bajeti inayotosheleza kwa ajili ya uwekaji wa nambari za utambulisho wa mali, na uhaba wa watumishi wenye mafunzo ya kutosha kuhusu matumizi sahihi ya mfumo.

Kushindwa kusajili mali kwenye GAMIS kunaathiri usahihi wa taarifa za kifedha. Pia, kunaondoa uwazi. Vilevile, huongeza hatari ya upotevu au usimamizi duni wa rasilimali. Mchanganuo wa taasisi ambazo hazijasajili mali kwenye mfumo zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na.43**.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ihakikishe kuwa taasisi zote husika zisajili mali zao katika GAMIS na kutumia kikamilifu mfumo huo kutayarisha taarifa sahihi za kifedha.**

### 10.4.5 Miradi ya Ujenzi Iliyoanzishwa Kabla ya Kupata Hati za Ardhi Sh. bilioni 13.09

Kifungu cha 29(1) (a)(b) na (c) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinataka pale ambapo kamishna anaamua kutoa haki ya kumiliki ardhi kwa mtu aliyewasilisha maombi

ya haki ya umiliki wa ardhi; anayemiliki ardhi chini ya haki ya umiliki; aliyekubali ofa ya haki ya umiliki wa ardhi; au anayestahili kwa njia nyingine haki ya umiliki wa ardhi, basi atapewa cheti kinachojulikana kama “cheti cha umiliki”. Aidha, Katibu Mkuu Kiongozi alitoa waraka Na. CAB142/626/01/A/42 wa tarehe 26 September 2014 ukielekeza juu ya upatikanaji wa Vyeti vya Haki ya Kumiliki Ardhi kwa viwanja vinavyomilikiwa na Serikali.
Nilikagua nyaraka zinazohusiana na utekelezaji wa miradi mipya ya ujenzi, ikijumuisha ofisi za utawala, miundombinu ya shule na vituo vya afya, iliyofadhiliwa na fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na mapato ya ndani yenye thamani ya Sh. bilioni 13.09 katika halmashauri 12, sekretarieti 3 za mikoa na TARURA na kubaini kuwa taasisi husika hazikupata hatimiliki katika maeneo ambayo miradi hii ilijengwa. Hii ni kinyume na matakwa ya sheria na waraka uliotajwa. Maelezo yamefupishwa kwenye **Kiambatisho Na.44**.

Ukosefu wa hatimiliki unatokana na ufuatiliaji usioridhisha kwenye ofisi ya Kamishna wa Ardhi. Kukosekana kwa kwa hatimiliki ya ardhi kunatoa mwanya mali hizi kutumika kinyume na malengo, kuvamiwa na kupoteza haki endapo kutatokea migogoro ya umiliki.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ihakikishe vyeti vya umiliki vinapatikana ili kulinda haki ya umiliki wa viwanja vinavyomilikiwa na taasisi za umma.**

### 10.4.6 Kutoendelezwa kwa Viwanja Vilivyouzwa Vyenye Ukubwa wa Mita za Mraba 978,636

Kifungu cha 34 (1) na (2) cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113 masharti ya utoaji wa hati miliki ambayo mpokeaji anapaswa kutii, miongoni mwa masharti mengine,ni kupata idhini ya mpango na ruhusa ya ujenzi ndani ya miezi sita tangu kupokea hati miliki endapo ardhi imetengwa kwa ajili ya ujenzi.

Tathmini yangu ya upangaji, upimaji, na uendelezaji wa ardhi ilibaini viwanja vya ukubwa wa mita za mraba 978,636 vinavyomilikiwa na taasisi 13 za umma katika Halmashauri ya Mji Kibaha vilivyotolewa kwa taasisi hizo kati ya mwaka 2012 hadi 2022 havijaendelezwa kama ilivyofafanuliwa katika

**Kiambatisho Na.45**. Kutokuendelezwa kwa viwanja hivi ni ukiukwaji wa moja kwa moja wa matakwa ya Sheria ya Ardhi kuhusu matumizi yenye tija ya ardhi.

Kutokuendeleza viwanja hivi kumechangiwa zaidi na ukosefu wa fedha pamoja na kutofautiana kwa vipaumbele miongoni mwa taasisi husika. Matokeo yake, ucheleweshaji huu unasababisha jamii kutonufaika kikamilifu na uwekezaji uliofanyika katika upangaji na upimaji ardhi.

**Ninaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na OR - TAMISEMI, kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha kuzikumbusha taasisi husika juu ya wajibu wa kuendeleza viwanja walivyotengewa kulingana na sheria husika. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuoanisha vipaumbele vyao na kushughulikia changamoto za kifedha ili kuhakikisha viwanja hivyo vinaendelezwa kwa mujibu wa sheria.**

### 10.4.7 Migogoro ya Ardhi dhidi ya Halmashauri - Sh.bilioni 74.04

Kifungu cha 167 (1) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, kinazipa mamlaka ya kipekee Mahakama ya Rufaa, Mahakama Kuu, Mahakama ya Wilaya ya Ardhi na Nyumba, Mabaraza ya Ardhi ya Kata, na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji kusikiliza na kutatua migogoro yote, mashtaka na michakato inayohusiana na ardhi.

Nilibaini kuwa mamlaka 29 za serikali za mitaa zilikuwa na mashauri 44 ya ardhi ambayo hayajafanyiwa maamuzi katika mahakama/mabaraza mbalimbali, ambapo madai dhidi ya halmashauri husika yalifikia jumla ya Sh. bilioni 74.04, pamoja na migogoro 53 ya ardhi isiyo na madai ya kifedha. Maelezo ya kesi hizo yanaoneshwa katika **Kiambatisho Na.46**

Ninahusisha mashauri yanayoendelea na masuala kama vile uchukuaji wa ardhi kwa matumizi ya umma bila fidia stahiki, ugawaji mara mbili wa viwanja, ununuzi holela wa ardhi, pamoja na masuala mengine. Kuwapo kwa madai ya hayo mahakamani kutaleta athari hasi za kifedha endapo halmashauri husika zitashindwa katika mashauri hayo.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia OR-TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, na Wizara ya Katiba na Sheria, washirikiane kuhakikisha kuwa mamlaka za serikali za mitaa zinazingatia sheria za ardhi zilizopo katika masuala yote ya usimamizi wa ardhi ili kuepusha migogoro inayotokana na uchukuaji wa ardhi, fidia, na ugawaji wa viwanja. Pia, wahakikishe ushirikishwaji wa vitengo vya sheria katika usimamizi wa ardhi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima na inayoweza kuzuilika.**

### 10.4.8 Kutotolewa kwa Hatimiliki kwa wanufaika wa Viwanja 1975 Vilivyolipiwa Kikamilifu Sh. bilioni 6.59

Kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 kinaeleza kuwa pale ambapo kamishna ataamua kutoa haki ya kumiliki ardhi kwa mtu ambaye ameomba haki ya kumiliki ardhi; yuko katika umiliki wa ardhi kwa haki ya kumiliki ardhi au kwa kukubali ofa ya haki ya kumiliki ardhi; au anastahili vinginevyo haki ya kumiliki ardhi, atamkabidhi cheti kinachoitwa "Cheti cha umiliki" kwa mtu huyo.

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni ilipokea mkopo wa Sh. bilioni 1.5 katika mwaka wa fedha 2021/22 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya programu ya Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa ardhi. Halmashauri ilipima na kuuza viwanja 2,220 ambavyo vililipiwa kikamilifu na wanufaika katika maeneo ya Gezaulole-Mwera, Kibada-Uvumba, na Pembamnazi-Tundwi Songani. Hata hivyo, kufikia Novemba 2024, ni wanufaika wa viwanja 245 pekee waliokuwa wamepokea hatimiliki, huku viwanja 1,975 vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.59, sawa na 89%, vikiwa bado havijapata hatimiliki.

Kutotolewa kwa hatimiliki za ardhi kunahusishwa na changamoto kama vile wanunuzi wa viwanja kutowasilisha nyaraka muhimu kama vitambulisho vya NIDA, uwasilishaji wa fomu namba 19 usiokamilika na kutosalimishwa kikamilifu kwa hatimiliki ya awali kutoka kwa mmiliki wa awali wa eneo la Pembamnazi-Tundwi Songani. Hali hii imewanyima wanunuzi wa viwanja haki ya kisheria ya umiliki wa ardhi, hivyo kupeleka kutokuwa na uhakika wa umiliki na kuwazuia wanunuzi kutumia ardhi husika kwa maendeleo au masuala ya kifedha.

**Ninapendekeza kwamba Serikali, kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, zishirikiane na uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kuwaelimisha wanunuzi wa viwanja kuhusu umuhimu wa kuwasilisha nyaraka zinazohitajika, kama vile vitambulisho vya NIDA na kukamilisha fomu namba 19 ili kurahisisha uchakataji wa hatimiliki.**

**Aidha, juhudi zinapaswa kufanyika ili kuharakisha ukamilishaji wa usalimishaji wa hatimiliki kutoka kwa mmiliki wa awali wa ardhi iliyouzwa, ili kuwezesha utoaji wa hatimiliki mpya.**

### 10.4.9 Upungufu kuhusiana na Ulipaji wa Fidia Sh. bilioni 4.72

Kifungu cha 3(1)(g) cha Sheria ya Ardhi Sura ya 113 kinaipa Serikali jukumu la kutoa fidia kamilifu, ya usawa, na ya haraka kwa watu ambao haki zao za ardhi zimebatilishwa au kuingiliwa, ikijumuisha fidia kwa thamani ya soko, usumbufu, usafiri, upotevu wa faida au makazi, pamoja na gharama nyinginezo. Vile vile, Kifungu cha 52(2) na (4) cha Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya mwaka 2016 kinataka uthaminishaji kufanyika pamoja na taarifa za uthamini kuandaliwa chini ya sheria hiyo; ambapo fidia itakuwa halali kwa muda wa miaka miwili tangu tarehe ya kuidhinishwa kwa taarifa hiyo na iwapo Mthamini Mkuu ameidhinisha uthamini unaohusiana na fidia.

Mapitio yangu kuhusu masuala ya fidia ya ardhi katika mamlaka za serikali za mitaa yamebaini kuwa mamlaka nne za serikali za mitaa zina madai ya fidia ya ardhi ya muda mrefu yenye jumla ya Sh. bilioni 4.72 kwa wamiliki wa ardhi, licha ya kupita kwa muda uliotakiwa kwa malipo ya fidia hiyo. Mathalani, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela tayari imetoa hati za umiliki wa viwanja vya shule tatu, licha ya kuwapo kwa madai ya muda mrefu kutoka kwa wamiliki 45 wa ardhi wa awali ambao bado hawajalipwa fidia zao. Taarifa zaidi zimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 73.**

**Jedwali Na.73: Mapungufu kuhusiana na Ulipaji wa Fidia**

| Na. | Halmashauri | Mapungufu | Kiasi husika (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mwanza | Madai ya fidia ya ardhi hayajalipwa kwa zaidi ya miaka mitatu | 3,849,050,412 |
| 2 | H/Jiji Mbeya | Madai ya fidia ya ardhi katika mradi wa Sistila hayajalipwa kwa zaidi ya miaka 12 tangu kuanzishwa kwa mradi huo mwaka wa fedha 2012/13 | 524,651,723 |
| 3 | H/M Ilemela | Viwanja vya shule mbili za sekondari na moja ya msingi vilitolewa hati miliki licha ya kuwepo kwa madai ya muda mrefu (Zaidi ya Miaka 10) ya fidia kwa wamiliki wa awali 45 wa ardhi hiyo | 280,926,634 |
| 4 | H/M Shinyanga | Fidia haijalipwa kwa watu walioathiriwa na mradi katika Kata ya Kolandoto, huku muda halali wa malipo hayo ukiwa umeisha tangu tarehe 14 Agosti 2023 | 65,074,224 |
| **Jumla ndogo- Madai ya muda mrefu ya Fidia** | | | **4,719,702,993** |

***Chanzo***: Majalada ya Idara ya Ardhi, Vitabu vya Fedha na Hati za Malipo Malipo

Ninahusisha upungufu uliobainika na usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa shughuli za ardhi, ikiwamo usimamizi wa madai ya fidia katika mamlaka za serikali za mitaa, hali migogoro ya ardhi.

**Ninaishauri Serikali kupitia, Wizara ya Ardhi, OR TAMISEMI na menejimenti ya mamlaka husika za serikali za mitaa, iboreshe usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za ardhi kwa kuhakikisha kuwa madai ya fidia kwa wanufaika wanaostahili yanatolewa kwa wakati, kulingana na sheria zinazohusika, ili kuzuia migogoro ya ardhi na adhabu zinazoweza kutokea, ikiwamo riba.**

### 10.4.10 Kusimama kwa Mradi wa Ujenzi Kutokana na Kukosekana Eneo la Ujenzi Sh. bilioni 2.89

Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 kinaitambua Halmashauri kama mamlaka ya upangaji ndani ya eneo lake la utawala. Aidha, Kifungu cha 9 kinaeleza kuwa madhumuni ya mpango mkuu wa upangaji ni kuhakikisha maendeleo endelevu kwa kuendeleza afya, usalama, utulivu, ustawi wa jamii, urahisi wa matumizi, na ufanisi wa kiuchumi, kwa lengo la kuboresha matumizi ya ardhi kwa kutoa miundombinu ya usafiri, huduma za kijamii kama maji na umeme na huduma nyingine za umma.

Nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo iliingia mkataba Na. LGA/180/2022-2023/W/08 na mkandarasi tarehe 26 Juni 2023 kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa halmashauri kwa gharama ya Sh. bilioni 2.89 kwa muda wa miezi 12. Mpango wa awali ulikuwa ni kujenga mradi huu katika eneo kilipo kiwanda cha tofali cha manispaa. Hata hivyo, kutokana na kutokuwa na uhakika kuhusiana na upatikanaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa mradi na upungufu katika mpango wa matumizi ya ardhi, mradi husika ulisitishwa kama ilivyobainika kupitia muhtasari wa kikao cha kamati ya fedha cha tarehe 28 Desemba 2023.

Athari za kifedha za ucheleweshaji wa miradi zinaweza kudhoofisha rasilimali za mamlaka za serikali za mitaa na kuathiri hali ya kifedha kwa ujumla. Aidha, kuna uwezekano kwamba halmashauri inaweza kuhamishia mradi katika eneo lisilo la kimkakati, ambalo huenda lisiwe na manufaa ya kiuchumi.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kwamba zoezi la kupanga na kupima ardhi linakuwa endelevu ili kuepuka kuchelewesha utekelezaji wa ujenzi wa miradi kutokana na**

**kutofanyika uamuzi kuhusiana na maeneo ya kutekeleza mradi au ukosefu wa viwanja vilivyopimwa.**

**Pia, menejimenti ya Manispaa ya Ubungo inapaswa harakisha mchakato wa kupata ardhi kwa ajili ya kujenga ukumbi wa shughuli za kijamii ili kuepuka ongezeko la gharama na kuhakikisha kuwa tathmini ya manufaa ya kiuchumi ya eneo la ujenzi inafanyika kabla ya mradi kutekelezwa.**

## 10.5 Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu

Upatikanaji wa rasilimali fedha ni changamoto kubwa kwa makundi yenye uhitaji zaidi, hususani wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, ambao mara nyingi hukumbana na ugumu wa kupata mikopo kutoka kwa taasisi za kifedha kutokana na ukosefu wa dhamana. Ili kukabiliana na changamoto hii, serikali ilianzisha mfuko wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu (WYDF) kwa lengo la kuwapatia uwezo kifedha bila dhamana kwa lengo la kuinua makundi haya maalumu wa kiuchumi. Hapo awali, mfuko huu uliendeshwa bila kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria, hali iliyosababisha utekelezaji usio thabiti, udhaifu katika usimamizi wa michango ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), na changamoto katika urejeshaji wa mikopo.

Kwa kutambua umuhimu wa uwezeshaji wa kiuchumi kwa wote, serikali iliboresha mfumo wa kisheria wa mfuko huu mwaka 2019, kwa kurekebisha sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa [Sura 290], na kuzitaka mamlaka za serikali za mitaa (halmashauri) kutenga 10% ya mapato yao ya ndani yasiyolindwa kwa ajili ya mfuko huu. Aidha, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilitoa muongozo wa mgawanyo wa utoaji wa mikopo kwa uwiano wa 40% kwa wanawake, 40% kwa vijana, na 20% kwa watu wenye ulemavu.

Licha ya juhudi hizi, changamoto zimeendelea kuathiri ufanisi wa mfuko huu. Masuala kama mikopo kutorejeshwa, halmashauri kushindwa kuchangia kikamilifu katika mfuko, na utoaji wa mikopo kwa vikundi vilivyositisha biashara, yameendelea kudhoofisha malengo ya mfuko. Kutokana na upungufu uliobainishwa, mnamo Machi 2023, Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliagiza yafanyike mapitio ya taratibu za utoaji mikopo. Kufuatia agizo hilo, Waziri Mkuu, aliagiza mamlaka zote za serikali za mitaa nchini kusitisha utoaji wa mikopo kuanzia Aprili 2023. Usitishaji huo ulilenga kutoa muda kwa Serikali kuweka utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo na kushughulikia

changamoto zilizobainishwa ikiwa ni Pamoja na kuanzisha mfumo imara na wazi wa usimamizi wa fedha za mfuko huo.

Hadi tarehe 30 Juni 2024, hakukuwa na mikopo iliyotolewa kufuatia usitishaji wa utoaji wa mikopo hiyo, hali iliyowaathiri kwa kiasi kikubwa walengwa waliotarajiwa kunufaika na mikopo hiyo. Ingawa hatua hiyo ililenga kuboresha usimamizi wa mfuko, imesababisha madhara yasiyokusudiwa, hasa katika urejeshaji wa mikopo iliyopita muda wake. Baadhi ya vikundi vilitafsiri kusitishwa huko kama msamaha wa madeni yao, jambo lililosababisha kushuka kwa urejeshaji wa mikopo ukilinganisha na miaka iliyopita.
Serikali ilitoa maelekezo ya kuanza tena utoaji wa mikopo mnamo Septemba 2024. Hata hivyo, vipo baadhi ya vikundi vyenye mikopo ambayo haijarejeshwa vinavyotaka mikopo mipya, kwa mtazamo kuwa mchakato wa utoaji mikopo ni mpya na kuwa umefuta madeni ya mikopo waliyokuwa nayo.

Ninatambua kuwa serikali, kupitia ofisi ya Rais TAMISEMI, imefanya maboresho katika mfumo wa kushughulikia na kuidhinisha mikopo. Miongoni mwa mabadiliko hayo ni kuondoa ushiriki wa moja kwa moja wa viongozi wa kisiasa kwenye mfumo wa uidhinishaji mikopo. Pia, imeshirikisha benki za biashara katika tathmini ya vikundi kabla ya kuidhinisha mikopo na katika utoaji wa mikopo hiyo; hii imeanza kwa halmashauri chache za mfano. Matokeo ya maboresho haya yanatarajiwa kupimwa katika kaguzi za mwaka wa fedha 2024/25.

Mapitio ya utekelezaji wa mfuko kwa mwaka wa fedha 2023/24 yanaonesha muendelezo wa changamoto za mfuko, kama urejeshaji hafifu wa mikopo na halmashauri kutochangia kikamilifu katika mfuko. Sura hii inabainisha maeneo yanayohitaji hatua za haraka za serikali ili kuhakikisha mfuko unatimiza malengo kusudiwa.

### 10.5.1 Changamoto Zinazoendelea na Hatua za Kuchukua

#### (i) Kuendelea kwa Changamoto ya Urejeshaji wa Mikopo

Licha ya mapendekezo niliyokwishatoa, tatizo la kutorejesha mikopo bado halijatatuliwa. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya Sh. bilioni 115.35 ilikuwa bado haijarejeshwa na vikundi katika halmashauri 171; na hakukuwa na hatua madhubuti zilizokuchukuliwa.

**Jedwali Na.74: Mikopo isiyorejeshwa na vikundi vilivyositisha biashara**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2023/24 | 171 | 115,350,186,616 |
| 2022/23 | 151 | 107,426,833,023 |
| 2021/22 | 180 | 88,424,780,330 |
| 2020/21 | 155 | 47,006,024,260 |
| 2019/20 | 130 | 27,790,189,049 |
| 2018/19 | 111 | 13,794,359,981 |
| 2017/18 | 90 | 10,044,453,656 |
| 2016/17 | 84 | 5,809,326,477 |

***Chanzo:*** Mikataba na Taarifa za Urejeshaji Mikopo

Ukosefu wa mifumo thabiti ya usimamizi na ufuatiliaji hafifu kwa halmashauri umechangia ongezeko la madeni yasiyolipwa. Iwapo hali hii itaendelea, inaweza kuhatarisha uendelevu wa mfuko na kuzuia upatikanaji wa fedha kwa wanufaika wengine watarajiwa.

**Ili kuhakikisha Mfuko unafikia malengo yake na unadumu kwa muda mrefu, ninarejea mapendekezo yangu ya awali kwamba halmashauri ziboreshe juhudi za ufuatiliaji ili kurejesha kiasi cha mikopo kilichobaki kutoka kwa vikundi vya wanufaika. Aidha, kwa maeneo ambayo kwa sasa benki za biashara zinashiriki katika utoaji wa mikopo, halmashauri zinapaswa kushirikiana kwa karibu na taasisi hizi ili kuimarisha tathmini za mikopo na kuboresha mikakati ya urejeshaji.**

### (ii) Michango ambayo haikuwasilishwa kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Kwa mujibu wa Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, (Sura ya 290 kilichorekebishwa mwaka 2019), mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kutenga na kupeleka 10% ya makusanyo ya mapato yao kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Michango hii inalenga kusaidia vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kupata msaada wa kifedha kwa shughuli za kiuchumi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mamlaka 76 za serikali za mitaa zilishindwa kuchangia kikamilifu 10% ya makusanyo ya mapato yao ya ndani kwenye mfuko huu. Jumla ya michango ambayo haijachangwa ni Sh. bilioni 10.17.

**Jedwali Na.75: Mwenendo wa michango ambayo haikuwasilishwa kwenye mfuko**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2023/24 | 76 | 10,172,358,570 |
| 2022/23 | 62 | 7,267,488,679 |
| 2021/22 | 53 | 5,062,050,675 |
| 2020/21 | 83 | 6,857,306,654 |
| 2019/20 | 82 | 5,720,140,159 |
| 2018/19 | 115 | 9,930,902,514 |

***Chanzo:*** Taarifa za Fedha za Halmashauri

Kutotimiza matakwa ya sheria ya kuchangia mfuko huu kunadhoofisha uwezo wa mfuko kupanua wigo wake na kusaidia wanufaika wengi zaidi. Kushindwa kuwasilishwa michango kunasababishwa na kutolipa kipaumbele suala la kutenga fedha 10% ya mapato kwa ajili ya mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Ninapendekeza kwa OR-TAMISEMI na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa husika kuhakikisha zinatenga na kuchangia10% ya mapato yake kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu kama sheria inavyotaka.**

### (iii) Mikopo inayodaiwa kwenye vikundi vilivyositisha shughuli za biashara

Kanuni ya 8 ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu ya mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kusimamia mchakato wa utoaji na usimamizi wa mikopo.

Baada ya kufanya tathmini ya mchakato wa urejeshaji wa mikopo iliyotolewa katika miaka ya iliyopita nilibaini kuwa mamlaka 32 za serikali za mitaa zilikuwa na jumla ya Sh. bilioni 6.42 za mikopo ambayo bado haijarejeshwa.

Baadhi ya vikundi vilivyonufaika havipo tena, huku vingine vikiwa vimesitisha shughuli za biashara, hali inayofanya urejeshaji wa mikopo hiyo kuwa mgumu. Hali hii inaathiri mtiririko wa fedha za mfuko na uwezo wake wa kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vingine. Aidha, kushindwa kurejesha mikopo hii kunasabaisha kuwapo kwa madeni yasiyolipika (chechefu), jambo linaloongeza hasara za kifedha na kuathiri uendelevu wa mfuko.

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuongeza ushirikishwaji wa benki za biashara katika tathmini, utoaji, usimamizi na urejeshaji wa mikopo. Aidha, OR-TAMISEMI iandae sera madhubuti ya kushughulikia mikopo isiyolipika ili kuboresha ufuatiliaji na kuimarisha mifumo ya urejeshaji, kuhakikisha mfuko unadumu.**

**Kiambatisho Na.1:Hati za ukaguzi na hitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na bajeti kwa mwaka 2023/24**

| Na. | Jina/ Taasisi | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Arusha | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 2 | H/W Arusha | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 3 | H/W Babati | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 4 | H/Mji Babati | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 5 | H/W Bagamoyo | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 6 | H/W Bahi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 7 | H/W Bariadi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 8 | H/Mji Bariadi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 9 | H/W Biharamulo | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 10 | H/W Buchosa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 11 | H/W Buhigwe | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 12 | H/W Bukoba | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 13 | H/M Bukoba | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 14 | H/W Bukombe | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 15 | H/W Bumbuli | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 16 | H/W Bunda | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 17 | H/Mji Bunda | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 18 | H/W Busega | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 19 | H/W Busokelo | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 20 | H/W Butiama | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 21 | H/W Chalinze | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 22 | H/W Chamwino | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 23 | H/W Chato | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 24 | H/W Chemba | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 25 | H/W Chunya | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi |
| 26 | H/Jiji Dar es Salaam | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |

| Na. | Jina/ Taasisi | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za bajeti |
|---|---|---|---|---|
| 27 | H/Jiji Dodoma | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 28 | H/W Gairo | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 29 | H/W Geita | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 30 | H/Mji Geita | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 31 | H/W Hai | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi |
| 32 | H/W Hanang | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 33 | H/W Handeni | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 34 | H/Mji Handeni | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 35 | H/Mji Ifakara | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi |
| 36 | Igunga H/W | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi |
| 37 | Ikungi H/W | Inayoridhisha | Imekidhi | Imekidhi |
| 38 | H/W Ileje | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 39 | H/M Ilemela | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 40 | H/W Iramba | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 41 | H/W Iringa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 42 | H/M Iringa | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Compliant with exception |
| 43 | H/W Itigi | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 44 | H/W Itilima | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 45 | H/M Kahama | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 46 | H/W Kakonko | Inayoridhisha | Imekidhi na baadhi ya mapungufu | Imekidhi na baadhi ya mapungufu |
| H/W Kongwa | 28,737,600 | H/W Sikonge | 35,605,600 |
| H/W Korogwe | 42,684,400 | H/W Simanjiro | 20,109,800 |
| H/Mji Korogwe | 38,541,600 | H/W Singida | 44,039,700 |
| H/W Kwimba | 34,004,800 | H/M Singida | 21,367,300 |
| H/W Kyela | 37,936,367 | H/W Songea | 28,181,300 |
| H/W Kyerwa | 36,000,000 | H/M Songea | 41,573,800 |
| H/W Lindi | 65,889,958 | H/W Songwe | 18,000,000 |
| H/M Lindi | 21,654,056 | H/W S'wanga | 25,672,900 |
| H/W Liwale | 14,610,100 | H/W Uyui | 26,380,800 |
| H/W Longido | 9,860,600 | H/M Tabora | 43,239,043 |
| H/W Ludewa | 29,811,400 | H/W Tandahimba | 82,500,300 |
| H/W Lushoto | 48,726,160 | H/Jiji Tanga | 94,132,900 |
| H/W Madaba | 1,000,000 | H/W Tarime | 28,433,700 |
| H/W Mafia | 6,290,500 | H/Mji Tarime | 3,000,000 |
| H/Mji Mafinga | 44,996,000 | H/M Temeke | 406,826,400 |
| H/W Magu | 41,332,514 | H/Mji Tunduma | 36,000,000 |
| H/Mji Makambako | 36,000,000 | H/W Tunduru | 54,277,200 |
| H/W Makete | 34,823,800 | H/M Ubungo | 198,594,300 |
| H/W Malinyi | 9,000,000 | H/W Ukerewe | 29,953,200 |
| H/W Manyoni | 35,590,200 | H/W Ulanga | 27,192,000 |
| H/W Masasi | 79,760,550 | H/W Urambo | 72,048,000 |
| H/Mji Masasi | 9,000,000 | H/W Uvinza | 9,000,000 |
| H/W Maswa | 43,109,900 | H/W Wanging'ombe | 27,102,650 |
| Jumla Ndogo (A) | 5,607,146,896 | Jumla Ndogo (B) | 4,191,368,320 |
| | | **Jumla Kuu (A+B)** | **9,792,515,216** |

## Kiambatisho Na.34:Kasi Ndogo ya Ujenzi na Miradi Isiyokamilika

| Na. | Jina la Halmashauri/Taasisi | Gharama ya Mradi (Sh.) | Maelezo ya Miradi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Kibaha | 103,792,350 | Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkurugenzi |
| | | 403,289,171 | Kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha (Serikali Kuu) - Awamu ya VI |
| 2 | H/W Kisarawe | 8,072,110,000 | Orodha inajumuisha miradi mbalimbali inayoendelea katika shule na vituo vya afya, kama vile mabweni, maabara, kumbi za chakula, nyumba za walimu, na majengo ya utawala. Miradi ya miundombinu kama |

| Na. | Jina la Halmashauri/Taasisi | Gharama ya Mradi (Sh.) | Maelezo ya Miradi |
|---|---|---|---|
| | | | vile chumba cha eksirei, ukumbi wa CHMT, na kiwanda cha korosho pia viko kwenye ujenzi. |
| | | 500,000,000 | Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Gwata |
| | | 173,000,000 | Ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kiluvya |
| 3 | H/W Mkuranga | 1,273,000,000 | Miradi iliyoorodheshwa inahusisha ujenzi wa madarasa mengi, nyumba za walimu, na miundombinu muhimu ya shule za msingi na sekondari, pamoja na miundombinu ya afya kama vile zahanati na nyumba ya daktari. |
| 4 | H/W Rufiji | 3,415,752,348 | Miradi inahusisha ujenzi wa shule mpya, madarasa, na miundombinu muhimu ya elimu, pamoja na maboresho ya miundombinu ya afya kama vile wodi za wazazi na ukarabati wa hospitali. Miradi mingine ni ujenzi wa majengo ya ofisi na skimu za umwagiliaji. |
| 5 | H/W Geita | 1,305,360,834 | Miradi hii inalenga ujenzi wa miundombinu muhimu, ikiwemo madarasa, maabara, vituo vya afya, na nyumba za wafanyakazi wa sekta ya afya ili kuboresha huduma za elimu na afya. |
| 6 | H/W Mlele | 244,646,165 | Miradi ya ujenzi wa miundombinu ya afya, elimu, na usafi wa mazingira, ikiwemo madarasa, ofisi, vyoo vya shimo, maabara za sayansi, na zahanati. |
| 7 | HW Mpanda | 895,000,000 | Ujenzi wa jengo la chakula na jiko, ujenzi wa bweni, kuanzisha wodi kamili ya mama na mtoto, ujenzi wa zahanati, kukamilisha jengo la OPD, ujenzi wa jengo la utawala, na uanzishwaji wa Zahanati ya Kabanga. |
| 8 | H/W Mpimbwe | 397,100,000 | Kukamilisha Kituo cha Afya cha Kibaoni na Kituo cha Afya cha Kasansa, pamoja na ujenzi wa Zahanati ya Luchima. Pia, kukamilisha jengo la 4-in-1 kwa wafanyakazi wa afya ili kuboresha huduma za afya. |
| 9 | H/W Kasulu | 200,000,000 | Ujenzi wa maduka 57 katika Bogwe |
| | | 900,000,000 | Ukarabati wa Hospitali ya Halmashauri |
| 10 | H/W Rombo | 150,000,000 | Ujenzi wa Nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED) |
| 11 | H/Mji Mbulu | 150,000,000 | Ujenzi wa Nyumba ya DED |
| | | 500,000,000 | Ujenzi wa Jengo la OPD, Maabara, Wodi ya Wajawazito (Theater), jengo la kufulia, shimo la kondo na taka za hospitali, vyoo vya nje, na njia za kutembelea katika Kituo cha Afya cha Kainam. |
| | | 3,816,515,078 | Miradi makao makuu inajumuisha ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri, Jengo la Kufulia, na Wodi ya Wajawazito. Vilevile, ujenzi wa kichomea taka, uzio, na njia za kutembelea ili kuboresha miundombinu katika eneo hilo. |
| 12 | H/W Kyela | 1,825,994,000 | Miradi inajumuisha ujenzi wa matundu 8 ya vyoo katika Shule ya Msingi Mbala, bweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Sama, na ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo katika Shule za Sekondari za Njisi, Lubele, Kyela, na Ipinda. Miradi ya afya inahusisha kukamilisha zahanati za Kasumulu, Kapamisya, Kyangala, na Kilasilo, pamoja na wodi ya wazazi katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela na maabara katika Kituo cha Afya cha Ngonga. |

| Na. | Jina la Halmashauri/Taasisi | Gharama ya Mradi (Sh.) | Maelezo ya Miradi |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 13 | H/W Kilosa | 1,288,909,043 | Miradi mbalimbali ya ujenzi katika Makao Makuu ya Halmashauri. |
| 14 | H/W Morogoro | 517,007,508 | Ujenzi wa majengo mbalimbali katika sekta ya afya katika Halmashauri ya Morogoro. |
| 15 | H/Mji Newala | 1,463,200,000 | Ujenzi wa wodi ya wazazi, Kitengo cha Dharura cha Matibabu (EMD), na kitengo cha radiolojia, pamoja na njia ya kutembelea. Pia, miradi ya elimu inahusisha ujenzi wa madarasa na vyoo katika shule kadhaa. |
| 16 | H/W Misungwi | 105,000,000 | Miradi mbalimbali ya ujenzi katika Makao Makuu ya Halmashauri. |
| 17 | H/W Msalala | 1,636,123,342 | Ujenzi wa majengo mbalimbali katika sekta ya afya na Kituo cha Mabasi cha Segese. |
| 18 | H/W Shinyanga | 1,303,800,000 | Nyumba za walimu na mabweni katika Shule ya Sekondari Puni, madarasa katika Lohumbo, na vyoo katika Ilola, Masengwa, na Tinde Girls. |
| | | 1,360,000,000 | Kasi ndogo katika ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri. |
| 19 | H/W Bariadi | 278,400,000 | Nyumba ya walimu katika Kijiji cha Banemhi, upanuzi wa OPD katika Zahanati ya Gasuma, ukarabati wa vyoo, usambazaji wa maji na umeme, na bweni kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi Igaganulwa. |
| 20 | H/W Ileje | 2,296,400,000 | Ujenzi wa madarasa matatu katika Shule ya Msingi Ngulungulu, jengo la utawala, na zahanati. |
| 21 | H/M Singida | 4,544,200,000 | Miradi ya halmashauri katika Makao Makuu na hospitali ya manispaa. |
| 22 | H/W Kaliua | 7,459,436,681 | Ujenzi wa shule za sekondari na mabweni katika maeneo mbalimbali. |
| 23 | H/W Nzega | 1,978,463,860 | Ujenzi na ukarabati wa mabwawa, mabweni, madarasa, maktaba, vyumba vya chakula, na vyoo. |
| 24 | H/Mji Nzega | 2,353,963,000 | Ujenzi wa nyumba za walimu na shule mpya. |
| 25 | H/M Tabora | 2,500,000,000 | Kasi ndogo ya ujenzi wa jengo la utawala. |
| 26 | H/W Handeni | 3,416,219,993 | Kasi ndogo katika ujenzi wa jengo la halmashauri. |
| 27 | H/W Muheza | 4,865,563,392 | Miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa shule, mabweni, na vituo vya afya. |
| 28 | H/Jiji Dodoma | 1,500,000,000 | Kasi ndogo ya ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Nala. |
| 29 | H/W Karagwe | 3,389,215,469 | Miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vyumba vya madarasa ya shule, vyoo, mabweni, na zahanati, iko katika hatua tofauti kuanzia ununuzi hadi ukamilishaji. Miradi mikuu kama vile Jengo la Utawala la Halmashauri na miundombinu ya shule za sekondari inasonga polepole na haijakamilika, huku baadhi yake ikiwa katika hatua ya kuezekwa. Hata hivyo, ucheleweshaji katika ununuzi na awamu za awali za ujenzi unaashiria hatari za kutokamilika kwa wakati. |
| 30 | H/W Manyoni | 370,846,967 | Shughuli za ujenzi ambazo hazijakamilika kwa ajili ya Nyumba ya Makazi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (DED) na majengo ya Hospitali ya Wilaya. |

| Na. | Jina la Halmashauri/Taasisi | Gharama ya Mradi (Sh.) | Maelezo ya Miradi |
|---|---|---|---|
| 31 | H/M Moshi | 656,617,431 | Ujenzi wa Uwanja wa Majengo Moshi haujakamilika. |
| | | 5,953,358,792 | Kasi ndogo ya ujenzi wa Hospitali ya Manispaa, kazi ambazo hazijakamilika ni pamoja na usakinishaji wa milango na madirisha, kazi za paa bado hazijakamilika, na nguzo za ghorofa ya kwanza, mihimili ya paa, na sehemu za sakafu bado hazijakamilika. |
| | | 170,000,000 | Ukarabati wa Soko la Majengo, ujenzi wa tanuri la kuchomea taka katika Kituo cha Afya cha Majengo, na ujenzi wa ofisi za mitaa katika Miembeni, Karanga, na Korongoni ni miradi ambayo bado haijakamilika kwa lengo la kuboresha miundombinu na utoaji wa huduma. Aidha, ujenzi wa kivuko cha Mto Baniani unalenga kuboresha upatikanaji wa huduma na muunganisho wa eneo hilo. |
| 32 | H/W Ngara | 2,712,080,075 | Miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Makao Makuu na Ngazi za Chini ambayo haijakamilika. |
| 33 | H/W Kwimba | 889,838,100 | Miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Makao Makuu na Ngazi za Chini, ikijumuisha Jengo la Halmashauri, ambayo haijakamilika. |
| **Jumla** | | **77,334,203,599** | |

### Kiambatisho Na.35:Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Kutembelea Miradi ya maendeleo

| Na. | Jina la Halmashauri | Gharama ya Mradi (Sh.) | Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Ukaguzi kwa kutembelea/Mapitio ya majalada ya miradi |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Meru | 397,400,000.00 | Kazi zilizobaki ni pamoja na ukamilishaji wa sketingi, vyoo, vifaa vya kunawia mikono, kufunga madirisha na milango, pamoja na usakinishaji wa shimo la maji taka. Bweni na vituo vya afya havijaanza kutumika kutokana na ukosefu wa vifaa muhimu kama vitanda, kichomea taka, shimo la kondo la nyuma, vyoo vya nje, vifaa vya matibabu, na nyaraka muhimu, ingawa mafundi wapo eneo la kazi na vifaa vipo kwa ajili ya ukamilishaji. |
| 2 | H/W Kibaha | 825,396,000.00 | Majengo yako katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji, lakini bado kuna mapungufu kadhaa, yakiwemo sketingi, paa, vifaa vya vyoo, na marekebisho ya upatikanaji wa huduma. Pia, huduma muhimu kama maji na umeme hazijaunganishwa. |
| 3 | H/W Rufiji | 2,047,500,000.00 | Wodi ya wanawake na jengo la upasuaji bado halijakamilika au halifanyi kazi kutokana na ukosefu wa vifaa vya usakinishaji, ufungaji usio sahihi wa huduma, na ukosefu wa mchakato sahihi wa ununuzi na uhakiki wa vifaa vya matibabu na mafundi. Aidha, miundombinu muhimu kama umeme, vyoo vya shimo, na vitanda vya bweni vina matatizo yasiyotatuliwa, huku usimamizi duni na tathmini zisizoridhisha zikichangia kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi. |

| Na. | Jina la Halmashauri | Gharama ya Mradi (Sh.) | Mapungufu Yaliyobainika Wakati wa Ukaguzi kwa kutembelea/Mapitio ya majalada ya miradi |
|---|---|---|---|
| 4 | H/W Mbulu | 889,083,972 | Miradi kadhaa ya ujenzi iliyokamilika ina mapungufu, ikiwa ni pamoja na mashimo ya maji taka yasiyofungwa, uvujaji wa paa, na kufungwa vibaya kwa mapazia ya madirisha katika Shule ya Sekondari ya Kainam, pamoja na nyufa kwenye kuta na sakafu katika Shule ya Sekondari ya Tlawi na Zahanati ya Gunyoda. |
| 5 | H/W Nzega | 381,200,000 | Miradi ya ujenzi ina mapungufu makubwa, ikiwa ni pamoja na eneo la kufulia lisilozungushiwa ukuta, miteremko mikali katika Shule ya Sekondari ya Nata hakukua na usawazishaji wa eneo, ubao wa kufundishia usio laini katika Shule ya Sekondari ya Mwangoye, kufungwa kwa madirisha ya alumini kwa udhaifu katika Zahanati ya Buhulyu, vyoo vya shimo visivyo na hewa ya kutosha katika Shule ya Sekondari ya Hamza Aziz, na mgawanyiko wa madarasa usio imara katika Shule ya Satellite ya Majengo. |
| 6 | H/W Mkinga | 343,532,920 | Miradi iliyotembelewa ina mapungufu, yakiwemo nyufa kwenye sakafu za madarasa katika Shule ya Msingi Maramba B kutokana na matumizi ya mapema, ukamilishaji duni na kutokukamilika kwa kuta katika Shule za Sekondari za Gombero na Mkinga, na ukosefu wa samani katika Shule ya Mkinga. Aidha, nyumba ya watumishi katika Shule ya Msingi ya Bamba Estate haijakamilishwa kwa kuwekwa vigae, mapazia ya milango, mfumo wa maji, shimo la kutiririsha maji taka, na umeme. |
| 7 | H/W Pangani | 347,000,000 | Miradi ya ujenzi haijakamilika licha ya fedha zote kutumika. Mapungufu ni pamoja na plasta mbovu, nyufa, na usakinishaji usiokamilika katika nyumba za walimu za Kigurusimba, Stahabu, na Buyuni, bweni lisilokamilika katika Shule ya Msingi Funguni, na kutotumika kwa vyoo vipya vya Shule ya Sekondari ya Funguni. |
| 8 | H/W Kilindi | 1,036,465,320 | Mapitio ya Miradi kwa mwezi Desemba 2024 yalionesha ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hakuna hata mmoja kati ya miradi nane iliyotembelewa iliyokamilika, na yote ilionesha mapungufu mbalimbali wakati wa ujenzi. |
| Jumla | | 6,267,578,212 | |

**Kiambatisho Na.36:Mapungufu ya Usimamizi wa Mikataba na Udhibiti wa Ubora katika Miradi ya Barabara za TARURA**

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Shinyanga-H/M Kahama | S10/021/2023/2024/W/64 | 154,500,000 | Changarawe yenye thamani ya Sh. milioni 45.67 na culvert lenye thamani ya Sh. milioni 22.06 kwenye Barabara ya Chalya-Malamba havikujaribiwa, na kuibua wasiwasi kuhusu ubora na kudumu. Aidha, |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | culvert ilijengwa kwenye eneo lisilotakiwa ch.1+180 licha ya maelekezo ya kuhamisha. Hali hii inaonesha udhaifu katika usimamizi wa miradi kwa TARURA Shinyanga. Menejimenti inashauriwa kufanya majaribio ya nyenzo, kuhakikisha utekelezaji wa miongozo kwenye miradi ijayo, na kujenga tena culvert kwenye eneo sahihi. |
| Shinyanga-H/M Kahama | S10/021/2023/2024/W/53 | 209,137,150 | Nilitembelea mradi mnamo tarehe 15 Oktoba 2024 Kahama MC na kubaini ujenzi usioridhisha wa mifereji ya maji kwenye Barabara ya S/M Majengo hadi Nyanshimbi kwa sababu ya mchanganyiko mbaya wa chokaa, kutokana na ukosefu wa usimamizi mzuri kutoka TARURA Shinyanga. Hali hii ilihatarisha ubora wa mifereji. Inashauriwa TARURA kuwawajibisha wakandarasi na kuboresha usimamizi ili kuhakikisha utekelezaji wa miongozo. |
| Mtwara-H/W Nanyamba | S10/015/2023/2024/W/39 | 478,627,000 | Katika tarehe ya kumaliza mradi, kasoro kadhaa zilionekana, ikiwemo kurekebisha alama za mradi, kushughulikia upungufu kwenye ujenzi wa mawe ya kingo na gabioni, kuondoa vifaa vya uchimbaji vilivyozidi, na kuchimba tena kingo za mto kwenye culvert. Uhakiki wa tarehe 3 Novemba 2024 ulibaini kuwa kasoro hizo hazijarekebishwa, na kuathiri malengo ya mradi. Inashauriwa masuala haya yarekebishwe haraka. |
| Simiyu-H/W Itilima | S10/2023/2024/W/10 | 3,329,570,000 | Kingo za Barabara Kutojengewa Ulinzi: Mnamo tarehe 15 Novemba 2024 nilitembelea mradi na kubaini kutokuwepo kwa ulinzi wa kingo za barabara kutoka Chainage 3+500 hadi 5+200 kwenye Barabara ya Itilima-Ikindilo. Usanifu wa barabara hii haukuzingatia kinga kwenye kingo, na kusababisha hatari za usalama kama ajali, kuanguka kwa watembea kwa miguu, na mmomonyoko wa udongo. TARURA inashauriwa kuweka ulinzi wa kingo za barabara ili kupunguza hatari hizi.<br>Vifaa vya Usalama Visivyotosheleza: Taarifa ya mradi ya Mwezi Septemba 2024 ilionesha kutotekelezwa kwa mahitaji ya vifaa vya usalama wakati wa matumizi ya kemikali ya Ecozyme, jambo linalokiuka Sheria ya OSHA ya 2003. Uvujaji huu, kutokana na usimamizi hafifu, unawaweka wafanyakazi katika hatari za kiafya. TARURA inashauriwa kuhakikisha utekelezaji wa vifaa vya usalama na kuboresha usimamizi ili kuepuka hatari. |
| Simiyu-H/W Bariadi | S10/022/2023/2024/W/01 | 895,150,000.00 | Kutokuzingatia usalama wa barabara kwa watumiaji wasio na magari<br>Nilibaini kutokuwepo kwa kingo za barabara kwenye mabega ya Barabara ya Dutwa-Mwamondi, kinyume na kifungu cha 4.9.3 cha Mwongozo wa Ubunifu wa Barabara (2011), kinachohitaji kuwepo kwa njia za watembea kwa miguu zilizozungukwa na kingo ili kutenganisha watumiaji wasio na magari katika vituo vya biashara na miji. Hii ilitokana na usanifu usioridhisha, na kuongeza hatari kwa watumiaji wa barabara, hasa waendesha pikipiki. Menejimenti ya TARURA inashauriwa kuhakikisha utekelezaji wa kingo za |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | barabara ili kuboresha usalama kwa watumiaji wote wa barabara. |
| Tabora-H/W Sikonge | S10/025/2023/2024/W/17 | 127,198,800 | Ushindiliaji na usawazishaji wa barabara kutofanyika ipasavyo kwenye Barabara ya Kiloleli-Kanyamsenga, na kusababisha uharibifu mkubwa wa barabara. |
| H/M Tabora | S10/025/2023/2024/W/87 | 467,805,564.27 | Barabara ya Dr. Kigwangala (Ch 0+000-0+620): Mti mmoja kati ya sita uliotakiwa kuondolewa uliachwa kando ya barabara. Vivuko vya barabara havikujazwa udongo kusawazishwa, sehemu kati ya Ch 0+200-0+500 hazikujazwa na kushindiliwa vya kutosha, na matatizo ya mkataba hayakutatuliwa hadi tarehe 10 Oktoba 2024.<br>Barabara ya KKKT (430m): Shughuli za kaya, ikiwemo mchanga na kokoto zilizohifadhiwa barabarani. Vivuko vya barabara havikujazwa udongo na kusawazishwa.<br>Mfereji wa Kalubania (350m): Kazi ya ujenzi wa mawe ilikamilika lakini haikujazwa udongo hivyo kuhatarisha umadhubuti wake.<br>Barabara ya Kaloleni-Magoweko (4.5km): Ingawa barabara iliundwa upya na miundombinu ikajengwa, ramani yake haikuwepo ili kuthibitisha kazi zilizokamilika. |
| Tabora-H/W Uyui | S10/025/2023/2024/W/88 | 474,996,557.10 | Udongo haukurudishwa ipasavyo kwenye baadhi ya maeneo na hivyo kusababisha mmomonyoko wakati wa msimu wa mvua. Vifaa visivyotumika kama kokoto na mawe havikutolewa wakati wa kuondoa vifaa, na mapungufu ya mradi (snags) yaliyobainika hayakuwa yameshughulikiwa. |
| Tabora-H/W Uyui | S10/025/2023/2024/TBR/W/22 | 308,075,334 | Katika Mkoa wa Tabora, nilibaini barabara duni kutokana na kutoshindiliwa vizuri na kucheleweshwa kukamilisha miradi kwa siku 28 baada ya tarehe ya kumaliza iliyorekebishwa ya 12 Septemba 2024. Changamoto hizi zimetokana na ukosefu wa usimamizi wa kutosha wakati wa ujenzi. Hali hii imesababisha hatari za usalama, gharama kubwa za matengenezo, na kupungua kwa imani ya jamii kwa kazi za TARURA. |
| Kilimanjaro-H/W Rombo | S10/009/2023/2024/W/108 | 1,396,969,700 | Mifereji haikukufanyiwa matengenezo<br>Uhakiki ulionesha kuwa mifereji ya pembeni ya Barabara ya Kikelelwa-Forest ilikuwa ikiharibika kutokana na ukosefu wa matengenezo bora, kinyume na Kifungu cha 8.16.1 cha Vipimo vya Matengenezo ya Barabara, 2010. Hali hii ilisababishwa na udhibiti duni kutokana na idadi ndogo ya wahandisi katika ofisi ya TARURA Rombo. Kukosa matengenezo bora kunaathiri uimara na kudumu kwa mifereji ya pembeni, na kusababisha kuharibika mapema na gharama kubwa za matengenezo. Inapendekezwa kwamba TARURA iongeze wahandisi na mafundi ili kuhakikisha utekelezaji wa matengenezo bora. |
| Kilimanjaro-H/W Same | S10/009/2023/2024/W/124, wenye thamani ya Sh. 1,033,775,154 na S10/009/2023/2024/ | 1,492,804,204 | Barabara Imejengwa Bila Kuwekwa Alama za Barabarani na Vizuizi katika Kona Kali za Milima<br><br>Katika mikataba S10/009/2023/2024/W/124 na S10/009/2023/2024/W/129 vizuizi, alama za |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | W/129 wenye thamani ya Sh. 459,029,050 | | barabara, na mabango ya tahadhari vilijumuishwa kwenye matakwa ya mkataba hiyo. Hata hivyo, nilitembelea maeneo ya mradi mnamo tarehe 29 Oktoba 2024 na kugundua kuwa vizuizi, alama na mabango havikuwepo kwenye barabara za miradi husika, katika maeneo ya madaraja na kona kali. Aidha, kati ya mabango kumi ya lazima yaliyojengwa chini ya mkataba S10/009/2023/2024/W/124, mabango tisa hayakuwepo licha ya malipo ya Sh. 4,000,000, kutokana na wizi na mabango mengine kutorejeshwa. Kukosekana kwa vipengele hivi vya usalama kunaongeza hatari ya ajali kwa watumiaji wa barabara. TARURA inashauriwa kuhakikisha miradi yote ya barabara inajumuisha mabango sahihi, kufunga mabango ya makaravati na madaraja, na kuweka mikakati ya kuzuia wizi na kuhakikisha uingizwaji wa mabango yaliyopotea kwa wakati. |
| H/Jiji Arusha | S10/001/2023/24/W/27 | 611,000,000.00 | Alama za Barabarani Hazikuwekwa<br>Tarehe 14 Oktoba 2024, michoro ya barabara haikuwa imekamilika. Timu ya usimamizi wa mradi, haikutoa cheti cha kukamilika au kuandaa orodha ya mapungufu (snag list) kwa shughuli ambazo hazijakamilika. Hii inahatarisha usalama barabarani kwani alama ni muhimu kwa kuongoza watumiaji wa barabara. TARURA inashauriwa kuhakikisha alama za barabarani na kazi zozote ambazo hazijakamilika zinakamilishwa bila kuchelewa. Zaidi ya hayo, timu ya usimamizi wa mradi inapaswa kufanya ukaguzi wa mwisho na kuandaa orodha ya mapungufu kushughulikia kazi ndogo zilizosalia. |
| Ruvuma-H/W Songea | S10/020/2023/2024/W/05 | 1,423,057,550 | Kingo za Barabara Hazikujengewa ili Kuzilinda Kwenye Barabara za Matomondo - Mlale na Songea DC HQ (2km)<br><br>Wakati wa ukaguzi wa miradi tarehe 27 Novemba 2024, nilibaini kingo za barabara ambazo hazikujengewa ili kuzilinda katika Barabara ya Matomondo-Mlale (Ch. 0+300 hadi 1+000 LHS, 0+200 hadi 0+500 RHS) na Barabara ya Songea DC HQ (Ch. 0+100 hadi 0+160 RHS), kinyume na Kifungu cha 3903(b) cha "Standard Specifications for Road Works, 2000". Maeneo haya hayakuwa na mifereji au kinga kama vile lami au zege, hali inayohatarisha ubora wa barabara kutokana na athari za hali ya hewa na shughuli za binadamu. TARURA inashauriwa kuhakikisha kingo za barabara zinalindwa kwa kutumia vifaa vinavyofaa ili kuongeza uimara wa barabara. |
| Ruvuma-H/W Nyasa | S10/020/2023/2024/W/32 | 609,363,350 | Kutokuwepo kwa kingo za daraja, Kifusi Kusombwa na Maji na Kutokuwepo kwa Alama za daraja<br>Mnamo tarehe 28 Novemba 2024 nilitembelea eneo la mradi na kubaini kuwa kifusi katika upande mmoja wa Daraja la Kilindi kwenye Barabara ya Litoromelo P/S-Kilindi kimeondolewa na maji na kusababisha kupungua kwa upana wa njia katika |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | sehemu ya kuingilia darajani. Pande zote za daraja zina mteremko mkali unaohitaji kurekebishwa na kujengewa pamoja na kingo na kuta za mashavu ya daraja. Aidha, alama za kuonesha daraja hazikuwa zimefungwa. TARURA Ruvuma inahimizwa kushughulikia masuala haya kwa kujaza upya, kurekebisha miteremko, na kujengea sehemu za kuingilia na kuta za mabawa ili kuhakikisha daraja linafanya kazi ipasavyo na kudumisha usalama. |
| Ruvuma-H/W Tunduru | S10/020/2023/2024/ W/52 | 679,156,000 | Barabara ya Nazareth Workshop-Church-Songea-Masasi: Mafuriko yalibainika kwenye mifereji ya pembeni kati ya Ch.0+00 hadi 0+060, ambapo maji yalitiririka kuelekea barabara ya dharula (Service Road) na kusababisha mmomonyoko wa udongo kwenye barabara inayovuka (R.C. Church-Njasi).<br><br>Barabara ya TUDECO-Tunduru Sec-Borrow Pit: Mmomonyoko ulionekana katika Ch.0+005, huku dalili za mmomonyoko chini ya barabara kuelekea darajani zikihitaji kifusi kujazwa upya. Nyufa zilionekana kwenye mifereji ya kingo kutoka Ch.0+200 (RHS) hadi darajani. |
| Geita - H/W Chato | S10/004/2023/2024/ W/12 | 286,076,703.00 | Tabaka la juu la barabara lisilo na ubora<br>Nilitembelea Barabara ya Kalema-Gatini-Nyabugera, na kubaini kuwa uharibifu katika tabaka la juu la barabara kutokana na mbinu duni za ujenzi na usimamizi hafifu. Ikiwa tatizo hili halitarekebishwa, linaweza kusababisha uharibifu wa haraka wa barabara, ongezeko la gharama za matengenezo, na kupungua kwa maisha ya barabara. TARURA inahimizwa kuhakikisha miundombinu ya mifereji inajengwa ili kulinda barabara na kuzuia gharama zisizo za lazima. Hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa kwa kuchimba mifereji ya pembeni, na mkandarasi anatakiwa kurekebisha kasoro kabla ya kipindi cha dhamana ya kasoro kwisha. |
| Geita - H/W Chato | S10/004/2023/2024/ W/63 | 470,607,354.72 | Ubora Duni wa Zege Katika Ujenzi wa Mifereji Kwenye Ch. 000+850<br>Nilitembelea Barabara ya Kahumo Bus Terminal (1.0 km) katika Wilaya ya Chato, na kubaini uwepo wa zege duni katika ujenzi wa mfereji wa pembeni kwenye Ch. 000+850. Zege hili lilikuwa likisambaratika kwa kuguswa kutokana na kutumika mchanga usiofaa. Tatizo hili lilisababishwa na usimamizi hafifu na ukosefu wa udhibiti wa ubora wakati wa ujenzi. TARURA inahimizwa kuhakikisha miundombinu ya mifereji inajengwa kwa viwango vinavyostahili ili kuepuka gharama zisizo za lazima kwa serikali na kuwasiliana na mkandarasi ili kurekebisha kasoro hizo ndani ya kipindi cha dhamana ya kasoro. |
| Geita- H/W Chato | S10/004/2023/2024/ W/33 | 479,392,530.00 | Nilitembelea Barabara ya Buseresere-Makurugusi na kubaini uharibifu wa barabara uliotokana na msongamano wa magari mazito na uwezo mdogo wa barabara. Aidha, ukosefu wa mifereji sahihi ya pembeni ulisababisha maji ya mvua kusomba kingo |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | na tabaka la barabara, na hivyo kuongeza uharibifu. Changamoto hizi zinaweka hatarini usalama wa watumiaji, kuongeza gharama za matengenezo, na kupunguza maisha ya barabara. TARURA inahimizwa kujenga mifereji ya maji, kulinda kazi zilizokamilika, na kuhakikisha mkandarasi anarekebisha kasoro hizo ndani ya kipindi cha dhamana ili kuzuia uharibifu zaidi na hasara ya kifedha. |
| H/W Geita | S10/004/2023/2024/ W/27 | 453,999,930.00 | Barabara ya CCM-Sheli ya Nassoro (0.25km)<br>Mnamo tarehe 9 na 10 Oktoba 2024 nilitembelea mradi na kubaini kuwa barabara iliyotengenezwa kwa lami haikuwekewa kingo zlizoimarishwa kwa mifereji ya pembeni au vifaa vya lami/zege, kinyume na Kifungu cha 3903(b) cha Vipimo vya Kawaida vya Ujenzi wa Barabara, 2000, na Aya ya 1.5.6 ya Mwongozo wa Ubunifu wa Tabaka za Barabara, 1999. Ukosefu wa bajeti ulitajwa kuwa chanzo cha tatizo hili. Kutokuwepo kwa mifereji na ulinzi wa mabega kunaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo, kuingia kwa maji kwenye tabaka za lami, na kuhatarisha usalama wa watumiaji wa barabara. TARURA inahimizwa kujenga mifereji ya maji na kuhakikisha kingo za barabara zinalindwa ipasavyo ili kulinda kazi zilizokamilika na kupunguza hasara ya fedha za umma.<br><br>Barabara ya Nyamasenga-Luhuha-Kizira<br>Nilitembelea mradi na kubaini uwepo wa mawe kwenye barabara na mashimo barabarani na kwenye kingo yaliyosababishwa na mmomonyoko wa udongo. Aidha, kufusi kwenye makaravati hakikujazwa na kushindiliwa vyema, huku mifereji ya maji ikiwa myembamba na ya kina kifupi, jambo linalozuia mtiririko wa maji. Mapungufu haya, ambayo yanatokana kazi duni ya mkandarasi, yana hatari ya kuathiri uimara wa miundombinu ya barabara na usalama wa watumiaji. TARURA inashauriwa kulazimisha hatua za marekebisho kutoka kwa mkandarasi ndani ya kipindi cha dhamana ya kasoro, kujenga mifereji ya maji sahihi, na kuhakikisha utekelezaji wa viwango vya ubora ili kuzuia uharibifu zaidi na hasara ya fedha. |
| H/W Geita | S10/004/2023/2024/ W/29 | 640,913,800.00 | Ukosefu wa Mfumo wa Mifereji ya Pembeni Kusababisha Mmomonyoko wa Barabara<br>Wakati wa ukaguzi wa eneo tarehe 9-10 Oktoba 2024 kwenye Barabara ya Katoro-Nyabulolo-Nyalwanzaja, ilibainika kuwa ukosefu wa mfumo wa mifereji ya pembeni ulisababisha mmomonyoko mkubwa, kusomba sehemu za barabara na kuzuia watumia barabara kupita kutokana na uwepo wa mawe na mashimo. TARURA inahimizwa kujenga mifereji ya maji, kulinda kazi zilizokamilika, na kuhakikisha mkandarasi anarekebisha kasoro ndani ya kipindi cha dhamana ili kuzuia uharibifu zaidi na gharama zisizo za lazima. |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Geita- H/W Nyang'hwale | S10/004/2023/2024/W/40 | 234,998,000.00 | Barabara kuwa karibu na makazi ya watu umezuia ujenzi wa mifereji ya maji, kwani mipaka ya barabara na maeneo ya hifadhi za barabara hayakuainishwa awali. TARURA inahimizwa kutoa kipaumbele kwa alama za mipaka ya barabara, kujenga mifereji ya maji muhimu ili kulinda kazi zilizokamilika, na kuzuia mmomonyoko au hasara ya fedha za umma. |
| Geita- H/W Mbongwe | S10/004/2023/2024/W/43 | 471,816,631.41 | Kuzuia kwa Makaravati Katika Sehemu ya Kutolea Maji<br>Nilitembelea mradi na kubaini kuwa matoleo ya karavati kwenye eneo la Nyakafuru (Nambari 40) yalikuwa yamezibwa na mkazi aliyejishughulisha na kilimo kwenye eneo hilo. Hii ilitokana na usimamizi hafifu na ukosefu wa elimu kuhusu kutunza miundombinu ya barabara. Kuzibwa kwa matoleo ya karavati kunaweza kusababisha mtiririko usiofaa wa maji, kusababisha mmomonyoko wa changarawe kwenye barabara na kusababisha upotevu wa fedha za umma. TARURA inahimizwa kushughulikia tatizo hili kwa kuhakikisha mifereji inajengwa ipasavyo, kutoa elimu kwa jamii, na kurekebisha kasoro ndani ya kipindi cha dhamana. |
| Iringa- H/W Kilolo | S10/005/2023/2024/W/105 | 99,987,000.00 | Kalvati lililojengwa halina miundombinu ya mapokeo ya maji kwenye Ch.4+200 |
| Iringa- H/Mji Mafinga | S10/005/2023/2024/W/56 | 165,511,250.00 | Kujaza kifusi kwenye daraja la Barabara ya Igoma-Ihanzutwa hakukufanyika ipasavyo. Aidha, kifusi kwenye makaravati kwenye Barabara ya Igombavanu-Mapogoro hakikujazwa kabisa. |
| Iringa- H/Mji Mufindi | S10/005/2023/2024/W/102 | 49,968,000.00 | Kingo zilionekana kutitia katika barabara ya Kitelewasi Kikombo road |
| H/M Iringa | S10/005/2023/2024/W/39 | 191,548,850.00 | Muungano Frelimo Road - Makaravati yaliyojengwa kwenye kiwanja cha binafsi yanahitaji kuhamishwa. Pia, katika Barabara ya Isoka B, miundombinu ya mifereji ya maji bado haijajengwa. |
| H/M Iringa | S10/005/2023/2024/W/46 | 239,473,740.00 | Barabara ya Lugenge: Kuna migogoro ambayo haijatatuliwa hadi tarehe ya ukaguzi ya Desemba 2024, ujenzi umesimama. Kwenye PSPF Zone 2: Kifusi hakikujazwa ipasavyo. |
| H/W Iringa | S10/005/2022/2023/W/48 | 543,655,600.00 | Barabara ya Isimani Ikengeza: Hakuna alama za barabara lakini malipo yamefanyika. Mifereji ya kukamata maji haijajengwa, na kuta za makaravati kwenye Ch. 6+750, 7+100, na 7+900 hazina zege la kutosha. |
| Kigoma - H/W Buhigwe | S10/074/2023/2024/W/26 | 1,817,522,590.00 | Ukaguzi wa tender Nambari S10/074/2023/2024/W/26 yenye thamani ya Sh. 1,817,522,590 ulionesha mapungufu katika ujenzi wa makaravati nane kwenye Barabara ya Bukoba hadi Muhunga. Kazi za kinga, kama mifereji ya maji, zilikuwa zikikosekana, jambo lililoongeza hatari ya mmomonyoko wa udongo. Nyufa zilionekana kwenye makaravati jambo linalohatarisha ubora wa ujenzi, na kuonesha kutotekeleza viwango vinavyohitajika. Ukosefu wa usimamizi na udhibiti wa ubora ndiko kulikosababisha matatizo haya. Uongozi wa |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | TARURA unapaswa kuhakikisha ujenzi wa mifereji ya maji unafanywa ipasavyo, kurekebisha nyufa kwenye makaravati, na kuboresha usimamizi ili kushughulikia mapungufu haya. |
| Kigoma - H/W Kibondo | S10/074/2023/2024/ W/35 | 887,436,869.00 | Uwepo wa Nguzo ya Umeme Ndani ya Eneo la Barabara<br>Ukaguzi wa mkataba Nambari S10/074/2023/2024/W/35, wenye thamani ya Sh. milioni 887.43, ulibaini kuwa nguzo ya umeme ilikuwa ikizuia eneo la barabara kwa muda wa miezi 14 licha ya TANESCO kuarifiwa. Haya yanazidisha hatari ya ajali na kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Uongozi unapaswa kuratibu na TANESCO ili kuhamisha nguzo hiyo. |
| Songwe- H/W Mbozi | S10/024/2023/2024/ W/51 | 949,995,680.00 | Kutojengwa kwa Kingo za Makaravati Kumesababisha Uharibifu wa Kazi Zilizokamilika<br>Barabara ya Ivugula-Ichesa, iliyo kwenye kipindi cha matazamio tangu tarehe 17 Mei 2024, haikujengewa kingo kwenye makaravati kutokana na makosa ya usanifu na upungufu wa bajeti, jambo linalosababisha mmomonyoko wa udongo na hatari ya uharibifu wa miundombinu. TARURA inapaswa kujumuisha hatua ujenzi wa kingo katika mipango ya baadaye, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, na kushughulikia kasoro zilizobainika kwa haraka. |
| Tanga- H/W Korogwe | S10/026/2023/2024/ W/01 | 379,941,900.00 | Uharibifu wa Barabara Kutokana na Shughuli za Kilimo cha Umwagiliaji Kwenye Mtandao wa Barabara wa TARURA<br>Mradi wa Barabara ya Buiko-Manyata-Toronto karibu na Bonde la Mto Pangani unakutana na uharibifu kutokana na shughuli za kilimo cha umwagiliaji, ambapo wakulima wanakata barabara ili kutengeneza mifereji. Udhaifu katika utekelezaji wa sheria za matumizi ya barabara umekuwa chanzo cha tatizo hili, na kusababisha uharibifu wa mara kwa mara na kuongezeka kwa gharama za matengenezo. TARURA inapaswa kuongeza ushirikiano na taasisi husika, kushirikisha watumiaji wa maji ili kushughulikia tatizo hili, na kujumuisha makaravati au au aina nyingine ya mifereji katika miundo ya barabara ili kuzuia uharibifu zaidi. |
| Njombe- H/W Makete | S10/017/2023/2024/ W/41 | 269,733,000.00 | Nilibaini kazi za kiwango cha chini kwenye marekebisho ya Barabara ya Madihani-Lufilyo (10.0km), ikiwemo uchimbaji usiokamilika wa mifereji ili kuruhusu mtiririko wa maji kwa urahisi hadi kwenye makaravati kwenye Ch. 2+000, 3+800, na 10+500. Pia, mfumo wa mifereji ya mawe kwenye Ch. 3+400 umeziba, na nyufa zilionekana kwenye msingi wa zege la mifereji. |
| Njombe- H/W Makete | S10/017/2023/2024/ W/44 | 293,200,000.00 | Kulikuwa na mapungufu kwenye ukarabati wa Barabara ya Makete-Nkenja (8.6 km), ikiwemo nyufa kwenye mifereji ya mawej na uchimbaji usiokamilika wa mifereji ya kukamata maji, jambo linazuia mtiririko wa maji kwa urahisi hadi kwenye makaravati. Haya yanadhihirisha mapungufu katika ubora wa ujenzi na utekelezaji wa kazi. |

| Halmashauri | Namba ya Mkataba | Gharama ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| H/Mji Njombe | S10/017/2023/2024/W/08 | 85,000,000.00 | Niibaini kazi za kiwango cha chini kwenye ukarabati mkubwa wa Daraja la Mahuna, ambapo kulikuwa na nyufazlioenea hadi kwenye nguzo za daraja. Hatua za haraka zinahitajika kushughulikia tatizo hili. |
| Njombe- H/W Ludewa | S10/017/2023/2024/W/53 | 228,097,000.00 | Nilibaini mapungufu kwenye ujenzi wa Barabara ya Lifuma-Mbwila katika miundombinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na daraja 1, daraja lenye jiwe linalobeba maji (solid drift) 1, na makaravati 10 ya mabomba ya RC. Masuala yaliyobainika ni pamoja na uchimbaji usiokamilika wa mifereji ya kukamata maji, kifusi kutoshindiliwa kwenye moja ya makaravati, na mmomonyoko wa udongo. Mvua kubwa zilisababisha sehemu za makaravati kujaa, na kuacha matundu madogomadogo kwenye kuta za karavati, na hivyo kuathiri hali ya makaravati. Haya yanadhihirisha mapungufu makubwa katika udhibiti wa ubora, na yaathiri uimara na ufanisi wa miundombinu iliyojengwa. |
| Jumla | | 21,896,287,637.50 | |

### Kiambatisho Na.37:Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Miongozo na Usanifu katika Miradi ya Barabara za TARURA

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Arusha- H/W Monduli | Mwaka wa Fedha 2023/24, TARURA Mkoa wa Arusha ilingia mkataba Na. S10/001/2023/2024/W/68 wenye thamani ya Sh. 474,982,440 kwa ajili ya kuboresha barabara za Makuyuni (km 0.65) hadi kiwango cha lami katika wilaya ya Monduli. Mradi ulianza tarehe 23 Novemba 2023 na kukamilika tarehe 21 Mei 2024 (Miezi 6) chini ya Mfuko wa Jimbo (CDF). | 474,982,440.00 | Uachilivu Katika Ubunifu na Ujenzi wa Barabara za Ufikiaji<br><br>Kifungu cha 1203 cha Maelezo ya Viwango vya Ujenzi wa Barabara 2000 kintaka barabara zinazoingia barabara kuu kujumuishwa katika miradi ya ujenzi ili kuhakikisha mzunguko wa magari na kulinda miundombinu. Mnamo tarehe 12 Oktoba 2024 nilitembelea mradi na kubaini kuwa uboreshaji wa Barabara ya Makuyuni haukujumuisha barabara zinazoingia kwenye barabara hiyo (access roads), jambo lilosababisha uharibifu wa mifumo ya mifereji na kujaa vumbi. Hii ilitokana na upungufu wa bajeti. TARURA inashauriwa kuhakikisha kuwa bajeti za baadaye zinajumuisha vipengele muhimu kama vile barabara za ufikiaji. |
| H/Jiji Arusha | Katika mwaka wa fedha 2023/24, Halmashauri ya Jiji la Arusha ilingia mkataba tarehe 2 Februari 2024 Na. 7003/2023/2024/W/48 kwa gharama ya Sh. 2,799,709,460.00 kwa ajili ya kuboresha barabara za T.C.A (km 0.68), Levolosi | 2,799,709,460.00 | Utekelezaji wa Mradi wa Barabara Bila Usanifu wa Kina wa Kihandisi<br><br>Ukaguzi wa mwaka 2023/24 ulionesha kuwa mradi wa barabara ulitekelezwa bila ubunifu wa kina wa uhandisi, jambo linalokiuka Mwongozo wa Barabara Ndogo (2016) na kuleta hatari ya ujenzi wa chini ya viwango, kuongezeka kwa gharama, na kutozingatia viwango vilivyowekwa. Hitaji la kutumia fedha |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | (km 0.2), C.C.M (km 0.14), Kaloleni (km 1), Kwa Benson (km 1), na Barabara za TRA-East Africa katika Jiji la Arusha. Mradi ulianza tarehe 11 Machi 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 11 Septemba 2024 (Miezi 6). Mradi huu unasimamiwa na TARURA - Wilaya ya Arusha. | | zilizoletwa ndani ya muda mfupi lilisababisha kutoandaliwa kwa usanifu huu muhimu.<br><br>Kutofautiana Kati ya Michoro ya Miongozo na Orodha ya Kiasi cha Kazi (BOQ)<br><br>Ukaguzi wa mwaka 2023/24 uligundua kutofautiana kati ya BOQ na michoro, ambapo BOQ ilielezea matumizi ya Changarawe kilichokandamizwa (CRR), huku michoro ikionesha matumizi ya Jiwe la Changarawe (CRS) kwa tabaka la chini la barabara. Hii ilitokana na kutokuwepo kwa mapitio ya kutosha ya michoro na nyaraka za zabuni. Utofauti huu unaweza kusababisha makosa katika utekelezaji, migogoro, ucheleweshaji, na kuongezeka kwa gharama. |
| Singida - H/W Iramba | Katika mwaka wa fedha 2023/24, TARURA Mkoa wa Singida ilingia mkataba Na. S10/023/2023/24/W/29 wenye gharama ya Sh. 1,499,925,000.00 uliofungwa tarehe 1 Novemba 2023 kwa ajili ya kuboresha barabara za mji wa Kiomboi (Mwanza km 0.48, Old Kiomboi-Salasala km 0.5, Kitila km 0.32, Nyerere km 0.14, na Swai km 0.08) hadi kiwango cha lami katika Halmashauri ya Iramba chini ya ufadhili wa Tozo. Mradi ulianza tarehe 8 Novemba 2023 na unatarajiwa kukamilika tarehe 3 Agosti 2024. | 1,499,925,000.00 | Kutokuzingatia Mahitaji ya Watumiaji katika vivuko<br><br>Nilibaini kuwa miundo ya barabara haikuzingatia ipasavyo mahitaji ya watumiaji kwa vivuko vya magari, hasa katika maeneo ya biashara kama Soko la Old Kiomboi. Ingawa vivuko vya waenda kwa miguu viliwekwa, kukosekana kwa vivuko vya magari kunapunguza upitikaji wa barabara na kuathiri utendaji wake kwa watumiaji.<br><br>Ujenzi Usio Kamili wa Mifereji ya Maji<br><br>Michoro inaelekeza ujenzi wa mifereji ya maji upande wa barabara zote, kama ilivyopangwa katika muundo ulioidhinishwa. Nilibaini kuwa, barabara ya Kitila ilikuwa na mifereji upande mmoja, kinyume na muundo ulioidhinishwa.<br><br>Mwangaza Hafifu wa Mtaa ya Barabarani<br><br>Nilibaini kuwa, baadhi ya taa za barabarani zilizowekwa kwenye barabara zina mwangaza hafifu ambao haukidhi viwango vinavyohitajika.<br><br>Kifusi Kilichochimbwa Kutotupwa Ipasavyo<br><br>Aya ya 2209 ya Vigezo vya Kawaida vya Kazi za Barabara, 2000, inasema kuwa, vitu vilivyochimbwa ambavyo haviwezi kutumika tena kwa kujaza lazima viondolewe kwenye eneo la mradi na viwekwe kwa njia sahihi au vitumike kwa |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | urejeshaji wa mashimo ya michanga. Niligundua kuwa, kifusi kilichochimbwa kiliachwa kando ya barabara hadi wakati natembelea mradi. Kifusi hiki hakikutupwa ipasavyo, kama inavyohitajika na aya ya 2209 wa Vigezo vya Kawaida vya Kazi za Barabara, 2000. |
| Singida-H/W Iramba | Katika mwaka wa fedha 2023/24, TARURA Mkoa wa Singida ilitekeleza mkataba Na. S10/023/2023/24/W/92 wenye thamani ya Sh. 291,113,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa mifereji, kujaza kifusi kwenye maeneo ya mifereji kando ya barabara ya Mtoa-Masimba-Kibaya na ujenzi wa karavati yenye seli 3 za zege ya nondo kwenye barabara ya Urughu-Haila-Ujungu katika Wilaya ya Iramba chini ya Mfuko wa Jimbo. Mkataba ulisainiwa tarehe 17 Aprili 2024, mradi ulianza tarehe 18 Aprili 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 14 Agosti 2024. | 291,113,000.00 | Kutokuwepo kwa Usanifu wa Kina wa Kihandisi kwenye Ujenzi wa Kalvati (Box culvert)<br><br>Ukaguzi uliofanyika tarehe 8 Oktoba 2024 ulibaini upungufu katika ujenzi wa karavati kwenye Barabara ya Urughu-Haila-Ujungu. Mradi huu haukuwa na Usanifu wa Kina wa Kihandisi, hivyo kukiuka Kanuni ya 137(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013, inayohitaji maandalizi na idhini ya nyaraka za kiufundi kabla ya kuanza mradi. Licha ya kuwa mradi huu ulikuwa ni wa dharura, ujenzi haukukamilika na ulifanyika kwa awamu, kinyume na dharura inayohitajika chini ya Kifungu cha 7(2)(c) cha Sheria ya Usimamizi wa Majanga, 2015. |
| Tabora-H/W Uyui | Mkataba Na. S10/025/2023/2024/W/10 kwa ajili ya Kuboresha Barabara na Ujenzi wa Mifereji kando ya barabara ya Tula-Mwamlela-Lutona (km 10 na mifereji 4), Magiri-Imalampaka-Kigwa (7km na mifereji 1), Lutende-Mwakadara (Simbodamalo) (km14.9 na mifereji 5), Mwadaudi-Nyankombe (11km na mifereji 6) katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui chini ya mfuko wa jimbo. | 491,860,500.00 | Ukaguzi uliofanyika tarehe 2 Novemba 2024 ulionesha kuwa katika makutano ambapo barabara zilizojengwa zilipojumuika na barabara zilizopo, karavati zilizojengwa na TANROADS hazikukidhi kiwango cha upana cha Barabara ya Daraja la DC6 cha mita 8. Kalvati kwenye Barabara ya Chuo (m 7.8), Barabara ya AIC Mjimwema (M 6.0), Barabara ya Soko la Mawese (m 7.2), na Barabara ya Inakwetu (m 7.5) zilikuwa nyembamba kuliko kiwango kinachotakiwa. Tofauti hii ilisababishwa na ukosefu wa uratibu kati ya TARURA na TANROADS, ambao ulishindwa kuzingatia mahitaji ya baadaye ya barabara za kuingia. Kalvati nyembamba zinaleta changamoto kwa wapoitaji kwa kuzuia ufanisi wa barabara na kuleta hatari kwa usalama. |
| Pwani-H/W Rufiji | Tarehe 11 Desemba 2023, TARURA ilisaini mkataba Na. S10/2023/2024/W/15 wenye thamani ya Sh. 11,495,250,044.64 kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la | 11,495,250,044.64 | Kupunguzwa kwa Urefu wa Daraja la Mohoro Kutoka Mita 100 Iliyoelekezwa Kwenye Usanifu hadi Mita 80 Bila Sababu za Misingi<br><br>Mradi wa Daraja la Mohoro, uliosanifiwa kwa upana wa mita 100 kulingana na |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | Mohoro katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji. Mradi ulianza tarehe 31 Januari 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 31 Julai 2025 (Miezi 18). | | Ripoti ya Haidrolojia na Haidroliki, ulitekelezwa kwa upana wa mita 80 kutokana na changamoto ya fedha. Mabadiliko haya, yaliyobainika wakati wa ujenzi, yalileta hitaji la kupitia upya usanifu ili kushughulikia upungufu wa uwezo wa daraja kupitisha maji ya kutosha. |
| Pwani-H/W Rufiji | Tarehe 08 Machi 2024, TARURA ilisaini mkataba Na. S10/2023/2024/W/17 wenye thamani ya Sh. 4,769,050,000 kwa Uboreshaji wa Barabara ya Utete-Kingupira (km 32) kwa kutumia Teknolojia ya “Mult-enzymic compound”. Mradi ulianza tarehe 8 Aprili 2024 na ulitarajiwa kukamilika ndani ya Miezi 12. | 4,769,050,000.00 | Ukosefu wa Taarifa ya Usanifu wa Lami katika Mradi wa Barabara ya Utete-Kingupira<br><br>Ukaguzi wa mradi wa maboresho ya barabara ya Utete-Kingupira (km 32) ulionesha kutokuwepo kwa taarifa ya usanifu wa lami, kinyume na mahitaji ya LVRM 2016 na Mwongozo wa Nyenzo na Usanifu wa Lami (1999). Kukosekana kwa ripoti hii kulitokana na kutegemea teknolojia mbadala (kiunganishi cha Enzymic), jambo linalooneshа kutokufuata ipasavyo michakato ya utunzaji kumbukumbu za usanifu. Bila ripoti hii, uimara wa lami iliyowekwa hauwezi kuthibitishwa ipasavyo. |
| Dodoma- H/W Chamwino | TARURA ilisaini mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/29 wenye thamani ya Sh. 7,874,965,401 tarehe 10 Oktoba 2023 kwa ajili ya kuboresha barabara km 6.95 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino hadi kiwango cha lami chini ya mradi wa majaribio wa ujenzi kwa kutumia teknolojia mbadala. | 7,874,965,401.00 | Ukosefu wa Eneo la Kusimama Mabasi na Kasoro Zilizogundulika<br><br>Ukaguzi wa mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/29 ulionesha kwamba maeneo ya mabasi hayakujumuishwa katika usanifu wa barabara, na hivyo hayakuwekwa katika sehemu zilizojengwa, huku pia kukiwa na kasoro zilizogundulika kwenye tabaka la barabara katika kilomita 1+270 ya Barabara ya Rashid Kawawa. Matatizo haya yalitokana na mapungufu kwenye usanifu na ukosefu wa udhibiti wa ubora wakati wa ujenzi. Ukosefu wa maeneo ya kusimama mabasi unaongeza msongamano wa magari barabarani na kuhatarisha usalama, huku kasoro kwenye uso wa barabara zikihatarisha uimara wa barabara na kuhitaji matengenezo mapema. |
| H/Jiji Dodoma | Katika mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24, TARURA ilitekeleza Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/18 na Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/20 kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara ya kuingia eneo la viwanda Nala (km 5.115) | 8,458,450,116.70 | Ukosefu wa Kivuko (Access Slab) katika Kilomita 1+170 na Kusababisha Kuziba kwa Mifereji ya maji<br><br>Kulingana na Sehemu ya 2.1 ya Vigezo vya Kawaida vya Kazi za Barabara (2000) na Kipengele cha 3.4.5 cha Mwongozo wa Ubunifu wa Barabara na Madaraja, maeneo ya kupita (access slabs) yanahitajika kuhakikisha usalama wakati |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | hadi kiwango cha lami katika Jiji la Dodoma kwa awamu ya I na II, kwa jumla ya gharama ya Sh. 4,660,127,060.95 na Sh. 3,798,323,055.75 mtawalia. | | wa kuvuka na kudumisha mifumo ya mifereji ya maji. Nilitembelea mradi mnamo tarehe 20 Septemba 2024, na kubaini kwamba katika Kilomita 1+170 hakukuwa na kivuko, jambo ambalo lilifanya watumiaji kujaza mifereji ya maji kwa udongo ili kutengeneza njia za kupita. Hali hii ilizuia mtiririko wa maji, na hivyo kuongeza hatari ya mafuriko na uharibifu wa barabara. |
| Mkoa wa Songwe | TARURA ilingia mkataba Na. AE/092/2022-2023/HQ/W/03 kwa ajili ya kuboresha Barabara ya Landani-Kiwira (km 5) pamoja na Daraja la Mwalisi kwa jumla ya Sh. 5,752,955,420 chini ya ufadhili wa Tozo kwa kipindi cha mkataba cha miezi kumi na miwili (12). | 5,752,955,420.00 | Ukosefu wa Mifereji ya Pembeni<br><br>Nilikagua jalada la mradi na kutembelea mradi mnamo tarehe 30 Septemba 2024, na kubaini ukosefu wa mifereji ya pembeni katika miradi ya barabara iliyokamilika, jambo linaloleta hatari ya mmomonyoko wa udongo na uharibifu wakati wa mvua kubwa. Kukosekana kwa mifereji hii kunatokana na upungufu wa bajeti, na hivyo kuweka hatari juu ya uimara na thamani ya fedha ya mradi. |
| Singida-H/W Manyoni | Mkataba Na. S10/023/2023/2024/W/95 kwa ajili ya Ujenzi wa Daraja la Nkonjigwe kwa kutumia mawe (Stone Masonry Arch Bridge) katika Ch. 5+060 kwenye Barabara ya Chibumagwa-Sasajila-Makasuku Itetema na Matengenezo ya Kawaida kwa Barabara ya Kintinku-Makanda (km 31) katika Wilaya ya Manyoni chini ya Mfuko wa Barabara. Mkataba ulisainiwa tarehe 17 Aprili 2024 (kufikia tarehe 18 Aprili 2024 hadi 30 Agosti 2024, iliyorekebishwa hadi tarehe 11 Oktoba 2024). | 624,781,200.00 | Kazi za Zilizoongezeka Kutokana na Utafiti pamoja na Usanifu Usioridhisha<br><br>Ukaguzi wa jalada za mikataba kwa miradi iliyoanzishwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2024, ulibaini mapungufu katika hatua za utafiti na usanifu, yaliyosababisha mabadiliko ya gharama ya Sh. 216,174,400 kwa mkataba uliotekelezwa. Ujenzi wa Daraja la mawe la Nkonjigwe na matengenezo ya kawaida ya barabara ya Kintinku-Makanda katika Wilaya ya Manyoni ilikuwa na ongezeko la gharama kutoka Sh. 408,606,800 hadi Sh. 624,781,200 kutokana na utofauti katika kati ya Orodha ya Kiasi cha Kazi (BOQs) na michoro kutokana na vipengele ambavyo havikujumuishwa katika BOQs. |
| H/W Singida | Mkataba Na. S10/023/2023/2024/W/67 kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara ya Mji wa Ilongero kwa viwango lami, Ujenzi wa Kalvati kwa mawe (Stone Masonry Box Culverts) kwenye barabara ya Mipilo-Mumbii-Mangida na Kazi za Matengenezo ya Kawaida kwenye Barabara ya Itaja-Mumbii katika | 950,000,000.00 | Kazi za Zilizoongezeka Kutokana na Utafiti pamoja na Usanifu Usioridhisha<br><br>Ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2024 ulionesha kwamba utafiti na usanifu duni ulisababisha mabadiliko ya gharama ya Sh. 63,299,395, hasa kutokana na vipengele visivyohesabiwa kama vile, maeneo yaliyojaa mafuriko na mabadiliko ya mto yaliyosababishwa na mvua kubwa. Utofauti huu unaonesha upungufu wa umakini katika hatua za utafiti na usanifu, na kusababisha |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | Wilaya ya Singida chini ya ufadhili wa Tozo. | | makosa katika makadirio ya kiasi na hatari ya migogoro ya kimkataba, miundombinu isiyo na ubora, na mahitaji makubwa ya matengenezo. |
| H/W Njombe | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/22 kwa ajili ya Kuboresha Barabara ya Itipingi-Kichiwa (Km 8), Barabara ya Kidegembye-Msima (Km 4.5) na Barabara ya Msima-Matiganjola (Km 5.6) hadi kiwango cha changarawe katika Wilaya ya Njombe kwa bei ya mkataba ya Sh. 527,474,702. Mradi ulipangwa kutekelezwa kwa kipindi cha siku 180, kuanzia tarehe 14 Septemba 2023 hadi 23 Machi 2024 chini ya ufadhili wa Tozo. | 527,474,702.00 | Nilitembelea miradi mnamo tarehe 4 Oktoba 2024 na kubaini mapungufu kadhaa: (a) Kalvati ya matundu 12 ilijengwa na kuwekewa muinuko, jambo linaloweza kupelekea mmomonyoko wa udongo; (b) Nyufa zilionekana kwenye kizingiti cha Kalvati sehemu ya kuingizia maji kwenye Chainage 4+300, ambayo yanaweza kuwa ni matokeo ya kutitia kwa ardhi au mchanganyiko hafifu wa saruji; (c) Kifusi hakikurejeshwa kikamilifu kwenye karavati kwenye Chainages 0+770 na 0+950, na hii inahatarisha uthabiti na kuweza kusababisha mmomonyoko wakati wa mvua kubwa. |
| Njombe-H/W Makete | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/37 kwa ajili ya Ujenzi wa Kalvati kwenye barabara ya Utanziwa-Imehe kwa bei ya mkataba ya Sh. 53,704,000 chini ya ufadhili wa Matengenezo ya Mfuko wa Barabara. | 53,704,000.00 | Nilitembelea miradi mnamo tarehe 4 Oktoba 2024 na kubaini mapungufu kadhaa: (a) Michoro ya "Box Culvert" haikuwa na mifumo ya mifereji ya kudhibiti mtiririko wa maji, na hivyo kuhatarisha mmomonyoko na uharibifu wa miundombinu wakati wa mvua kubwa; (b) Kingo (Guardrail) yenye thamani ya Sh. 6,500,000, iliyolipwa kwa mujibu wa Cheti cha Malipo (IPC) 1, haikuwa imewekwa; (c) Eneo la mradi halikuwa na nyenzo za usalama kama vile alama za tahadhari au vizuizi kwa watembea kwa miguu na magari; na (d) Kifusi hakikuwa kimerejeshwa kwa ukamilifu kuzunguka karavati na hivyo kuhatarisha uthabiti na kuweka uwezekano wa mmomonyoko wa udongo. Matatizo haya yanaashiria mapungufu makubwa katika michoro, kuzingatia usalama, na utekelezaji wa ujenzi kulingana na miongozo. |
| H/W Njombe | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/24 kwa ajili ya Kuboresha Barabara ya Ikuna-Ikondo km 14.286 hadi kiwango cha changarawe chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF). | 362,758,600.00 | Katika kazi ya kuboresha Km 14.28 za barabara ya Ikuna-Ikondo kwenda kiwango cha changarawe nilibaini kutokamilika kwa mitaro ya kukusanya maji ambayo pia ilijaa uchafu, kutoshindiliwa vizuri kwa charabara katika Chainage 1+600 na 2+000 na kusababisha vumbi jingi na mitaro ya kuchepusha maji kufunga. Mapungufu haya yanaonesha upungufu katika mbinu za ujenzi na matengenezo duni. |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| H/Mji Njombe | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/07 kwa ajili ya Ukarabati Mkubwa wa Daraja kwenye Barabara ya Kifanya - Mkondoo wenye thamani ya Sh. 84,999,956 chini ya Mfuko wa Matengenezo ya Barabara. | 84,999,956.00 | Ukarabati mkubwa wa daraja la barabara ya Kifanya-Mkondoo, lenye thamani ya Sh. 84,999,956, ulibainika kuwa na dosari, ikiwa ni pamoja na uwepo wa nyufa kwenye sakafu ya daraja na kutokamilishwa kwa kifusi. Hii inaashiria ubora usioridhisha wa ujenzi, na inahatarisha uimara na usalama wa daraja hilo. |
| H/Mji Njombe | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/10 kwa ajili ya Ukarabati Mkubwa wa Daraja kwenye Barabara ya Lwangu - Iwungilo wenye thamani ya Sh. 89,998,700 chini ya Mfuko wa Matengenezo ya Barabara. | 89,998,700.00 | Ukarabati mkubwa wa daraja la barabara ya Lwangu-Iwungilo, lenye thamani ya Sh. 89,998,700, ulibainika kuwa na dosari kutokana kutokamilishwa kwa kifusi, jambo linalohatarisha ubora wa ujenzi na uimara wa daraja. |
| H/Mji Njombe | Mkataba Na. S10/017/2023/2024/W/14 kwa ajili ya Ukarabati Mkubwa wa Daraja kwenye Barabara za Utalingolo-Igagala na DR. Rwanda wenye thamani ya Sh. 181,162,000 chini ya ufadhili wa Tozo. | 181,162,000.00 | Ukarabati mkubwa wa barabara za Utalingolo-Igagala na Dr. Rwanda ulibainika kuwa na dosari za ujenzi, ikiwa ni pamoja na mmomonyoko wa ardhi kutokana kutoshindiliwa vizuri na kutekeleza mradi kinyume na usanifu, ambapo sehemu ya sakafu ya daraja haikushikanishwa na kuta za mashavu ya daraja na kuacha pengo la cm 30. Hii inaonesha kutofuata viwango vya ujenzi na matakwa ya usanifu. |
| H/M Mtwara | Mkataba Na. AE/092/2022-2023/MT/W/56 kwa ajili ya Uboreshaji wa Barabara ya Shangani Estate (km 1) chini ya ufadhili wa Tozo. | 474,830,600 | Mapungufu kwenye Usanifu Yaliyopelekea Mabadiliko ya Kazi za Sh. 30,000,000<br><br>Mapitio ya mikataba yalionesha kuwa Wakala alijumuisha vipengele vyenye thamani ya Sh. 30,000,000 kwenye BOQs kwa ajili ya Kuboresha Barabara ya Shangani Estate (1km) ambavyo havikuwepo awali kwenye hatua za utafiti na usanifu. Tofauti hii, inayohusisha kazi kama vile kuboresha tabaka la chini, kugandisha udongo kwa kutumia sementi, na kusawazisha, inaonesha upungufu katika usanifu. Kuingizwa kwa vipengele hivi baada ya utafiti kunaleta wasiwasi kuhusu umakini wa mipango ya Wakala na usahihi wa gharama ya mkataba. |
| Mtwara-H/W Nanyamba | Mkataba Na. S10/015/2023/2024/W/37 kwa ajili ya Uboreshaji wa Barabara ya Nyundo - Narunga - Ziwani - Njengwa (km 1) hadi kiwango cha lami (Double Surface | 474,912,000 | Mapungufu kwenye Usanifu Yaliyopelekea Mabadiliko ya Kazi za Sh. 44,030,000<br><br>Mapitio ya mkataba wa kuboresha Barabara ya Nyundo-Narunga-Ziwani-Njengwa yalionesha kutokuwekwa kwa |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | Dressing) chini ya ufadhili wa mfuko wa jimbo. | | kazi na pia kuongezwa kwa kazi zenye thamani ya Sh. 44,030,000, ikiwa ni ishara ya mapungufu katika michakato ya utafiti na usanifu. Kurekebisha kazi wakati wa utekelezaji kunaonesha kutokuwa na umakini wa kutosha, jambo linaloweza kuathiri ubora na uthabiti wa miundombinu. Inapendekezwa kufanya tafiti kamili na usanifu sahihi ili kuhakikisha mahitaji ya mradi yanafanana. Pia kuwepo na bajeti kwa kazi zilizokosekana ambazo ni muhimu kwa uthabiti wa barabara hiyo. |
| Geita-H/W Geita, H/Mji Geita na H/W Chato | Mkataba Na. S10/004/2023/2024/W/115 wenye thamani ya Sh. 200,000,000 kwa ajili ya Uboreshaji wa Barabara ya Lekatugeme - Mkoani (km 1.25) hadi kiwango cha lami (Double Surface Dressing) katika Geita TC chini ya fedha za dharura. Mkataba Na. S10/004/2023/2024/W/27 wenye thamani ya Sh. 453,999,930.00 kwa ajili ya Uboreshaji wa Barabara ya CCM - Sheli ya Nassoro (km 0.25) hadi kiwango cha lami (Double Surface Dressing) na uboreshaji hadi kiwango cha changarawe (km 12.0), pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji (Culverts 10) katika Barabara ya Nyamasenga - Luhuha - Kizira, Geita DC chini ya ufadhili wa Tozo. Mkataba Na. S10/004/2023/2024/W/63 wenye thamani ya Sh. 470,607,354.72 kwa ajili ya Uboreshaji wa Barabara ya Kituo cha Mabasi cha Kahumo (km 1.0) hadi kiwango cha lami (Double Surface Dressing) katika Wilaya ya Chato chini ya ufadhili wa Tozo. | 1,124,607,285 | Kutokuwepo kwa Michoro ya Taa za Barabarani<br><br>Mapitio ya mikataba yalionesha kwamba miradi ya barabara ilijumuisha ufungaji wa taa za barabarani za jua, lakini hakukuwa na michoro ya kiufundi inayohitajika, jambo linalokiuka viwango vya usanifu. Thamani ya taa za barabarani ilikuwa Sh. 189,000,000 kwa Mkataba S10/004/2023/2024/W/115, Sh. 36,000,000 kwa Mkataba S10/004/2023/2024/W/27, na Sh. 175,000,000 kwa Mkataba S10/004/2023/2024/W/63. Kukosekana kwa michoro hii kunaweza kupelekea changamoto ya mkandarasi kuelewa nini cha kufanya, makossa katika utekelezaji na ucheleweshaji wa kazi. TARURA inashauriwa kuweka mikakati ya udhibiti wa ubora ili kuhakikisha kuwa vipengele vyote muhimu, ikiwemo michoro, vinajumuishwa katika mikataba kabla ya kusaini. |
| Kagera-H/M Bukoba | Mkataba Na. S10/006/2023/2024/W/64 kwa ajili ya Ujenzi wa matengenezo ya sehemu zenye uharibifu (patchworks) katika | 199,032,500.00 | Kukosekana kwa Mpango wa Kuondoa Mashimo ya Barabarani<br><br>Ukaguzi wa Mkataba No. S10/006/2023/2024/W/64 kwa ajili ya matengenezo ya mashimo kwenye |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | barabara za Manispaa ya Bukoba wenye thamani ya Sh. 199,032,500 chini ya Mfuko wa Matengenezo ya Barabara (Roads Fund Maintenance). | | barabara za Manispaa ya Bukoba (Sh. 199,032,500) ulionesha kutotekelezwa kwa Kanuni za Barabara na Kodi za Mafuta za 2016 kutokana na kukosekana kwa mpango wa kuziba mashimo ya barabarani, ambayo inapaswa kuelezea idadi, ukubwa, na maeneo ya mashimo. Kukosekana kwa nyaraka hii kunakwamisha ufuatiliaji, kuongeza hatari ya kazi zisizothibitishwa, na mapungufu katika mipango. Inashauriwa kuwa mikataba ijayo ijumuishe mpango wa kuondoa mashimo ya barabarani ili kuhakikisha mipango, utekelezaji, na ufuatiliaji sahihi. |
| Tabora-H/W Uyui | TARURA ilitekeleza mkataba Na. S10/022/2023/2024/W/31 wenye thamani ya Sh. 964,747,910 kwa ajili ya uboreshaji na ujenzi wa makaravati ya mviringo na ya sanduku katika barabara mbalimbali za Wilaya ya Uyui chini ya fedha za tozo ya mafuta. Mkataba ulisainiwa tarehe 7 Septemba 2023, na awali ulikuwa ukamilike tarehe 6 Machi 2024 lakini uliongezwa hadi tarehe 13 Juni 2024. | | Kukosekana kwa Nguzo za Ulinzi kwa Maeneo ya Mwinuko wa Changarawe<br><br>Nilitembelea mradi mnamo tarehe 3 Novemba 2024, na kubaini dosari katika ujenzi wa makaravati kwenye miradi ya barabara. Hususan, nguzo za ulinzi zilizopakwa rangi hazikuwekwa kwenye maeneo ya mwinuko wa takriban mita 1.5, kinyume na Kifungu 9.7.1 cha Mwongozo wa Ubunifu wa Jiometri ya Barabara wa 2011, ambacho kinataka kuwepo kwa vizuizi vya usalama ili kulinda watumiaji wa barabara. Aidha, kiwango cha mwisho cha changarawe kilizidi urefu wa ukuta wa mbele wa makaravati, na kuyafanya yasionekane barabarani, hususan katika Barabara ya Igalula-Kawekapima. Kukosekana kwa nguzo za ulinzi kulitokana na kutozingatia kikamilifu usalama wa barabara wakati wa usanifu na utekelezaji wa mradi. Dosari hii inaongeza hatari ya ajali na kuhatarisha uimara wa miundombinu. Uongozi wa TARURA unashauriwa kutilia mkazo usalama wa barabara na kuhakikisha uendelevu wa kazi zinazotekelezwa. |
| | | 964,747,910 | Uwepo wa ufa kwenye Shavu la Kalavati<br><br>Ilibainika kuwa kuna ufa wa upana wa mm 5 hadi 7 kwenye shavu la kulia (RHS wingwall) la karavati katika Barabara ya Mwakashanhala. Tatizo hili limetokana na tofauti ya mshikamano wa udongo (differential settlement) na matibabu duni ya udongo wa juu (topsoil treatment).<br><br>Nyufa hizi zinahatarisha uthabiti wa mwinuko wa barabara na uimara wa karavati. Uongozi wa TARURA |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | unashauriwa kufanya matengenezo ya kutosha ili kulinda makaravati na kuhakikisha yanafikia muda wake wa matumizi kama ilivyokusudiwa kwenye usanifu. |
| | | | Ujenzi Duni wa Sakafu ya Kuingilia na Kutokea kwa Makaravati<br><br>Ukaguzi ulibaini mmomonyoko wa udongo chini ya sakafu za makaravati katika barabara za Usagali-Milamboitobo na Mwakashanhala kutokana na ukosefu wa "anchor beam", kinyume na matakwa ya Low Volume Road Manual (2016). Tatizo hili lilitokana na usanifu duni na mapitio ya usanifu yasiyoridhisha, hali inayohatarisha uthabiti wa makaravati. Uongozi wa TARURA unashauriwa kuhakikisha miradi ya ujenzi inazingatia viwango na taratibu zilizowekwa ili kudumisha uimara na ufanisi wa miundombinu. |
| H/Jiji Mwanza | Mnamo tarehe 26 Oktoba 2023, TARURA ilisaini mkataba wa maboresho ya sehemu korofi katika barabara za Luchelele (km 0.50), Bismark (km 0.50), Mwananchi Mahinakati (km 0.20), na Buhongwa-Bulale-Mwasonge (km 0.30) hadi kiwango cha lami katika Jiji la Mwanza. Mkataba huu, wenye thamani ya Sh. 1,050,000,000 chini ya Mfuko wa Matengenezo ya Barabara, ulianza kutekelezwa tarehe 15 Novemba 2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 13 Aprili 2024. | 1,050,000,000 | Kasoro Zilizobainika kwenye Barabara za Buhongwa-Bulale-Mwasonge (0.30 Km) na Luchelele (0.50 Km)<br><br>Ukaguzi wa tarehe 26 Oktoba 2024 ulibaini kasoro zifuatazo: Nyufa kwenye mifereji ya maji katika Chainage 0+95 na 0+100, Ubavu wa barabara ulioharibika katika Chainage 0+290 kwenye barabara ya Buhongwa-Bulale-Mwasonge (0.30 km), Ujenzi duni wa mifereji ya maji katika Chainage 0+100 kwenye barabara ya Luchelele (0.50 km). Kasoro hizi zilisababishwa na tabaka la barabara kutoshindiliwa vizuri na kazi isiyo na ubora. TARURA inashauriwa kurekebisha matatizo haya kwa kuhakikisha barabara inashindiliwa vyakutosha na uboreshaji wa kazi yote kabla ya makabidhiano ya mradi. |
| Wilaya ya Ilala na Wilaya ya Kigamboni | Mnamo tarehe 14 Agosti 2022, TARURA ilisaini mkataba AE/0/92/2022/2023/HQ/W/08 wa kuboresha barabara ya Chanika-Homboza (km 4.54) hadi kiwango cha lami chini ya fedha za tozo katika Wilaya ya Ilala. Mradi ulianza tarehe 21 Septemba 2022, huku tarehe ya awali ya kukamilika ikiwa 20 Julai 2023, kwa gharama ya Sh. | 8,077,961,411.05 | Kufutika Mapema kwa Michoro ya Barabarani<br><br>Ukaguzi ulibaini kufutika mapema kwa michoro ya barabarani katika Chainage 0+1100-1200 kwenye barabara ya Tungi-Mjimwema (1.2 km), Wilaya ya Kigamboni, Chainage 0+000 kwenye barabara ya Chanika-Homboza (4.54 km), Wilaya ya Ilala. Tatizo hili lilisababishwa na msongamano mkubwa wa magari katika maeneo ya karibu yenye barabara za changarawe/mchanga na ukosefu wa vipimo vya ubora wa alama hizo. |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | 6,652,982,931. Vilevile, mnamo tarehe 2 Oktoba 2023, TARURA ilisaini mkataba S10/002/2023/2024/W/11 wa kuboresha barabara ya Tungi-Mjimwema (km 1.27) hadi kiwango cha lami (Awamu ya VII) chini ya fedha za tozo katika Wilaya ya Kigamboni. Mradi ulianza tarehe 9 Oktoba 2023 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 6 Aprili 2024, kwa gharama ya Sh. 1,424,978,480.05. | | Kudhoofika huku husababisha gharama zisizopangwa za matengenezo. TARURA inashauriwa kuhakikisha upimaji wa ubora wa alama za barabarani unafanyika kabla ya uwekaji ili kuongeza umadhubuti wake.<br><br>Mapungufu Kwenye Kujenga Mifereji ya Maji<br><br>Ukaguzi uliofanyika tarehe 11 Oktoba 2024 ulibaini kasoro katika ujenzi wa mifereji ya maji kwenye barabara ya Tungi-Mjimwema (1.2 km) katika Chainage 0+360 (RHD na RHS), Kigamboni na barabara ya Tukuyu (0.62 km) katika Chainage 0+620, Ilala. Kasoro hizi, hasa katika usanifu wa wa mteremko, zimeathiri mtiririko wa maji na kusababisha maji kutuama kwenye mifereji. TARURA inashauriwa kurekebisha miundombinu hii ili kuhakikisha mifereji inafanya kazi ipasavyo na kuepuka uharibifu wa barabara.<br><br>Uwepo wa Nyufa Barabarani<br><br>Ukaguzi wa tarehe 12 Oktoba 2024 ulibaini nyufa na kasoro katika Chainage 0+620 LHD na 0+600 LHD kwenye Barabara ya Chanika-Homboza (4.54 km), Wilaya ya Ilala. Tatizo hili lilisababishwa na kushindwa kushughulikia kiwango cha maji chini ya ardhi wakati wa ujenzi, hali inayoweza kupunguza uimara wa barabara. TARURA inashauriwa kurekebisha kasoro hizi kabla ya kukamilisha mradi. |
| Manayara-H/W Kiteto | Mnamo tarehe 25 Agosti 2024, TARURA Manyara iliingia mkataba wa uboreshaji wa barabara katika Wilaya ya Kiteto, ukiwemo ukarabati wa sehemu korofi, matengenezo ya kawaida, na ujenzi wa miundombinu kwenye barabara mbalimbali chini ya mkataba Na. S10/011/2023/2024/W/10, wenye thamani ya Sh. 294,590,000 na kufadhiliwa na mfuko wa matengenezo ya barabara (RF Maintenance). | 294,590,000 | Uharibifu na Kuziba kwa Mifereji ya Maji<br><br>Ukaguzi wa tarehe 7 Oktoba 2024 katika Wilaya ya Kiteto ulibaini mifereji ya maji iliyoharibika na kuzibwa na mabaki ya mazao kutokana na matengenezo duni na ukosefu wa usimamizi. Hali hii inaweza kusababisha mmomonyoko wa udongo, mafuriko, na gharama kubwa za matengenezo. TARURA inashauriwa kurekebisha uharibifu huo, kuondoa taka zilizoziba mifereji, na kuelimisha jamii kuhusu utupaji sahihi wa taka. |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| Manayara-H/W Kiteto | Mnamo tarehe 2 Aprili 2024, TARURA Manyara iliingia mkataba wa ujenzi wa makaravati mawili kwenye barabara za Orkine-Songambele na Engusero-Orkine katika Wilaya ya Kiteto chini ya mkataba Na. S10/011/2023/2024/W/02, wenye thamani ya Sh. 356,146,200 na kufadhiliwa na Tozo ya Mafuta. Mradi ulianza tarehe 9 Aprili 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Aprili 2024. | 356,146,200 | Ukosefu wa Ulinzi kwenye Mashavu ya Maravati<br><br>Ukaguzi wa tarehe 7 Oktoba 2024 ulibaini kuwa mashavu ya makaravati ya 2-cell na 4-cell hayajalindwa ipasavyo, jambo linaloongeza hatari ya mmomonyoko wa udongo wakati wa mvua kubwa na kuhatarisha uimara wa miundombinu hiyo. Hali hii imetokana na mbinu duni za ujenzi na usimamizi hafifu. TARURA inashauriwa kuchukua hatua za haraka kwa kuhakikisha ujazaji udongo sahihi, ushindiliaji mzuri, na utekelezaji wa hatua za kudhibiti mmomonyoko wa udongo. Aidha, TARURA inapaswa kuzingatia vipimo vya usanifu na kuboresha usimamizi wa miradi ili kuepusha matatizo kama haya siku zijazo. |
| Manayara-H/W Kiteto | Mnamo tarehe 3 Aprili 2024, TARURA Manyara iliingia mkataba wa matengenezo ya barabara na maboresho ya maeneo korofi katika mji wa Kibaya na barabara za jirani. Mkataba huo, Na. S10/011/2023/2024/W/11, wenye thamani ya Sh. 221,450,200, ulipangwa kutekelezwa kuanzia tarehe 11 Machi hadi 15 Julai 2024, ukiwa umefadhiliwa na Mfuko wa Matengenezo ya Barabara (RF Maintenance). | 221,450,200 | Ukaguzi wa tarehe 7 Oktoba 2024 ulibaini kuongezwa kwa siku 90 za mradi bila uthibitisho wa kutosha kutokana na mvua za El Niño, huku kazi za mifereji ya maji zikiwa hazijakamilika. Aidha, udongo uliochimbwa haukuondolewa ipasavyo, kinyume na viwango vilivyowekwa. Changamoto hizi zilitokana na usimamizi hafifu. TARURA inashauriwa kuthibitisha uhalali wa nyongeza za muda, kuhakikisha kazi zinakamilika kwa wakati, na kutekeleza uondoaji sahihi wa udongo uliochimbwa ili kukidhi viwango vya ujenzi. |
| Pwani-H/W Mkuranga | Katika mwaka wa fedha 2023/24, TARURA Mkoa wa Pwani ilisaini mkataba Na. S10/018/2023/2024/W/88 kwa ajili ya ukarabati wa barabara za Mwanambaya-Mipeko (3 km), Mwanambaya-Korogwe (2.5 km), Vikindu Police Station-TSN Petrol Station (2.5 km), na ujenzi wa Kalvati (box culverts) kwenye barabara za Vikindu Police Station-TSN Petrol Station na Mlamleni-Kisasa katika Wilaya ya Mkuranga. Mkataba huu ulianza na thamani ya Sh. | 474,998,894.32 | Uwepo wa Makorongo ya Momonyoko katika Karavati Culvert la Chainage 2+900 kwenye Barabara ya Mlamleni-Kisasa<br><br>Kulingana na Kanuni za 2211(a) za Vipimo vya Kazi za Barabara (2000), udongo wa kujaza kwenye makaravatiunapaswa kukidhi viwango vya ubora wa tabaka kuepuka mmomonyoko na kuhakikisha uthabiti. Nilitembelea mradi mnamo tarehe 29 Novemba 2024 na kubaini makorongo ya mmomonyoko wa ardhi kwenye karavati lililopo kwenye Chainage 2+900 katika barabara ya Mlamleni-Kisasa. Kifusi kilichotumika kama inavyohitajika kwenye (Kifungu na. 2.3.1 cha BOQ), hakikukidhi viwango vya ubora na vilivyokusudiwa. Aidha, mashimo yalionekana katika matoleo ya |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | 457,743,000, lakini ulirekebishwa hadi Sh. 474,998,894.32 chini ya Fedha za Maendeleo ya Jimbo. Mradi ulianza tarehe 8 Septemba 2023 na kumalizika tarehe 10 Juni 2024. | | karavati, hali inayoweza kusababisha uharibifu zaidi wa miundombinu.<br><br>Vikwazo vya bajeti vilizuia matumizi ya changarawe inayofaa kutoka kwa Shimo la Kigamboni. Masuala haya yanahatarisha uthabiti wa culvert, kuongeza gharama za matengenezo, na kutishia upitikaji wa barabara. TARURA inashauriwa kushughulikia masuala haya kwa kutumia kifusi chenye ubora kwa ajili ya kujaza na kutekeleza hatua za kudhibiti mmomonuoko. |
| | | | Upungufu wa Mitaro kwenye Chainage 1+500km katika Barabara ya Mwanambaya-Mipeko<br><br>Sehemu ya 5.7 ya Mwongozo wa Usanifu wa Jiometri ya Barabara, 2011, inasisitiza umuhimu wa mifumo ya mifereji katika utendaji wa barabara, ambapo kushindwa kwa mifereji mara nyingi husababisha matatizo ya miundombinu. Nilipotembelea mradi tarehe 29 Novemba 2024, nilibaini kuwa sehemu za Chainage 1+500 km kwenye Barabara ya Mwanambaya-Mipeko zilikuwa na upungufu wa mitaro, kinyume na Kifungu na. 8.16.1 cha BOQ, ambayo inataka mitaro ya zege yenye "BRC mesh". Hii ilisababisha mmomonyoko wa udongo na tabaka la barabara kuondolewa kutokana na maji kutiririka barabarani bila kudhibitiwa, hivyo kuongeza hatari ya uharibifu wa barabara mapema na gharama za matengenezo za juu. Ninapendekeza kwa Menejimenti ya TARURA kupanga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa mitaro kwenye sehemu zenye uhitaji. |
| H/W Tabora | Mkataba Na. S10/025/2023/2024/W/112 kwa ajili ya matengeneo ya sehemu korofi na Ujenzi wa karavati kubwa 2(Box Culverts), Kingo za barabara na Ujenzi wa karavati za kawaida 2 kwenye barabara ya Kakola Mwibiti katika Wilaya ya Tabora (Kazi za Dharura). | 198,476,625 | Kifusi hakikurejeshwa vyema kwenye Makaravati, jambo linaloweza kusababisha kutuama kwa maji wakati wa mvua na hivyo kufupisha muda wa uimara wa makaravati. Ingawa kifusi cha G25 kilitumika kwa kazi za barabara ukosefu wa nyasi kwenye kuta za pembeni kunahatarisha uharibifu wa miundombinu kwenye kipindi cha mvua. |
| H/W Iringa | Mkataba Na. S10/005/2022/2023/W/123 : Ujenzi wa Daraja la mawe (Stone Masonry Arch Bridge) kwenye barabara ya | 119,860,000.00 | Maji hayapitii kutoka kwenye daraja kwa sababu mifereji ya maji kwenye pande za madaraja ipo juu zaidi ya kiwango cha maji. Inashauriwa kwa TARURA kuboresha usimamizi na kuhakikisha |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | Kigonzile-Nduli chini ya Fedha za Dharura za Mfuko wa Barabara. | | kumalizika kwa kazi kwa wakati, huku ikitilia mkazo marekebisho ya makosa haya ili kuhakikisha mifereji inafanya kazi kama ilivyokusudiwa. |
| H/Jiji Dodoma | Katika mwaka wa fedha 2022/23 na 2023/24, TARURA ilitekeleza Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/18 na Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/20 kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara ya kuingia eneo la viwanda Nala (km 5.115) hadi kiwango cha lami katika Jiji la Dodoma kwa awamu ya I na II, kwa jumla ya gharama ya Sh. 4,660,127,060.95 na Sh. 3,798,323,055.75 mtawalia. | 8,458,450,116.70 | Mapungufu kwenye Ujenzi wa Barabara Inayoingia Barabara Kuu "Access Road"<br><br>Ukaguzi wa mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/18&20 ilionesha mapungufu kadhaa katika ujenzi wa barabara, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa kinga (guardrails) kwenye mifereji (chainage 0+000, 3+700, 4+500), ukosefu wa "headwalls" kwenye makaravati, na mto kutokuchongewa vizuri kudhibiti uelekeo wa maji. Haya yalisababisha kutuama kwa uchafu katika chainage 0+000. Pia, Nilibaini mifereji kwenye chainage 2+900 haikuwa ikipitisha maji vizuri na kifusi kwenye chainage 0+720 hadi 0+780 hakikujazwa vyema. Hii inapunguza uimara wa mifereji husika. Aidha, njia za watembea kwa miguu kuanzia chainage 3+660 hadi 4+415 hazikuwa zimekamilika, na pia kulikuwa na jiwe lililozuial maji katika mfereji kwenye chainage 4+595.<br><br>Mapungufu haya yalitokana na usimamizi hafifu, kushindwa kuzingatia viwango vya usanifu, na ukosefu wa ukaguzi wa kazi wa kina. Athari ni pamoja na hatari za usalama, mifereji isiyo na ufanisi, uharibifu wa barabara, na upungufu wa ufanisi wa barabara. TARURA inashauriwa weka "guardrails", kujenga "headwalls", kuboresha mifereji, kujaza vyema kifusi, kukamilisha ujenzi wa njia za watembea kwa miguu, na kuondoa vikwazo ili kuboresha usalama na kudumu kwa barabara. |
| Mkoa wa Kigoma | Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/10 kwa ajili ya uboreshaji wa barabara ya Kasulu - Kabanga - Kasumo - Muyama (km 12.50) Awamu ya I hadi kiwango cha lani, kwa gharama ya Sh. 16,786,784,795 (Tozo). | 16,786,784,795 | Ukaguzi wa Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/10 wa Uboreshaji wa Barabara ya Kasulu-Kabanga-Kasumo-Muyama kwenda kiwango cha lami ulibaini mabadiliko yasiyothibitishwa ya gharama kiasi cha Sh. 290,912,280 katika kipengele 36.01(a) (uchimbaji wa kawaida wa udongo). Kiasi kiliongezeka kutoka 26,629.11 $m^3$ hadi 75,114.49 $m^3$ kwa bei ya Sh. 6,000 kwa kila mita za ujazo, kilichoonyeshwa kwenye Hati ya Malipo (IPC) 3, bila ushahidi wa kuthibitisha mabadiliko hayo. Hii inatilia shaka |

| Mkoa/Halmashauri | Taarifa za Mradi | Thamani ya Mkataba (Sh.) | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|---|
| | | | uwezekano wa manufaa binafsi kwa msimamizi wa mradi na mhandisi wa TARURA. TARURA inashauriwa kudai kurudishwa kwa kiasi hicho cha fedha kilichokosa uthibitisho na kuimarisha michakato ya uthibitishaji kwa mabadiliko kwenye miradi ya baadaye ili kuhakikisha uwajibikaji na thamani ya fedha. |
| Mkoa wa Songwe | Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/03 wenye thamani ya Sh. 5,752,956,420 (Tozo) kwa uboreshaji wa barabara ya Landani - Kiwira (km 5) ikiwa ni pamoja na barabara ya Mwalisi (km 40) Awamu ya I hadi kiwango cha lami. | 5,752,956,420.00 | Ukaguzi wa Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/03 wa Uboreshaji wa Barabara ya Landani-Kiwira ulibaini ongezeko lisiloidhinishwa la gharama ya mkataba cha Sh. 185,530,422 bila idhini ya Bodi ya Zabuni, kinyume na Kanuni ya 110(5) ya Sheria ya Ununuzi ya Umma (PPR), 2013. Agizo la Mabadiliko Na. 1 lilifikia kiasi cha awali cha mkataba lakini lilikondoa fedha kwa ajili ya dharula bila kutoa sababu ya msingi, jambo lililosababisha ongezeko la gharama ya mkataba. Upungufu huu unadhoofisha udhibiti wa bajeti, unasababisha kukiukwa kwa kanuni za ununuzi, na kudhoofisha ufanisi katika usimamizi wa kifedha. TARURA inashauriwa kuzingatia kwa ukamilifu kanuni za ununuzi na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani kwa usimamizi wa mkataba na idhini za mabadiliko ya kazi.<br><br>Pia, Ukaguzi wa Agizo la Mabadiliko Na. 1 kwa Mkataba Na. AE/092/2022/2023/HQ/W/03 ulibaini upungufu wa nyaraka za kuthibitisha ongezeko la Sh. 1,265,962,150 na punguzo la Sh. 1,103,526,250, jambo lililoibua mashaka kuhusu usahihi na uaminifu wa mabadiliko hayo. Ukosefu wa ushahidi wa kutosha unaashiria usimamizi usioridhisha wa fedha, hivyo kudhoofisha uaminifu wa kifedha wa mradi. TARURA inashauriwa kuhakikisha mabadiliko haya yanahakikiwa na kuthibitishwa. Pia TARURA iimarishe michakato ya kukagua mabadiliko ya mikataba ili kuhakikisha uwepo wa nyaraka sahihi na uwajibikaji. |
| **Jumla** | | **91,812,945,497.41** | |

## Kiambatisho Na.38:Hasara kutokana na madai yasiyolipwa na Bima ya Afya NHIF

| Na. | Halmashauri | Kiasi cha madai ombwa (Sh.) | Madai lipwa (Sh.) | Madai kataliwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Chamwino | 434,272,627 | 292,805,501 | 141,467,126 |
| 2 | H/W Bagamoyo | 419,827,572 | 314,423,285 | 105,404,287 |

| Na. | Halmashauri | Kiasi cha madai ombwa (Sh.) | Madai lipwa (Sh.) | Madai kataliwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 3 | H/M Shinyanga | 366,985,177 | 269,452,695 | 97,532,482 |
| 4 | H/ Jiji Arusha | 556,326,036 | 476,555,393 | 79,770,643 |
| 5 | H/W Mkinga | 94,351,302 | 17,353,321 | 76,997,981 |
| 6 | H/ Jiji Dar es Salaam | 574,085,494 | 506,633,590 | 67,451,904 |
| 7 | H/M Ubungo | 826,151,139 | 761,108,668 | 65,042,471 |
| 8 | H/M Kahama | 620,447,472 | 565,391,291 | 55,056,181 |
| 9 | H/W Mbogwe | 126,216,988 | 75,602,176 | 50,614,812 |
| 10 | H/W Same | 467,822,642 | 417,383,493 | 50,439,149 |
| 11 | H/M Musoma | 376,603,759 | 332,950,133 | 43,653,626 |
| 12 | H/W Kongwa | 251,481,103 | 209,516,426 | 41,964,677 |
| 13 | H/W Iramba | 223,626,845 | 181,742,402 | 41,884,443 |
| 14 | H/W Busega | 198,382,079 | 158,729,415 | 39,652,664 |
| 15 | H/Jiji Dodoma | 254,702,998 | 219,708,761 | 34,994,237 |
| 16 | H/M Sumbawanga | 89,606,219 | 56,313,587 | 33,292,632 |
| 17 | H/W Chemba | 116,323,562 | 84,347,361 | 31,976,201 |
| 18 | H/Mji Geita | 179,109,974 | 147,582,791 | 31,527,183 |
| 19 | H/W Igunga | 272,763,944 | 244,045,304 | 28,718,640 |
| 20 | H/W Shinyanga | 144,836,987 | 117,347,424 | 27,489,563 |
| 21 | H/W Chalinze | 178,186,565 | 151,443,619 | 26,742,946 |
| 22 | H/Mji Njombe | 179,043,630 | 155,547,534 | 23,496,096 |
| 23 | H/W Rombo | 206,286,970 | 184,291,314 | 21,995,656 |
| 24 | H/W Rufiji | 101,632,714 | 84,408,057 | 17,224,657 |
| 25 | H/W Mkalama | 107,145,065 | 90,042,717 | 17,102,348 |
| 26 | H/W Gairo | 143,947,639 | 128,741,998 | 15,205,641 |
| 27 | H/W Bumbuli | 78,107,844 | 65,233,685 | 12,874,159 |
| 28 | H/W Arusha | 112,385,700 | 99,791,597 | 12,594,103 |
| 29 | H/W Mpimbwe | 32,426,531 | 21,400,123 | 11,026,408 |
| 30 | H/W Longido | 103,667,945 | 94,969,713 | 8,698,232 |
| 31 | H/W Mlele | 81,906,043 | 73,836,450 | 8,069,593 |
| 32 | H/W Mpanda | 37,223,025 | 30,193,025 | 7,030,000 |
| 33 | H/W Maswa | 194,004,756 | 187,175,372 | 6,829,384 |
| 34 | H/W Bariadi | 57,046,496 | 50,741,521 | 6,304,975 |
| 35 | H/M Tabora | 63,921,677 | 60,127,983 | 3,793,694 |
| | **Jumla** | **8,270,856,519** | **6,926,937,725** | **1,343,918,794** |

### Kiambatisho Na.39:Upungufu wa vifaa tiba vilivyo agizwa kutoka bohari ya dawa

| Na. | Halmashauri | Vifaa lipiwa (Sh.) | Vifaa pokelewa (Sh.) | Vifaa visivyopokelewa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kilindi | 700,000,000 | 13,912,212 | 686,087,788 |
| 2 | H/Jiji Tanga | 634,673,406 | 0 | 634,673,406 |
| 3 | H/W Ushetu | 662,258,844 | 65,485,857 | 596,772,987 |
| 4 | H/W Same | 652,193,338 | 174,053,128 | 478,140,210 |
| 5 | H/Mji Handeni | 400,000,000 | 0 | 400,000,000 |
| 6 | H/W Lushoto | 633,998,836 | 279,471,147 | 354,527,689 |
| 7 | H/W Shinyanga | 368,112,965 | 25,886,499 | 342,226,466 |
| 8 | H/W Chemba | 400,000,000 | 74,715,858 | 325,284,142 |
| 9 | H/W Tabora | 1,175,000,000 | 886,121,887 | 288,878,113 |
| 10 | H/W Karatu | 280,618,182 | 0 | 280,618,182 |
| 11 | H/M Mtwara | 350,000,000 | 78,316,759 | 271,683,241 |

| Na. | Halmashauri | Vifaa lipiwa (Sh.) | Vifaa pokelewa (Sh.) | Vifaa visivyopokelewa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 12 | H/W Korogwe | 418,573,692 | 151,891,085 | 266,682,607 |
| 13 | H/W Liwale | 901,564,943 | 641,983,316 | 259,581,627 |
| 14 | H/W Mkalama | 401,667,427 | 146,071,477 | 255,595,950 |
| 15 | H/W Kiteto | 699,977,564 | 454,733,911 | 245,243,653 |
| 16 | H/W Musoma | 553,340,415 | 313,646,949 | 239,693,466 |
| 17 | H/W Pangani | 400,000,000 | 183,950,393 | 216,049,607 |
| 18 | H/W Mlele | 669,093,554 | 456,069,895 | 213,023,659 |
| 19 | H/W Bukombe | 211,401,853 | 0 | 211,401,853 |
| 20 | H/W Tandahimba | 350,000,679 | 180,937,931 | 169,062,748 |
| 21 | H/W Ulanga | 155,020,667 | 0 | 155,020,667 |
| 22 | H/W Longido | 400,000,000 | 252,131,405 | 147,868,595 |
| 23 | H/W Nanyumbu | 700,000,000 | 557,729,730 | 142,270,270 |
| 24 | H/W Kilosa | 700,000,000 | 558,255,158 | 141,744,842 |
| 25 | H/W Handeni | 299,595,768 | 210,837,969 | 88,757,799 |
| 26 | H/M Moshi | 76,716,570 | 0 | 76,716,570 |
| 27 | H/W Bahi | 400,000,000 | 334,728,437 | 65,271,563 |
| 28 | H/W Misungwi | 400,000,000 | 335,874,245 | 64,125,755 |
| 29 | H/W Mtwara | 99,790,507 | 63,544,799 | 36,245,708 |
| 30 | H/W Nachingwea | 66,230,218 | 42,139,899 | 24,090,319 |
| 31 | H/Mji Geita | 231,543,520 | 219,942,684 | 11,600,836 |
| | **Jumla** | **14,391,372,948** | **6,702,432,630** | **7,688,940,318** |

**Kiambatisho Na.40:Orodha ya Taasisi Zenye Magari, Pikipiki na Mali Nyingine Zilizoharibika**

| Na | Jina la Taasisi | Magari | Pikipiki | Mali Nyingine (Grader, Wheel Loaders, Compressor, Matrekta) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | S/M Mtwara | 9 | - | - | 9 |
| 2 | S/M Morogoro | 5 | - | - | 5 |
| 3 | S/M Shinyanga | 5 | - | - | 5 |
| 4 | S/M Kilimanjaro | 3 | - | - | 3 |
| 5 | S/M Kigoma | 6 | - | - | 6 |
| 6 | S/M Geita | 2 | - | - | 2 |
| 7 | S/M Singida | 6 | - | - | 6 |
| 8 | S/M Simiyu | 11 | - | - | 11 |
| 9 | S/M Tanga | 7 | - | - | 7 |
| 10 | S/M Njombe | 7 | - | - | 7 |
| 11 | Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) | 8 | - | - | 8 |
| | **Jumla ya Sehemu-S/M na LGTI** | **69** | **-** | **-** | **69** |
| 12 | H/W Mlimba | 12 | - | - | 12 |
| 13 | H/W Rufiji | 5 | - | - | 5 |
| 14 | H/W Maswa | 5 | - | - | 5 |
| 15 | H/W Mkuranga | 4 | - | - | 4 |
| 16 | H/W Mlele | 10 | - | - | 10 |
| 17 | H/W Moshi | 12 | 30 | - | 42 |
| 18 | H/W Msalala | 5 | - | - | 5 |
| 19 | H/W Mwanga | 13 | - | - | 13 |

| Na | Jina la Taasisi | Magari | Pikipiki | Mali Nyingine (Grader, Wheel Loaders, Compressor, Matrekta) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 20 | H/W Tandahimba | 6 | - | - | 6 |
| 21 | H/W Mtama | 1 | - | - | 1 |
| 22 | H/M Mtwara | 14 | - | - | 14 |
| 23 | H/M Musoma | 5 | - | - | 5 |
| 24 | H/W Nachingwea | 13 | - | - | 13 |
| 25 | H/W Shinyanga | 4 | - | - | 4 |
| 26 | H/W Bariadi | 5 | - | - | 5 |
| 27 | H/W Bukombe | 7 | - | - | 7 |
| 28 | H/W Busega | 8 | - | - | 8 |
| 29 | H/W Chemba | 7 | - | - | 7 |
| 30 | H/W Handeni | 11 | - | - | 11 |
| 31 | H/Manipsaa Kahama | 2 | - | - | 2 |
| 32 | H/W Kibaha | 6 | - | - | 6 |
| 33 | H/W Lindi | 5 | - | - | 5 |
| 34 | H/W Igunga | 13 | - | - | 13 |
| 35 | H/Jiji Arusha | 23 | - | 9 | 32 |
| 36 | H/W Babati | 4 | - | - | 4 |
| 37 | H/Manipsaa Babati | 6 | - | - | 6 |
| 38 | H/W Butiama | 4 | - | - | 4 |
| 39 | H/W Mpanda | 7 | - | - | 7 |
| 40 | H/W Same | 7 | 12 | - | 19 |
| 41 | H/W Itigi | 3 | - | - | 3 |
| 42 | H/W Itilima | 6 | 18 | 1 | 25 |
| 43 | H/W Kibiti | 3 | - | - | 3 |
| 44 | H/W Hanang' | 8 | - | - | 8 |
| 45 | H/W Mpwapwa | 8 | - | - | 8 |
| 46 | H/Manipsaa Mpanda | 7 | - | - | 7 |
| 47 | H/W Meatu | 18 | - | 3 | 21 |
| 48 | H/W Monduli | 5 | - | - | 5 |
| 49 | H/W Magu | 10 | - | - | 10 |
| 50 | H/Manipsaa Kondoa | 1 | - | - | 1 |
| 51 | H/W Manyoni | 1 | - | - | 1 |
| 52 | H/W Simanjiro | 10 | - | - | 10 |
| 53 | H/Manipsaa Ilemela | 10 | - | - | 10 |
| 54 | H/W Urambo | 8 | - | - | 8 |
| 55 | H/W Ukerewe | 6 | - | 1 | 7 |
| 56 | H/W Sengerema | 4 | - | 1 | 5 |
| 57 | H/W Nyang'hwale | 4 | - | - | 4 |
| 58 | H/W Sikonge | 10 | - | - | 10 |
| 59 | H/W Siha | 8 | 8 | 1 | 17 |
| 60 | H/W Kilindi | 2 | 7 | - | 9 |
| 61 | H/W Mbulu | 10 | - | - | 10 |
| 62 | H/Manipsaa Dodoma | 2 | - | - | 2 |
| 63 | H/W Kisarawe | 9 | - | - | 9 |
| 64 | H/Manipsaa Makambako | 2 | 4 | - | 6 |
| 65 | H/W Ludewa | 2 | 3 | - | 5 |
| 66 | H/W Chato | 13 | 16 | - | 29 |
| 67 | H/W Njombe | 6 | - | - | 6 |
| 68 | H/W Kilolo | 5 | - | - | 5 |
| 69 | H/Manipsaa Iringa | 10 | - | - | 10 |
| 70 | H/Manipsaa Sumbawanga | 10 | - | - | 10 |
| 71 | H/W Sumbawanga | 11 | - | - | 11 |
| 72 | H/W Nkasi | 4 | - | - | 4 |
| 73 | H/W Kalambo | 6 | - | - | 6 |

| Na | Jina la Taasisi | Magari | Pikipiki | Mali Nyingine (Grader, Wheel Loaders, Compressor, Matrekta) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 74 | H/Manipsaa Songea | 10 | - | 1 | 11 |
| 75 | H/W Namtumbo | 2 | - | - | 2 |
| 76 | H/W Meru | 6 | - | 1 | 7 |
| 77 | H/W Bumbuli | 2 | - | - | 2 |
| 78 | H/W Gairo | 5 | - | - | 5 |
| 79 | H/W Kondoa | 3 | - | - | 3 |
| 80 | H/Manipsaa Mwanza | 2 | - | 2 | 4 |
| 81 | H/W Nzega | 7 | - | - | 7 |
| **Jumla ya Sehemu-Halmashauri** | | **483** | **98** | **20** | **601** |
| **Jumla Kuu** | | **552** | **98** | **20** | **670** |

### Kiambatisho Na.41:Orodha ya Taasisi Zenye Mali Bila Bima

| Na | Jina la Taasisi | Magari ya Mifereji | Pikipiki/Mali Nyingine | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Iramba | 4 | 0 | 4 |
| 2 | H/W Misungwi | 3 | 1 | 4 |
| 3 | H/W Bumbuli | 2 | 0 | 2 |
| 4 | H/W Busega | 9 | 0 | 9 |
| 5 | H/W Handeni | 1 | 0 | 1 |
| 6 | H/Manispaa Kahama | 0 | 35 | 35 |
| 7 | H/Manispaa Lindi | 11 | 0 | 11 |
| 8 | H/W Maswa | 4 | 0 | 4 |
| 9 | H/W Mkalama | 3 | 0 | 3 |
| 10 | H/W Mlele | 7 | 0 | 7 |
| 11 | H/W Mpanda | 0 | 20 | 20 |
| 12 | H/W Msalala | 9 | 2 | 11 |
| 13 | H/W Mtama | 5 | 0 | 5 |
| 14 | H/Manispaa Musoma | 12 | 0 | 12 |
| 15 | H/W Nachingwea | 8 | 0 | 8 |
| 16 | H/Jiji Arusha | 38 | 7 | 45 |
| 17 | H/W Iringa | 8 | 10 | 18 |
| 18 | H/W Itilima | 9 | 0 | 9 |
| 19 | H/W Mpwapwa | 8 | 0 | 8 |
| 20 | H/W Meatu | 13 | 0 | 13 |
| 21 | H/W Singida | 1 | 0 | 1 |
| 22 | S/M Dar Es Salaam | 12 | 0 | 12 |
| 23 | H/W Kilindi | 2 | 0 | 2 |
| 24 | H/W Kisarawe | 9 | 0 | 9 |
| 25 | H/Jiji Mbeya | 13 | 0 | 13 |
| 26 | H/Manispaa Sumbawanga | 6 | 0 | 6 |
| 27 | H/W Nkasi | 19 | 0 | 19 |
| 28 | H/W Kalambo | 13 | 8 | 21 |
| 29 | H/W Busokelo | 4 | 0 | 4 |
| 30 | H/W Chato | 18 | 0 | 18 |
| 31 | H/W Kondoa | 8 | 0 | 8 |
| 32 | H/W Kwimba | 17 | 0 | 17 |
| 33 | H/W Mbeya | 13 | 0 | 13 |
| 34 | H/W Nyasa | 11 | 0 | 11 |
| 35 | H/W Rungwe | 6 | 0 | 6 |
| Jumla | | 306 | 83 | 389 |

### Kiambatisho Na.42:Orodha ya Taasisi zenye Mali ambazo Hazijasajiliwa katika mfumo wa GAMIS

| Na. | Jina la Taasisi | Thamani ya Mali Zilizoripotiwa Kabla ya Uchakavu (Shs.) | Thamani ya Mali Zilizoorodheshwa katika GAMIS (Shs.) | Thamani ya Mali Zisizosajiliwa (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) | 5,281,500,080 | 0 | 5,281,500,080 |
| 2 | S/M Shinyanga | 17,974,582,479 | 0 | 17,974,582,479 |
| 3 | S/M Tanga | 27,157,225,000 | 6,369,249,723 | 20,787,975,277 |
| 4 | S/M Singida | 26,870,451,521 | 0 | 26,870,451,521 |
| 5 | H/W Lushoto | 75,916,192,000 | 0 | 75,916,192,000 |
| 6 | H/W Tarime | 135,205,055,598 | 0 | 135,205,055,598 |
| 7 | H/W Kongwa | 58,586,856,808 | 0 | 58,586,856,808 |
| 8 | H/Mji Bunda | 32,439,820,443 | 1,172,788,400 | 31,267,032,043 |
| 9 | H/W Kilosa | 157,642,906,228 | 0 | 157,642,906,228 |
| 10 | H/W Morogoro | 72,614,643,198 | 0 | 72,614,643,198 |
| 11 | H/W Tandahimba | 48,342,319,157 | 0 | 48,342,319,157 |
| 12 | H/W Mvomero | 42,378,965,552 | 0 | 42,378,965,552 |
| 13 | H/Jiji Arusha | 331,801,765,763 | 0 | 331,801,765,763 |
| 14 | H/Mji Babati | 59,859,203,966 | 0 | 59,859,203,966 |
| 15 | S/M Kagera | 15,796,928,943 | 0 | 15,796,928,943 |
| 16 | H/W Kibiti | 31,580,479,455 | 0 | 31,580,479,455 |
| 17 | H/W Kigoma | 43,686,404,000 | 0 | 43,686,404,000 |
| 18 | H/W Bukoba | 60,841,083,937 | 0 | 60,841,083,937 |
| 19 | H/Mji Masasi | 34,130,463,278 | 0 | 34,130,463,278 |
| 20 | H/W Mpwapwa | 63,526,369,511 | 0 | 63,526,369,511 |
| 21 | H/W Muleba | 99,719,242,954 | 0 | 99,719,242,954 |
| 22 | H/W Kyerwa | 73,145,808,099 | 0 | 73,145,808,099 |
| 23 | H/W Madaba | 26,471,700,899 | 0 | 26,471,700,899 |
| 24 | H/W Biharamulo | 42,270,578,276 | 0 | 42,270,578,276 |
| 25 | H/W Singida | 65,849,086,692 | 0 | 65,849,086,692 |
| 26 | H/WUkerewe | 65,202,405,410 | 0 | 65,202,405,410 |
| 27 | H/W Ikungi | 44,497,421,747 | 0 | 44,497,421,747 |
| 28 | H/W Ngara | 27,209,952,005 | 0 | 27,209,952,005 |
| 29 | H/W Rorya | 35,027,512,387 | 0 | 35,027,512,387 |
| 30 | H/W Kilindi | 40,099,924,060 | 0 | 40,099,924,060 |
| 31 | H/W Missenyi | 43,352,274,823 | 0 | 43,352,274,823 |
| 32 | H/W Busokelo | 47,700,748,144 | 0 | 47,700,748,144 |
| 33 | H/W Mbeya | 83,095,205,098 | 0 | 83,095,205,098 |
| 34 | H/W Mbinga | 58,762,287,644 | 0 | 58,762,287,644 |
| 35 | H/W Nyasa | 52,298,156,987 | 0 | 52,298,156,987 |
| 36 | H/W Songea | 41,327,309,981 | 0 | 41,327,309,981 |
| 37 | H/WTunduru | 85,600,014,009 | 0 | 85,600,014,009 |
| 38 | H/W Wanging'ombe | 42,378,965,552 | 0 | 42,378,965,552 |
| 39 | H/W Karagwe | 62,763,708,195 | 0 | 62,763,708,195 |
| 40 | H/W Kyela | 46,465,520,109 | 0 | 46,465,520,109 |
| 41 | H/W Sikonge | 48,160,327,299 | 28,115,544,932 | 20,044,782,367 |
| **Jumla** | | **2,473,031,367,287** | **35,657,583,055** | **2,437,373,784,232** |

## Kiambatisho Na.43:Miradi mipya iliyojengwa kabla ya kupata hatimiliki

| Na. | Jina la Halmashauri | Maelezo ya Mali | Thamani (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Mji Kibaha | Ujenzi wa shule za Msingi Kongowe, Kidimu, Miembesaba, Shule ya Sekondari Simbani na shule mpya katika kata ya Mkuza | 1,610,998,425 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Maelezo ya Mali | Thamani (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 2 | H/W Biharamulo | Ujenzi wa Kibindi SM, Kituo cha Afya Bisibo na Zahanati tano za Kisuma, Mubaba, Kitwechembogo, Kisonga na Migango | 1,329,336,000 |
| 3 | H/W Rufiji | Ujenzi wa Ofisi ya Kata Chumbi, Wodi ya Wajawazito Zahanati ya Mbwara, Shule Shikizi ya Chemchem na shule za sekondari za Muhoro, Chemchem, Rufiji, Ujamaa na Mkongo | 1,327,414,348 |
| 4 | H/Manispaa Lindi | Ujenzi wa maegesho ya malori Mnazi Mmoja, Zahanati ya Mkupanga, Shule ya Sekondari Kiwawa, Hospitali ya Halmashauri, Nyumba ya Mkurugenzi na Shule ya Msingi Mpilipili | 1,302,289,488 |
| 5 | H/W Mpwapwa | Nyumba za wakuu wa Idara, Ujenzi wa shule mpya ya sekondari - Wangi, Mangaliza, Lufufu na Zahanati ya Itende | 1,198,000,000 |
| 6 | H/W Shinyanga | Ujenzi wa Shule ya Msingi Lyabusalu | 1,111,890,563 |
| 7 | H/W Kishapu | Ujenzi/Umaliziaji wa Nyumba ya Mkurugenzi, Shule Mpya ya Sekondari Masagala, Kituo cha Basi Maganzo, Kishapu Girls na Zahanati ya Dugushilu | 826,400,000 |
| 8 | H/W Kilwa | Ujenzi/Umaliziaji wa Nyumba ya Mkurugenzi, Shule ya Sekondari Kiwawa, Vituo vya Afya Zinga na Kipindimbi, Zahanati za Singino, Liwiti na Mkondaji | 676,220,489 |
| 9 | H/W Mwanga | Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari ya Toloha | 584,280,028 |
| 10 | H/W Kondoa | Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Bukulu | 388,418,046 |
| 11 | H/Mji Bariadi | Ujenzi wa Zahanati za Gisadi, Imalilo, Mbiti, Nyangaka na Sanugu | 334,821,428 |
| 12 | H/W Ushetu | Ujenzi wa Shule za Sekondari Mweli na Sabasabini | 318,000,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **11,008,068,815** |
| 13 | Wakala wa Barabara (TARURA) | Ujenzi wa jengo la maabara Kibaha Mjini (Kiwanja Na. 36/1) lenye thamani ya Sh. 27,165,000 | 27,165,000 |
| 14 | S/M Tabora | Ujenzi wa ofisi za maafisa wa tarafa katika Usoke, Igagala, Kazaroho, Choma, Ilolangulu na Kiwere | 837,964,706 |
| 15 | S/M Ruvuma | Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya (Songea), (Hatua ya III - Ardhi), Mkuu wa Mkoa (Hatua ya III), Katibu Tawala Msaidizi (Hatua ya II - Ardhi), Ofisi ya Tarafa ya Sasawala na nyumba ya Mkuu wa Wilaya (Mbinga) | 682,032,624 |
| 16 | S/M Pwani | Ujenzi wa ofisi za tarafa katika Kwaruhombo, Kisiju na Kikale na ukarabati wa nyumba ya makazi ya RAS huko Kibaha | 535,086,938 |
| **Jumla Ndogo** | | | **2,082,249,268** |
| **Jumla Kuu** | | | **13,090,318,083** |

## Kiambatisho Na.44:Viwanja ambavyo havijaendelezwa

| Na. | Jina la Taasisi | Na. ya kiwanja | Kitalu | Mahali | Ukubwa kwa mita za Mraba (m2) | Tarehe ya Ugawaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kituo cha Polisi | 285 | A | CBD | 5,404 | 07/01/2012 |
| | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 296,297 na 298 | B | Kibaha | 13,682 | 07/01/2020 |
| | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 1 | E | Saeni | 486,296 | 01/01/2017 |
| | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 3 | E | Saeni | 407,304 | 01/01/2017 |
| | Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi, Mkoa wa Pwani | 41 na 43 | E | Eneo la Biashara | 5,442 | 04/01/2022 |

| Na. | Jina la Taasisi | Na. ya kiwanja | Kitalu | Mahali | Ukubwa kwa mita za Mraba (m2) | Tarehe ya Ugawaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | 598 | A | CBD | 10,719 | 07/01/2014 |
| | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhi Tanzania | 264 | B | Mizani | 10,000 | 07/01/2021 |
| | Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) | 24 | E | Kibaha | 1,651 | - |
| | Ofisi ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu | 165,166,168,170 na 172 | B | Lulanzi | 10,064 | 01/01/2021 |
| | Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) | 218 | Eneo la Taasis | Mkoani | 7,795 | 10/01/2014 |
| | Mahakama ya Tanzania | 28 | E | Kibaha | 2,747 | 10/01/2022 |
| | Benki Kuu ya Tanzania | 190 na 191 | A | CBD | 14,328 | 10/01/2016 |
| | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu | 215 | | Mkoani | 3,204 | 01/01/2016 |
| **Jumla** | | | | | **978,636** | |

## Kiambatisho Na.45:Mashauri ya Ardhi dhidi ya Halmashauri

| SN | Jina la Halmashauri | Maelezo ya Kesi | Kiasi kinachodaiwa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Babati | Mwananchi Mmoja na Wengine 5 dhidi ya (i) Halmashauri ya Kijiji cha Magara (ii) Kijiji cha Manyara (iii) Kijiji cha Maweni (iv) Kijiji cha Kisangani (v) Halmashauri ya Wilaya ya Babati | 70,000,000,000 |
| 2 | H/Jiji Mbeya | Shauri la Ardhi Na. 6853/2024 | 600,000,000 |
| 3 | H/Jiji Mbeya | Shauri la Ardhi Na. 7950/2024 | 500,000,000 |
| 4 | H/W Simanjiro | Shauri la Ardhi Na. 63/2022 | 350,000,000 |
| 5 | H/W Kibaha | Shauri la Ardhi Na. 150/2023 katika Mahakama Kuu ya Tanzania (Kitengo cha Ardhi) | 300,000,000 |
| 6 | H/M Mpanda | Shauri la Madai Na. 6/2023 | 300,000,000 |
| 7 | H/M Mpanda | Shauri la Madai Na. 9/2023 | 290,000,000 |
| 8 | H/W Karatu | Shauri la Ardhi Na. 10038/2024 | 200,000,000 |
| 9 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 82/2018 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya - Tanga | 190,259,704 |
| 10 | H/MJI Kasulu | Shauri la Ardhi Na. 46/2020 | 175,000,000 |
| 11 | H/Jiji Mbeya | Shauri la Ardhi Na. 2/2023 - Mahakama Kuu | 150,000,000 |
| 12 | H/Mji Handeni | Shauri la Ardhi Misc Na. 208340 | 112,000,000 |
| 13 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 10/2023 Mahakama Kuu - Tanga | 100,000,000 |
| 14 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la 24/2023 Mahakama Kuu | 91,137,000 |
| 15 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 1202/2024 - Mahakama Kuu | 79,600,000 |
| 16 | H/W Muleba | Shauri la Ardhi Na. 6063 - Mahakama Kuu ya Bukoba | 75,000,000 |
| 17 | H/W Mkuranga | Shauri la Ardhi Na. 7456/2024 | 60,000,000 |
| 18 | H/Mji Kasulu | Shauri la Ardhi Na. 67/2016 | 57,000,000 |
| 19 | H/M Mpanda | Shauri la Madai Na. 4/2021 | 40,000,000 |
| 20 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 76/2017 Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya - Tanga | 40,000,000 |
| 21 | H/Jiji Kigoma Ujiji | Shauri la 07/2024 - Mahakama ya Rufaa | 40,000,000 |
| 22 | H/Mji Handeni | Maombi Na. 52/2016 | 35,000,000 |
| 23 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 18/2023 Mahakama Kuu - Tanga | 35,000,000 |

| SN | Jina la Halmashauri | Maelezo ya Kesi | Kiasi kinachodaiwa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 24 | H/M Shinyanga | Maombi Misc Na. 39/2022 | 35,000,000 |
| 25 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 58/2016 Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya - Tanga | 26,000,000 |
| 26 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 3472/2024 - Mahakama Kuu | 25,000,000 |
| 27 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 42/2023 - Mahakama Kuu | 19,035,000 |
| 28 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 50/2012 - Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya - Tanga | 15,000,000 |
| 29 | H/Mji Kasulu | Shauri la Ardhi Na. 40/2019 | 15,000,000 |
| 30 | H/Jiji Tanga | Maombi Na. 57/2019 - Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya | 12,000,000 |
| 31 | H/W Nkasi | Shauri la Ardhi Na. 28350/2024 | 12,000,000 |
| 32 | H/W Mbulu | Shauri la Madai Na. 44/2024 - Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Babati | 10,000,000 |
| 33 | H/W Buhigwe | Rufaa ya Shauri la Ardhi Na. 84/2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kigoma | 10,000,000 |
| 34 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 26846/2024 - Mahakama Kuu | 10,000,000 |
| 35 | H/W Karatu | Shauri la Ardhi Na. 61/2022 | 7,500,000 |
| 36 | H/W Muleba | Shauri la Madai Na. 17/2023 - Mahakama Kuu - Bukoba | 5,000,000 |
| 37 | H/W Buhigwe | Maombi ya Ardhi Na. 102/2019 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kigoma | 4,000,000 |
| 38 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 22/2023 - Mahakama Kuu | 2,700,000 |
| 39 | H/W Karatu | Shauri la Ardhi Na. 60/2023 | 2,500,000 |
| 40 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la 6906/2024 - Mahakama Kuu | 2,122,000 |
| 41 | H/W Muleba | Shauri la Madai ya Ardhi Na. 8299/2024 - Mahakama Kuu ya Bukoba | 2,000,000 |
| 42 | H/W Buhigwe | Rufaa ya Shauri la Ardhi Na. 65/2020 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kigoma | 2,000,000 |
| 43 | H/M Kigoma Ujiji | Shauri la Ardhi Na. 1463/2024 - Mahakama Kuu | 1,240,000 |
| 44 | H/W Muleba | Shauri la Madai ya Ardhi Na. 8299/2024 - Mahakama Kuu - Bukoba | 1,000,000 |
| **Jumla ya Madai** | | | **74,039,093,704** |

ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
4 Barabara ya Mahakama , Tambukareli
S.L.P 950, 41104 Dodoma
Tel: +255 (026) 2161200
Fax: +255 (026) 2321245
Barua pepe: ocag@nao.go.tz

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

UHURU NA UMOJA